# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA SITA

**Kikao cha Nne – Tarehe 3 Februari, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae!

Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

**MHE. ESTHER A. MAHAWE - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

**MWENYEKITI:** Ahsante! Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Benardetha Mushashu.

Na. 42

### Madai Mbalimbali ya Walimu

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Walimu wamekuwa wakiidai Serikali stahiki zao mbalimbali na tatizo hili la kutowalipa kwa muda muafaka limekuwa likijirudia rudia:-

(a) Je, walimu wanadai stahiki zipi na kwa kiasi gani?

(b) Je, Serikali imejipangaje kutatua tatizo hilo na kulimaliza kabisa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernadetha Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya walimu yasiyo ya mishahara ni shilingi bilioni 26 hadi kufikia Desemba, 2016. Deni hili limeshahakikiwa na kuwasilishwa hazina kwa taratibu za mwisho ili liweze kulipwa.

Aidha, madeni yanayotokana na mishahara ni shilingi bilioni 18.1. Uhakiki wa deni la shilingi bilioni 10 umekamilika na linasubiri kulipwa kupitia akaunti ya mtumishi anayedai. Deni linalobaki la shilingi bilioni 8.06 linaendelea kuhakikiwa ili liweze kulipwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kudhibiti uzalishaji wa madeni, mamlaka za Serikali za Mitaa zimetakiwa kutohamisha walimu endapo hakuna bajeti iliyotengwa. Vilevile Serikali imeondoa kipengele kinachohitaji mwalimu akubali cheo chake kwanza ili aweze kulipwa mshahara wake mpya baada ya kupandishwa daraja jambo ambalo lilisababisha malimbikizo makubwa ya mishahara. Aidha, Serikali imeweka utaratibu wa kukusanya madeni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili yaweze kupatikana, kuhakikiwa na kulipwa kwa walimu wanaoidai kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mushashu.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka nenda, miaka rudi tofauti na kada nyingine za watumishi, kero imekuwa madeni ya walimu, madeni ya walimu. Leo hii mnatuambia kwamba madeni ya walimu yamefikia takribani shilingi bilioni 34 *plus*. Walimu hawa wanaidai Serikali wengine kama matibabu, likizo, kwa miaka zaidi ya mmoja hadi miwili. Walimu waliopandishwa mishahara miezi 12 iliyopita hadi leo hawajalipwa huo mshahara wanausikia harufu tu. Walimu wengine wamestaafu zaidi ya miezi sita hawajapata mafao yao.

Ningependa kujua kwa kuwa sasa hivi Serikali mnasema mmeshahakiki ni lini, na mnipe tarehe na mwezi hawa walimu watakuwa wamelipwa haya madeni kwa sababu wamechoka kila siku madeni ya walimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna walimu waliosimamia mitihani mwaka 2015. Leo hii tunazungumza mwaka 2017, kwa nini hadi leo hawajalipwa na ni lini Serikali itakuwa imewalipa hiyo stahili yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, kwanza tuweke kumbukumbu vizuri. Katika kada ambayo Serikali katika njia moja ua nyingine imekuwa ikishiriki vizuri sana katika ulipaji wa madeni ni kada ya walimu. Ukiangalia miaka mitatu mfululizo, *trend* ya malipo ya madeni ya walimu ambayo tulikuwa tumezungumza hapa katika Bunge kila wakati, kwa kweli Serikali inajitahidi sana. Na ndio maana katika kipindi cha sasa hata ukiangalia katika mwezi wa 11 uliopita huu kuna baadhi ya madeni ya walimu *especially* katika baadhi ya Wilaya, Halmashauri, kwa mfano kuna Temeke na Halmashauri zingine kulikuwa na *outstanding* deni karibuni ya shilingi bilioni moja nayo ililipwa vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana katika ulipaji wa madeni mapya mengine; ndio maana Serikali ilikuwa inafanya zoezi zima la uhakiki. Na bahati nzuri, ofisi yetu ya TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Hazina ndio ilishiriki, na jambo hili sasa hivi limekamilika. Na ndio maana nimesema hapa siwezi kutoa *deadline* ni lini, deni hilo litalipwa lakini kwa sababu mchakato wa uhakika umekamilika, hili

deni la shilingi bilioni 26 ninaamini sasa hazina si muda mrefu mchakato wa malipo utaanza kuanza.

Naomba Mheshimiwa Mbunge, najua uko makini katika hili lakini amini Serikali yako kwa vile zoezi la uhakiki ambalo lilikuwa ni changamoto limekamilika basi walimu hawa si muda mrefu wataweza kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la deni la kusimamia mitihani na ndio maana nilisema deni hili lilikuwa ni miongoni mwa madeni haya ambayo yaliyohakikiwa ambayo takribani ilikuwa ni shilingi bilioni sita.

Naomba tuondoe hofu walimu wangu katika mchakato wa sasa walimu hawa wote wataendelea kulipwa ili mradi kila mtu haki yake iweze kulipwa, na Serikali haitosita kuhakikisha inawahudumia vyema walimu wake kwa sababu italeta tija kubwa sana katika sekta ya elimu.

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Hongoli ajiandae Mheshimiwa Masoud.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kuna watumishi ambao walipandishwa daraja kama alivyosema muuliza swali wa kwanza, na kupokea mshahara mpya mwaka jana; na kisha hiyo mishahara ikasitishwa na sasa hivi watumishi hawa ambao ni walimu na watumishi wa afya kuna baadhi yao wameshastaafu, na wengine wanatarajia kustaafu miezi ijayo hii.

Je, Serikali itatumia hesabu gani katika ku-*calculate*, itatumia mshahara upi? Ule wa zamani au mshahara mpya katika kukokotoa kile kiinua mgongo cha mwisho? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa watumishi ambao walikuwa wameingia katika utumishi wa umma, halafu baadaye wakaambiwa warudi nyumbani, tumeshawarudisha watumishi 421 na kwa sasa tayari wameshalipwa takribani watumishi 379, 42 tumewarudishia waajiri wao ili waweze kukamilisha baadhi ya taratibu za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja yake ya pili kwamba unakuta wengine wameshastaafu, lakini ni kiwango gani kitatumika katika kukokotoa mafao yao? Nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wote wanaosikiliza, kwa wale ambao wanastaafu wanapewa kipaumbele miezi miwili kabla ya tarehe ya kustaafu mishahara yao inarekebishwa na watakuwa wamepata katika cheo stahiki ili waweze kutokuathirika na mafao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya walimu yasiyo ya mshahara ni pamoja na deni la walimu kwa Serikali juu ya posho na kufundishia yaani *teaching allowance* ambayo ni ahadi ya Serikali tangu mwaka 2012 ambayo ilitolewa kule Mtwara siku ya Walimu Duniani.

Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada kuweza kuwalipa na kuwapatia fedha zao walimu hawa deni wanalolidai, posho la kufundishia yaani *teaching allowance* kwa haraka inavyowezekana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA YA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kwa hali ya sasa tunachokifanya ni kuhakikisha kwa kadri iwezekano kusaidia sekta ya elimu. Ndio maana kabla sijajibu hili swali sasa hivi ukiangalia Serikali yetu kwa kazi kubwa waliyoifanya sasa hivi, mwanzo ukiangalia Walimu Wakuu, hata Waratibu wa Elimu mwanzo walikuwa hawalipwi hizi *allowances*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali hivi sasa toka mwaka jana kuanzia Waratibu wa Elimu, Wakuu wa Shule za Msingi na Wakuu wa Shule za Sekondari hivi sasa wote wanalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama kuna madeni mengine yoyote Serikali iko katika michakato mbalimbali kuyalipa madeni haya yote. Naomba niwahakikishie ndugu zangu Wabunge kwamba Serikali yetu jukumu letu kubwa ambalo tunalilenga sasa hivi, kwa sababu tunataka kuhakikisha ubora wa elimu lazima madeni haya yote yatalipwa na kama nilivyosema madeni yote ambayo yamehakikiwa kupitia Hazina yatalipwa madeni hayo. Tunataka walimu wetu wawe na morali ya kufanya kazi katika mazingira yao ya kazi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya hiyo hiyo Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini.

Na. 43

**Upungufu wa Vyumba vya Madarasa na Maabara**

**MHE.VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

Baada ya Serikali kutoa tamko la elimu bure wananchi wamekuwa wagumu sana kutoa michango mbalimbali ya kuboresha elimu.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kumaliza tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa na vyumba vya maabara katika shule za msingi na sekondari?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Elimu Msingi bila Malipo unazingatia uendeshaji wa shule bila ada na michango kutoka kwa wazazi au walezi. Hata hivyo, mpango huo haujaondoa dhamira na uzalendo wa jamii kuchangia shughuli za maendeleo ya nchi yao kwa hiari. Kwa uzalendo wa wananchi walioonesha hivi karibuni Serikali imefanikiwa kupiga hatua za maendeleo katika sekta mbalimbali. Mfano, katika kufanikisha utengenezaji wa madawati kwa asilimia 97.2 kwa shule za msingi na asilimia 100.3 kwa shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa rai kwa wananchi wote ambao wamekuwa wagumu katika kushiriki shughuli za maendeleo wabadilishe mwenendo wao na kuwa na uzalendo kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkakati wa kupunguza tatizo la nyumba, vyumba vya madarasa na maabara, Serikali katika bajeti ya mwaka 2016/2017 imetenga shilingi bilioni 29.3 kwa ajili yya ujenzi wa vyumba vya madarasa 3,306 kwa shule za msingi na shilingi bilioni 16.3 zimetengwa kujenga vyumba vya madarasa 1,047 kwa shule za sekondari. Aidha, kupitia *MMES II* zimetengwa shilingi bilioni 23.6 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vyumba 1,642. Kwa upande wa maabara Serikali imetenga shilingi bilioni 18.9 kwa ajili ya

ukamilishaji wa vyumba 2,135 vya maabara. Serikali itaendelea kutenga bajeti kila mwaka wa fedha na kuwashirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo katika kufanikisha upatikanaji wa elimu bora hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE.VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, na ameendelea kusema hapa kwamba hii michango tunahitaji kuendelea kuwahamasisha wananchi ili waweze kuchangia. Lakini ukiangalia kwa mapungufu tuliyokuwanayo kwa maana ya madawati, vyumba vya madarasa pamoja na maabara; ni mapungufu makubwa sana na kwa sababu wananchi wengi wanaamini kwamba michango ni hiari kama alivyosema Naibu Waziri, hatuoni kama tutashindwa kutekeleza azma yetu ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanaweza kupata elimu bora kwa sababu wanafunzi wengi wataendelea kukosa vyumba vya madarasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tunatambua kwamba wazazi pamoja na shughuli kubwa wanazozifanya pamoja na kujenga *hostel,* lakini bado ukiangalia wale wanafunzi wa kike zile gharama zote za kuwasomesha kwenye zile *hostel* bado ni gharama za wazazi. Ni kwa nini Serikali isikubali kugharimia hizo gharama za *hostel* baada ya kuwa hizi *hostel* zimejengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mathayo kwa sababu katika rekodi pale juzi juzi ameweza kushiriki utoaji wa mifuko 200 ya *cement* kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika eneo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefika pale Musoma Mjini, nimeweza kutembelea nimeona kazi kubwa anayofanya. Kwa hiyo, imani yangu kwa ile kazi unayoifanya na nadhani mnataka mjenge takribani vyumba karibuni 200 vinatakiwa vikamilike ndani ya mwezi Machi, naomba tuwaunge mkono kwa sababu mnafanya kazi njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kusema kwa mkakati huu tutashindwa, naomba nikuhakikishie ndio maana mwaka huu tunakamilisha vyumba vingi kwa kutenga karibu shilingi bilioni 29, na ndugu zangu Wabunge

naomba niwaambie huku *site* tunakotoka sasa hivi ukienda huko utakuta kazi kubwa sana ya ujenzi wa madarasa inaendelea. Naamini katika muda huu ambao tuko hapa Bungeni, Mbunge mwingine akirudi katika *site* kwake atakuta kwamba kuna madarasa mengine katika eneo lake hata alikuwa hajatarajia yameshakamilika. Hii yote ni juhudi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwahakikishie Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tutajitahidi kuhakikisha azma ya Serikali kuwapatia wananchi wake elimu bora inafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala zima la zile *hostel* zilizojengwa changamoto ni kubwa sana, katika suala la vijana hasa watoto wetu wa kike kwamba ikiwezekana kwamba zile *hostel* zilizojengwa Serikali igharamie. Naomba niseme hili ni wazo ngoja tutalifanyia kazi, kwa sababu kugharamia *hostel* zote Tanzania ni bajeti kubwa sana na hizi zimejengwa makusudi ni *hostel* za kata ziko katika maeneo yetu. Lengo ni mtoto anaenda shuleni na kurudi lakini kwa sababu changamoto ya uzito kwa wanafunzi ni vyema tujenge *hostel* nasema tuendelee na mpango huu wa sasa pale Serikali kwa kushirkiana na wadau mbalimbali itakavyoona kwamba nini tufanye, lengo ni kuboresha wananchi katika kata zetu tutafanya hivyo kwa kadri inavyowezekana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani ilijigamba kwamba itatoa elimu bure na utekelezaji wa elimu bure kwa mujibu wa watafiti wa haki elimu inahitaji takribani shilingi bilioni 700 kwa mwaka mmoja wa fedha. Na hali ilivyo sasa hivi, fedha mnazopeleka ni kidogo tu za fidia ya ada.

Je, mko tayari sasa kuwaambia Watanzania mmeshindwa kutekeleza elimu bure ili Watanzania wachangie suala la elimu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Watanzania wanafahamu. Wakati hatuna programu ya elimu bure, vijana wengi walikuwa wanakosa hata hii elimu ya

msingi, wengine walikuwa wanatishwa vitumbua kwenda kuuza barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi nilipita kule katika Mkoa wa Kagera, nilipofika pale Nyakanazi, shule ambayo mwaka huu ime-*register* wanafunzi wengi zaidi ya wanafunzi 800 wa shule ya msingi peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kutoa elimu bure hii kusaidia mitihani, gharama za ada, hata suala zima la posho, ni jambo kubwa sana. Mimi naamini ndio maana kwa rekodi mwaka huu inatuonesha vijana wengi sasa hivi wanaripoti shule za seondari ukilinganisha na kipindi cha mwanzo, kwa sababu mwanzo wazazi walikuwa wanashindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kikubwa zaidi naomba tuamini kwamba Serikali katika jambo hili imeleta ukombozi mkubwa. Na hili niseme kwa vile Serikali tumejipanga na hili nimelisema sehemu mbalimbali, changamoto yetu inatufanya tunataka tuseme lazima *private schools* sasa si muda mrefu zitatakiwa zijipange vizuri, kwa sababu tunaenda kwa kasi kubwa ya ajabu. Huku tunakokwenda tutakwenda kupata mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu Watanzania wote tutaungana pamoja, hii nchi yote ni ya kwetu, Watanzania wote ni wa kwetu na watoto ni wa kwetu tusaidiane kuhakikisha Tanzania inafika mahali salama katika suala zima la utoaji wa elimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Maria Kangoye.

Na. 44

**Uhaba wa Watumishi Katika Halmashauri Nchini**

**MHE. MARIA N. KANGOYE** aliuliza:-

Kumekuwepo uhaba wa watumishi katika Halmashauri nyingi nchini ambao unaleta athari katika utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kwa kutotoa huduma katika kiwango kinachohitajika.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuajiri wataalam hasa vijana waliomaliza vyuo ambao wanazurura mitaani kwa ukosefu wa ajira?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndilla Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kukabiliana na upungufu wa watumishi wa umma Serikali imekuwa ikitenga bajeti ya ikama na mishahara na kutoa vibali vya ajira mpya kwa taasisi zote za umma ikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa, kama ilivyo kwa sekta zote za ajira katika utumishi wa umma kwa kutegemea kiwango cha kukua kwa uchumi. Kwa kuzingatia sera za kibajeti, Serikali imetenga pia nafasi za ajira mpya katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo zitajazwa kwa awamu, ambapo watumshi wa umma wapatao 5,074 hadi sasa wameshaajiriwa, ikiwemo watumishi wa hopsitali mpya ya Mloganzira. Aidha, tayari Serikali imetoa kibali cha kuajiri walimu wa masomo ya hisabati, sayansi, mafundi sanifu wa maabara za shule za Serikali wapatao 4,348.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kutoa rai kwa mamlaka za ajira kutumia vizuri rasilimali watu walizonazo kwa kuwapanga watumishi wa umma kwa kuzingatia uwiano sahihi ili kuweza kukabiliana na changamoto za upungufu wa watumishi wa umma.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kumekuwa na utaraibu wa wastaafu kuongezewa mikataba ya kufanya kazi. Je, Serikali haioni kwamba hii ni sababu mojawapo ya ukosefu wa ajira kwa vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kati ya Wilaya saba za Mkoa wa Mwanza, Wilaya sita ambazo ni Sengarema, Ilemela, Nyamagana, Misungwi na Magu, pamoja na Ukerewe, zinategemea asilimia kubwa ya mapato yake kutoka kwenye sekta ya uvuvi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri vijana wenye taaluma ya uvuvi ili kuweza kukidhi haja ya elimu ya kilimo cha samaki pembezoni mwa Ziwa Victoria? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, hili swali lina Wabunge wengi. Lijibu kwa kifupi liwaingie vizuri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kuhusiana na Serikali kuongezea muda wastaafu au kuwapa mkataba wa ajira, nipende kusema yafuatayo; kwanza kabisa tunao waraka ambao ndio mwongozo unaotoa taswira au mwongozo ni watu gani au kada zipi ambazo zinastahili kuweza kuongezewa mkataba wa ajira.

Nipende tu kusema kwamba kwa sasa kipaumbele kipo kwa marubani, kipaumbele kipo kwa wahadhiri wa vyuo vikuu na hao ndio wanaopewa mikataba. Lakini ni lazima wao pia wanapoomba kuongezewa mkataba wa ajira baada ya kustaafu, ni lazima waweze kuwasilisha mpango wao wa kurithishana madaraka, lakini vilevile ni lazima na wenyewe waweze kutoa wamefanya jitihada gani za kuhakikisha kwamba wanawawezesha watumishi wengine walioko chini yao kuhakikisha kwamba wanaweza ku-*take over* baada ya wao kuondoka katika nafasi hizo walizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili hasa katika ajira za vijana na ameongelea zaidi katika ajira za uvuvi; kwanza nipende tu kusema kwamba Mkoa wa Mwanza katika takribani Wilaya zake nne tunatambua ndizo ambazo zina upungufu mkubwa wa watumishi ikiongozwa na Wilaya ya Buchosa, Wilaya ya Kwimba pamoja na Wilaya ya Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika ikama ya mwaka huu 2016/2017 nitolee tu mfano katika Wilaya ya Ukerewe, wavuvi wasaidizi takribani watano wamepangiwa na hizo ni katika nafasi chache ambazo zimewekwa katika utaratibu wa ikama ya mwaka 2016/2017. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kada ambazo zina upungufu mkubwa katika Halmashauri hizo tutazipa kipaumbele ili kuhakikisha kwamba, wanaweza kufanya kazi kwa ufanisi na kwa uweledi mkubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Ghasia, jiandae Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyozungumza ni Februari tunaelekea Juni, mwaka wa fedha unaishia na Mkoa wa Mtwara ni miongoni mwa mikoa ambayo ina tatizo kubwa la watumishi na hasa wa sekta ya afya. Nilitaka kufahamu ni lini hicho kibali kitatolewa na ajira hizo zitaajiriwa? Kwa sababu ninavyo vituo viwili vya afya vyenye vyumba vya upasuaji, lakini hakuna upasuaji unaofanyika kwa sababu hakuna watumishi na Wilaya nyingine zote za Mkoa wa Mtwara hali ni hiyo hiyo, ni lini kibali kitatolewa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri anataka kujua ni lini tu. Unaweza kumwambia bajeti ya… *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa namna anavyofuatilia masuala mazima ya utumishi na tunatambua pia, na yeye alishakuwa Waziri wa Utumishi na alifanya kazi kubwa na nzuri sana hapo alipokuwa na sisi tumeweza kuvaa viatu vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sasa, kama nilivyoeleza, tumeanza na watumshi wa sekta ya elimu pamoja na mafundi sanifu wa maabara na tunatarajia ifikapo mwezi wa tatu wataweza kuingia katika ajira. Kwa upande wa watumishi wa sekta ya afya, muda si mrefu tutaanza pia awamu yao na ninadhani kati ya mwezi wa tatu mpaka wa nne watakuwa wameshaingia katika utumishi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwita jiandae Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Ni kweli kwamba kuna changamoto nyingi kwa watumishi wa umma, ni pungufu kwa uwezo mdogo wa Serikali kuajiri na wengine wametumbuliwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nijue ni nini kauli ya Waziri wa Utumishi kwa watumishi wale ambao wanashushwa vyeo, wanadhalilishwa na kutukanwa na viongozi, hasa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa na ukizingatia matokeo ya *form four* yametoka, wameanza kutumbuliwa. Sasa nini kauli ya Serikali kuwatia moyo waliopo kazini na kuwatia moyo ambao watapata ajira, ili wajue wataenda mahali salama wakafanye kazi nzuri kutumikia Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme tu kwamba masuala mazima ya nidhamu, ajira pamoja na upandishwaji wa vyeo na kushushwa vyeo yanaongozwa na kanuni, sheria na taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema tu ni kwamba, kama kuna ambaye anaona kanuni hazikufuatwa, basi tuweze kupata taarifa ili tuweze kufuatilia. Lakini tumekuwa tukitoa miongozo mbalimbali kwa viongozi wa kisiasa pamoja na watendaji kuhakikisha kwamba, wanazingatia Sheria ya Utumishi wa Umma, wanazingatia Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, pamoja na Kanuni za Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, nipende tu kusema kwamba kama kuna mtumishi ambaye naona yeye hakutendewa haki basi asisite kuwasilisha malalamiko yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Dkt. Kigwangalla naona umesimama sana labda ulikuwa na majibu. Waziri TAMISEMI umesimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana yaliyotolewa na Waziri Mheshimiwa Kairuki, napenda niongezee tu kwenye swali lililoulizwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kumekuwa na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kutokana na watumishi wazembe. Na mtambue kwamba katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tulisema kwamba kwa watumishi wazembe hatutakubali kuendelea nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue nafasi hii kusema kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wamegawiwa maeneo yao ya utawala na wanasimamia masuala yote, lakini wanasimamia yote kwa mujibu wa sheria. Haiwezekani unapewa pesa ya *basket fund,* wewe ni *DMO* halafu huzitumii na watu wanakosa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya utafiti katika mikoa minne, ziko hela nyingi kwenye Halmashauri hazitumiki, wanataka kuzifanyia nini? Mnasema tusichukue hatua, haiwezekani. Haiwezekani unapewa shule una walimu zaidi ya 15 pamoja na changamoto zilizopo ambazo ni haki yao kuzidai, lakini si sababu ya wao kutokutimiza wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tu kwamba Wakuu wa Mikoa wanayo haki ya kisheria kuchukua hatua kwa mtumishi yeyote awe ni Mkuu wa Shule, kwa mfano uteuzi wa Mkuu wa Shule unateuliwa na *RAS* ambaye ndio Katibu Mkuu wa Mkoa. Kwa hiyo, Mkuu wa Mkoa akichukua ile hatua, nimekuwa nikiulizwa na Wabunge wengi hapa kwamba mbona wanaingilia mambo mengine. Jamani, mkumbuke mlikuwa mnasema watumishi wetu ni

wazembe. Ngonjeni kidogo tubanane ili twende kwenye ufanisi na Watanzania wanangojea hayo mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwasihi tu Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane. Wenzetu nao wale ni binadamu katika namna moja au nyingine wanaweza wakafanya makosa, tuwasiliane, turekebishane, ndio maana ya *administration and leadership.* Si kwamba wao hawakosei, wanaweza wakakosea kwa namna moja ama nyingine, lakini na mazingira yale tuyaangalie, lakini huku nikitambua kwamba watumishi nao wana haki yao, lakini na wao pia watekeleze majukumu tuliyowapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa baada ya majibu ya Waziri, tunaendelea. Mheshimiwa Japhet Hasunga. Ngoja ngoja, Mheshimiwa Japhet ngoja, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilitaka kuongezea tu kwenye jibu linalohusu mkakati wetu wa kupeleka huduma za upasuaji kwenye vituo vya afya nchini wakati hakuna watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwishakutoa maelekezo kama Serikali kwa Makatibu Tawala wote wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kufanya *redistribution* ya watumishi ndani ya maeneo yao, kuwatoa kwenye maeneo ambapo wapo wengi na kuwapeleka kwenye vituo hivyo ambavyo tunataka vitoe huduma za upasuaji. Huu ni mkakati wa muda tukisubiri mkakati wa kudumu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Hasunga.

Na. 45

**Mafunzo Kwa Watumishi na Viongozi wa Umma**

**MHE. JAPHET N HASUNGA** aliuliza:-

Kwa kuwa watumishi na viongozi wengi wamekuwa wanaingia kwenye madaraka mbalimbali ya nchi bila kupewa mafunzo ya kuwaandaa kama ilivyo katika nchi nyingi duniani na kama ilivyo kwenye vyombo vya majeshi yetu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa viongozi wote wanapewa mafunzo ya awali kabla ya uteuzi wa madaraka yoyote katika utumishi wa umma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwapatia mafunzo ya awali watumishi na viongozi wa umma kabla ya uteuzi wa madaraka yoyote katika utumishi wa umma ili waweze kuuelewa utumishi wa umma na kufahamu misingi yake, sheria, kanuni na taratibu za utendaji kazi na kuwapatia stadi za uongozi zinazowezesha kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi. Katika kutekeleza azma hii Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(a) Imeandaa na kuendesha mafunzo elekezi kwa watumishi wanaoteuliwa kushika nafasi za uongozi ili waweze kumudu madaraka mapya.

(b) Imeendelea kutoa mafunzo ya uongozi *(Leadership Development Programmes),* kwa watumishi waandamizi kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, lakini pia kuwaandaa kwa ajili ya kushika nafasi za uongozi pindi watakapoteuliwa kushika nafasi hizo. Mafunzo hayo yamekuwa yakiendeshwa na taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo Taasisi ya Uongozi, Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Mtandao *(TaGLA),* Chuo Kikuu cha Mzumbe pamoja na ESAMI. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 watumishi waandamizi 1,397 waliweza kupatiwa mafunzo ya uongozi.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Serikali imeanzisha Chuo cha Taifa cha Ulinzi *(National Defence College of Tanzania)* kinachotoa mafunzo ya uongozi kwa Maafisa Waandamizi wa Kijeshi na Kiraia *(Inter Service Training)* kwa kuhusisha Maafisa wa Jeshi na wa Kiraia *(Defence-Civil Staff Training)* ikiwa ni pamoja na kuwapatia uelewa wa masuala ya usalama na hivyo kuwajengea uwezo wa kutambua athari za kiusalama wanapotunga na kutekeleza sera, sheria na maamuzi mbalimbali ya kiutendaji.

(d) Mheshimiwa Mweenyekiti, lakini pia, Serikali kupitia Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kimetoa mafunzo kwa viongozi waandamizi 86 na kiko

katika maandalizi ya kuandaa utaratibu wa kuwa na mafunzo ya lazima kwa Maafisa Waandamizi katika utumishi wa umma *(Mandatory Course for Senior Officers in the Public Service)*. Mafunzo haya ya lazima yanalenga kuwawezesha Maafisa Waandamizi kujua majukumu ya msingi ya uongozi na usimamizi katika taasisi za umma, hivyo kuwaandaa na kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu hayo pindi watakapoteuliwa kushika nafasi za uongozi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hasunga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, *sorry*.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007/2008 Serikali kupitia Ofisi ya Rais - Utumishi ilikipa Chuo cha Utumishi wa Umma kikishirikiana na chuo kimoja cha Macintosh cha Canada kuandaa *framework* ya kuwandaa viongozi ambayo ilijulikana kama *Leadership Competence Framework*. Na katika *framework* hiyo ilikuja na sifa 24 yaani *leadership competencies* 24. Sasa, je, ni lini Serikali itakuwa tayari sasa kuziingiza hizo *competencies* katika mafunzo ambayo tayari yameandaliwa na Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa katika utaratibu wa majeshi yetu kuna utaratibu kwamba mtu hawezi kupata cheo chochote mpaka kwanza apate mafunzo fulani. Sasa kwa kuwa Serikali imesema inaandaa utaratibu wa kozi ambazo zitakuwa ni lazima kwa watumishi wa umma waandamizi. Je, ni lini sasa tamko la Serikali hizo kozi zitaanza ili watumishi hawa wawe wanafundishwa na wanaandaliwa ili wawe mahiri kabla hawajapata uteuzi wa madaraka ya aina yoyote?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Hasunga, alikuwa ni mtumishi wa Chuo cha Utumishi wa Umma kwa hiyo, anaifahamu sekta hii vizuri sana na anakifahamu chuo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza kwamba ni lini sasa Serikali itakuwa tayari kuingiza zile sifa 24 za uongozi katika mafunzo yake; nisema tu kwamba sasa tunaandaa utaratibu katika hayo mafunzo ya lazima,

utakapokamilika na zile sifa zote 24 katika *leadership competence* zitaweza kuingizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, ni lini sasa katika mafunzo ya *in-service,* kabla watu hawajapandishwa cheo yataweza kuwekewa utaratibu, nipende tu kusema kwamba pamoja na haya tumeandaa pia, utaratibu wa kuwa na *assessment centre* ambao tutaweza kuweka kuwa na *pool* ya watu mbalimbali ambao wana-*managerial positions* ambazo wakati wowote wanaweza wakateuliwa. Watakuwa *tested,* lakini pamoja na hayo pia, kutakuwa na yale mafunzo ya lazima ambayo niliyaeleza awali yatakapokamilika basi wataweza kupatiwa na tutakuwa hatuwezi kupandisha cheo mtu kabla hajapata mafunzo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde, jiandae Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Tatizo la viongozi kukosa semina elekezi juu ya masuala ya uongozi yamekuwa yakionekana kuanzia ngazi za juu, kwa mfano mdogo tu hapa katika swali lililopita unakuta Mawaziri wamejibu, Naibu Waziri naye anajibu kwa hiyo, *protocol* inakuwa inaonekana pale haijafuatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala langu ninalotaka kujua ni kwamba taratibu kama hizi, viongozi ambao wanakosa semina za mafunzo elekezi na *contradiction* inaonekana ndani ya Bunge lako Tukufu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde, uliza swali lako la nyongeza acha mambo mengine.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio nauliza swali.

**MWENYEKITI:** Unapoteza muda wa Bunge, uliza swali lako.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka nijue makosa kama haya yataendelea mpaka lini kwa viongozi ambao hawana semina kama Mawaziri? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, mjibu kuhusu semina elekezi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na semina elekezi au mafunzo elekezi kabla watu hawajaingia katika madaraka nimeshaeleza awali.

Lakini pili, kwa mwaka huu wa fedha peke yake Taasisi ya Uongozi imetoa mafunzo kwa viongozi 544, lakini pia tumekuwa tukitoa mafunzo kwa Mawaziri, tumekuwa tukitoa mafunzo kwa Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na nafasi nyinginezo na tutaendelea kufanya hivyo kila wakati itakapobidi.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya viongozi katika ngazi za Wilaya, hasa ma-*DC* na ma-*DAS,* wengi wao wamekuwa wababe na wamekuwa wakitumia madaraka yao kuwanyanyasa wananchi kwa kisingizio eti wao ni Marais wa Wilaya. Wakati nafahamu katika uchaguzi uliopita tumemchagua Rais mmoja tu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Je, Serikali haioni hili linaweza kuwa ni tatizo kubwa sana? Na inawezekana kama tutaendelea bila kufanya utafiti wa kutosha na kuwachunguza watu hawa wanaweza kuharibu hata imani ya wananchi kwa Chama cha Mapinduzi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kama nilivyosema muda mfupi uliopita kwamba hawa ni binadamu na ni Watanzania wenzetu. Na kutokana na kazi na *nature* ya kazi wanazozifanya inawezekana mahali fulani kukatokea mikwaruzano, lakini tatizo la mtu mmoja haliwezi kuwa la watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanafanya kazi nzuri sana. Wanatusaidia maana wao ndio wasimamizi kwa niaba ya Serikali katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa jana lilitokea swali ambalo lilikuwa linataka kufahamu kofia au nafasi ya Mkuu wa Mkoa. Mkuu wa Mkoa ana kofia mbili, ana kofia ambazo zinashuka kwa Rais zile mbele, *Head of Executive and Head of State. The President is Head of State and at the same time Head of Executive.* Wakuu wa Mikoa wanashukiwa na zile kofia mbili na ndio maana wanalindwa na bunduki kati ya saba mpaka kumi na moja na askari saba hadi kumi na moja. Na ni haki yao wao kulindwa kwa sababu wanafanya maamuzi mazito, wanaweza wakaingilia jambo ambalo haliendi sawa kwa sababu ndio wawakilishi wa Serikali katika maeneo yao. Na kwa hiyo lazima vyombo vya ulinzi na usalama viwalinde kwa sababu ya *nature* ya kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge ni suala la mawasiliano, sio na ninyi tena kutunishiana ubabe kule. Kinachowezekana kutokea kule sasa ikiwa hivyo itaonekana nani ni nani. Lakini kama tukiletewa, inapotokea upungufu tunaweza tukashughulikia *administratively* tu na jambo likaenda vizuri, kama nilivyosema hawa nao ni binadamu. Kwa hiyo, pale ambapo tunapata fursa tumekuwa tukitoa maelekezo… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** kwao na tumekuwa tukitoa hata kwa maelekezo ya maandishi na wala semina sio jambo la msingi sana. Lakini kubwa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wameshakuelewa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Lakini kubwa hapa ni maelekezo na mtu kujua wajibu wake. *(Makofi)*

Na. 46

**Wagonjwa Wanaokwenda Kutibiwa Nje Kutoka Zanzibar Kulazimika Kupata Rufaa Kutoka Muhimbili**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Mgonjwa anapotoka Zanzibar na kupelekwa kwa matibabu nje ya nchi analazimika kupata rufaa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili licha ya kuwepo kwa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, Zanzibar ambayo ina madaktari wenye uwezo kama wale wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

(a) Je, kwa nini Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja haijapewa uwezo wa kutoa rufaa ya matibabu nje ya nchi?

(b) Je, kuinyima uwezo huo Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kutoiamini hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Mendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Jimbo la Chumbuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, sio kweli kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja haina uwezo wa kutoa rufaa kwa wagonjwa wanaohitaji kupelekewa nje ya nchi kwa huduma za afya ambazo hazipatikani katika hospitali hiyo. Hospitali ya Mnazi Mmoja ina uwezo na ina utaratibu wake wa kutoa rufaa kwa wagonjwa wanaolazimika kupelekwa nje ya nchi kwa matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Hospitali ya Mnazi Mmoja inaweza kutoa rufaa kwa wagonjwa kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili au hospitali nyingine yoyote watakayoona inafaa. Aidha, wagonjwa wengine kutoka Zanzibar huwa wanakuja Tanzania Bara kupata huduma za hospitali zilizopo bara bila kupata rufaa ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wagonjwa hawa wanapohitaji kupelekwa nje ya nchi watapewa rufaa na hospitali ya mwisho inayowapa huduma kwa wakati huo. Hospitali hiyo inaweza kuwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili au nyingine yoyote ile ya ngazi ya Kitaifa. Wagonjwa hawa hawawezi kurudishwa Zanzibar kwenda kupewa rufaa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kuwa hospitali ya Mnazi Mmoja imenyimwa uwezo wa kutoa rufaa kwa wagonjwa wanaotakiwa kupelekwa nje ya nchi kwa uchunguzi na matibabu. Hospitali ya Mnazi Mmoja ina uwezo kamili wa kutoa rufaa kwa wagonjwa wanaotakiwa kupelekwa nje ya nchi na imejiwekea utaratibu wake wa kufanya hivyo.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka nyuma kulikuwa kuna utaratibu wa Wizara zetu mbili hizi kukutana na kubadilishana uzoefu na vikao hivyo vilivyokuwa vinafanyika vilikuwa vina tija ndani yake ambavyo vilipelekea Madaktari Bingwa kutoka Muhimbili kuja Zanzibar na kutoa ushirikiano mkubwa. Vikao hivyo sasa hivi havifanyiki kwa muda mrefu kidogo. Je, Serikali ina kauli gani kuhusu vikao hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba Serikali ina mpango gani na vikao hivyo? Vikao hivyo havijawahi kufutwa na havitofutwa kwa sababu Wizara hizi mbili (Wizara ya Afya ya Jamhuri ya Muungano na Wizara ya Afya ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar) zimekuwa na utamaduni huo na zinaona utamaduni huo ni mzuri na zitauendeleza. Hivyo, tutaendelea kuvihuisha ili viwe *active* zaidi kuliko ilivyokuwa katika mwaka huu mmoja wa uchaguzi uliopita. Lakini kuanzia mwezi Januari tayari tumekwisha kufanya kikao kimoja, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Ussi.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa swali kwenye Wizara ya Afya. Suala linalotokea Hospitali ya Mnazi Mmoja ni sawasawa kabisa na masuala yanayotokea katika Hospitali ya Rufaa ya Ndanda, Mkoa wa Mtwara. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi alipotembelea alitoa ahadi ya wafanyakazi wasiopungua 85; hivi ninavyoongea sasa hivi hospitali ya Rufaa ya Ndanda inakaribia kukosa hadhi ya kuitwa Rufaa kwa sababu kuna Daktari Bingwa mmoja tu. Je, Wizara yake ina mpango gani wa kuwawezesha watu hawa ili waendelee kutoa huduma kwa sababu ni hospitali ambayo ina vifaa vingi lakini inakosa wataalam wa kuvitumia?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba mpango tulionao ni kusubiri kibali kutoka kwa wenzetu wa utumishi kitoke, kitakapotoka tutaajiri Madaktari Bingwa kwa kiasi ambacho tutakuwa tumekasimiwa na kuwatawanya kwenye hospitali zote za Rufaa za Mikoa nchini ikiwemo Hospitali ya Ndanda. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Changamoto za mahospitalini zimekuwa nyingi na moja kati ya kero kubwa ambayo wananchi wanaipigia kelele ni kile kitendo ambacho mwananchi akiuguza mgonjwa wake na hatimaye akapoteza maisha haruhusiwi kuchukua mwili wa marehemu mpaka alipe gharama za matibabu ambazo kimsingi hazikumsaidia mgonjwa wake mpaka amefariki dunia. Kitendo hiki kinatengeneza taswira mbaya kwa wananchi kuonesha kwamba Serikali haijali utu na haithamini utu wa wananchi wake.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba endapo mwananchi atafiwa na mgojwa wake lile deni la matibabu asamehewe ili familia ijikite tu katika kushughulikia suala la mazishi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hili ni swali jipya, lakini wewe ni mzoefu mjibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba kwanza nakanusha kwamba Serikali haithamini utu wa Watanzania, hapana Serikali ina thamini sana utu wa Watanzania wote na ndio maana ikaweka utaratibu mzuri sana wa kutoa huduma za afya kwa watu wote hata wasiojiweza. Tanzania ni miongoni mwa nchi chache sana ambazo zinawapa usawa wa huduma tena bure kwa kuwahudumia takribani asilimia 67 ya wagonjwa wote hapa nchini bure bila gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa wale wachache ambao wanatengeneza hiyo asilimia 33 ya wanaochangia huduma za afya, kama itajitokeza kwa bahati mbaya baada ya kuhudumiwa akafariki halafu Sheikh Mtolea unasema sasa pale ndio utu wake unaanza, sio sahihi. Utu wa Mtanzania upo akiwa anaumwa, akiwa anahudumiwa kwenye hospitali na hata ikatokea bahati mbaya umauti ukamkuta utu uko pale pale. Lakini gharama za mtu ambaye amekwishahudumiwa iwe alipona ama kwa bahati mbaya alipoteza maisha; zipo pale pale ni lazima ziwe *compensated* na Serikali haiwezi kuziondoa.

Na. 47

**Kumuinua Mwanamke Kiuchumi**

**MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza:-

Ni azma ya Serikali ya CCM kumuinua mwanamke kiuchumi na azma hiyo ilipelekea Serikali kuanzisha Benki ya Wanawake.

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kufungua madirisha ya benki hiyo mikoani hasa Mkoa wa Iringa ambapo kuna *Community Bank (MUCOB)* iliyopo Wilayani Mufindi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Desemba, 2016 Benki ya Wanawake imefanya kazi katika mikoa saba ambayo ni Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Iringa, Njombe, Mbeya na Ruvuma. Mwaka 2014 madirisha mawili yalifunguliwa Iringa Mjini na Makambako na hadi kufikia Desemba, 2016 jumla ya wajasiriamali 6,850; wanawake wakiwa 5,350 na wanaume wakiwa ni 1,500 walipata mikopo kupitia madirisha hayo ambayo wajasiriamali wa Mufindi nao wamefaidika. Aidha, benki imefungua vituo vya kutolea mikopo 252 kufikia Desemba, 2016 na Mufindi kuna kituo kimoja kilichopo Mafinga ambacho kimetoa mikopo ya jumla ya shilingi milioni 120 kwa wateja 146, wanawake wakiwa 117 na wanaume wakiwa 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania imeingiza suala la kufungua dirisha katika Benki ya Wananchi ya Mufindi *(MUCOB)* kwenye mpango mkakati wa mwaka 2012 mpaka 2017. Tunatarajia dirisha hili litafunguliwa mara tu tutakapopata fedha za kutekeleza mpango huu. Benki ya Wanawake ina mkakati wa kuenea nchi nzima, lakini kikwazo kikubwa ni ukosefu wa mtaji. Endapo benki itafanikiwa kupata mtaji wa kutosheleza itaweza kufungua ofisi zaidi mikoani ili kuwahudumia wananchi wengi zaidi na kwa ukaribu. *(Makofi)*

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Kwako Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na majibu hayo mazuri pia nikupongeze umekuwa *champion* mzuri wa vijana, watoto na wanawake na unatambua kuwa wanawake wengi hususani Mkoa wa Iringa wanakiu kubwa ya kujitafutia maendeleo ya kwao pamoja na watoto wao. Na kikwazo kikubwa kimekuwa upatikanaji wa hii mitaji na mikopo yenye riba nafuu. Pamoja na jitihada za Serikali za kufungua hivi vituo viwili pale Mkoa wa Iringa na kama ulivyokiri huu mchakato wa kufungua dirisha pale *MUCOB* umechukua muda mrefu, sasa ningeomba pia utupe kipaumbele na *time frame* ni lini sasa pale *MUCOB* tutegemee kituo hiki ili hawa akinamama waepukane nah ii adha ya kupata mitaji yao? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, namshukuru Mheshimiwa Rose Tweve kwanza kwa kunipa *compliment*, mara chache sana Wabunge huwa wanawapongeza Serikali wanapofanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *time frame* ni mpaka tutakapopata fedha kwa ajili ya kutunisha mtaji wa benki yetu. Lakini jambo la faraja ni kwamba kwa

ahadi niliyoitoa hapa hapa Bungeni kwake yeye mwenyewe na kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba tuna-*cosider* kufungua dirisha pale *MUCOB* bado iko pale pale na ndio maana tumeiingiza kwenye mpango mkakati wetu. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.kwa kuwa ni miaka mingi sasa kila tunapoulizia kuhusiana na suala hili la Benki ya Wanawake kuanzishwa Zanzibar, mimi mwenyewe nimeulizia mara nne mpaka leo tawi hili halijafunguliwa kule Zanzibar. Na kuna mara moja niliulizia Mheshimiwa Waziri Ummy alinijibu kwamba ilitakiwa Serikali ya Zanzibar ichangie shilingi milioni 10. Nataka niulize ile shilingi milioni 10 ishalipwa ili hii benki ianzishwe au kama haitolipa hiyo shilingi milioni 10 ndio basi wanawake wa Zanzibar hatutopata benki hii? Mchakato wake ukoje? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Faida kwa kuuliza swali hili mara nyingi sana. Nina uhakika ndio maana wanawake wa Zanzibar wameendelea kumchagua kuja kuwawakilisha hapa Bungeni kwa sababu amekuwa balozi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu letu ni kwamba shilingi milioni 10 bado haijapatikana lakini azma yetu ya kufungua tawi Zanzibar iko pale pale na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan amejitolea kutupa eneo kwa ajili kufungulia tawi hilo la benki yetu pale Zanzibar; tutaendelea kufuatilia kwa ukaribu. Na nitakapofanya ziara kwa ajili ya kufuatilia tumekwama wapi kwa ajili ya tawi hili la Zanzibar nitamshirikisha Mheshimiwa Faida. *(Makofi)*

Na. 48

**Riba Kubwa Katika Mabenki**

**MHE. ISSA A. MANGUNGU** aliuliza:-

Riba kubwa katika benki zetu nchini imekuwa kikwazo kikubwa kwa wanawake na vijana kupata mikopo.

(a) Je, Serikali ipo tayari kuandaa utaratibu maalum wa riba elekezi itakayowawezesha wanawake na vijana kupata mikopo benki kwa riba nafuu ili waweze kujikwamua kiuchumi?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuziagiza benki za biashara kulegeza masharti ya dhamana kwa vijana na wanawake ambayo yanarefusha mchakato wa upatikanaji wa mikopo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala, lenye kipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mabenki na Taasisi za Fedha nchini ya mwaka 1991, Serikali iliruhusu benki binafsi kutoa huduma za kibenki hapa nchini kinyume na ilivyokuwa hapo awali ambapo huduma hizo zilikuwa zinatolewa na vyombo vya fedha vya Serikali tu. Hatua hii ilikusudia kuongeza ushindani katika sekta ya fedha na kuhakikisha kwamba huduma za kibenki zinatolewa kwa ufanisi na kwa kutegemea nguvu na mfumo wa soko huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na maombi mbalimbali juu ya kupunguza viwango vya riba ikiwa ni pamoja na Benki Kuu kuweka ukomo wa riba au riba elekezi ya mikopo. Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991, Benki Kuu imepewa dhamana ya kusimamia sekta ya fedha na usimamizi wa mabenki hapa nchini. Kama msimamizi wa mabenki, Benki Kuu kuweka ukomo wa riba sio tu inapingana na jukumu lake la msingi la kusimamia mabenki hayo, bali pia inapingana na mfumo wa uchumi wa soko huria. Kutoa maelekezo kwa mabenki kutumia viwango fulani vya riba katika biashara zao kutaifanya Benki Kuu kukosa nguvu na mamlaka ya kuyachukulia mabenki hatua endapo yatapata hasara kwa kutumia riba ambayo Benki Kuu imeelekeza. Hivyo basi, Benki Kuu haina mamlaka kisheria ya kuweka ukomo au riba elekezi itakayotumiwa na mabenki katika kutoa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya riba katika mabenki na taasisi nyingine za kifedha hupangwa kwa kutegemea nguvu ya soko, sifa za mkopaji, ushindani katika soko, gharama za upatikanaji wa fedha, mwenendo wa riba za dhamana za Serikali, gharama za uendeshaji na matarajio ya mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Benki Kuu imeendelea na jukumu lake la msingi la kuhakikisha kuwa mfumo huu unaendeshwa kwa kuzingatia sheria zilizowekwa ili kulinda maslahi ya Taifa na uchumi kwa kusimamia na kudhibiti mambo yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa ingezeko la ujazi wa fedha linaenda sambamba na mahitaji halisi ya uchumi ili kudhibiti mfumuko…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya Bunge, *please*. Waheshimiwa naomba utulivu kwenye Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** ...kuhakikisha kuwa ongezeko la ujazi wa fedha linaenda sambamba na mahitaji halisi ya uchumi ili kudhibiti mfumuko wa bei;

(ii) Ongezeko la mikopo ya mabenki haliathiri uzalishaji mali na linalingana na malengo ya ujazi wa fedha;

(iii) Soko la dhamana za Serikali linaendeshwa kwa ufanisi ili liweze kutoa riba elekezi kulingana na hali ya soko na uchumi kwa ujumla; na

(iv) Mwisho kuhimiza mabenki na taasisi zote za fedha kutumia takwimu za *Credit Reference Bureau.*

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini swali langu la msingi niliuliza ni utaratibu gani mtaweza kuwasaidia makundi maalum ya wanwake na vijana ili waweze kupata mikopo kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili nilitaka kuuliza, kwa kuwa kuna ugumu na sheria zinazoibana Serikali kusimamia riba hizi. Ni lini sasa Serikali itatusaidia kutimiza ile ahadi ya shilingi milioni 50 kila kijiji na mtaa ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu na kinamama wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi; kwa mujibu wa Sheria Benki Kuu haiwezi kutoa maelekezo ya kuleta riba elekezi ili kuweza kusimamia mabenki haya yaweze kufanya vizuri katika soko letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu shilingi milioni 50 kama ambavyo Serikali imekuwa ikisema; tunaendelea kuandaa utaratibu na kwenye bajeti yetu ya fedha ya mwaka 2016/2017 tumetenga bajeti hii na tutaweza kuitekeleza kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Sofia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa jibu la msingi la Mheshimiwa anasema Benki Kuu haiwezi kuingilia kutoa bei elekezi, tunawezaje kusaidia Benki ya Wanawake iweze kutoa riba ndogo kwa kupata ushauri kutoka kwenye Wizara yake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi jiandae Mheshimiwa Anatropia.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo, kwa mujibu wa sheria Benki Kuu haiwezi kutoa hiyo riba elekezi na napenda niseme kwamba riba hizi zilizopo ni kwa mujibu wa Sera ya Riba ya mwaka 1992. Kwa hiyo, lazima tuendane na sera tuliyoipitisha humu Bungeni ili kuweza kuhakikisha kwamba sekta ya fedha inafanya vizuri ndani ya uchumi wetu na kwa Benki ya Wanawake naamini Mheshimiwa Waziri wa Afya anaweza kulisimamia hili na kuweza kutoa riba ambayo ni nzuri, lakini hawezi kukiuka misingi ile iliyowekwa na Sera ya Riba ya mwaka 1992.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia, ajiandae Mheshimiwa Issaay Mbunge wa Mbulu Mjini.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika siku za hivi karibuni tumeshuhudia leseni za kufanya biashara katika Manisapa mbalimbali zinatolewa baada ya kupatikana kwa *tax clearance,* lakini ukweli ni kwamba sio biashara zote hasa biashara ndogo zinahitaji wakati mwingine *tax clearance,* haioni ni wakati muafaka kuweka *categories* za biashara ambazo wanaweza kupewa leseni bila hata *tax clearance* badala ya kinachofanyika sasa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili ni swali la kutoa leseni ambalo ni swali jipya ambalo tumeondoka katika riba, kwa hiyo naomba niseme tu tuna viwango ili kuweza kutoa leseni katika biashara zote zinazoendeshwa ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, kama hawajafikia ndani ya kiwango kile kinachohitajika mfanyabiashara huyo wala hatozwi na wala hapewi leseni lakini akishavuka yale malengo ya biashara yake tayari anatakiwa apewe leseni na tunasimamia kama moja ya njia za kukusanya mapato yetu.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Pamoja na mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwezesha elimu bure, upatikanaji wa madawati na pia watumishi hewa kuondolewa, naomba kufahamu, kwa sasa Watanzania wengi hasa akinamama katika

*SACCOS* zao wamekuwa na hamu kubwa ya kufanya biashara. Je, Serikali inachukua hatua gani kuwezesha *SACCOS* za akinamama katika halmashauri zote zipate hela za kutosha? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ikumbukwe kwamba sote humu ndani Waheshimiwa Wabunge sisi ni Wajumbe katika Mabaraza yetu ya Halmashauri, hivyo tunatoa asilimia tano katika mapato ya halmashauri na hayo ni katika kuimarisha vikundi vyetu vya *VICOBA* pamoja na *SACCOS* zilizopo ndani ya halmashauri zetu. Nitoe wito tu kwa Waheshimiwa Wabunge, tusimamie kwa ufasaha asilimia hizo tano za mapato ndani ya Halmashauri zetu ili ziweze kuwafikia wananchi wetu hasa akina mama na vijana ili kuweza kuinua uchumi wao.

Na. 49

**Maendeleo ya Kimasomo kwa Wanafunzi wa Kike**

**MHE. HALIMA ALI MOHAMMED** aliuliza:-

Wasichana wanaohitimu kidato cha sita wanakuwa na ufaulu mzuri lakini wanapojiunga na vyuo vya elimu ya juu ufaulu wao huanza kushuka hadi wengine hufikia kusimamishwa masomo kwa sababu ya ufaulu hafifu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wasichana katika elimu yao ya juu ili ufaulu wao uweze kuongezeka na kufikia malengo yao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Ali Mohammed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufaulu wa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu wa jinsi zote kwa kiasi kikubwa hutegemea juhudi binafsi katika kuzingatia masomo kwa kadri ya maelekezo ya uhadhiri wao. Hata hivyo, mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi wa kike kwa baadhi ya vyuo vikuu yana changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa *hostel* na hivyo kusababisha wanafunzi hao kupanga nyumba za kuishi mitaani na hivyo kutumia muda mwingi katika kutafuta usafiri na mahitaji yao muhimu ya kujikimu. Hali kadhalika, katika mazingira kama hayo, kwa namna moja au nyingine baadhi

ya wasichana hujiingiza katika vitendo vinavyoweza kuchangia kushuka kwa ufaulu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za makusudi katika kuweka mazingira stahiki kwa wanachuo zikiwemo ujenzi wa *hostel* katika vyuo vikuu ambazo umuhimu wa pekee unatolewa kwa wanafunzi wa kike na watu wenye ulemavu.

Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali imetoa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa *hostel* zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,840 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na utaratibu huo wa kuongeza mabweni utaendelea pia katika vyuo vingine.

Aidha, katika vyuo vikuu vya umma na binafsi kunatolewa huduma za ushauri na unasihi Dawati la Jinsia na Dawati la Malalamiko kwa nia ya kukabiliana na changamoto zinazoweza kuathiri ufaulu wa wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashauri wanafunzi wa kike kuzingatia masomo kwa umakini wa hali ya juu na kujiepusha na vitendo ambavyo vinaweza kusababisha ufaulu duni na hivyo kushindwa kufikia malengo waliyojiwekea.

**MHE. HALIMA ALI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa kuna malalamiko makubwa yanayohusiana na kubainika kwamba kuna rushwa ya ngono katika vyuo vyetu, jambo ambalo linapelekea wasichana wengi kupata ufaulu mdogo, lakini vilevile wasichana wengine kutoroka shule, lakini kama haitoshi kuna wasichana ambao wamefanya maamuzi ya kujiua na ushahidi upo. Sasa je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya utafiti ni kiasi gani wasichana wameathirika na rushwa ya ngono?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wasichana wetu wanapatiwa elimu kuhusiana na rushwa ya ngono?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli taarifa hizo za rushwa za ngono zimekuwa zikisikika na hata hivi karibuni ilijitokeza taarifa ya aina hiyo kwa mwalimu mmoja ambaye ameendelea kuchukuliwa hatua na niseme tu kwamba suala la kufanya utafiti ni suala jema, mimi nichukulie kwamba ntalichukua ili kujifunza tatizo hilo kwa

undani zaidi. Lakini niwaombe pia wanafunzi wa kike kutoa ushirikiano, lakini pia hata wanafunzi wa kiume wanaweza kusaidia kutoa ushirikiano kwa mambo ambayo yanajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika suala la elimu, sisi wenyewe tumekuwa tukiongea na wanafunzi kupitia wakati tofauti tofauti tunapowatembelea, lakini pia nafahamu kuna taasisi mbalimbali zinazoshughulika na masuala ya kijinsia zimekuwa zikiendelea kuelimisha. Niwaombe pia hata Waheshimiwa Wabunge mnapopata nafasi muweze pia kuongea na wasichana hao ili kuweza kusaidiana kwa pamoja kuona kwamba wote tunakuwa pamoja katika kupigana na kupambana kwamba rushwa za ngono zisipatikane katika shule na hata katika maeneo ya kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mwalimu Bilago, ajiandae Mwalimu Amina Mollel.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala la ufaulu wa watoto wa kike elimu ya juu inategemea na ufaulu wa watoto haohao wa kike kwenye shule za chini *(O-Level* na *A-level),* sasa kumekuwa na tatizo la watoto wa kike wanaobeba mimba wakiwa shuleni kuachishwa masomo, na hili tumekuwa tukilizungumza muda mrefu; ni lini Serikai italeta utaratibu hapa Bungeni, sheria itungwe ili watoto wa kike wanaobeba mimba shuleni wakishajifungua waruhusiwe kuendelea na shule? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo limezungumziwa katika nyakati tofauti tofauti, hivi karibuni pia tulipitisha mpango wa kushughulikia masuala yoyote yanayohusika na unyanyasaji kwa watoto wa kike na suala hilo limekuwa likishughulikiwa mia na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na tayari rasimu ya mwanzo ya mwongozo imeshatoka namna gani tufanye na pia niliweza kwenda kutembelea Zanzibar kuongea na Mheshimiwa Waziri kule kuweza kujua wenzetu wamekuwa wakifanya vipi katika eneo hilo, tukajifunza changamoto ambazo zilikuwa zinajitokeza kwa upande wao kwa mfano mwingine anaweza akasema anapata mimba na aliyempa mimba akasema anataka kumuoa katika mazingira kama hayo. Lakini mwisho wa yote tunaamini kwamba tutaweza kutekeleza kuona kwamba fursa zinatolewa kwa mtoto wa kike aliyepata mimba kuweza kurudi shuleni.

Changamoto tu ni namna gani, je arudi kwenye shule ileile, je unyanyapaaji utakuwepo au apewe shule maalum, ndiyo hayo ambayo wadau mbalimbali wanaendelea kutoa mawazo lakini mwisho wa yote tutatekeleza mapema iwezekanavyo.

**MHE. AMINA S. MOLELL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Katika vyuo vikuu suala la miundombinu kwa watu wenye ulemavu ni tatizo, na mfano katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni moja ya changamoto inayochangia wanafunzi wengi hasa watoto wa kike katika kwenda madarasani na hata katika suala zima la mitihani ni tatizo kwao kutokana na changamoto mbalimbali zilizopo. Je, Serikali inatoa kauli gani na hasa kwa kuzingatia chuo hiki ni kikongwe, lakini mpaka leo miundombinu bado ni tatizo na ni kikwazo kwa watu wenye ulemavu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri jibu wewe ni mzoefu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa mujibu wa sera kwa ajili ya watu wenye ulemavu, inazungumzia kuwawekea mazingira bora ya kujifunzia na kufundishiwa. Kwa hali ya sasa ni kwamba tunayo majengo ambayo yamejengwa zamani na unakuta kweli yana changamoto ya miundombinu, lakini tunachofanya ni kwamba tunashauri madarasa yale yenye wanafunzi wenye ulemavu wahakikishe yanakuwa ni yale yanayofikika, kwa mfano kama darasa lina mwanafunzi mwenye ulemavu ni vyema likachaguliwa lile ambalo liko katika *ground floor* ili mwanafunzi yule aweze kufika darasani bila usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majengo yote mapya yanayojengwa tumeagiza kwamba lazima kila jengo liwekewe miundombinu inayomuwezesha mtu mwenye ulemavu kufikia katika eneo lolote analohitaji kuishi au kujifunzia na hivyo imekuwa ikifanyika na ni rai yangu kusema kwamba hata hiyo miundombinu inayowekwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu iwe ni ile inayozingatia viwango vinavyohusika, kwa sabau sasa hivi unakuta kwamba kuna shule zinapokaguliwa ili zionyeshe miundombinu yenye ulemavu zinaweza zikaonesha tu kwamba kuna lile tuta *(rump)* limewekwa pale lakini unakuta jinsi ambavyo limewekwa lina msimamo mkubwa kiasi kwamba hata huyo mtu mwenye ulemavu anapata shida, kwa hiyo lazima kuzingatia viwango vinavyohusika katika kuweka miundombinu ya watu wenye ulemavu ikiwemo kuweka lifti. ahsante.

Na. 50

**Kituo cha Biashara cha Taifa Kilichopo London**

**MHE. SAED A. KUBENEA** aliuliza:-

Kituo cha Biashara cha Taifa - *Tanzania Trade Center* kilichopo London, Uingereza kimeripotiwa kuwa kinakabiliwa na uhaba wa fedha za kukiendesha na kulipa watumishi wake kutokana na kukosa fedha kutoka Hazina jambo ambalo linasababisha kuzorota kwa kazi za kituo hicho na kukabiliwa na mzigo mzito wa madeni.

(a) Je, Serikali inaweza kueleza hali ya kituo hicho kwa sasa ikoje?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha hali ya kifedha na kiutendaji ya kituo hicho ambacho kimesaidia sana kutangaza Tanzania nje ya nchi inakuwa imara na kufanya kazi zake kwa ufanisi?

(c)Je, ni kiasi gani cha fedha kinachodaiwa na kituo hicho na watu mbalimbali nchini Uingereza na hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO (K.n.y WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Biashara cha London kilianzishwa mwezi Oktoba, 1989 kufuatia uamuzi na maagizo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais mwaka 1989. Lengo la kituo hicho lilikuwa ni kuhamasisha biashara baina ya Tanzania na nchi za Ulaya, hususan Uingereza kwa kutangaza fursa za biashara na uwekezaji na kuvutia wawekezaji kutoka Tanzania na Ulaya kuchangamkia fursa hizo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanzishwa kwake kituo kimefanikiwa sana katika kutekeleza majukumu yake licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali zitokanazo na ufinyu wa bajeti na upungufu wa rasilimali watu. Changamoto hizo zimefanya kituo hicho kushindwa kuendana na kasi inayotakiwa ya mabadiliko duniani yanayotokana na matumizi ya teknolojia katika mifumo ya uenezaji wa taarifa na habari ulimwenguni. Ili kulinda heshima

ya Taifa na watumishi waliokuwepo katika kituo hicho, Serikali imeamua kukifunga rasmi kituo hicho na kuhamisha majukumu yake kutekelezwa na Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Mjini London.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kituo kimefungwa na majukumu yake kutekelezwa na Ofisi yetu ya Ubalozi Mjini London, Serikali itaangalia uwezekano wa kuongeza bajeti ya Ubalozi wetu ili kukidhi majukumu ya ziada yaliyoongezeka.

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Novemba, 2016 Wizara ilipokea na kulipa deni la jumla ya shilingi 129,896,360 kutoka kituo hicho cha London ikiwa ni madai ya pango, maji, simu, umeme na gharama za kufunga kituo hicho.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kituo hiki kilipoanzishwa mwaka 1989 tayari Tanzania ilikuwa na Ubalozi Mjini London ambao ulianzishwa mwaka 1961, na moja ya jukumu la kituo hiki ni kuvutia uwekezaji na hasa suala la utalii ambao unachangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa. Je, nini kilionekana kimeshindikana wakati huo kufanywa na Ubalozi na ambacho sasa kinaweza kufanywa na Ubalozi huo?

(b) Kwa kuwa kituo kimefungwa na miongoni mwa madai makubwa ambayo Serikali ilikuwa inadaiwa ni posho za wafanyakazi wa kituo waliopo London, mishahara ya wafanyakazi na kodi za nyumba za wafanyakazi wetu waliopo London.

Je, Serikali inaweza kutoa tamko gani juu ya madai ya wafanyakazi wa kituo hiki waliopo London kama wameshalipwa fedha zao na kama wamerejeshwa nchini, je, wamelipwa fedha zao za kujikimu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema yalikuwa ni maagizo ya Mheshimiwa Rais lakini pia naomba ikumbukwe kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imesema na inatekeleza sasa kuboresha na kupeleka watumishi wote katika balozi zetu zote duniani ili kuhakikisha wao wanafanya kazi husika na zinazostahiki kufanywa na balozi setu.

Kwa hiyo agizo lile halikuwa la makosa na sasa Serikali ya Awamu ya Tano imerejesha jukumu hili ndani ya Ubalozi ambalo ni moja ya majukumu yake na Ubalozi wetu unaendelea kufanya vizuri.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, niseme kama Naibu Waziri wa Fedha, madai tuliyoyapata ni shilingi 129,896,000 na ndiyo ambayo tunayalipa kama kuna watumishi ambao wanadai posho zao na haki zao zozote naomba watuletee ili tuweze kuhakiki na tutaweza kulipa kama ambavyo tumelipa deni lililotangulia.

Na. 52

**Meli ya MV Butiama**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Ni zaidi ya miaka mitano sasa tangu Meli ya MV Butiama isitishe huduma zake katika Ziwa Victoria kati ya Mwanza na Nansio (Ukerewe) hali inayosababisha shida na usumbufu mkubwa wa usafiri kwa wakazi wa Ukerewe.

(a) Je, ni lini meli hiyo ya MV Butiama itatengenezwa na kuendelea kutoa huduma kati ya Mwanza na Nansio?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta meli mpya hasa ikizingatiwa kuwa meli ya MV Clarius imechakaa sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Kuna swali moja tumeliruka tutarudi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.6 katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ili kufanya matengenezo makubwa ya meli ya MV Butiama iliyositisha kutoa huduma zake tangu mwaka 2010 kutokana na hitilafu kubwa ya injini zake. Zabuni kwa ajili ya kupata mkandarasi wa kufanya kazi hiyo zilikwishatangazwa na sasa kazi ya uchambuzi wa kina inaendelea. Matarajio yetu ni mkandarasi kuanza ukarabati huo mwezi Machi, 2017 na kumaliza mwezi Novemba, 2017

(b) Kuhusu mpango wa kujenga meli mpya kwa ajili ya kutoa huduma kati ya Mwanza na Nansio, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuimarisha huduma ya usafiri wa majini katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Baada ya MV Butiama kusita kufanya shughuli zake pale kulikuwa na meli ya MV Clarius ambayo nayo imesimama kufanya kazi na kuna taarifa kwamba itatengenezwa na watu wa *MSCL* ili iendelee kufanya shughuli zake lakini meli hii imekuwa chakavu, inahitaji matengenezo makubwa. Sasa kwa kuwa wenye jukumu la kutengeneza ni *MSCL* wenyewe lakini wanatatizo kubwa sana la fedha. Je, Serikali sasa haioni kwamba kuna haja ya kuwasaidia hawa *MSCL* kwa kuwapa fedha za kutosha ikiwepo pamoja na pesa za *OC* ili waweze sasa kutengeneza meli hii iweze kufanya kazi katika mazingira mazuri ikizingatiwa ni ya muda mrefu na katika hali halisi ya sasa kumsafirisha abiria kwa saa tatu majini akiwa amekalia viti vya mbao si kitu kizuri sana?

Swali la pili; ratiba za meli kutoka Mwanza kwenda Ukerewe zina mahusiano ya moja kwa moja na ratiba za vivuko vingine. Kwa mfano, Kivuko cha MV Nyerere kutoka Mgolola kwenda Ukala sasa kumekuwa na matatizo ya kutowiana kwa ratiba kiasi kwamba wasafiri wanakaa muda mrefu. Kwa mfano, akifika Nansio anakaa kwa saa tano ili apate usafiri mwingine wa kumpeleka kisiwa cha Ukala. Je, Serikali haioni sababu za msingi za kuainisha ratiba ya vivuko hivi ili kuondoa gharama kubwa ambazo wasafiri wanazipata wanapokuwa safarini? Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la kwanza, nakubaliana naye kwamba kuna haja ya kuwaongezea uwezo wa kifedha ikiwa ni pamoja na fedha za *OC* ili *MSCL* waweze kutekeleza wajibu wao na hasa katika kuikarabati meli hii ya MV Clarius.

Kwa upande wa pili, ratiba nimepokea ombi lake, nitawasiliana na taasisi hizi mbili zinazohusika, TEMESA pamoja na *MSCL* waangalie kama kuna uwezekano wa kurekebisha ratiba zao, lakini kwa mazingira ninayoyafahamu, tukirekebisha kutakuwa na tatizo vilevile la kuwasumbua wale wa Ukala

wakakaa muda mrefu sana kusubiri MV Clarius ifike, ilete abiria. Tutaangalia kama kutakuwa na uwezekano wa kutafuta njia nyingine kuweza hili kuliweka sawa ili wananchi waweze kunufaika na huduma hizo mbili za kivuko pamoja na Meli.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, Waziri amekubali ratiba zenu zote atawatembelea. Swali la Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Justus Nditiye.

Na. 51

**Uhitaji wa Kiwanda cha Sukari - Kibondo**

**MHE. ENG.ATASHASTA J.NDITIYE** aliuliza:-

Nchi yetu bado ina upungufu mkubwa sana wa sukari na kwa kuwa Wilayani Kibondo kuna ardhi oevu kwenye Bonde la Mto Malagarasi na Lupungu ipatayo ekari 52,000 na wananchi wako tayari kutoa ushirikiano kwa matumizi ya ardhi hiyo.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta mwekezaji wa kiwanda cha sukari katika eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO (K.n.y WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Justus Nditiye, Mbunge wa Muhambwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuwa katika Nchi yetu kuna upungufu wa sukari kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Viwanda vyetu vyote kwa pamoja vina uwezo wa kuzalisha tani 300,000 za sukari ya mezani na hakuna uzalishaji wa sukari ya viwandani ilihali mahitahi ya Sukari kwa matumizi ya nyumbani na viwandani ikikadiriwa kuwa tani 610,000 hivyo uhitaji wa uwekezaji katika sekta hiyo ya viwanda vya sukari ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa upungufu huo, Serikali imeshatambua na inaendelea kuainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari katika Mikoa mbalimbali ikiwemo Morogoro, Mara, Pwani, Songwe na Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Bonde la Mto Malagarasi lililopita katika vijiji kumi vya Kasaya, Kibuye, Kigina, Kukinama, Kumsenga, Kumshwabure, Magarama, Nyakasanda, Nyalulanga na Nyarugusu ni moja ya maeneo ambayo Serikali imeyaainisha kwa ajili ya kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari. Tayari Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo kwa kushirikiana na Wananchi na Kampuni ya *Green Field Plantations* imefanya vikao vya uhamasishaji katika vijiji vyote kumi na hivi karibuni wataanza taratibu za upimaji wa ardhi. Mradi huu utahusisha jumla ya hekta 25,000 sawa na ekari 61,776 ambapo Kampuni ya *Green Field Plantations* italima hekta 20,000 na itawasaidia wakulima wadogo pembejeo na teknolojia ili waweze kulima hekta 5,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimshukuru Mheshimiwa Mbunge na Mkuu wa Wilaya ya Kibongo kwani barua walizotuma Wizarani ziliongeza kasi hii, tuendelee kushirikiana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nditiye.

**MHE. ENG. ATASHASTA J.NDITIYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana, jina langu ni Atashasta Justus Nditiye au *Engineer* Nditiye inatosha. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wazawa *Green Field Plantations* walianza mchakato wa kufuatilia eneo hilo toka mwezi wa pili mwaka jana na tuliwapa ushirikiano namshukuru sana Mkuu wa Wilaya pamoja na wananchi wa Jimbo la Muhambwe, lakini ilipofika mwezi wa nane ameondoka mpaka sasa hivi ninapoongea hajarudi. Tunadhani ni muhimu sana tupate mwekezaji *competitor* kwa ajili ya ku-*speed up* suala la yeye kuja kufanya shughuli za uwekezaji kama tunavyotarajia ili wananchi wasije wakakata tamaa. Ni lini Serikali inafikiria kutafuta mwekezaji mwingine ikiwezekana hata wa kutoka nje ili kuweza kuwekeza katika Kiwanda cha sukari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika kuelekea kwenye sera ya viwanda katika nchi yetu tuna wabunifu wengi sana na katika Wilaya yetu ya Kibondo kwa mfano, kuna kijana amebuni magodoro yanayotumia mifuko ya *plastic* na kila alipojaribu kuwasiliana na *COSTECH* kwa ajili ya ushauri wamekuwa hawampi ushirikiano wa kutosha. Ni lini Serikali inajipanga kuwaongezea uwezo *COSTECH* ili wanapopata maswali kutoka kwa wabunifu wadogo wadogo waweze kuwatembelea na kuwapa ushauri? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata taarifa kwamba hapa mwekezaji aliondoka na hajarejea na kama alivyosema Serikali yetu ya Awamu ya Tano ni Serikali ya viwanda. Tutamleta mwekezaji mwingine kama alivyosema na siyo mmoja bali wawili, watatu kuongeza *competition* na ufanisi hilo nimelichukua na Serikali inalifanyia kazi, watakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubunifu na *COSTECH;* kwanza nikiri kwamba huyo mwanafunzi na nimwambie Mheshimiwa Mbunge mwanafunzi huyo ni mwanafunzi wangu niliyemfundisha *Masters* Chuo Kikuu Mzumbe. Namfahamu na tulimfundisha na sasa anaendelea na ubunifu huo na *COSTECH* pamoja na Chuo Kikuu Mzumbe tumepanga kumuendeleza mwanafunzi huyo pamoja na wabunifu wote wanaoibuka ndani ya Nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gashaza. Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niongezee kwa hoja ya msingi iliyozungumzwa. Mwekezaji huyo katika Bonde la Malagarasi aliyeko Muhambwe pia yuko mwekezaji mwingine anaitwa *Kigoma Sugar* yuko Bonde la Malagarasi upande wa Wilaya ya Kasulu. Wote hawa inaonekana wameshindwa na kama sisi Kasulu tunataka ardhi yetu ekari 100,000 tumnyang'anye sasa tuweze kutafuta mwekezaji mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba basi juhudi hizo za kutafuta mwekezaji zifanyike kote Muhambwe na Wilaya ya Kasulu kwa sababu wote wako kwenye Bonde hilo la Malagarasi. Kwa hiyo, swali langu ni kuomba tu Serikali wawekezaji wote hao wa zamani wameshindwa, hawapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Wawekezaji wameshindwa tafuta Wawekezaji wapya ndiyo jibu lake tu hilo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme siyo kwa Wilaya ya Muhambwe na Kasulu tu, niseme kwa Wilaya zote na maeneo yote ya uwekezaji na hasa uwekezaji kwa ajili ya kilimo cha miwa pamoja na viwanda vya sukari. Naomba tupatiwe taarifa ili Serikali tuchukue hatua mara moja kama walipewa ardhi basi naamini Waziri wa Ardhi yupo makini tutaichukua ardhi hiyo na kumpa mwekezaji mwingine.

Kwa hiyo, niombe Waheshimiwa Wabunge tupate taarifa ya wawekezaji wote wanaonekana ni wababaishaji na wameshindwa kufanya kazi, tushirikiane na Tanzania ya viwanda inawezekana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yussuf Salim.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri. Pamoja na Tanzania kwamba tuna maeneo mengi mazuri kwa ajili ya kilimo cha miwa na viwanda tulivyonavyo vya sukari na pamoja na mbwembwe nyingi za Serikali ya Awamu ya Tano iliyonazo kukuza uchumi, lakini bado bei ya sukari katika nchi yetu ni kubwa sana na uwezo wa wananchi wetu ni mdogo. Je, ni lini Serikali itaangalia sasa uwezekano wa kupunguza bei ya sukari ili ifikie angalau pale tulipokuwa na tatizo la sukari wananchi wetu waweze kumudu kununua sukari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikanushe Serikali ya Awamu ya Tano siyo ya kibabaishaji tunafanya kazi na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa tathmini ya mwezi Januari viwanda vyetu vya ndani vimeshazalisha asilimia 86 ya uhitaji wa sukari ndani ya nchi yetu, kwa hiyo, ninauhakika kwa *demand* na *supply* nguvu hii tayari tukishaweza kuzalisha asilimia mia moja bei ya sukari itashuka. Tukumbuke tu Waheshimiwa Wabunge nchi hii ni huru na inafuata soko huria, hatuwezi kuingilia hilo na turuhusu sasa Viwanda vyetu viweze kuzalisha asilimia mia moja na bei ya sukari itashuka na wananchi wetu watafurahia Serikali yetu ya Awamu ya Tano utendaji wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 53

**Serikali Kuwasaidia Walimu Kupata Mikopo**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia walimu kupata mikopo ya muda mrefu na yenye riba nafuu ili waweze kujenga nyumba bora za kuishi?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa viti maalum kama ifuatavyo:-

Serikali inao Mfuko wa mikopo ya nyumba kwa watumishi wa Serikali inaowezesha watumishi kupata mikopo ya nyumba wakiwemo walimu. Mikopo hiyo inaweza kurejeshwa ndani ya miaka 30 lakini kabla ya mtumishi kustaafu. Masharti makuu ya kupata mkopo huo ni mhusika kuwa na hati ya kumiliki ardhi pamoja na uwezo wa kurejesha mkopo anaohitaji na kubakia na angalau theluthi moja ya mshahara wake kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 1995 mpaka 2016 jumla ya walimu 95 walipata mikopo yenye jumla ya shilingi 892,254,796.50. Walimu hao ni kutoka Mikoa ya Dodoma, Tabora, Mwanza, Morogoro, Pwani, Bukoba, Musoma na Dar es Salaam.

Aidha, Serikali kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Bima ya Afya pamoja na Shirika la Nyumba la Taifa imeanzisha *Watumishi Housing Company* mwaka 2013. Lengo kuu la kuanzisha kwa Kampuni ya *Watumishi Housing* ni kujenga nyumba za gharama nafuu kwa ajili ya kuuzia watumishi wa umma na mashirika yake. Kampuni hii tayari imefanya makubaliano na Benki tano za biashara ili zitoe mikopo ya kununua nyumba kwa watumishi kwa masharti nafuu. Benki hizo ni Azania, *CRDB, NMB, BOA* na *Exim.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Watumishi Housing Company* imeingia pia makubaliano na Mamlaka ya Elimu ya Sekondari kujenga nyumba zipatazo 240 katika mikoa 23 ya Tanzania Bara. Hivi sasa ujenzi wa nyumba 90 kwa ajili ya walimu unaendelea katika Mkoa ya Mtwara - Nanyumbu, Tandahimba na Liwale, Mkoa wa Morogoro - Kilosa, Jiji la Tanga - Mkinga, Pwani - Msata na Rufiji pamoja na Jiji la Dar es Salaam - Wilaya ya Ilala eneo la Mvuti na Singida eneo la Mkalama na pia katika Mikoa ya Simiyu na Shinyanga.

Aidha Wizara yangu kupitia *mortigage financing* chini ya *TMRC* na *BOT* imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 374,515,110,203 kwa wananchi 4,065 wakiwemo walimu kupitia mabenki 54 yaliyopo nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na juhudi za Serikali ambazo nazipongeza sana lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ina mfuko ambao unawapa watumishi wa Serikali mikopo ya muda mrefu ya nyumba, watumishi hao ni pamoja na walimu. Lakini naweza kusema kwamba mfuko huo haupo wazi kwa walimu wote Tanzania na wala kwa watumishi wengine. Je, Serikali imejipanga vipi sasa katika kutoa elimu juu ya mfuko huu ambao unatolewa mikopo yaani mikopo inayotolewa kwa Serikali imejipanga vipi kutoa elimu kwa walimu na watumishi wengine wa Serikali ili waweze kufaidika na mkopo huo wa nyumba wenye gharama nafuu? *(Makofi)*

Swali la pili; Kwa kuwa Serikali imeonyesha wazi dhamira ya kutaka kuwasaidia walimu na watumishi wengine kupitia Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii lakini mifuko hii inajenga nyumba zenye gharama kubwa sana kuanzia milioni 50 kwenda juu mpaka milioni 75 gharama ambazo mwalimu wa kawaida hawezi kuzimudu.

Je, kwa nini Serikali sasa isiwashawishi Mifuko hiyo ya Jamii ikatoa mikopo ya fedha taslimu kwa walimu waweze kujijengea nyumba zao wenyewe kwa gharama nafuu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza alitaka tu tutoe elimu kwa ajili ya walimu kufahamu kwamba kuna mfuko ambao unawawezesha wao kuweza kupata mkopo kwa ajili ya nyumba.

Naomba niseme kwamba mfuko huu tulionao Serikalini siyo kwa ajili ya walimu tu, ni mfuko kwa ajili ya watumishi ambao wanaweza kukopeshwa kupitia mfuko wa Serikali.

Kwa hiyo, elimu ambayo tunaweza kuitoa ni pamoja na sisi wenyewe Wabunge kuweza kutoa elimu hii katika Halmashauri zetu kupitia vikao vyetu vya Mabaraza ya Madiwani ili waweze kuwafahamisha pia walimu huko waliko pamoja na watumishi wengine wa kawaida kwamba wanaweza wakapata fursa hiyo kupitia Serikalini. Kwa hiyo, hili ni la kwetu tumelichukua pamoja lakini tushirikiane wote ili kuweza kufikisha ujumbe huu.

La pili, dhamira ya hizi Hifadhi za Jamii katika ujenzi wa nyumba anasema zina gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba nimezungumzia suala la *Watumishi Housing* ambalo ni Shirika ambalo limeanzishwa na Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii na Shirika hili linatoa nyumba zake kwa gharama nafuu wala hazina gharama kubwa sana isipokuwa masharti yake yalipo ni lazima kwanza uwe na dhamana ambayo inaweza ikakusaidia katika kuweza kurudisha mkopo ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mabenki yale ambayo yanatoa mkopo huu *once* ukishakubaliana na benki kwamba sasa unataka kuchukua mkopo, Shirika ndiyo linawasiliana na wewe katika hali halisi ya kutaka kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba nyumba zinazojengwa ziko katika *size* mbalimbali, kwa hiyo bei ya nyumba na gharama yake itategemea pia na ukubwa wa nyumba. Kwa hiyo, tunapokuwa na mashirika mengi yanayofanya shughuli za ujenzi, ushindani utakuwepo lakini na ubora wa nyumba utakuwepo. Kwa hiyo, itakuwa ni juhudi ya mtu mwenyewe na kuweza kuchagua ni shirika lipi unataka wewe likujengee nyumba katika gharama ile ambayo unaweza, lakini nyumba ziko za gharama nafuu kulingana na vipato vya wananchi wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ningependa tu kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba pamoja na mikakati hii mizuri ambayo Serikali inayo katika kuwasaidia watumishi wakiwemo Walimu kupata mikopo ya muda mrefu, sasa ni lini Serikali itazishauri au itazielekeza hizi Halmashauri zetu zote nchini kuhakikisha kwamba kila zinapofanya zoezi la upimaji wa ardhi Walimu wanapewa kipaumbele katika kupata maeneo ambayo pamoja na mkopo watakaopata basi ardhi isiwe kikwazo kwao na waweze kumudu ujenzi huu wa sasa? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake anataka kujua ni lini Walimu watapewa kipaumbele kuweza kupewa viwanja pale ambapo Halmashauri zinapima. Ninachoweza kusema tu ni kwamba mipango ya upimaji katika Halmashauri

zetu tunaiandaa wenyewe katika vikao vyetu. Kwa hiyo, katika kutoa vipaumbele kwenye kupima, nadhani kwa sababu tumeona kwamba Walimu wana tatizo kubwa ni jukumu letu pia kuhakikisha kwamba tunapopima maeneo basi tunatenga kwa ajili ya watumishi na si Walimu tu kama ambavyo tunavyofanya katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pale ambapo panakuwa pana hitaji kubwa, ni jukumu letu sisi wenyewe kuweza kusema sasa tunapima viwanja sehemu fulani tunawapa watumishi. Kwa upande wa Mwanza, tayari kuna viwanja zaidi ya 500 ambavyo vilipimwa kwa ajili ya watumishi wote kwa ujumla na sio Walimu tu. Kwa hiyo hii inawezekana inaweza kufanyika, ni mipango ya Halmashauri husika.

**MWENYEKITI:** Ahsante! Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Kibamba.

Na. 54

**Fidia kwa Wananchi wa Mloganzila**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza:-

Wananchi wa Mloganzila waliopisha ujenzi wa *MUHAS* hawakulipwa fidia ya ardhi au angalau "mkono wa kwaheri" na wapo wenye madai ya 'kupunjwa' fidia ya maendelezo:-

(a) Je, ni lini wananchi hao watapewa malipo yao kama Serikali ilivyoahidi?

(b) Je, ni kwa namna gani Serikali imeshughulikia madai ya mapunjo ya fidia ya maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Kibamba, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya kuwalipa fidia ya hisani au mkono wa heri iliyotolewa na Serikali mnamo tarehe 20 Mei 2015 italipwa baada ya kupata fedha. Malipo haya hayajafanyika kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ililipa kiasi cha Sh. 8,067,904,700 kwa ajili ya fidia ya maendelezo katika ardhi kwa wananchi 1,919 katika kipindi cha mwaka 2008 mpaka 2010. Aidha, mwaka 2011 Serikali ilitenga kiasi cha sh. 1,610,374,700 kwa ajili ya fidia ya wananchi 619 waliosalia. Fedha hizi zililipwa kama fidia ya maendelezo kwa wananchi waliokuwa wamewekeza ndani ya shamba ambalo lilikuwa mali ya Serikali. Serikali haidaiwi mapunjo kwa kuwa fidia ilishalipwa kwa mujibu wa Sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri katika sehemu (a) ya swali hajajibu swali. Niliuliza ni lini hii fidia ya hisani italipwa lakini hajajibu ni lini na Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi anafahamu kwamba jambo hili ni la muda mrefu. Mwaka 2009 aliyekuwa Waziri wa Ardhi wakati huo Chiligati aliahidi wangelipwa milioni tisa, hawakulipwa mpaka mwaka 2015 wananchi wakaandamana kwenda Wizarani, Serikali ikaahidi kulipa milioni mbili badala ya ile milioni tisa. Sasa sehemu (a) ni vyema Waziri akajibu ni lini hasa Serikali italipa hii fidia. Au inataka sasa kwa kuwa wakati ule tuliandamana kwenda Wizara ya Ardhi sasa tuandamane kwenda kwa Mheshimiwa Magufuli ajibu ni lini hasa hii fidia italipwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu (b) ya swali. Serikali imesema kwamba haidaiwi mapunjo ya fidia ya maendelezo. Hili jibu la Serikali ni jibu la uongo. Mwezi Aprili mwaka 2014 tulikuwa pamoja na Rais Dkt. Jakaya Kikwete pale Mloganzila, jambo hili likajitokeza na Rais akataka vielelezo tukamkabidhi na sio Rais tu, Wizarani kuna nakala za fomu za watu ambao kimsingi walipunjwa fidia za maendelezo kinyume kabisa na thamani halisi ya mali zilizokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu Serikali imejibu uongo hapa Bungeni; je, Serikali iko tayari kurudi kwenda kuchunguza malalamiko ambayo yako tayari Wizarani? Vielelezo vyote viko Wizarani na ikalipa fidia ya maendelezo pamoja na kujibu maswali kwa ukweli? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nilijibu swali lake (a) analosema kwamba sikulijibu. Nadhani katika majibu ya awali nilipojibu sehemu (a) na (b) nimesema

kwamba watalipwa baada ya kupatikana fedha na hii haijalipwa kutokana na ufinyu wa pesa sasa siwezi kuweka *commitment* ya Serikali hapa...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Swali ni lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, muda wako subiri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** ….. wakati natambua wazi kwamba haya mambo yanakwenda kwa bajeti…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Jibu swali, swali ni lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** ….. kama halipo katika bajeti siwezi kukwambia ni kesho tutalipa au kesho kutwa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Bajeti ya lini sasa?

**MWENYEKITI:** Unajua Mheshimiwa Mnyika unakaa nje ya Bunge siku nyingi sana, ukirudi hujui kuna Kanuni humu ndani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Lissu kaa chini, Mheshimiwa Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nilitaka kutoa ufafanuzi huo. Kwa sababu ukisema unaweka *commitment* leo na pesa haijapatikana, atakuja kusema baadaye kwamba tumedanganya Bunge na sisi hatutaki kulidanganya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu pia hakuna mahali ambapo tumedanganya Bunge. Kwanza kwa sababu hata hao unaowasema wamekuwa wakija sana ofisini wakidai madai yao na tunawaambia nini kilikwisha fanyika na mpaka sasa kitu gani ambacho wanadai. Lakini ukiangalia pale hakuna mapunjo ambayo wanatakiwa walipwe isipokuwa ile iliyosemwa ya hisani ambayo tunasema watakuja kulipwa baada ya kupatikana ndiyo hiyo ambayo Serikali inaifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hatuwezi kusema kwamba kuna watu walipunjwa na ukizingatia kwamba eneo lile ambalo watu wanalipigia kelele bado ilikuwa ni sehemu ya Serikali. Ilikuwa ni viwanja vya Serikali isipokuwa

kulikuwa na vijiji vilivyokuwa vinatambulika mle na ndiyo maana Serikali ikawa tayari kulipa fidia ya maendelezo katika yale maeneo waliyokuwa nayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Mnyika, kama huridhiki na swali, Kanuni ziko *very clear.* Kanuni 45 ukishuka mpaka fasili ya (3) inakupa fursa kuiomba tena Serikali kama hujaridhika. Huna haja ya kujibu wakati Waziri anaongea.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Muda wetu umekwisha sana. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu.

Na. 55

**Hitaji la Kituo cha Polisi Wilaya ya Maswa**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Wilaya ya Maswa ni moja ya Wilaya kongwe hapa nchini, lakini haina kituo cha Polisi cha Wilaya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayo Wilaya 162 na kati ya hizo tumefanikiwa kujenga vituo vya Polisi katika Wilaya 97. Serikali ina mpango wa kujenga vituo vya Polisi katika Wilaya 65 zilizosalia kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, tumepata jengo ambalo litafanywa kuwa kituo cha Polisi cha Wilaya wakati tukisubiri utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa vituo vya Polisi nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira hadi hapo hali ya fedha itakapokuwa nzuri tutakamilisha ujenzi wa vituo vya Polisi katika Wilaya zilizosalia Maswa ikiwa miongoni mwao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya kuridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kituo cha Polisi cha Maswa ni cha muda, kiko kwenye hifadhi ya barabara ambapo kinaweza kikabomolewa wakati wowote ili kupisha ujenzi wa barabara; je, ni lini Serikali itajenga kituo cha kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa vile tatizo lililoko Wilaya ya Maswa liko sawa kabisa na tatizo lililoko Wilaya ya Itilima, hakuna kituo cha Polisi cha Wilaya; je, ni lini Serikali itajenga kituo cha Polisi cha Wilaya ya Itilima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa maswali umekwisha. Hili ndilo swali la mwisho na ndiyo majibu ya mwisho.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther alitaka kujua ni lini Serikali itajenga kituo cha Polisi Itilima pamoja na Kituo cha Kudumu Maswa. Naomba nimjulishe Mheshimiwa Esther kwamba kama nilivyojibu katika swali langu la msingi ni kwamba tunatambua upungufu wa vituo 65 nchi nzima katika Wilaya 65 ikiwemo Maswa na Itilima. Kwa hiyo, pale ambapo tutafanikiwa kupata fedha za ujenzi huu tutatoa kipaumbele katika maeneo hayo kama ilivyo maeneo mengine ya Wilaya zilizobakia 65 ambazo hazina vituo vya Polisi mpaka sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwisha na maswali yetu yamekwisha, sasa nina matangazo, nitaanza na matangazo ya wageni.

Wageni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika ni wageni kumi wa Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe ambao ni viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wakiongozwa na Dkt. Vincent Mashinji, Katibu Mkuu wa CHADEMA. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni. Karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya UKIMWI, Bajeti na Huduma na Maendeleo ya Jamii kuwa kutakuwa na semina kuhusu afya na uzazi na watoto wachanga kesho Jumamosi saa 8.30 mchana kwenye ukumbi wa Morena *Hotel*. Semina hii imeandaliwa pamoja na Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)* na Bunge letu. Aidha, Mheshimiwa Spika, atakuwa mgeni rasmi wenye ufunguzi wa semina hii.

Pamoja na Kamati hizi tatu, Wabunge wanachama wa Vyama vya Idadi ya Watu Utepe Mweupe na *TAPAC* pia wanaalikwa kushiriki.

Katibu wa Kamati ya Utendaji wa *TAPAC* anaomba kuwatangazia wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa *TAPAC* kwamba leo tarehe 3 saa 7.00 mchana mara baada ya Bunge kuahirishwa kutakuwa na kikao kifupi cha Kamati ya Utendaji ya *TAPAC,* kwa ajili ya kupitia mpango kazi wa *TAPAC*. Kikao kitafanyika katika mgahawa wa Bunge.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa Kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo! Mwongozo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Ahsante! Waheshimiwa tazameni Kanuni. Nikishamwita Katibu, nimesimama, nimekaa nimemwita Katibu…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umekaa haraka sana, hujatupa nafasi hata kidogo.

**MWENYEKITI:** Kuwa *alert* kwenye shughuli zako za Kibunge…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakuwa kama tunavamiana, haraka haraka umekaa hapo. Naomba mwongozo wako!

**MWENYEKITI:** Hebu kaeni chini!

Katibu!

Tunamwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti endelea, nusu saa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA– MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupa tena afya njema kwa mwaka huu wa 2017. Pili, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuongoza kwa weledi na umahiri Bunge hili la 11. Kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria tunawatakia afya njema katika Mwaka 2017 ili mzidi kutimiza majukumu yenu kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekitu, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ina wajibu wa kuwasilisha Taarifa yake ya Mwaka katika Bunge lako Tukufu kwa madhumuni ya kujadiliwa kabla ya Mkutano wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii ya Mwaka inawasilishwa kwa mara ya kwanza tangu kuundwa kwa Kamati hii Mwezi Januari 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti tarifa hii ina sehemu kuu nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majukumu ya Kamati. Kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya 6(2) fasili ya 7(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ni moja kati ya Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta inayosimamia Wizara tatu ambazo ni, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu) na Wizara ya Katiba na Sheria. Majukumu ya Kamati hii ni pamoja na:-

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(iii) Kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia na mbinu mbalimbali zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati. Ili kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zinazoendana na matakwa ya…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa hizi ndiyo maelekezo ya Serikali kuzifanyia kazi. Sasa naona mnatangatanga sana na Kanuni ya 66 hairuhusu mtu kutoka kwenye kiti chake kwenda kiti kingine. Naomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA– MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti utaniongezea muda.

Kanuni ya 117(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 kuhusu Ushirikishaji wa Wadau na kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na 2016/2017 pamoja na njia zilizotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia zilizotumika ni pamoja na kukutana na kufanya vikao vya pamoja kati ya Kamati na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2015/2016 *(Budget Performance Reports)* pamoja na Taarifa za utekelezaji za Wizara na Taasisi hizo kwa kipindi cha Nusu Mwaka *(Mid-Year Performance Reports)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ni kupata ufafanuzi kutoka kwa Mawaziri ili kupata maelezo kuhusu matukio maalum yaliyojitokeza katika kipindi hiki katika Wizara na Taasisi inazozisimamia. Kwa mfano, katika Mkutano wa Tano, Bunge la 11, Kamati ilipokea taarifa maalum kutoka Kitengo cha maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu namna Serikali ilivyokabiliana na changamoto zilizojitokeza katika janga la tetemeko la ardhi Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ni kufanya ziara kwa kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za

Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 ili kujiridhisha na ufanisi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuwaalika wadau mbalimbali kwa ajili ya kutoa maoni yao kwenye Miswada ya Sheria iliyotekelezwa kwenye Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) na 117(8) (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kuwasilisha mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahsusi zilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati za Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Taasisi mbalimbali za Serikali na Asasi za Kiraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizofanyika. Mara baada ya kuteuliwa, Wajumbe wa Kamati walifanya uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa mujibu wa Kanuni ya 116(10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kwa kumteua Mheshimiwa Mchengerwa Mohamed ambaye ndiye mimi niliyesimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Najma Giga kuwa Makamu Mwenyekiti katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imetekeleza shughuli zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza, mafunzo kwa wajumbe kuhusu kazi na majukumu ya Kamati. Kwa kuzingatia kuwa Wajumbe wa Kamati ni wapya, ilionekana ni vema kuwapatia mafunzo kuhusu kazi na majukumu ya Kamati, Mafunzo hayo yalitolewa tarehe 21 Januari, 2016.

Baada ya kupatiwa mafunzo hayo, tarehe 23 Januari, 2016 wajumbe waliandaa Mpango Kazi wa Kamati kwa kipindi cha Januari hadi Juni, 2016. Lengo la mafunzo lilikiwa ni kujenga uelewa wa Wajumbe na kufahamu kazi na majukumu ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafunzo kwa Wajumbe kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara. Kwa kuzingatia umuhimu wa majukumu ya Kamati ya kuzisimamia Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu) na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Wajumbe walipatiwa mafunzo ili waweze kufahamu kwa kina

Muundo na Majukumu ya Wizara pamoja na Sera na Sheria mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara hizo. Mafunzo haya yalifanyika Tarehe 8 hadi 14 Februari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara. Kamati ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na taasisi zake. Taarifa hizo ni kama zifuatazo:-

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka, Shule ya Sheria Tanzania, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Tume ya Marekebisho ya Sheria, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Tume ya Utumishi wa Mahakama

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu) kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zifuatazo:-

Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Ofisi ya Msajili Mkuu wa Vyama vya Siasa, Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi, Mamlaka ya Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii *(SSRA)*, Baraza la Taifa la Uwezeshaji, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Shirika la Tija la Taifa, Tume ya Usuluhishi na Utatuzi, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)* kuhusu utekelezaji wa uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma na mwisho kabisa ni Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa Wizara na taasisi zake lilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyoainishwa katika Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Baada ya kujadili Taarifa hizo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutembelea na kukagua utekekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara na taasisi inazozisimamia ambayo ilitengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Miradi iliyokaguliwa ipo chini ya Vifungu vifuatavyo:-

Fungu 37 (Mradi Na. 6575) - Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 31(Mradi Na. 6389) - Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) na Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kuchambua Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane 7(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati yangu ilichambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara na taasisi inazozisimamia kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa ajili ya kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yanaelezewa kwa kina katika sehemu ya pili na tatu ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, sita, uchambuzi wa Miswada ya Sheria. Kamati yangu ilijadili na kuchambua Miswada ya Sheria mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1), ikisomwa pamoja na nyongeza ya Nane 7(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017, Kamati ilichambua na kujadili Miswada ifuatayo:-

(i) Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 6 wa Mwaka 2016; Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 7 wa Mwaka 2016

(ii) Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa, Na. 4 wa Mwaka 2016;

(iii) Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 3 wa Mwaka 2016 ;

(iv) Muswada wa Sheria ya Huduma za Sheria, Na. 14 wa Mwaka 2016 na;

(v) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 4 wa Mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha Bunge la Bajeti wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Moja, Kamati iliwasilisha taarifa tatu kuhusu uchambuzi wa bajeti za Wizara na taasisi inazozisimamia kama ifuatavyo:

(i) Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Ofisi yaWaziri Mkuu;

(ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Ofisi yaMakamu wa Rais; na

(iii) Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili, Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati. Maelezo ya jumla, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yatakayotolewa taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa ni changamoto ambazo zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kuleta tija kwa Taifa. Masuala hayo ni pamoja na:-

(a) Masuala ya Ujumla ambayo ni:-

(i) Semina na Mafunzo
(ii) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

(iii) Ufinyu na ukomo wa bajeti kwa taasisi zote ambazo Kamati inazisimamia;

(iv) Uchambuzi wa Miswada;

(v) Ufinyu wa muda kwa Kamati kwa ajili ya kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo;

(vi) Kukosekana kwa umakini katika baadhi ya miradi inayoendeshwa kwa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi *(Public Private Partnerships)*.

(b) Ofisi ya Makamu wa Rais ( Muungano)

Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, kujengwa katika viwango visivyoridhisha.

(c) Wizara ya Katiba na Sheria;

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) kutengewa fedha kidogo sana katika kila bajeti kwa miaka zaidi ya mitatu mfululizo hali inayosababisha Tume kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

(d) Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu;

(i) Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma kutengewa fedha kidogo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

(ii) Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kutengewa Fedha kidogo katika mwaka wa fedha 2015/2016 na hivyo kuathiri utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyoainishwa hapo juu.

*Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati, Semina na Mafunzo. Kamati katika kipindi cha Januari 2016 mpaka Januari 2017 ilipatiwa Semina pamoja na mafunzo kutoka kwenye taasisi na asasi mbalimbali za kiraia kwa ajili ya kujenga uelewa wa masuala mbalimbali ya kisheria. Taasisi ambazo zimetoa mafunzo kwa Kamati katika kipindi hiki ni kama ifuatavyo:-*

*(i) Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa chini ya Mradi wake wa* Legislative Support Program (UNDP-LSP);

*(iii) Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake* (UN-Women) *kwa kushirikiana na Umoja wa Wabunge Wanawake wa Tanzania (TWPG);*

*(iii) Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA);*

*(iv) Jukwaa la Uchambuzi wa Sera Tanzania;*

*(v) Shirika la Uwezeshaji wa Watoa Msaada wa Kisheria;*

*(vi) Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania;*

*(vii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu;*

*(viii) Chama cha Mawakili Tanganyika;*

*(ix) Mtandao wa Mashirika Yanayotoa Msaada wa Kisheria Tanzania;*

*(x) Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi;*

*(xi) Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi* (National Economic Empowerment Council) *katika mradi wa* ''Host Community Engagement in Local Content'' *(Ushiriki wa Jamii katika Uwekezaji).*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafunzo yaliyotolewa, Wajumbe wamejengewa uwezo kuhusu mambo ya sheria. Aidha, katika mafunzo kuhusu sheria, sera, taratibu, majukumu na muundo wa taasisi wanazozisimamia yaliyotolewa tarehe 21 Januari hadi 8 Februari, 2016, Wajumbe walipata uelewa mpana uliowasaidia katika uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazozisimamia.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) na kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa Wizara na taasisi inazozisimamia kama ifuatavyo:-

(a) Ofisi ya Waziri Mkuu - Fungu 37

(i) Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Kigamboni na Nyumba za Makazi Kijichi Kigamboni ulio chini ya *NSSF* ;na

(ii) Mradi wa Uimarishaji wa Kitengo cha Maafa (Mradi Na. 6575).

(b) Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Fungu 31

Mradi wa Ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli - Dar es Salaam (Mradi Na. 6389).

(c) Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria (Fungu 41)

Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hizo, Kamati ilibaini kuwa Miradi mingi iliyotengewa fedha haikutekelezwa ipasavyo kutokana na fedha ndogo iliyotolewa. Kwa mfano mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekua ikiomba fedha kiasi cha Shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa muda wa miaka mfululizo, (mwaka 2014/2015, 2015/2016 na 2016/2017). Pamoja na kuomba fedha hizo katika vipindi hivyo tofauti, ofisi hii haikupokea fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilibaini kwamba, kulikuwa na matumizi yasiyoridhisha ya fedha za umma katika baadhi ya miradi na kuagiza mamlaka zinazohusika kufanya uchunguzi maalum kuhusu matumizi ya fedha na ubora wa miradi hiyo na kutoa taarifa kwa Kamati. Kwa mfano, katika Fungu 31 (Ofisi ya Makamu wa Rais), Kamati ilibaini jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, limejengwa chini ya viwango na iliagiza uchunguzi ufanyike katika mradi huo ili kujiridhisha na matumizi ya fedha *(value for money)* na hatua kali zichukuliwe kwa watendaji wote waliohusika katika mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kwamba kuna baadhi ya miradi iliendeshwa kwa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi *(Public Private Partnerships)* na katika miradi kama hii, kulihitajika umakini mkubwa ili Serikali ipate faida na kuwa na maslahi bora. Kwa mfano Kamati ilitembelea Mradi wa daraja la Kigamboni (Daraja la Nyerere) na kukagua hatua za utekelezaji wa mradi huo ambao ulizinduliwa tarehe 16 Aprili, 2016 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Pamoja na mradi huu, Kamati pia ilikagua mradi wa Nyumba za *NSSF* za Kigamboni - Mtoni Kijichi. Miradi hii yote iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika Miradi hii, Kamati ilibaini kwamba kulikuwa na haja kwa Serikali kwa upande mmoja na *NSSF* kwa upande mwingine, kujiridhisha na ukweli au upotoshaji wa ukweli kuhusu tuhuma mbalimbali zilizoandikwa na vyombo vya habari kuhusu miradi hii, hasa mradi wa *Dege Eco Village* ulioko Kigamboni ambao ni mradi wa ubia kati ya *NSSF* na Kampuni ya *Azimio Holdings,* lakini pia

Kamati iliagiza uletwaji wa mkataba kati ya kampuni husika na *NSSF* mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha Kamati na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kilichofanyika, Dodoma tarehe 27 Novemba, 2016, Kamati iliarifiwa kwamba, taasisi za Serikali kama Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)*, Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii *(SSRA)*, Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa *(PCCB)* na vyombo vingine vya Usalama, vinaendelea na uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu wa matumizi mabaya ya fedha katika miradi ya *NSSF* na zipo katika hatua za mwisho za kukamilisha ripoti zao. Kamati ilitoa muda kwa Serikali kukamilisha ripoti hizi na inategemea kupewa taarifa kamili ya uchunguzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa ukomo wa bajeti kwa taasisi ambazo Kamati inazisimamia. Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa taarifa za bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Wizara na taasisi inazozisimamia kama ifuatavyo:-

(i) Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Fungu 26);
(ii) Ofisi ya Makamu wa Rais (Fungu 31);

(iii) Ofisi Binafsi ya Waziri ya Waziri Mkuu (Fungu 25);

(iv) Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37);

(v) Tume ya Usuluhishi na Utatuzi (Fungu 15);

(vi) Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (Fungu 27);

(vii) Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Fungu 61);
(viii) Kazi na Ajira(Fungu 65);

(ix) Wizara ya Sheria na Katiba(Fungu 41);

(x) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16);

(xi) Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka (Fungu 35);

(xii) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55);

(xiii) Tume ya Mabadiliko ya Sheria (Fungu 59); na

(xiv) Tume ya Usuluhishi wa Mahakama (Fungu 12).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya kazi ya uchambuzi wa bajeti ya Wizara na taasisi hizi na kulishauri Bunge lako Tukufu kuzipitisha bajeti zake pamoja na changamoto zilizoonekana katika kila taasisi. Kwa mfano, katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na makadirio ya mapato na matumizi ya Tume kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilibaini kwamba, Tume imekuwa ikitengewa fedha kidogo sana katika kila bajeti kwa miaka zaidi ya mitatu iliyopita na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake ipasavyo. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Tume iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha Sh. 5,578,338,000 lakini ilipokea kiasi cha Sh. 2,571,887,401 tu, sawa na asilimia 46.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya jitihada za kutosha ili bajeti ya Tume iongezwe kwa kupeleka ombi katika Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa lengo la kuishawishi Serikali kuongeza bajeti ya Tume. Hata hivyo, jitihada hizi hazikufanikiwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, kutokana na ukomo wa bajeti, hivyo Serikali iliahidi kulifanyia kazi suala hili katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Miswada ya Sheria. Kama nilivyoeleza hapo awali, katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017, Kamati imefanya uchambuzi wa Miswada sita ya Sheria na kuwasilisha taarifa za uchambuzi wa Miswada hiyo katika Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa Tatu wa Bunge Juni, 2016; Mkutano wa Nne wa Bunge Septemba, 2016; Mkutano wa Tano wa Bunge Novemba, 2016; na Mkutano huu wa Sita wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya mashauriano ya kina na Serikali katika Miswada hii na kutoa mapendekezo mbalimbali ya kuboresha sheria zilizopendekezwa ambayo yalikubaliwa na Serikali na Miswada hii kupitishwa na Bunge na kuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada iliyofanyiwa uchambuzi na kupitishwa na Bunge kuwa Sheria ni kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 6 wa Mwaka 2016;

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 7 wa Mwaka 2016;

(iii) Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa, Na. 4 wa Mwaka 2016;

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 3 wa Mwaka 2016;

(v) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 4 wa Mwaka 2016; na

(vi) Muswada wa Utoaji Huduma ya Kisheria, Na.14 wa Mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa Miswada, Kamati imekuwa na changamoto kuhusu uelewa wa kina kuhusu madhumuni na sababu za kufanya marekebisho kwenye sheria mbalimbali. Hii inatokana na kukosekana kwa uelewa mpana kuhusu sheria zinazofanyiwa marekebisho au sheria mpya kabla ya kuanza kufanya uchambuzi. Hii ni changamoto kubwa ambayo inahitaji kuangaliwa kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu, Kamati pia ilishauri Serikali kwa wale wataalam wanaokuja mbele ya Kamati wawe na uelewa wa sheria husika, kwani ilitokea katika Kamati zilizopita, kiongozi wa Serikali alifika mbele ya Kamati na kutoelewa kitu ambacho alikuwa anakielezea kwenye marekebisho ya sheria husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ufinyu wa Muda na Bajeti kwa Kamati kwa ajili ya kukagua Miradi ya Maendeleo. Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaokwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti na muda unakwamisha shughuli za Kamati kwa kiasi kikubwa. Kamati ya Katiba na Sheria inasimamia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) ambayo ina miradi Unguja na Pemba. Siku za kikanuni za Kukagua Miradi ya Maendeleo ni siku saba ambazo kiuhalisia hazitoshi kukagua Miradi ya Maendeleo kwa ufanisi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, Mapendekezo ya Kamati, Utoaji Fedha kwa Wakati Kutoka Hazina. Kwa kuwa, fedha za utekelezaji wa bajeti kutoka Hazina zimekuwa hazitolewi kwa kiwango kilichoidhinishwa na Bunge na kwa kuwa fedha zinazotolewa zimekuwa zinachelewa kufika katika Wizara na taasisi husika na kwa kuwa Wizara na taasisi hizi zimeathiriwa na kupewa kiwango kidogo na kuchelewa kufika kwa fedha kidogo zinazopatikana, jambo ambalo linaathiri utekelezaji wa majukumu yao pamoja na Miradi ya Maendeleo; hivyo basi Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba; Serikali kupitia Hazina itoe fedha kwa Wizara na taasisi zote kwa wakati na hasa katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha ili taasisi hizi ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukomo wa Bajeti; kwa kuwa ukomo wa bajeti ni suala la msingi katika uidhinishaji wa matumizi ya fedha za umma na kwa kuwa zipo baadhi ya Taasisi ambazo zimekwama kutekeleza majukumu yao ya msingi kwa kukosa fedha kutokana na ukomo wa bajeti, hivyo basi Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba Serikali iongeze ukomo wa bajeti ili Taasisi ambazo zipo katika hali mbaya ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika Mwaka wa fedha ujao (2017/2018) Serikali iongeze fedha katika taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ili kuboresha mazingira ya utoaji haki na hasa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu- 55 ), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16), Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (Fungu 35) na Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati kupata uzoefu kutoka nchi nyingine. Kwa kuwa Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya mbalimbali za Kimataifa na kwa kuwa kuna umuhimu wa kujifunza na kupata uzoefu wa utungaji wa sheria kutoka nchi ambazo tayari zimetunga sheria zinazofanana na sheria zinazopendekezwa kutungwa; hivyo basi, Kamati inaliomba Bunge lako liazimie kwamba; Kamati itengewe fedha za kutosha katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018, ili ipate nafasi ya kutembelea nchi zitakazobainika kuwa zimetunga na zinatekeleza sheria kwenye maeneo ambayo nchi yetu inapendekeza kutunga sheria mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uelewa wa Kamati Kuhusu Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikiwasilisha Miswada ya Sheria mbalimbali kwa ajili ya kuzifanyia marekebisho ikiwa ni pamoja na kuwasilisha Miswada ya utungaji wa Sheria mpya; na kwa kuwa kuna umuhimu wa Kamati

kujielimisha kwa kina kuhusu madhumuni na sababu za kufanyiwa marekebisho kwa Sheria husika pamoja na kujua kwa kina dhana kuhusu mapendekezo ya utungaji wa Sheria mpya; hivyo basi, Kamati inaliomba Bunge lako liazimie kwamba; Kamati ipatiwe semina za uelewa wa kutosha kutoka kwenye Taasisi zinazohusika na Miswada au sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kuhusu malengo na sababu za kuleta mabadiliko ya Sheria husika, ikiwa ni pamoja na Miswada ya Mapendekezo ya Sheria mpya .

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kwa kuwa Suala la usimamizi wa Serikali ni suala muhimu sana la Kikatiba; kama nilivyosema ibara ya 63; na kwa kuwa muda uliowekwa kikanuni wa ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo hautoshi hivyo basi, Kamati inaliomba Bunge lako liazimie kwamba; Kanuni ya 98(1) iliyotoa muda wa siku saba wa Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo ifanyiwe mapitio kwa lengo la kuongeza idadi ya siku za Kamati kukagua miradi ya maendeleo ili kuziwezesha Kamati kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati. Bunge lina wajibu wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977; na kwa kuwa Bunge linafanya kazi na kutekeleza majukumu yake kupitia Kamati za Bunge; na kwa kuwa Kamati ya Katiba na Sheria imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu kwa mujibu wa nyongeza ya 8(6)(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, hivyo basi, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba Wizara, Ofisi na Taasisi zote zinazosimamiwa na Kamati hii kutekeleza maagizo yote ya Kamati kwa wakati na kuendelea kutoa Taarifa za utekelezaji huo katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) iendelee kuratibu ufanisi wa masuala ya Muungano kwa kujali maslahi ya pande zote mbili za Muungano na maslahi mapana ya nchi kwa mujibu wa Sheria za ndani ya nchi pamoja na za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Mawaziri wanaohusika na Uandaaji wa Kanuni chini ya Sheria Mama za Kisekta zilizopitishwa na Bunge waharakishe uundaaji wa Kanuni hizo ili kurahisisha utekelezaji bora wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria napenda kukushukuru binafsi, kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano mlioutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Mawaziri wote na Watendaji Wakuu wote wa Wizara na Taasisi ambazo Kamati inazisimamia kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Shukrani za pekee ziwaendee Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa January Makamba; na Waziri wa Katiba na Sheria Dokta Harrison Mwakyembe; Manaibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Mavunde Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Luhaga Mpina wa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Makatibu Wakuu wote wa Wizara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa George Masaju Mbunge na Wanasheria wote, Waandishi wa Sheria chini ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Serikali ambao wametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Miswada. Vilevile napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mshauri Mkuu wa Mambo ya Sheria, Ofisi ya Bunge Ndugu Pius Mboya pamoja na Wanasheria wote walioshiriki katika shughuli za uchambuzi wa Miswada kwenye Kamati ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie nafasi hii kutambua mchango wa wadau na taasisi ambazo zimeshirikiana na Kamati wakati wa kutekeleza majukumu katika kipindi cha mwaka Januari, 2016 hadi Januari, 2017. Kwa uchache naomba kuwashukuru wadau wafuatao:-

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake, Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Chama cha Mawakili Tanganyika, Jukwaa la Katiba Tanzania, Mtandao wa Watoa Msaada wa Kisheria Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo cha Mipango Dodoma, Chuo cha *CBE,* Tawi la Dodoma, Taasisi ya Uwezeshaji wa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria, Jukwaa la Wahariri Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri na kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ambavyo imeorodheshwa katika Taarifa yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretariati yote ya Bunge chini ya Uongozi wa Dokta Thomas Kashilillah kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati; Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge; Ndugu Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi; Ndugu Angelina Sanga; Makatibu wa Kamati; Ndugu Stella Bwimbo na Ndugu Dunford Mpelumbe kwa umakini na weledi wao katika kufanikisha kazi zao. Pamoja na msaidizi wa Kamati Ndugu Raheli Masima kwa kuihudumia Kamati vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ilitakiwa iungwe! Wajumbe wako wasimame tu!

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Wajumbe wa Kamati!

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Haya, imeshaungwa mkono. Ahsante.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KWA KIPINDI CHA JANUARI 2016 HADI JANUARI 2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

[*Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*]

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kutupa tena uzima na uhai kwa Mwaka huu 2017. Pili, napenda kukupongeza

wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuongoza kwa weledi na umahiri Bunge hili la 11. Kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria tunawatakia afya njema katika Mwaka 2017 ili mzidi kutimiza majukumu yenu kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,Toleo la Januari 2016, Kamatiya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ina wajibu wa kuwasilisha Taarifa yake ya Mwaka katika Bunge lako Tukufu kwa madhumuni ya kujadiliwa kabla ya Mkutano wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii ya Mwaka inawasilishwa kwa mara ya kwanza tangu kuundwa kwa Kamati hii Mwezi Januari 2016.

Taarifa hii inaelezea shughuli za Kamati kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017 na imegawanyika katika Sehemu Kuu nne(4) zifuatazo:-

i. Sehemu ya kwanza inatoa Maelezo ya Jumla;

ii. Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;

iii. Sehemu ya Tatu ambayo inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na

iv. Sehemu ya Nne ambayo ni hitimisho la taarifa.

### 1.2 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya 6, Kifungu cha 2 na Fasili ya 7 Kifungu cha 1 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ni moja kati ya Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta inayosimamia Wizara tatu ambazo ni, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu na Wizara ya Katiba na Sheria. Majukumu ya Kamati hii ni:-

i. Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;

ii. Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

iii. Kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

iv. Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**1.3 Njia na Mbinu mbalimbali zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati.**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 117 (3), (5), (8), na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 kuhusu Ushirikishaji wa Wadau na kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2015/2016 na 2016/2017. Njia zilizotumika ni:-

i. Kukutana na kufanya vikao vya pamoja kati ya Kamati na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2015/2016 (Budget Performance Reports) pamoja na Taarifa za utekelezaji za Wizara na Taasisi hizo kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Mid - Year Performance Reports).

ii. Kupata ufafanuzi kutoka kwa Mawaziri ili kupata maelezo kuhusu matukio maalumu yaliyojitokeza katika kipindi hiki katika Wizara na Taasisi inazozisimamia. Kwa mfano katika Mkutano wa Tano Bunge la 11, Kamati ilipokea Taarifa Maalumu kutoka Kitengo cha Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu namna Serikali ilivyokabiliana na changamoto zilizojitokeza katika janga la tetemeko la Ardhi Mkoani Kagera.

iii. Kufanya ziara kwa kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 ili kujiridhisha na ufanisi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati;

iv. Kuwaalika Wadau mbalimbali kwa ajili ya kutoa maoni yao kwenye Miswada ya Sheria iliyoletwa kwenye Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) na 117(8) (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016;

v. Kuwasilisha mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahsusi zilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati za Mwaka wa Fedha wa 2016/2017; na

vi. Kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Taasisi mbalimbalimbali za Serikali na Asasi za Kiraia.

### 1.4 Shughuli zilizofanyika

**Mheshimiwa Spika**, mara baada ya kuteuliwa, Wajumbe wa Kamati walifanya uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imetekeleza shughuli zifuatazo:-

#### 1.4.1 Mafunzo kwa Wajumbe kuhusu Kazi na Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia kuwa Wajumbe wa Kamati ni wapya, ilionekana ni vema kuwapatia mafunzo kuhusu Kazi na Majukumu ya Kamati, Mafunzo hayo yalitolewa tarehe 21 Januari, 2016. Baada ya kupokea mafunzo hayo, tarehe 23 Januari, 2016 Wajumbe waliandaa Mpango Kazi wa Kamati kwa kipindi cha Januari hadi Juni, 2016. Lengo la mafunzo likiwa ni kujenga uelewa wa Wajumbe na kufahamu kazi na majukumu ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria.

#### 1.4.2 Mafunzo kwa Wajumbe kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia umuhimu wa majukumu ya Kamati ya kuzisimamia Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Wajumbe walipatiwa mafunzo ili waweze kufahamu kwa kina Muundo na Majukumu ya Wizara pamoja na Sera na Sheria mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara hizo. Mafunzo haya yalifanyika Tarehe 8 hadi 14, Februari 2016.

#### *1.4.3 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara*

***Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na Taasisi zake. Taarifa hizo ni kama zifuatazo:-***

i. Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya :-

- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka;
- Shule ya Sheria Tanzania;
- Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini;
- Tume ya Marekebisho ya Sheria;
- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;na

- Tume ya Utumishi wa Mahakama

ii Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zifuatazo:-

- Tume ya Taifa ya Uchaguzi;
- Ofisi ya Msajili Mkuu wa Vyama vya Siasa;
- Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi;
- Mamlaka ya Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii; (SSRA)
- Baraza la Taifa la Uwezeshaji;
- Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi;
- Shirika la Tija la Taifa; na
- Tume ya Usuluhishi na Utatuzi.
- Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) kuhusu utekelezaji wa uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma,
- Kazi na Ajira

**Mheshimiwa Spika,** lengo la kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Wizara na Taasisi zake ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyoainishwa katika Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Baada ya kujadili Taarifa hizo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika sehemu ya Tatu ya Taarifa hii.

### 1.4.4 Kutembelea na kukagua utekekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha, Kamati ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara na Taasisi inazozisimia ambayo ilitengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Miradi iliyokaguliwa ipo chini ya Vifungu vifuatavyo:-

- Fungu 37 (Mradi Na. 6575) - Ofisi ya Waziri Mkuu

- Fungu 31(Mradi Na. 6389) - Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)

- Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

### 1.4.5 Kuchambua Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane (7) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati yangu ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa ajili ya kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yanaelezewa kwa kina katika Sehemu ya Pili na Tatu ya Taarifa hii.

### 1.4.6 Uchambuzi wa Miswada ya Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu ilijadili na kuchambua Miswada ya Sheria mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1), ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017 Kamati ilichambua na kujadili Miswada ifuatayo:-

- Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 6 wa Mwaka 2016;
- Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 7 wa Mwaka 2016;
- Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa, Na. 4 wa Mwaka 2016;
- Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 3 wa Mwaka 2016 ;
- Muswada wa Sheria ya Huduma za Kisheria, Na. 14 wa Mwaka 2016 na;
- Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 4 wa Mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Bunge la Bajeti wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge la 11, Kamati iliwasilisha Taarifa Tatu(3) kuhusu uchambuzi wa Bajeti wa Wizara na Taasisi inazozisimamia kama ifuatavyo;

- Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Ofisi ya Waziri Mkuu;
- Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Ofisi ya Makamu wa Rais; na
- Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017, naomba sasa nitoe Taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, masuala yatakayotolewa Taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa ni changamoto ambazo zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kuleta tija kwa Taifa. Masuala hayo ni :-

**e) Masuala ya Ujumla**

- Semina na Mafunzo
- Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;
- Ufinyu na ukomo wa Bajeti kwa Taasisi zote ambazo Kamati inazisimamia;
- Uchambuzi wa Miswada;
- Ufinyu wa Muda kwa Kamati kwa ajili ya kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo;
- Kukosekana kwa umakini katika baadhi ya Miradi inayoendeshwa kwa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (Public Private Partnerships).

**f) Ofisi ya Makamu wa Rais ( Muungano)**

· Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, kujengwa katika viwango visivyoridhisha.

**g) Wizara ya Katiba na Sheria**

· Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) kutengewa fedha kidogo sana katika kila bajeti kwa Miaka zaidi ya Mitatu (3) mfululizo hali inayo sababisha Tume kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**h) Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera,Bunge,Kazi,Ajira,Vijana na Watu Wenye Ulemavu**

· Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma kutengewa fedha kidogo kwa mwaka wa fedha 2015/2016

· Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kutengewa Fedha kidogo katika Mwaka wa fedha 2015/2016 na hivyo kuathiri utendaji kazi wake

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyoainishwa hapo juu.

**2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati**

***2.2.1 Semina na Mafunzo***

***Mheshimiwa Spika,****Kamati katika kipindi cha Januari 2016 mpaka Januari 2017 ilipatiwa Semina/mafunzo kutoka kwenye Taasisi na Asasi mbalimbali za Kiraia kwa ajili ya kujenga uelewa wa masuala mbalimbali ya kisheria. Taasisi ambazo zimetoa mafunzo kwa Kamati katika kipindi hiki ni kama ifuatavyo:-*

· *Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa chini ya Mradi wake wa Legislative Support Program (UNDP-LSP);*

· *Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake(UN-Women) kwa kushirikiana na Umoja wa Wabunge Wanawake wa Tanzania (TWPG);*

· *Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA);*

· *Jukwaa la Uchambuzi wa Sera Tanzania (Policy Forum);*

· *Shirika la Uwezeshaji wa Watoa Msaada wa Kisheria (LSF);*

· *Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA);*

· *Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);*

· *Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS);*

· *Mtandao wa Mashirika Yanayotoa Msaada wa Kisheria Tanzania (TANLAP);*

· *Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) na;*

· *Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi (National Economic Empowerement Council) katika mradi wa ''Host Community Engagement in Local Content'' yaani ''Ushiriki wa Jamii katika Uwekezaji.*

***Mheshimiwa Spika,*** *kutokana na mafunzo yaliyotolewa, Wajumbe wamejengewa uwezo kuhusu mambo ya Sheria. Aidha, katika mafunzo kuhusu Sheria, Sera, Taratibu, Majukumu na Muundo wa Taasisi wanazozisimamia yaliyotolewa Januari 21 hadi Februari 8, 2016, Wajumbe walipata uelewa mpana uliowasaidia katika uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazozisimamia.*

***2.2.2 Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) na kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa Wizara na Taasisi inazozisimamia kama ifuatavyo:-

**i. Ofisi ya Waziri Mkuu - Fungu 37**

· Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Kigamboni na Nyumba za Makazi Kijichi Kigamboni ulio chini ya NSSF ;na

· Mradi wa Uimarishaji wa Kitengo cha Maafa (Mradi Na. 6575).

**ii. Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Fungu 31**

· Mradi wa Ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli - Dar es Salaam (Mradi Na. 6389)

**iii. Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria(Fungu 41)**

· Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16)

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hizo, Kamati ilibaini kuwa Miradi mingi iliyotengewa fedha haikutekelezwa ipasavyo kutokana na fedha ndogo kutolewa. Kwa mfano mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekua ikiomba fedha kiasi cha Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000/=) kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mwansheria Mkuu wa Serikali kwa muda wa Miaka Mitatu (3) mfululizo, yaani Mwaka 2014/2015, 2015/2016 na 2016/2017 . Pamoja na kuomba fedha hizo katika vipindi hivyo tofauti, Ofisi hii haikupokea fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilibaini kwamba, kulikuwa na matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Umma katika baadhi ya Miradi na kuagiza Mamlaka zinazohusika kufanya uchunguzi maalumu kuhusu matumizi ya fedha na ubora wa Miradi hiyo na kutoa Taarifa kwa Kamati. Kwa mfano, katika Fungu 31 (Ofisi ya Makamu wa Rais), Kamati ilibaini jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, limejengwa chini ya viwango na iliagiza uchunguzi ufanyike ili kujiridhisha na matumizi ya fedha (Value for Money**)** katika Mradi huo na hatua kali zichukuliwe kwa watendaji wote waliohusika katika Mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kwamba kuna baadhi ya Miradi iliendeshwa kwa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (Public Private Partnerships) na katika Miradi kama hii, kulihitajika umakini mkubwa ili Serikali ipate faida na kuwa na maslahi bora. Kwa mfano Kamati ilitembelea Mradi wa Daraja la Kigamboni (Daraja la Nyerere) na kukagua hatua za utekelezaji wa Mradi huo ambao ulizinduliwa tarehe 16 Aprili 2016 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Pamoja na mradi huu, Kamati pia ilikagua Mradi wa Nyumba za NSSF za Kigamboni - Mtoni Kijichi. Miradi hii yote iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika Miradi hii, Kamati ilibaini kwamba kulikua na haja kwa Serikali kwa upande mmoja na NSSF kwa upande mwingine, kujiridhisha na ukweli au upotoshaji wa ukweli kuhusu tuhuma mbalimbali zilizoandikwa na vyombo vya habari kuhusu Miradi hii, hasa Mradi wa Dege Eco Village ulioko Kigamboni ambao ni Mradi wa ubia kati ya NSSF na Kampuni ya Azimio Holdings.

**Mheshimiwa Spika**, katika kikao cha Kamati na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kilichofanyika, Dodoma tarehe 27 Novemba 2016, Kamati iliarifiwa kwamba, Taasisi za Serikali kama Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB) na vyombo vingine vya Usalama, vinaendelea na uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu wa matumizi mabaya ya fedha katika

Miradi ya NSSF na zipo katika hatua za mwisho za kukamilisha ripoti zao. Kamati ilitoa muda kwa Serikali kukamilisha ripoti hizi na inategemea kupewa Taarifa kamili ya uchunguzi huu.

**2.2.3. Ufinyu na ukomo wa Bajeti kwa Taasisi ambazo Kamati inazisimamia**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Taarifa za Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa Wizara na Taasisi inazozisimamia kama ifuatavyo:-

xv. Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Fungu 26);
xvi. Ofisi ya Makamu wa Rais(Fungu 31);
xvii. Ofisi Binafsi ya Waziri ya Waziri Mkuu(Fungu 25);
xviii. Ofisi ya Waziri Mkuu(Fungu 37);
xix. Tume ya Usuluhishi na Utatuzi(Fungu 15);
xx. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa(Fungu 27);
xxi. Tume ya Taifa ya Uchaguzi(Fungu 61);
xxii. Kazi na Ajira(Fungu 65);
xxiii. Wizara ya Sheria na Katiba(Fungu 41);
xxiv. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali(Fungu 16);
xxv. Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka(Fungu 35);
xxvi. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora(Fungu 55);
xxvii. Tume ya Mabadiliko ya Sheria (Fungu 59) na
xxviii. Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya kazi ya uchambuzi wa bajeti ya Wizara na Taasisi hizi na kulishauri Bunge lako Tukufu kuzipitisha bajeti zake pamoja na changamoto zilizoonekana katika kila Taasisi. Kwa mfano katika uchambuzi wa

Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume kwa Mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilibaini kwamba, Tume imekua ikitengewa fedha kidogo sana katika kila bajeti kwa Miaka zaidi ya Mitatu (3) iliyopita na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake ipasavyo. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Tume iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha **Shilingi 5,578,338,000/=** lakini ilipokea kiasi cha **Shilingi 2,571,887,401/= tu.** Sawa na asilimia 46.1.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya jitihada za kutosha ili bajeti ya Tume iongezwe kwa kupeleka ombi katika Kamati ya Bunge ya bajeti kwa lengo la kuishawishi Serikali kuongeza bajeti ya Tume. Hata hivyo jitihada hizi hazikufanikiwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kutokana na ukomo wa bajeti. Hivyo Serikali iliahidi kulifanyia kazi suala hili katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**2.2.4. Uchambuzi wa Miswada ya Sheria**

**Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza hapo awali, Kamati katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017, imefanya uchambuzi wa Miswada 6 ya Sheria na kuwasilisha Taarifa za uchambuzi wa Miswada hiyo katika Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa tatu wa Bunge Juni, 2016, Mkutano wa nne wa Bunge Septemba, 2016, Mkutano wa Tano wa Bunge Novemba, 2016 na Mkutano huu wa Sita wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya mashauriano ya kina na Serikali katika Miswada hii na kutoa mapendekezo mbalimbali ya kuboresha Sheria zilizopendekezwa ambayo yalikubaliwa na Serikali na Miswada hii kupitishwa na Bunge na kuwa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Miswada iliyofanyiwa uchambuzi na kupitishwa na Bunge kuwa Sheria ni kama ifuatavyo:-

- Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya SheriaMbalimbali, Na. 6 wa Mwaka 2016;

- Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 7 wa Mwaka 2016;

- Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa, Na. 4 wa Mwaka 2016;

- Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 3 wa Mwaka 2016;

- Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 4 wa Mwaka 2016; na

- Muswada wa Utoaji Huduma ya Kisheria, Na.14 wa Mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa miswada, Kamati imekuwa na changamoto kuhusu uelewa wa kina kuhusu madhumuni na sababu za kufanya marekebisho kwenye sheria mbalimbali. Hii inatokana na kukosekana kwa uelewa mpana kuhusu sheria zinazofanyiwa marekebisho au sheria mpya kabla ya kuanza kufanya uchambuzi. Hii ni changamoto kubwa ambayo inahitaji kuangaliwa kwa kina.

**2.2.5. Ufinyu wa Muda na Bajeti kwa Kamati kwa ajili ya kukagua Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,**Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa fedha unaoisha. Mheshimiwa Spika, ufinyu wa Bajeti na muda unakwamisha shughuli za Kamati kwa kiasi Kikubwa. Kamati ya Katiba na Sheria inasimamia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) ambayo ina Miradi Unguja na Pemba. Siku za Kikanuni za Kukagua Miradi ya Maendeleo ni siku saba ambazo kiuhalisia hazitoshi kukagua Miradi ya Maendeleo kwa ufanisi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

## SEHEMU YA TATU

## 3. MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 3.1 UTOAJI FEDHA KWA WAKATI KUTOKA HAZINA

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA,** fedha za utekelezaji wa bajeti kutoka Hazina zimekua hazitolewi kwa kiwango kilichoidhinishwa na Bunge,

**Na KWA KUWA** fedha zinazotolewa zimekuwa zinachelewa kufika katika Wizara na Taasisi husika;

**NA KWA KUWA**,Wizara na Taasisi hizi zimeathiriwa kwa kupewa kiwango kidogo na kuchelewa kufika kwa fedha kidogo zinazopatikana, jambo ambalo linaathiri utekelezaji wa majukumu yao pamoja na Miradi ya Maendeleo ;

**HIVYO BASI ;** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba; Serikali kupitia Hazina itoe fedha kwa Wizara na Taasisi zote kwa wakati na hasa katika robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha ili Taasisi hizi ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## 2.2 UKOMO WA BAJETI

**Mheshimiwa Spika**,

**KWA KUWA**, Ukomo wa bajeti ni suala la msingi katika uidhinishaji wa matumizi ya fedha za Umma,

**NA KWA KUWA**, zipo baadhi ya Taasisi ambazo zimekwama kutekeleza majukumu yao ya msingi kwa kukosa fedha kutokana na ukomo wa bajeti,

**HIVYO BASI**; Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba;

i) Serikali iongeze ukomo wa bajeti ili Taasisi ambazo zipo katika hali mbaya ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

ii) Katika Mwaka wa fedha ujao (2017/2018) Serikali iongeze fedha katika taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ili kuboresha mazingira ya utoaji haki, na hasa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu- 55 ), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16), Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (Fungu 35) na Tume ya Utumishi wa Mahakama (12).

## 2.3 KAMATI KUPATA UZOEFU KUTOKA NCHI ZINGINE

**Mheshimiwa Spika**,

**KWA KUWA**, Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya mbalimbali za Kimataifa;

**NA KWA KUWA**; kuwa kuna umuhimu wa kujifunza na kupata uzoefu wa utungaji wa sheria kutoka nchi ambazo tayari zimetunga sheria zinazofanana na Sheria zinazopendekezwa kutungwa;

**HIVYO BASI**;Kamati inaliomba Bunge lako liazimie kwamba;

Kamati itengewe fedha za kutosha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, ili ipate nafasi ya kutembelea nchi zitakazobainika kuwa zimetunga na

zinatekeleza Sheria kwenye maeneo ambayo nchi yetu inapendekeza kutunga Sheria mpya.

### 2.4 UELEWA WA KAMATI KUHUSU SHERIA ZINAZOFANYIWA MAREKEBISHO

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA**; Serikali imekuwa ikiwasilisha Miswada ya Sheria mbalimbali kwa ajili ya kuzifanyia marekebisho ikiwa ni pamoja na kuwasilisha Miswada ya utungaji wa Sheria mpya;

**NA KWA KUWA**; kuna umuhimu wa Kamati kujielimisha kwa kina kuhusu madhumuni na sababu za kufanyiwa marekebisho kwa Sheria husika pamoja na kujua kwa kina dhana kuhusu mapendekezo ya utungaji wa Sheria mpya;

**HIVYO BASI**; Kamati inaliomba Bunge lako liazimie kwamba;

Kamati ipatiwe semina za uelewa wa kutosha kutoka kwenye Taasisi zinazohusika na Miswada au Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kuhusu malengo na sababu za kuleta mabadiliko ya Sheria husika, ikiwa ni pamoja na Miswada ya Mapendekezo ya Sheria mpya .

### 2.5 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**,

**KWA KUWA**,Suala la usimamizi wa serikali ni suala muhimu sana la Kikatiba;

**NA KWA KUWA**; Muda uliowekwa Kikanuni wa ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo hautoshi;

**HIVYO BASI**; Kamati inaliomba Bunge lako liazimie kwamba; Kanuni ya 98(1) inayotoa muda wa siku Saba wa Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo ifanyiwe mapitio kwa lengo la kuongeza idadi ya siku za Kamati kukagua miradi ya maendeleo ili kuziwezesha Kamati kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi.

### 2.6 UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**,

**KWA KUWA**, Bunge lina wajibu wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

**NA KWA KUWA**, Bunge linafanya kazi na kutekeleza majukumu yake kupitia Kamati za Bunge;

**NA KWA KUWA**,Kamati ya Katiba na Sheria imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane (6) (2) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016;

**HIVYO BASI**; Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba;

i) Wizara, Ofisi na Taasisi zote zinazosimamiwa na Kamati hii kutekeleza maagizo yote ya Kamati kwa wakati na kuendelea kutoa Taarifa za utekelezaji huo katika muda uliopangwa;

ii) Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano iendelee kuratibu kwa ufanisi masuala yote ya Muungano kwa kujali maslahi ya pande zote mbili za Muungano na maslahi mapana ya nchi kwa mujibu wa Sheria za nchi na za Kimataifa;

iii) Mawaziri wanaohusika na Uandaaji wa Kanuni chini ya Sheria Mama za Kisekta zilizopitishwa na Bunge waharakishe uundaaji wa Kanuni hizo ili kurahisisha utekelezaji bora wa Sheria hizo.

**SEHEMU YA NNE**

## 4. HITIMISHO

### 4.2. Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano mlioutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Mawaziri wote na Watendaji Wakuu wote wa Wizara na Taasisi ambazo Kamati inazisimamia kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka Mmoja Uliopita. Shukrani za Pekee ziwaendee Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mhe. Jenista Mhagama Mb, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mhe. January Makamba Mb, na Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Harrison G. Mwakyembe Mb, Manaibu Waziri Mhe. Antony Mavunde wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Mhe. Luhaga

Mpina wa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Makatibu Wakuu wote wa Wizara hizi.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. George Masaju Mb, na Wanasheria wote Waandishi wa Sheria chini ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Serikali (CPD) ambao wametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Miswada.Vilevile,napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mshauri Mkuu wa Mambo ya Sheria Ofisi ya Bunge (CPLC) Ndg.Pius Mboya pamoja na wanasheria wote wa hiyo walioshiriki katika shughuli za uchambuzi wa Miswada kwenye kamati ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia nitumie nafasi hii kutambua mchango wa Wadau na Taasisi ambazo zimeshirikiana na Kamati wakati wa kutekeleza Majukumu katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017. Kwa uchache naomba kuwataja Wadau wafuatao:-

· Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP);

· Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN-WOMEN);

· Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG)

· Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC),

· Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS),

· Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA),
· Mtandao wa Watoa Msaada wa Kisheria Tanzania (TANLAP),

· Chuo Kikuu cha Dodoma,

· Chuo cha Mipango Dodoma;

· Chuo cha CBE Tawi la Dodoma;
· Taasisi ya Uwezeshaji wa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria LSF) ; na

· Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF);

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri na kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD) kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb- M/Mwenyekiti
3. Mhe Ally Saleh Ally, Mb –Mjumbe
4. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb –Mjumbe
5. Mhe Taska Restituta Mbogo, Mb –Mjumbe
6. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb –Mjumbe
7. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb- Mjumbe
8. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb- Mjumbe
9. Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb –Mjumbe
10. Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb-Mjumbe
11. Mhe. Ussi Pondeza, Mb- Mjumbe
12. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb –Mjumbe
13. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb- Mjumbe
14. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb- Mjumbe
15. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb –Mjumbe
16. Mhe. Mhe. Riziki Shahali Mngwali, Mb- Mjumbe
17. Mhe. Joram Ismail Hongoli, Mb- Mjumbe
18. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb –Mjumbe
19. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb –Mjumbe
20. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb –Mjumbe
21. Mhe. Selemani Zedi, Mb –Mjumbe
22. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb –Mjumbe
23. Mhe. Selemani Nchambi, Mb –Mjumbe
24. Mhe. Juma Kombo Hamad, Mb –Mjumbe
25. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb – Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretariati yote ya Bunge chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Stella Bwimbo na Ndg. Dunford Mpelumbe kwa

umakini na weledi wao katika kufanikisha kazi za Kamati na Msaidizi wa Makatibu Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia Kamati vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo haya naomba kutoa hoja.

……………………….
Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA KATIBA NA SHERIA**

3 FEBRUARI 2017

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa! Mwenyekiti, Kamati ya Bunge na Serikali za Mitaa!

**MHE. ESTER A. MAHAWE – (K.n.y. MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha taarifa hii, napenda kusema mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna gazeti moja la wiki lililochapishwa hapa nchini ambalo katika Toleo lake Namba 376 la Tarehe 30 Januari, 2017 liliandika habari iliyokuwa na Kichwa cha Habari kisemacho, "UFISADI NDANI YA OFISI YA JPM". Katika habari hiyo ambayo mwandishi anaongelea uwekezaji usio na tija katika Shirika la Elimu Kibaha, ameihusisha Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kurejea baadhi ya sehemu za Taarifa iliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenye Kamati, ya tarehe 23/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa haihusiki kwa namna yoyote ile na utoaji wa taarifa hizo zilizotumika kuandika habari hiyo. Aidha, ni vyema waandishi wa gazeti hilo wakazingatia utaratibu wa kupata taarifa kabla ya kuandika habari zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa taarifa yote ya shughuli za Kamati katika kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 iingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Shughuli ya Kamati ya Huduma ya Bunge ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2016/2017. Utangulizi; Maelezo ya Awali. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majukumu; shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi hicho, ni kwa mujibu wa majukumu ya kikanuni yaliyotamkwa katika Kanuni ya nne (4) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Vilevile kwa mujibu wa Kanuni 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati itasimamia shughuli za Ofisi ya Rais, kwa kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) na TAMISEMI, kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka na kufuatilia utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia Zilizotumika Kutekeleza Majukumu; mbinu mbalimbali zilitumika kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(i) Mafunzo mahususi ya awali (*primary trainings*) kwa Wajumbe wa Kamati;

(ii) Vikao vya Wizara, Taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais;

(iii) Uchambuzi wa Taarifa mbalimbali za kiutendaji kutoka Ofisi ya Rais; na

(iv) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ya Serikali kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na Semina za kuwajengea uwezo *(capacity building)* Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mantiki ya kutumia mbinu hizo tofauti ni kuwaongezea uelewa Wajumbe wa Kamati kuhusiana na nyanja ambazo watazisimamia na kuishauri Serikali. Kujifunza ni sifa kubwa ya kiongozi ndiyo maana Rais wa zamani wa Marekani, John F. Kenedy aliwahi kusema, na hapa nanukuu:-

*Leadership and learning are indispensable to each other.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, *Uongozi na Kujifunza ni vitu muhimu sana vinavyotegemeana*. Ni kwa mantiki hiyo, ilikuwa ni muhimu kutumia mbinu mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha Wajumbe wa Kamati wanajifunza kuhusiana na majukumu wanayopaswa kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shughuli Zilizotekelezwa na Kamati; ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo katika kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Janauri, 2017:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya maendeleo katika Mikoa ya Dar-es-Salaam, Pwani, Kigoma na Mwanza, ambayo inatekelezwa chini ya Ofisi ya Rais. Mantiki ya ukaguzi huo ni kujiridhisha iwapo miradi hiyo ina thamani halisi ya fedha *(value for money)* iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais; Kamati ilitekeleza jukumu hili kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) na ilichambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Uchambuzi huu ulilenga kuiwezesha Kamati kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji kutoka Ofisi ya Rais; katika kipindi hicho Kamati ilipokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utekelezaji kutoka Ofisi ya Rais. Taarifa hizo zilihusu utekelezaji wa shughuli za kawaida na masuala mahsusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziara za Ukaguzi wa Shughuli za Ofisi ya Rais; Kamati ilitembea na kukagua shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Ofisi ya Rais, kupitia Taasisi na Idara zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili; Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati. Maelezo ya Jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii ya Taarifa inaelezea kwa ufasaha, majukumu yaliyotekelezwa na Kamati kwa kipindi chote cha mwaka mmoja. Ili kutimiza azma hiyo, uchambuzi wa kina wa matokeo ya shughuli hizo umefanyika, ukiainisha Wizara, Taasisi au Idara zinazohusika; tasnia husika; mafanikio na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, Kamati iliweza kukutana na kutembelea Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na Idara na Taasisi zilizo chini yake kama zinavyoonekana katika ukurasa wa tisa na kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Yaliyojitokeza; Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo. Hili ni miongoni mwa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, ambayo inatekelezwa chini ya Ofisi ya Rais, katika Mikoa ya Dar-es-Salaam, Pwani, Kigoma na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi iliyotembelewa na Kamati ni kama ifuatavyo; Mpango wa TASAF wa kunusuru Kaya Maskini *(Productive Social Safety net)* Kigoma, Dar-es-Salaam na Mwanza. Mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania *(Tanzania Strategic Cities Project)*. Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) katika Wilaya ya Magu, Mwanza. Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Dar-es-Salaam *(DART)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kuhusiana na miradi hiyo yanapatikana katika ukurasa wa 11 hadi 18 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais. Kamati ilishughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais ambayo inahusisha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, yenye Mafungu 28 na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yenye Mafungu 10, kwa kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Uchambuzi huo unapatikana kuanzia ukurasa wa 18 hadi 25 wa Taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji; Kamati ilitekeleza kazi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 7(1)(c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Rushwa nchini, Utendaji wa TAKUKURU na Mikakati ya Kutokomeza Rushwa. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ndiyo chombo kilichokabidhiwa na Serikali jukumu la kupambana na rushwa nchini. Hata hivyo, miaka ya karibuni chombo hiki kimejikuta katika lawama nyingi kutoka ndani na nje ya nchi kwamba, kumekosa ufanisi katika mapambano yake dhidi ya rushwa nchini. Utafiti uliofanywa na Mashirika yanayopima hali ya rushwa katika ngazi ya Kanda na Kimataifa ya Mo Ibrahim na *Transparecy International* miaka michache iliyopita ulibainisha kuongezeka kwa vitendo vya rushwa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua kuwa rushwa ni adui wa haki. Kunapokuwa na rushwa dhana ya utawala bora inakiukwa, wananchi wanakosa huduma bora na haki za msingi, Serikali inapoteza mapato na maendeleo ya nchi yanazorota. Mtaalam wa mambo ya Utawala, Pratibha Patil, aliwahi kusema na hapa nanukuu:-

*Corruption is the enemy of development and good governance. It must be got rid of. Both the government and the people at large must come together to achieve this national objective.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri isiyo rasmi, anachoeleza mtaalam huyu ni kwamba, rushwa ni adui wa maendeleo na utawala bora. Ni lazima iondolewe. Pande zote, Serikali na watu kwa ujumla ni lazima waungane ili kufikia lengo hili la Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya changamoto zote hizo, hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano, zimeanza kuimarisha utendaji wa TAKUKURU, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua dhidi ya Watendaji wa Serikali wanaotuhumiwa kwa vitendo vya rushwa na kukiuka Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mafanikio ambayo TAKUKURU imeanza kuyapata ni pamoja na kuongeza idadi ya chunguzi ili kubaini rushwa na kuanzisha Kitengo cha Ufuatiliaji na Urejeshaji wa Fedha/Mali za Umma kutoka kwa Watuhumiwa (*Asset Tracing and Recovery),* ambavyo vimesaidia kuokoa fedha za umma kiasi cha Shilingi bilioni 43.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, TAKUKURU iko katika mchakato wa kuanzisha Maabara ya Utambuzi *(Forensic Laboratory)* ili kusaidia kuongeza ufanisi wa kiutendaji. Aidha, Kamati inashauri TAKUKURU iongeze juhudi katika kuelimisha umma kuhusiana na athari za rushwa, pamoja na kuhamasisha matumizi ya namba ya simu ya bure 113 katika kutoa taarifa zinazohusiana na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inamkumbusha kila mmoja wetu kutimiza wajibu wake katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kukataa kuomba na kupokea na kutoa taarifa pale anapoona mazingira ya rushwa. Ni wazi kwamba, iwapo kila mmoja wetu atasimama katika nafasi yake na kupinga uovu, vita itakuwa rahisi na rushwa itatokomezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanafalsafa na Mwanasayansi mahiri duniani, Albert Einstein aliwahi kusema na hapa nanukuu:-

*Dunia ni mahali hatari pa kuishi, si kwa sababu ya watu ambao ni waovu, bali ni kwa sababu ya watu ambao hawafanyi lolote dhidi ya uovu*

Hebu tuchukue hatua dhidi ya uovu huu wa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maboresho ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* uko katika Awamu ya Tatu ya Utekelezaji wake tangu Agosti, 2012 ambapo Mpango wa Kunususru Kaya Maskini ndio unatekelezwa. Mpango huu unalenga kuwezesha Kaya Maskini zilizotambuliwa na jamii kupata ruzuku ili ziweze kumudu mahitaji ya chakula, elimu, afya, lishe bora kwa watoto na kuwekeza katika miradi ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Disemba, 2016 ikiwa ni miaka minne tangu kuanza kutekelezwa kwa mpango huu hapa nchini, jumla ya Shilingi bilioni 445.2 zilikuwa zimeshatumika kuwalipa Walengwa katika Kaya 1,055,091 huku kati ya hizo Kaya 26,775 zikiwa ni za watu wenye ulemavu. Aidha, kama sehemu ya utekelezaji wa mpango huu, Walengwa 406,974 wamenufaika na utekelezaji wa Miradi ya Kutoa Ajira za Muda ipatayo 4,068 ambapo jumla ya Shilingi bilioni 39.16 zimetumika kuwalipa ujira. Miradi hiyo inatekelezwa katika halmashauri 52 nchini na baadhi inahusu ujenzi na ukarabati wa majosho, uchimbaji wa visima na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango huu umeonesha mafanikio makubwa kwa Walengwa kwani wameweza kumudu kugharamia huduma muhimu kama vile, chakula, elimu na afya na wengine wametumia ruzuku hiyo kuboresha makazi na kuanzisha miradi ya ujasiriamali ili kujiongezea kipato. Aidha, mpango huu umeonekana kufanya vizuri zaidi katika Visiwa vya Unguja na Pemba, ikilinganishwa na baadhi ya maeneo ya Tanzania Bara kutokana na wakazi wa huko kuwa wawazi na wenye dhamira njema pale wanapofikiwa na Watendaji wa *TASAF*. Walengwa hao wametumia sehemu ya ruzuku kama mitaji na kuanzisha miradi ya kiuchumi kwa lengo la kujikwamua dhidi ya umaskini. Ni vyema wakazi wa Tanzania Bara wakaiga utaratibu huu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo mpango huu umekumbwa na changamoto kadhaa ambazo hata hivyo Uongozi wa *TASAF* umechukua hatua stahiki za kukabiliana nazo. Zipo changamoto kadhaa, lakini kubwa ni Kaya zisizo na sifa kunufaika na utaratibu wa kupokea ruzuku. Zoezi la uhakiki wa Kaya Maskini lililoendeshwa nyumba kwa nyumba katika maeneo ambayo mpango huu unatekelezwa, lilibaini jumla ya Kaya 55,692 sawa na asilimia 5.27 ya Kaya zote zinazonufaika ambazo zilinufaika bila kuwa na sifa na vigezo stahiki. Kaya hizo zimeondolewa katika mpango na zitaingizwa Kaya zenye sifa za kunufaika. Aidha, kubainika na kuondolewa kwa Kaya hizo kumeokoa jumla ya Shilingi bilioni 6.427 ambazo zingelipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, baadhi ya wananchi wamekuwa na uelewa mdogo au fikra potofu kuhusiana na fedha za *TASAF*. Hii inatokana na kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusiana na vyanzo vya fedha hizo. Kwa mfano; wapo wanaoamini kwamba fedha hizi zinatokana na Kundi la *Freemason* hivyo kuogopa kuingia katika utaratibu wa kupokea ruzuku za Kaya maskini ili hali wanakabiliwa na kiwango kikubwa cha umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri wananchi hawa waelimishwe vya kutosha kuhusiana na mpango huu, ikiwa ni pamoja na kuelezwa kinagaubaga kwamba, fedha za *TASAF* ni msaada kutoka kwa wahisani kumi na mkopo kutoka Benki ya Dunia, ambao Taifa linawajibika kuulipa. Aidha, Serikali itimize kikamilifu wajibu wake wa kuchangia moja ya tatu ya fedha za utekelezaji wa *TASAF*, huku ikianza kujiandaa kuuwezesha mpango huu kuendelea baada ya mwaka 2023, pale wahisani watakapojitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala Bora na uzingatiaji wa Sheria Nchini; utawala bora ni moja ya nguzo muhimu katika ujenzi wa jamii yenye umoja, usawa, mshikamano, uadilifu na uwajibikaji. Ili kutekeleza dhana hii kikamilifu, ni

lazima uwepo utawala wa kisheria unaozingatia misingi ya demokrasia pamoja na haki za binadamu. Nchi yetu kama Taifa linalofuata demokrasia, inaendeshwa kwa kuzingatia utawala wa sheria kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za karibuni, jamii imeshuhudia baadhi ya Watendaji wa Serikali wakichukua nafasi ya mhimili wa Mahakama, kwa kuhukumu na kuwatia hatiani moja kwa moja baadhi ya Watumishi wa Umma bila kujua kwamba, wanakiuka misingi ya Katiba waliyoapa kuilinda. Ibara ya 13(6)(2) ya Katiba inazuia mtu anayeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mwenye kosa hilo hadi itakapothibitishwa na Mahakama yenye mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya Mkurugenzi wa Halmashauri kumuamuru mwalimu wa sekondari adeki darasa mbele ya wanafunzi wake eti kwa sababu ni chafu, au Mkuu wa Mkoa kutumia lugha zisizo na staha katika hadhara kwa kuita watumishi kuwa ni wezi, wajinga, wasiokuwa na akili timamu, hawa ndio vichaa tunaohangaika nao, ni kudhalilisha utu wa mtu na kuvunja misingi ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya wametumia vibaya mamlaka waliyopewa, kwa kuamrisha Watumishi wa Umma kuwekwa ndani, kwa makosa ambayo hayastahiki adhabu hizo. Ipo mifano kadhaa ikiwa ni pamoja na Mkuu wa Mkoa mmojawapo nchini aliyeamuru Daktari wa Mkoa awekwe rumande kwa sababu hakutangaza kuwepo kwa ugonjwa wa kipindupindu. Mkuu wa Wilaya mojawapo Jijini Dar es Salaam, aliyeamuru watumishi waliochelewa kufika kazini wawekwe ndani na Mkuu wa Wilaya mojawapo Mkoani Arusha, aliyeamuru mwandishi wa habari wa kituo kimoja cha televisheni nchini awekwe ndani kwa kuandika habari kuhusiana na kero ya ukosefu wa maji, ambayo Mkuu huyo wa Wilaya aliitafsiri kuwa ni uchochezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua na kuthamini juhudi za Serikali za kurejesha nidhamu ya uwajibikaji katika utumishi wa umma, hivyo katika hali na mazingira ya aina yoyote ile, kamwe haiwezi kutetea watumishi wazembe na wasiotekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Hata hivyo, ingependa kuona Watumishi wa aina hiyo, wakichukuliwa hatua za kinidhamu na kiuwajibikaji kwa mujibu wa taratibu zilizopo (Kanuni za Utumishi wa Umma, 2014).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitumie fursa hii kuwakumbusha viongozi wote ikiwa ni pamoja na sisi Wabunge kwamba, dhamana ya uongozi tuliyonayo tunapaswa kuitekeleza kwa kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu zilizopo. Kinyume na hapo tutakuwa tumeshindwa kutimiza wajibu wa kuwa mfano kwa wale tunaowaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgogoro wa Kiuongozi Katika la Shirika la Elimu Kibaha *(SEK)*. Tarehe 21 Oktoba, 2016 Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, ilitembelea Shirika la Elimu Kibaha, Mkoani Pwani. Katika ziara hiyo Kamati ilikutana na watendaji na wafanyakazi wa Shirika la Elimu Kibaha na kutembelea uwekezaji wa Kampuni ya *Organia Limited*. Kampuni hiyo imekodisha eneo la *SEK* kwa ajili ya uzalishaji wa vifaranga wa kuku wa nyama na mayai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara Wajumbe walipata malalamiko ya Watumishi wa SEK kuhusiana na uongozi mbovu katika taasisi hiyo. Watumishi hao walidai kwamba, Mkurugenzi amekuwa akiongoza kwa ubabe, kuna ufujaji wa mali za Shirika na hakuna ushirikishwaji katika maamuzi ya msingi ya Shirika. Aidha, kumekuwa na ukiukwaji wa taratibu na Kanuni za Mikataba, jambo ambalo limesababisha *SEK* kuingia katika uwekezaji ambao hauna tija kwa Shirika na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanikiwa kupata nakala za baadhi ya mikataba ya ukodishaji wa maeneo ambayo Shirika la Elimu Kibaha, limeingia na Kampuni ya *Organia Limited.* Kupitia mikataba hiyo Kamati imebaini kiwango kidogo cha gharama ya ukodishaji (*rent*) wa eneo la *Plot. No*. 22 lenye ukubwa wa hekta 105,084. Eneo hilo limekodishwa kwa kipindi cha miaka 33 kwa malipo ya pamoja ya Dola za Marekani 21,016.8. Hii ni sawa na hekta moja kukodishwa kwa Dola za Marekani 200 katika kipindi chote cha miaka 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba mwingine ni ukodishaji wa eneo la hekta 87.23 lenye mradi wa kuzalisha kuku wa nyama na mayai, uliokuwa chini ya Shirika la Elimu Kibaha. Eneo na mali hizo vimekodishwa kwa kipindi cha miaka 25 kwa thamani ya Dola za Marekani 60,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaelewa Ofisi ya Rais – TAMISEMI inafahamu jambo hili na imechukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kuiandikia Mamlaka ya Uteuzi na kupendekeza hatua za kuchukuliwa dhidi ya Mkurugenzi wa *SEK.* Hata hivyo, inapenda kutahadharisha kwamba, jambo hili ni la muda mrefu na kadri linavyoendelea kuchukua muda linatoa mwanya wa mgogoro wa watumishi kuendelea, pamoja na mali za *SEK* kuendelea kufujwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Bunge liitake Serikali kuchukua hatua za haraka kuhusiana na mgogoro wa kiuongozi uliopo, ikiwa ni pamoja na Mkurugenzi kukaa pembeni ili kupisha uchunguzi wa kina. Aidha, mikataba ambayo *SEK* imeingia na mwekezaji wa Kampuni ya *Organia* ipitiwe upya ili kujiridisha iwapo ina tija kwa shirika hilo na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam *(DART)*. Tarehe 25 Januari, 2017 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, alizindua rasmi Mradi wa Mabasi Yaendayo kasi Jijini Dar es Salaam *(DART),* na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya tatu kutekeleza mradi wa aina hii Barani Afrika, baada ya Afrika Kusini na Morocco.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umelenga kupunguza au kutatua kabisa kero za usafiri Jijini Dar es Salaam ambazo zinasababishwa na ongezeko kubwa la idadi ya wakazi, kupanuka haraka kwa Jiji, uchakavu na upungufu wa miundombinu iliyopo, pamoja na kukosa ubora kwa huduma ya usafiri ambayo inatolewa na sekta binafsi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu utatekelezwa kwa awamu sita (6) ambapo barabara zenye jumla ya kilomita 130.3 zitajengwa kwenye njia kuu zote za Jiji la Dar es Salaam, ambazo ni Morogoro, Kilwa, Nyerere, Ali Hassan Mwinyi na Bagamoyo. Awamu ya kwanza ya mradi imekamilika ikiwa na barabara zenye urefu wa kilomita 20.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanza kwa mradi huu ni sehemu ya mafanikio ambayo Kamati inajivunia kwani wajumbe walikuwa bega kwa bega na Serikali katika kuhakikisha mradi huu unaanza. Mradi huu umekuwa na mafanikio kadhaa kwa Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na; kupunguza msongamano wa magari barabarani, kupunguza gharama za usafiri hasa kwa matumizi ya gari binafsi, kutoa ajira zaidi ya 900; fursa za kibiashara kama vile maegesho ya magari na mazingira rafiki kwa walemavu, wazee na wanafunzi**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya mafanikio hayo, mradi umekuwa ukikabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo wafanyabiashara ndogondogo (Wamachinga) kuendesha biashara zao kandokando ya barabara hiyo, na na watumiaji wengine wa barabara kutoheshimu miundombinu ya *DART.* Mfano; ni waendesha pikipiki, baiskeli, magari na hasa daladala ambao wamekuwa wakivamia barabara za *DART,* jambo ambalo mara nyingine limekuwa likisababisha ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa kutambua umuhimu wa mradi huu na changamoto za usafiri katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam Kamati inashauri Serikali kuongeza jitihada katika kutekelezaji awamu tano zilizosalia ili kuwezesha wakazi wa maeneo mengine ya Dar es Salaam kunufaika na huduma hii ya usafiri. Aidha, utekelezaji wa mradi huu una manufaa makubwa kwa ustawi wa Jiji la Dar es Salaam na Taifa kwa ujumla kwani shughuli za kiuchumi katika Jiji hili, zina mchango wa moja kwa moja katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu; Maoni na Mapendekezo. Maoni ya Kamati kuhusiana na shughuli ilizotekeleza katika kipindi chote cha mwaka mmoja, ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake yameanishwa katika taarifa ya Kamati kuanzia ukurasa wa 50 hadi 54.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni mapendekezo ambayo yamezingatia kwa sehemu kubwa matokeo ya uchambuzi wa shughuli zilizotekelezwa katika kipindi chote cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utendaji wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) na Hali ya Rushwa nchini. Kwa kuwa, hatua zinazochukuliwa na Serikali ili kuimarisha utendaji wa TAKUKURU zimeanza kuonesha matunda kwa kupunguza vitendo vya rushwa nchini na kwa kuwa, Taasisi hiyo imeongeza uchunguzi, kuchukua hatua dhidi ya Watuhumiwa wa rushwa na kuokoa fedha za umma kwa kutumia Kitengo cha Ufuatiliaji na Urejeshaji wa Fedha/Mali za Umma kutoka kwa watuhumiwa (*Asset Tracing and Recovery);* Kamati inapendekeza Serikali iendelee kuiwezesha TAKUKURU kuimarisha utendaji wake ikiwa ni pamoja na kukamilisha mchakato wa kuanzisha maabara ya utambuzi *(Forensic Laboratory)* ili kusaidia kuongeza ufanisi wa kiuchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maboresho ya Mpango wa *TASAF*. Kwa kuwa, mpango wa *TASAF* wa kunusuru kaya maskini nchini umeonesha mafanikio makubwa licha ya kasoro kadhaa zinatokana na baadhi ya watendaji wa Halmashauri wanaohusika kukosa uwazi na uadilifu katika uwajibikaji wao; Kamati inaishauri Serikali kuimarisha uwezo wa Halmashauri katika kusimamia miradi ya *TASAF* ili itekelezwe kikamilifu na kwa ufanisi. Aidha, kuimarisha mifumo ya kuwatambua Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ili kuzuia Kaya zisizo na sifa kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tathmini ya Ujazaji wa Fomu za Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa kuwa, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi nchini inashindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu kutokana na ufinyu wa bajeti; na kwa kuwa, hali hiyo imeathiri zoezi la kutembelea Viongozi wa Umma waliojaza fomu za maadili kwa lengo la kukagua ili kujiridhisha iwapo walitoa taarifa sahihi; Kamati inashauri Bunge liitake Serikali kuiwezesha Sekretarieti hii kifedha ili iweze kusimamia kikamilifu masharti ya Sheria ya Maadili kwa Viongozi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais ya Ushauri wa Mafuta na Gesi. Kwa kuwa, Sekta ya mafuta na gesi ni mpya nchini na uvunaji wa raslimali hizo ndiyo utachangia kwa sehemu kubwa kuiwezesha nchi yetu kuingia katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025; na kwa kuwa, wananchi hawana elimu ya kutosha kuhusiana na uvunaji na usimamizi wa raslimali hizo, jambo ambalo limefanya wawe na mashaka kwamba, huenda raslimali hizo zisinufaishe kikamilifu Taifa kama ilivyo kwa sekta ya madini; basi, Kamati inashauri Serikali ikamilishe muundo wa Ofisi ya Rais ya Ushauri wa Mafuta na Gesi ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu, ambapo ni pamoja na kutoa elimu na taarifa kwa wananchi kwa kila hatua inayoendelea katika utafiti wa mafuta na uzalishaji wa gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri kutenga asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuwezesha vijana na wanawake. Kwa kuwa, Halmashauri nyingi zimebainika kutotenga kikamilifu asilimia kumi ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi vijana na wanawake; na kwa kuwa, hatua hiyo inachangia vijana na wanawake waendelee kukosa mitaji na uwezo wa kutekeleza shughuli zao za kiuchumi ili waweze kujikwamua na kiuchumi, Kamati inapendekeza Bunge lako Tukufu kuitaka Serikali kuandaa na kuwasilisha Bungeni, Muswada wa Sheria ambao utaweka masharti ya usimamizi wa agizo hilo, ili vijana na wanawake waweze kunufaika na utaratibu huo na hivyo kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Walimu *(TSC)*. Kwa kuwa, Tume ya Utumishi wa Walimu imeanza kazi kwa kusuasua kutokana na uhaba wa fedha za bajeti iliyotengwa katika mwaka huu wa fedha; na kwa kuwa, hali hiyo inasababisha Tume hiyo kushindwa kushughulikia kikamilifu changamoto zinazowakabili walimu wa shule za msingi na sekondari nchini na kusababisha kuendelea kuporomoka kwa elimu nchini; Kamati inashauri Serikali kuipatia tume fedha za kutosha na kuifanyia marekebisho sheria iliyoianzisha ili kuondoa kasoro zilizopo na hivyo kuiwezesha kushughulikia kero za Walimu, ili waweze kutimiza majukumu yao katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utoaji wa Elimu Bila Malipo. Kwa kuwa mpango wa Serikali wa kutoa elimu ya msingi hadi kidato cha nne bila malipo, umewezesha kuwepo na ongezeko kubwa la wanafunzi; na kwa kuwa, ongezeko hilo limezalisha changamoto za utoaji wa elimu bora kutokana na upungufu wa miundombinu ya kielimu kama vile madarasa, nyumba za Walimu, matundu ya vyoo, pamoja na upungufu wa Walimu; Kamati inaishauri Serikali kutafutia ufumbuzi changamoto hizo, ikiwa ni pamoja na kuajiri Walimu zaidi, kulipa madeni na kuboresha maslahi kwa waliopo ili kunusuru kiwango cha elimu kisiendelee kuporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgogoro wa Kiuongozi Katika Shirika la Elimu Kibaha *(SEK)*. Kwa kuwa, imebainika uwepo kwa mgogoro wa kiuongozi katika Shirika la Elimu Kibaha, unaodaiwa kusababishwa na Mkurugenzi Mkuu; na kwa kuwa, mgogoro huo umesababisha hali ya kutoelewana baina ya watumishi na uongozi wa shirika, Kamati inashauri Serikali kupitia mamlaka yake ya uteuzi kushughulikia mgogoro huo kwa kumsimamisha Mkurugenzi ili apishe uchunguzi ili kuweza kuchunguza na kuchukua hatua stahiki kwa kasoro zitakazobainika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali ipitie upya mikataba ya uwekezaji ambayo shirika limeingia na Kampuni ya *Organia* ili kuona iwapo ina tija kwa Shirika na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi. Kwa kuwa awamu ya kwanza ya mradi wa mabasi yaendayo kasi wa Jijini Dar es Salaam *(DART),* ulianza kutoa huduma ya usafiri mwezi Mei, 2016 kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na kuzinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 25 Januari; huduma hiyo ya usafiri wa *DART* imeonesha mafanikio makubwa.

Kamati inapendekeza sehemu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, omba tu zote ziingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

**MHE. ESTHER A. MAHAWE – MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tamka…

**MHE. ESTHER A. MAHAWE – MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nawashukuru Wenyeviti wote kwa kuwasilisha kwa uadilifu mkubwa sana.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

**SEHEMU YA KWANZA**

**MAELEZO YA JUMLA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 2.7 MAELEZO YA AWALI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inakusudia kuelezea shughuli zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha uhai wa mwaka mmoja tangu ilipoundwa, na kuchambua matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo. Aidha, mbinu mbalimbali zilizotumika kutekeleza majukumu hayo zimeanishwa, sawia na maoni na mapendekezo ya Kamati kwa Bunge kuhusu namna bora ya kuishauri na kuisimamia Serikali katika utendaji wake.

### 2.8 MAJUKUMU

**Mheshimiwa Spika,** shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi hicho, ni kwa mujibu wa majukumu ya kikanuni yaliyotamkwa katika Kanuni ya 4 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Kwa mujibu wa Kanuni hiyo, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, itasimamia shughuli za Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, kupitia Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati itasimamia shughuli za Ofisi ya Rais, kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) na TAMISEMI;

(b) kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge;

(c) kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka; na

(d) kufuatilia utekelezaji wa Majukumu.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, ni muhimu kuzingatia kwamba, majukumu yote yaliyoanishwa Kikanuni, yanalenga kutimiza matakwa ya Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ambayo inatamka bayana kwamba;

***"...Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya Wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii"***

## 2.9 NJIA ZILIZOTUMIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya kuisimamia na kuishauri Serikali ni mazito na muhimu, hivyo yanahitaji umakini, kujitoa na weledi mkubwa ili kuyatekeleza kikamilifu. Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, imetambua, imethamini na imekubali utekelezaji wa dhamana hiyo kupitia Ofisi ya Rais (Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa).

**Mheshimiwa Spika,** aidha, ili kukidhi kiu ya Wananchi ya kuona Bunge likitimiza wajibu wake kikamilifu, mbinu mbalimbali zilitumika kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(a) Mafunzo mahususi ya awali (***primary trainings***) kwa Wajumbe muda mfupi baada ya kuundwa kwa Kamati, ili kuwajengea uelewa wa jumla kuhusu Muundo na Majukumu ya Kamati, pamoja na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ambazo Kamati itazisimamia wakati wa utekelezaji wa majukumu yake;

(b) Vikao na Wizara, Taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais, ili kufahamu muundo, majukumu na shughuli zinazotekeleza;

(c) Uchambuzi wa Taarifa mbalimbali za kiutendaji kutoka Ofisi ya Rais;
(d) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ya Serikali iliyotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge; na
(e) Semina za kuwajengea uwezo (capacity building) Wajumbe wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mantiki ya kutumia mbinu hizo tofauti ni kuhakikisha kwamba, Wajumbe wa Kamati wanajielimisha vya kutosha kuhusiana na nyanja mbalimbali ambazo wanapaswa kuisimamia na kuishauri Serikali.

Kujifunza ni sifa kubwa ya Kiongozi ili kuwa na uelewa wa mambo yanayojiri, na ndiyo maana Rais wa zamani wa Marekani, John F. Kenedy aliwahi kusema, na hapa ninanukuu;

***"Leadership and learning are indispensable to each other"***
Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, ***"Uongozi na Kujifunza ni vitu muhimu sana vinavyotegemeana"***.

Ni kwa mantiki hiyo, ilikuwa ni muhimu kutumia mbinu mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha Wajumbe wa Kamati wanajifunza na kupata uelewa wa kutosha kuhusiana na majukumu wanayopaswa kuyatekeleza.

## 2.10 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 7 (1) ya Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo katika kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Janauri, 2017:-

### *2.10.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;*

**Mheshimiwa Spika,** ili kuzingatia Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ilitembelea na kukagua miradi

ya maendeleo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kigoma na Mwanza, ambayo inatekelezwa chini ya Ofisi ya Rais.

Mantiki ya ukaguzi huo ni kuiwezesha Kamati kujiridhisha iwapo utekelezaji uliofanyika una thamani halisi ya fedha "***value for money***" iliyotolewa au la, ili waweze kuishauri vyema Serikali katika bajeti ya mwaka unaofuata.

### *2.10.1*

### *2.10.2 Kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais;*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitekeleza jukumu hili kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2), ambapo ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais; Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Uchambuzi huo ulikuwa na lengo la kuiwezesha Kamati kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

### *2.10.3 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji kutoka Ofisi ya Rais,*

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho Kamati ilipokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utekelezaji kutoka Ofisi ya Rais. Taarifa hizo zilihusu utekelezaji wa shughuli za kawaida, pamoja na masuala mahsusi yaliyojitokeza na kushughulikiwa na Serikali.

### *2.10.4 Kushiriki katika Semina za ndani*

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kushiriki katika Semina mbili zilizoandaliwa na Ofisi ya Bunge, kupitia Mpango wa kuwajengea Wabunge uwezo (*Legislative Support Programme*), ambao unafadhiliwa na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP). Semina hizo zililenga kuwaongezea ujuzi (skills) Wajumbe katika maeneo ya Uchambuzi wa Bajeti, Miswada ya Sheria na Mikataba, pamoja na kuwakumbusha kuhusu Majukumu na Wajibu wa Kibunge katika kuisimamia na kuishauri Serikali.

### *2.10.5 Ziara za Ukaguzi wa shughuli za Ofisi ya Rais*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kukagua shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Ofisi ya Rais, kupitia Taasisi na Idara zake. Ziara hizi zilitoa fursa kwa Wajumbe kujiridhisha kuhusiana na utekelezaji huo ikilinganishwa na Taarifa za Utekelezaji ambazo ziliwasilishwa na Serikali mbele ya Kamati.

# SEHEMU YA PILI

## 3.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya Taarifa inaelezea kwa ufasaha, Majukumu yaliyotekelezwa na Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka mmoja. Ili kutimiza azma hiyo, uchambuzi wa kina wa matokeo ya shughuli hizo umefanyika, ukianisha Wizara, Taasisi au Idara iliyohusika; tasnia husika; mafanikio na changamoto.

Aidha, kwa lengo la kufafanua zaidi na kuongeza uelewa kwa baadhi ya maeneo ya uchambuzi wa matokeo, sehemu hii itatumia takwimu.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, Kamati iliweza kukutana au kutembelea Ofisi ya Rais kama ifuatavyo:-

#### *3.1.1 Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;*

a) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
b) Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
c) Tume ya Utumishi wa Umma;
d) Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma,

e) Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa,
f) Ofisi ya Ushauri ya Mafuta na Gesi,
g) Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU),
h) Mpango wa Kurasimisha Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA),
i) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF),
j) Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute),
k) Wakala wa Serikali Mtandao, (eGA);
l) Chuo cha Utumishi wa Umma; na
m) Mfuko wa Kujitegemea wa Rais (PTF),

#### *3.1.2 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)*

a) Tume ya Utumishi wa Walimu;
b) Wakala wa Mabasi yaenddayo Haraka Dar es Salaam (DART)
c) Mikoa Ishirini na Sita (26) ya Tanzania Bara;
d) Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI);

e) Shirika la Elimu Kibaha(SEK);
f) Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF); na
g) Shirika la Masoko Kariakoo – Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** mambo yanayochambuliwa katika sehemu hii kuhusiana na Wizara/Taasisi/Idara zilizoanishwa hapo juu yamejikita katika maeneo yafuatayo:-

a) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
b) Uchambuzi wa Bajeti;
c) Taarifa za Utekelezaji; na
d) Ziara za Ukaguzi wa shughuli za kiutendaji;

### 3.2 Yaliyojitokeza

#### *3.2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo*

**Mheshimiwa Spika,** hili ni miongoni mwa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, ambayo inatekelezwa chini ya Ofisi ya Rais, katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kigoma na Mwanza.

Mantiki ya ukaguzi huu kama ilivyoelezwa awali ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kujiridhisha iwapo utekelezaji uliofanyika una thamani halisi ya fedha "**value for money**" iliyotolewa au la, ili hatimaye waweze kuishauri Serikali katika bajeti ya mwaka unaofuata. Baadhi ya miradi iliyotembelewa ni hii ifuatayo:-

**(a) Mpango wa TASAF wa kunusuru Kaya Maskini (Productive Social Safety net) Kigoma, Dar es Salaam na Mwanza**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ni utekelezaji wa TASAF, Awamu ya Tatu ambayo inalenga kuzisaidia Kaya Maskini zaidi nchini kwa kuzipatia ruzuku ya fedha ili ziweze kuboresha hali ya upatikanaji wa mlo, ili hatimaye ziboreshe mahudhurio ya watoto shuleni pamoja na Kliniki kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Kwa mantiki hiyo mahudhurio ya Watoto shuleni na Kliniki, vimekuwa vigezo vikuu vya kuzingatiwa ili Wazee, Wajane, Wagane na Watoto, ambao ni

walengwa waendelee kunufaika na utaratibu wa kupokea fedha. Mpango huu unatekelezwa katika mikoa yote nchini, hata hivyo katika kipindi hiki Kamati ilitembelea mikoa hiyo mitatu.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mkoa wa Kigoma, Kamati ilitembelea Wilaya ya Kigoma Mjini (Ujiji), hususan Mitaa ya Mkese na Kibwe, iliyopo katika Kata ya Kagera. Kwa ujumla Mitaa hiyo ina Kaya 460 zinazonufaika na mpango huu, na hadi wakati huo jumla ya **shilingi milioni 129.7** zilikuwa zimelipwa kwa Kaya hizo katika Awamu Kumi.

**Mheshimiwa Spika,** Mkoani Dar es Salaam, Kamati ilitembelea Wilaya ya Kinondoni na kukagua Miradi ya Uhawilishaji fedha katika Mtaa wa Hananasifu, uliopo Kata ya Hananasifu na Mtaa wa Kisiwani uliopo Kata ya Makumbusho. Mitaa hiyo kwa ujumla wake ina Kaya 267 ambazo zinanufaika na utaratibu huu na hadi wakati huo jumla ya **shilingi milioni 54.3** zilikuwa zimelipwa kwa Awamu Nne.

Aidha, Kamati ilikagua Zahanati ya Hananasifu ambayo ilijengwa na TASAF Awamu ya Pili. Zahanati hiyo imekuwa msaada mkubwa kwa Wakazi wa Kata hiyo kwani imewapunguzia usumbufu wa kufuata huduma za afya maeneo ya mbali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mkoa wa Mwanza, Kamati ilitembelea Wilaya ya Nyamagana, Mitaa ya Wananchi na Isegenge B iliyopo Kata ya Mahina. Mitaa hiyo ina jumla ya Kaya 404 za Walengwa na tayari **shilingi milioni 84.5** zilikuwa zimelipwa katika Awamu Tano.

Aidha, TASAF imejenga vyumba vitatu vya Madarasa katika Sekondari ya Mlimani, iliyopo Kata ya Pamba kwa gharama ya **shilingi milioni 60.2** na Zahanati ya Tambukareli katika Kata ya Butimba, kwa gharama ya **shilingi milioni 54.2.** Ujenzi huo umechangia kuboresha huduma za elimu na afya katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla utekelezaji wa miradi ya TASAF umekuwa na manufaa kwa jamii, ikiwa ni pamoja na kuzisaidia Kaya maskini kupunguza makali ya umaskini. Hata hivyo, katika Mpango wa kusaidia kaya maskini, baadhi ya wanufaika wameingizwa katika mpango huo bila kuwa na sifa, na hivyo kuwanyima wenye sifa fursa ya kunufaika na utaratibu huo.

Kamati ilishauri Uongozi wa TASAF kufanya tathmini ili kuwabaini Wanufaika wa mpango huo wasio na sifa na kuwaondoa, kisha kuwaingiza wenye sifa wale waliachwa.

**(b) Mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania (*Tanzania Strategic Cities Project*)**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania (Strategic Cities Project – TSCP) ambao ulilenga kuboresha miundombinu, kuimarisha taasisi kwa kuongeza vitendea kazi na kujenga uwezo wa Watumishi, uanza kutekelezwa kuanzia Mwaka 2008 hadi 2015.

Mradi huu ambao ulifadhiliwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Denmark, ulilenga Miji Saba ambayo ni Kigoma Ujiji, Arusha, Tanga, Mwanza, Mbeya, Arusha, Mtwara na Dodoma. Kamati iliweza kutembelea Mikoa ya Kigoma na Mwanza.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mkoa wa Kigoma mradi huu umehusisha ujenzi wa vituo vitatu (3) vya mabasi katika eneo la Masanga, Matofalini na Kigoma Mjini, vyenye uwezo wa kuhudumia magari 238. Gharama iliyotumika kutekeleza mradi huo ni **shilingi bilioni 4.6**

Aidha, mradi ulihusisha ujenzi wa kilomita 9.0 za barabara kwa kiwango cha lami, mitaro ya maji machafu na kuweka taa za barabarani katika barabara za Airport – Mwasenga – Gungu; Job Lusinde; na Mji Mwema kwa gharama ya **shilingi bilioni 11.3.**

Vilevile, kupitia Mradi huu Manispaa ya Kigoma imejenga sehemu ya kisasa ya kutupia taka eneo la Msimba, Vituo 38 vya kukusanyia taka na ujenzi wa Mifereji ya Maji ya Mvua katika maeneo ya Lubengera na NHC Katubuka, kwa gharama ya **shilingi bilioni 7.**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mkoa wa Mwanza, Mradi wa TSCP umewezesha kujengwa kwa kiwango cha lami barabara Nne (4), mifereji ya maji machafu pamoja na kuweka taa za barabarani kwa thamani ya **shilingi bilioni 10.5** kama ifuatavyo:-

- Pansiansi - Buzuruga yenye urefu wa kilomita 7.29 kwa **shilingi bilioni 4.8;**
- Tunza Loop yenye urefu wa kilomita 4.78 kwa **shilingi bilioni 3.6;**

- Mkuyuni - Butimba yenye urefu wa kilomita 2.45 kwa **shilingi bilioni 1.7;**
- Liberty yenye urefu wa kilomita 0.25 kwa **shilingi milioni 482.4**.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa miradi ya TSCP umeonesha manufaa makubwa sana, kwani umeboresha miundombinu ya barabara, ujenzi wa mitaro ya maji na uwekaji wa taa za barabarani katika Manispaa za Mikoa iliyotembelewa na Kamati. Aidha, Watumishi wa Manispaa hizo wamejengewa uwezo na kupatiwa vitendea kazi. Kamati inashauri miradi hii itekelezwe pia katika Mikoa mingine iliyobaki ili kusaidia uboreshaji wa miundombinu katika Manispaa zake.

**(b) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) katika Wilaya ya Magu, Mwanza**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Kijiji cha Kitongosima, katika Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza ili kukagua Mradi wa Urasimishaji wa Ardhi ya Kijiji. Zoezi la hili lilikuwa shirikishi na limewezesha Wanakijiji kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi ambao umehusisha kutenga maeneo ya kilimo, makazi, malisho na huduma za kijamii.

Kupitia mpango huu, mashamba 1,139 yamepimwa na Hati 1200 zimeandaliwa, na hadi wakati huo Hati 331 zilikuwa zimesajiliwa, kwa gharama ya shilingi 35,000/= kwa Hati ya shamba lenge ukubwa wa hekari Tano. Utekelezaji wa Mpango huu umegharimu jumla ya **shilingi milioni 44**, na zoezi litakapokamilika litawezesha jumla ya **shilingi milioni 95** kukusanywa kutokana na malipo ya Hati.

Wajumbe wa Kamati wanaipongeza Serikali kwa mpango huu na kuomba utekelezwe kote nchini kwani ni njia bora ya kutatua migogoro ya ardhi baina ya Wakulima na Wafugaji katika maeneo yenye kadhia hiyo.

Aidha, Hati za Umiliki wa Ardhi zinazotokana na MKURABITA zinaweza kutumiwa na Wananchi kama dhamana ya mikopo katika Benki mbalimbali nchini na hivyo kuwainua kiuchumi.

**(d) Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) ambao unatekelezwa chini ya Fungu 56, kupitia Kifungu 1003. Jumla ya shilingi **bilioni 3.2** ziliidhinishwa kwa ajili ya

kugharamia usimamizi na uratibu wa ujenzi wa miundombinu ya mradi huu, ambao unatarajiwa kupunguza msongamano na kusaidia kutatua tatizo la usafiri wa Umma katika Jiji la Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, Kamati ilikuta Awamu ya Kwanza ya Mradi, ikiwa katika hatua za mwisho, na iliridhishwa na utekelezaji wake. Aidha, kwa kuzingatia ugeni wa mradi huo, Kamati iliishauri Serikali kuhakikisha Mradi huo unaanza haraka ili Wananchi waweze kuelewa dhamira ya Serikali katika kutatua kero ya usafiri Dar es Salaam, na kukabiliana na foleni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kutumia fursa hii kuipongeza Serikali kwani huduma ya Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam ilianza tarehe 10 Mei, 2016 na sasa Wakazi wa Dar es Salaam wananufaika na huduma hiyo ambayo kwa kweli imesaidia kupunguza kero ya usafiri jijini humo.

### *3.2.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais*

**Mheshimiwa Spika,** hili ni jukumu la Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2), ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Kamati ilishughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais ambayo inahusisha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, yenye Mafungu 28; na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yenye Mafungu 10, kwa kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/16 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali, kwa Mwaka wa Fedha 2016/17. Uchambuzi huo ulitekelezwa kama ifuatavyo:-

**(a) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilianza Vikao vya Uchambuzi wa Bajeti tarehe 08 Aprili, 2016 na kuendelea hadi tarehe 15 Aprili, 2016. Katika kipindi hicho Kamati ilipitia na kuchambua Mafungu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yafuatayo:-

1) **Fungu 56 –** Ofisi ya Rais – TAMISEMI
2) **Fungu 2 –** Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)
3) **Fungu 70 –** Mkoa wa Arusha
4) **Fungu 88 –** Mkoa wa Dar Es Salaam
5) **Fungu 63 –** Mkoa wa Geita
6) **Fungu 78 –** Mkoa wa Mbeya
7) **Fungu 90 –** Mkoa wa Songwe

8) **Fungu 89 –** Mkoa wa Rukwa
9) **Fungu 80 –** Mkoa wa Mtwara
10) **Fungu 85 –** Mkoa wa Tabora
11) **Fungu 84 –** Mkoa wa Singida
12) **Fungu 75 –** Mkoa wa Kilimanjaro
13) **Fungu 71 –** Mkoa wa Pwani
14) **Fungu 36 –** Mkoa wa Katavi
15) **Fungu 81 –** Mkoa wa Mwanza
16) **Fungu 73 –** Mkoa wa Iringa
17) **Fungu 87 –** Mkoa wa Kagera
18) **Fungu 54 –** Mkoa wa Njombe
19) **Fungu 74 –** Mkoa wa Kigoma
20) **Fungu 76 –** Mkoa wa Lindi
21) **Fungu 95 –** Mkoa wa Manyara
22) **Fungu 77 –** Mkoa wa Mara
23) **Fungu 47 –** Mkoa wa Simiyu
24) **Fungu 86 –** Mkoa wa Tanga
25) **Fungu 72 –** Mkoa wa Dodoma
26) **Fungu 82 –** Mkoa wa Ruvuma
27) **Fungu 83 –** Mkoa wa Shinyanga
28) **Fungu 79 -** Mkoa wa Morogoro

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi huo Kamati ilibaini kwamba, bajeti imeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka wa Uchaguzi 2015; Hotuba ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa uzinduzi wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Novemba, 2015; na Vipaumbele vya Bajeti vya Fungu husika.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi ulionesha kwamba, Fedha nyingi zimeelekezwa kwenye Matumizi ya Maendeleo ikilinganishwa na Matumizi ya Kawaida, na Halmashauri nyingi zimeanza kutumia Mfumo wa Kielektroniki katika ukusanyaji wa Mapato. Aidha, ilibainika kwamba, Halmashauri nyingi hazitengi kikamilifu Asilimia Kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi Vijana na Wanawake; na zinategemea sehemu kubwa ya Bajeti ya Maendeleo kutoka nje ili kutekeleza miradi ya sekta muhimu za Afya, Elimu na Maji.

**Mheshimiwa Spika, k**wa upande wa upatikanaji wa fedha katika Mwaka wa bajeti uliopita, Kamati ilibaini kwamba, kulikuwa na mwenendo mzuri kwa upande wa Fedha za Maendeleo ikilinganishwa na Fedha za Matumizi ya

Kawaida. Takwimu zilibainishwa kwamba, wakati fedha za maendeleo zilipatikana kutoka Hazina kwa zaidi ya **asilimia 85,** upatikanaji wa fedha za Matumizi ya kawaida ilikuwa ni kwa **asilimia 46** tu.

Aidha, Kamati ilibaini ongezeko la Bajeti ya Maendeleo kwa asilimia 9.9, hii ikiwa ni kutoka **shilingi bilioni 350.9** katika Mwaka wa Fedha 2014/15 hadi **shilingi bilioni 385.8** katika Mwaka wa Fedha 2016/17. Ongezeko hilo lilienda sambamba na kupungua kwa utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa kiwango cha asilimia 1.4, hii ikiwa ni kutoka asilimia 15.4 katika Mwaka wa Fedha 2015/16 hadi asilimia 14.0 katika Mwaka wa Fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo ongezeko la Fedha za Maendeleo liliathiri upande wa Fedha za Matumizi ya Kawaida, kwani bajeti ilipungua kwa kiwango kikubwa. Upungufu huo ulisababisha vifungu vingi vya kuendeshea Ofisi kukosa fedha jambo ambalo limeathiri sana shughuli za uendeshaji katika Ofisi za Serikali.

Kamati inashauri Serikali kutambua kwamba, ongezeko la fedha za Maendeleo linapaswa kwenda sambamba na ongezeko la Matumizi ya Kawaida, kwani usimamizi madhubuti wa Miradi ya Maendeleo utategemeana na uendeshaji madhubuti wa ofisi.

### (b) Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma, Kamati ilipitia na kuchambua bajeti kwa Mafungu yafuatayo:-

1. Fungu 20 – Ikulu;
2. Fungu 3 - Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
3. Fungu 32 -Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
4. Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
5. Fungu 67 - Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
6. Fungu 94 – Tume ya Utumishi wa Umma;
7. Fungu 09 - Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma;
8. Fungu 6 - Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi;
9. Fungu 4 - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; na
10. Fungu 11- Ofisi ya Ushauri wa Mafuta na Gesi.

**Mheshimiwa Spika,** hapa pia ilibainika kwamba, bajeti iliandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka wa Uchaguzi 2015; na Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 na maeneo muhimu ya kuzingatia yaliyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mafungu yake, ilikuwa na mtiririko mzuri wa upatikanaji wa fedha katika Matumizi ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida, kwani ilikuwa ni zaidi ya Asilimia 74.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati ilibaini ongezeko la Bajeti ya Maendeleo kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ambayo ilishuka, katika Mwaka wa Fedha 2016/17. Kwa tafsiri ya Kamati, huenda hali hii inatokana na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano kuelekeza fedha nyingi katika Miradi ya Maendeleo ikilinganishwa na Matumizi ya Kawaida, tofauti na Awamu zilizotangulia.

Hata hivyo, Kamati ina mtazamo kwamba, kupungua kwa kiwango kikubwa kwa Fedha za Matumizi ya Kawaida, kunaathiri uendeshaji wa Ofisi na hivyo kusababisha kukosekana kwa ufanisi wa kiutendaji miongoni mwa Watumishi wa Umma.

#### *3.2.3 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji;*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitekeleza kazi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 7(1) (c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**(a) Hali ya Rushwa nchini, Utendaji wa TAKUKURU na mikakati ya kutokomeza rushwa nchini;**

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ndiyo chombo kilichokabidhiwa na Serikali jukumu la kupambana na rushwa nchini. Hata hivyo, miaka ya karibuni chombo hiki kimejikuta katika lawama nyingi kutoka ndani na nje ya nchi kwamba, kimekosa ufanisi katika mapambano yake dhidi ya rushwa nchini.

Utafiti uliofanywa na Mashirika yanayopima hali ya rushwa katika ngazi ya Kanda na Kimataifa ya "**Mo Ibrahim** na **Transparecy International"** miaka

michache iliyopita ulibainisha kuongezeka kwa vitendo vya rushwa nchini Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** wote tunatambua kuwa rushwa ni adui wa haki. Kunapokuwa na rushwa dhana ya utawala bora inakiukwa, Wananchi wanakosa huduma bora na haki za msingi, Serikali inapoteza mapato, na maendeleo ya nchi yanazorota. Mtaalamu wa mambo ya Utawala, **Pratibha Patil,** aliwahi kusema na hapa ninanukuu;

***"Corruption is the enemy of development and good governance. It must be got rid of. Both the government and the people at large must come together to achieve this national objective"***

Kwa tafsiri isiyo rasmi, anachoeleza Mtaalamu huyu ni kwamba, ***"Rushwa ni adui wa maendeleo na utawala bora. Ni lazima iondolewe. Pande zote, Serikali na watu kwa ujumla ni lazima waungane ili kufikia lengo hili la kitaifa"***

**Mheshimiwa Spika,** licha ya changamoto hizo, hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano, zimeanza kuimarisha utendaji wa TAKUKURU, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua dhidi ya Watendaji wa Serikali wanaotuhumiwa kwa vitendo vya rushwa, na kukiuka Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utumishi wa Umma.

Miongoni mwa mafanikio ambayo TAKUKURU imeanza kuyapata ni pamoja na kuongeza idadi ya chunguzi ili kubaini rushwa na kuanzisha Kitengo cha Ufuatiliaji na Urejeshaji wa Fedha/Mali za Umma kutoka kwa Watuhumiwa (***Asset Tracing and Recovery),*** ambavyo vimesaidia kuokoa fedha za Umma kiasi cha **shilingi bilioni 43.7.** Vilevile, TAKUKURU iko katika mchakato wa kuanzisha Maabara ya Utambuzi ***(Forensic Laboratory)*** ili kusaidia kuongeza ufanisi wa kiutendaji.

Aidha, Kamati inashauri TAKUKURU iongeze juhudi katika kuelimisha Umma kuhusiana na athari za rushwa, pamoja na kuhamasisha matumizi ya Namba ya simu ya bure "113" katika kutoa taarifa zinazohusiana na rushwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakumbusha kila mmoja wetu kutimiza wajibu wake katika mapambano dhidi ya rushwa, kwa kukataa kuomba au kupokea, na kutoa taarifa pale anapoona mazingira ya rushwa. Ni wazi kwamba, iwapo kila mmoja wetu atasimama katika nafasi yake na kupinga uovu huu, vita itakuwa rahisi na rushwa itatokomezwa.

Mwanafalsafa na Mwanasayansi mahiri duniani, Albert Einstein aliwahi kusema na hapa ninanukuu "***Dunia ni mahali hatari pa kuishi, si kwa sababu ya Watu ambao ni waovu, bali ni kwa sababu ya Watu ambao hawafanyi lolote dhidi ya uovu"***. Hebu tuchukue hatua dhidi ya uovu huu wa rushwa.

**(c) Maboresho ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF);**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) uko katika Awamu ya Tatu ya Utekelezaji wake tangu Agosti, 2012 ambapo Mpango wa Kunususru Kaya Masikini ***(Productive Social Safety Net***) ndiyo unatekelezwa. Mpango huu unalenga kuwezesha Kaya Maskini zilizotambuliwa na jamii kupata ruzuku ili ziweze kumudu mahitaji ya chakula, elimu, afya, lishe bora kwa Watoto na kuwekeza katika miradi ya ujasiriamali.

Viwango vya ruzuku ambavyo hutolewa kwa mwezi ni **shilingi 10,000/=** kwa Kaya isiyokuwa na Mtoto/watoto; na **shilingi 14,000/=** kwa Kaya yenye Mtoto/Watoto.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Desemba, 2016 ikiwa ni miaka minne(4) tangu kuanza kutekelezwa kwa mpango huu hapa nchini, jumla ya **shilingi bilioni 445.2** zilikuwa zimeishatumika kuwalipa Walengwa katika **Kaya 1,055,091** huku kati ya hizo **Kaya 26,775** zikiwa ni za watu wenye ulemavu.

Aidha, kama sehemu ya utekelezaji wa mpango huu, **Walengwa 406,974** wamenufaika na utekelezaji wa Miradi ya kutoa Ajira za muda ipatayo **4,068** ambapo jumla ya **shilingi bilioni 39.16** zimetumika kuwalipa ujira. Miradi hiyo inatekelezwa katika Halmashauri 52 nchini, na baadhi inahusu ujenzi na ukarabati wa majosho, uchimbaji wa visima na uhifadhi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mpango huu umeonesha mafanikio makubwa kwa Walengwa kwani wameweza kumudu kugharamia huduma muhimu kama vile, chakula, elimu na afya, na wengine wametumia ruzuku hiyo kuboresha makazi na kuanzisha miradi ya ujasiriamali ili kujiongezea kipato.

Aidha, mpango huu umeonekana kufanya vizuri zaidi katika Visiwa vya Unguja na Pemba, ikilinganishwa na baadhi ya maeneo ya Tanzania Bara, kutokana na Wakazi wa huko kuwa wawazi na wenye dhamira njema pale wanapofikiwa na Watendaji wa TASAF. Walengwa hao wametumia sehemu ya ruzuku kama mitaji na kuanzisha miradi ya kiuchumi kwa lengo la kujikwamua

dhidi ya umaskini. Ni vyema Wakazi wa Tanzania Bara nao wakaiga utaratibu huu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo Mpango huu umekumbwa na changamoto kadhaa ambazo, hata hivyo Uongozi wa TASAF umechukua hatua stahiki za kukabiliana nazo. Zipo changamoto kadhaa, lakini kubwa ni Kaya zisizo na sifa kunufaika na utaratibu wa kupokea ruzuku.

Zoezi la uhakiki wa Kaya Maskini lililoendeshwa nyumba kwa nyumba katika maeneo ambayo Mpango huu unatekelezwa, lilibaini jumla ya Kaya 55,692 (Sawa na asilimia 5.27 ya Kaya zote zinazonufaika) ambazo zilinufaika bila kuwa na sifa na vigezo stahiki. Kaya hizo zimeondolewa katika Mpango na zitaingizwa Kaya zenye sifa za kunufaika. Aidha, kubainika na kuondolewa kwa Kaya hizo kumeokoa jumla ya **shilingi bilioni 6.427** ambazo zingelipwa.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, baadhi ya Wananchi wamekuwa na uelewa mdogo au fikra potofu kuhusiana na fedha za TASAF. Hii inatokana na kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusiana na vyanzo vya fedha hizo. **Kwa mfano;** wapo wanaoamini kwamba fedha hizi zinatokana na Kundi la Freemason na hivyo kuogopa kuingia katika utaratibu wa kupokea ruzuku za Kaya maskini, ili hali wanakabiliwa na kiwango kikubwa cha umaskini.

Kamati inashauri Wananchi hawa waelimishwe vya kutosha kuhusiana na Mpango huu, ikiwa ni pamoja na kuelezwa kinagaubaga kwamba, fedha za TASAF ni msaada kutoka kwa Wahisani Kumi (10) na Mkopo kutoka Benki ya Dunia, ambao Taifa litawajibika kuulipa.

Aidha, Serikali itimize kikamilifu wajibu wake wa kuchangia moja ya tatu (1/3) ya fedha za utekelezaji wa TASAF, huku ikianza kujiandaa kuuwezesha mpango huu kuendelea baada ya Mwaka 2023, pale Wahisani watakapojitoa.

**(c) Tathmini ya Zoezi la Ujazaji Fomu za Maadili kwa Viongozi wa Umma;**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza utaratibu huu wa Kikatiba unaomtaka kila Kiongozi wa Umma, kuwasilisha tamko rasmi(Fomu za Maadili) la mali anazomiliki na madeni, katika kipindi cha siku thelathini baada ya kupata wadhifa, kila mwisho wa Mwaka ifikapo Tarehe 31 Desemba, na pale anapokoma kutumikia wadhifa huo.

Kamati inatambua na kupongeza jitihada za Serikali katika kuhimiza ujazaji wa fomu hizi, hata hivyo chombo kilichopewa dhamana ya kusimamia utaratibu huu (Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma), hakina fedha za kutosha kufanya hivyo. Kwa mantiki hiyo, Kamati haioni tija inayoweza

kupatikana, iwapo Sekretarieti hiyo haiwezi kuwakagua waliojaza fomu kwa lengo la kujiridhisha iwapo wametaja mali na madeni yote yanayowahusu au la.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa, Serikali ilianzisha chombo hiki baada ya kubaini kwamba lipo hitaji kubwa la kufanya hivyo, basi inawajibika kuhakikisha inatenga Fedha za kutosha na kuzitoa kwa wakati ili kuiwezesha Sekretarieti kusimamia kikamilifu mpango huu kwa lengo la kulinda Maadili kwa Viongozi wa Umma na kwa mustakabali na ustawi wa Taifa letu.

**(d) Utawala Bora katika kusimamia Rasilimali za Gesi na Mafuta kwa ajili ya maendeleo endelevu;**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, Dira ya Taifa ya Maendeleo inalenga kuifanya nchi yetu kuingia katika uchumi wa kati ifikapo Mwaka 2025.

Rasilimali za Nishati ya Gesi na Mafuta, ndizo zinaonekana kuwa fursa kubwa ya kuliwezesha Taifa kufikia hatua hiyo ya ukuaji wa kiuchumi. Hata hivyo, ili Taifa lifikie hatua hiyo na kunufaika na uvunaji wa raslimali hizo bila kuingia katika migogoro kama ilivyo kwa baadhi ya nchi zenye raslimali hizo duniani, utawala bora unahitajika sana katika usimamizi.

**Mheshimiwa Spika,** ni jambo la kujivunia kwamba, nchi yetu imepiga hatua kubwa katika kuzingatia vipengele vingi vya Mwongozo wa Kimataifa wa Utawala Bora na Usimamizi wa Maliasili (*Natural Resource Charter*). Baadhi ya vipengele hivyo ni pamoja na Msingi wa kisheria wa Sheria ya Mafuta na Gesi Asili ya Mwaka 2015, Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uzinduaji, ya Mwaka 2015, na Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi Asili ya Mwaka 2015.

Hata hivyo, pamoja na hatua hiyo iliyofikiwa, bado Serikali inahitaji kuzingatia mambo kadhaa ili kuepuka changamoto zinazoweza kujitokeza. Mambo hayo ni pamoja na:-

i. Kuandaa Mkakati wa pamoja juu ya usimamizi wa rasilimali za Mafuta na Gesi Asili;
ii. Kuhakikisha kuna uwazi na uwajibikaji;
iii. Utoaji wa Leseni uwe wazi na wa haki;
iv. Serikali imiliki Taarifa za Kijiolojia;
v. Serikalii ihakikishe inapata mapato stahiki kutoka Sekta ya Mafuta na Gesi Asili;

vi. Kuzuia athari za Mazingira kwa Jamii zilizo karibu na Miradi ya Mafuta na Gesi; na

vii. Matumizi ya Mapato yatakayotokana na Mafuta na Gesi yatumike kwa kuzingatia uwiano baina ya kizazi cha sasa na vijavyo.

**(e) Tathmini ya Mkakati wa Serikali wa kuondoa Watumishi Hewa;**

**Mheshimiwa Spika,** tatizo la Watumishi Hewa limekuwa donda ndugu katika Utumishi wa Umma. Hali hii ambayo imesababisha upotevu mkubwa wa fedha za Umma, imechangiwa kwa sehemu kubwa na kuporomoka kwa maadili miongoni mwa Watumishi wa Umma.

Kamati inatambua na kupongeza juhudi ambazo zimechukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kupambana na tatizo hili. Zoezi lililoendeshwa na Serikali limesaidia kuokoa fedha nyingi za Umma ambazo zilikuwa zinalipwa kwa Watumishi wasiostahili.

Hata hivyo, kwa upande mwingine mapambano dhidi ya tatizo hili yamekuwa na athari kwa kusababisha Watumishi wengine kukosa stahiki zao za kiutumishi kama vile, kupandishwa vyeo, kupata uhamisho, nyongeza ya mshahara na Wahitimu wa vyuo waliopo katika soko la ajira kuendelea kusubiri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali ikamilishe zoezi hili na kuruhusu taratibu nyingine za kiutumishi kuendelea ili Watumishi wasiendelee kukosa stahiki zao. Vilevile, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya Watumishi wote ambao wamebainika kusababisha Wafanyakazi Hewa, ili kukomesha tabia hiyo.

Aidha, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuna mfumo madhubuti na shirikishi ***(intergratted assuarence system***) ambao utawezesha mifumo muhimu kuwa na mahusiano na hivyo kurahisisha mpango wa uhakiki na kuufanya kuwa endelevu.

**(f) Tathimini ya Utendaji wa Tume ya Utumishi wa Umma;**

**Mheshimiwa Spika,** Tume hii ni chombo muhimu ambacho kinatekeleza jukumu la urekebu katika Utumishi wa Umma. Hupokea na kushughulikia rufaa na malalamiko ya Watumishi wa Umma dhidi mamlaka zao za nidhamu. Aidha, Tume hii ina dhamana ya kusimamia uendeshaji wa raslimali watu katika

Utumishi wa Umma, kwa lengo la kuhakikisha unazingatia sheria, kanuni na taratibu za Utumishi wa Umma.

Kamati inatambua na kukiri kwamba, uwepo wa Tume hii ni muhimu sana hasa kwa maendeleo na mustakabali wa Utumishi wa Umma nchini. Hata hivyo, Tume hii inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na ukosefu wa Ofisi, uhaba wa vitendea kazi na ufinyu wa Bajeti, na hivyo kuathiri utendaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza kwamba, ni muhimu kuwa na chombo madhubuti kitakachosimamia na kuhimiza uzingatiaji wa maadili katika Utumishi wa Umma. Ni kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaiwezesha Tume hii kwa kuipatia vifaa na fedha ili iweze kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa kikamilifu. Kukiacha chombo hiki muhimu bila uwezo wa kujiendesha, ni sawa na kuweka rehani maadili katika Utumishi wa Umma.

### (g) Utawala Bora na uzingatiaji wa Sheria nchini

**Mheshimiwa Spika,** utawala bora ni moja ya nguzo muhimu katika ujenzi wa jamii yenye umoja, usawa, mshikamano, uadilifu na uwajibikaji. Ili kutekeleza dhana hii kikamilifu, ni lazima uwepo utawala wa kisheria unaozingatia misingi ya demokrasia pamoja na haki za binadamu. Nchi yetu kama Taifa linalofuata Demokrasia, inaendeshwa kwa kuzingatia utawala wa sheria kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Katika siku za karibuni, jamii imeshuhudia baadhi ya Watendaji wa Serikali wakichukua nafasi ya muhimili wa Mahakama, kwa kuhukumu na kuwatia hatiani moja kwa moja baadhi ya Watumishi wa Umma bila kujua kwamba, wanakiuka misingi ya Katiba waliyoapa kuilinda. Ibara ya 13(6)(2) ya Katiba inazuia mtu anaeshitakiwa kwa kosa la jinai, kutendewa kama mwenye kosa hilo hadi itakapothibitishwa na Mahakama yenye mamlaka.

Hatua ya Mkurugenzi wa Hamlmashauri kumuamuru Mwalimu wa Sekondari adeki darasa mbele ya Wanafunzi wake ati kwa sababu ni chafu, au Mkuu wa Mkoa kutumia lugha zisizo na staha katika hadhara kwa kuita Watumishi kuwa ni wezi, wajinga, wasiokuwa na akili timamu "hawa ndio vichaa tunaohangaika nao" ni kudhalilisha utu wa mtu na kuvunja misingi ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya wametumia vibaya mamlaka waliyopewa, kwa kuamrisha Watumishi wa Umma kuwekwa ndani, kwa makosa ambayo hayastahiki adhabu hiyo. Ipo mifano

kadhaa ikiwa ni pamoja na Mkuu wa Mkoa mmojawapo nchini aliyeamuru Daktari wa Mkoa awekwe rumande kwa sababu hakutangaza kuwepo kwa Ugonjwa wa Kipindupindu; Mkuu wa Wilaya mojawapo Jijini Dar es Salaam, aliyeamuru Watumishi waliochelewa kufika kazini wawekwe ndani, na Mkuu wa Wilaya mojawapo Mkoani Arusha, aliyeamuru Mwandishi wa Habari wa Kituo kimoja cha Televisheni nchini awekwe ndani kwa kuandika habari kuhusiana na kero ya ukosefu wa maji, ambayo Mkuu huyo wa Wilaya aliitafsiri kuwa ni uchochezi.

Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 1997 (The Regional Administration Act), Sura ya 97; kupitia vifungu vya 7 (1) and 15 (1) imeweka masharti muhimu kwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ikiwa atahitaji kutumia mamlaka ya kuamrisha mtu akamatwe. Vifungu hivyo vinaeleza kwamba, atafanya hivyo pale tu ambapo atakuwa amejihakikishia kuwa kosa lililotendwa na mhusika athari yake huwa ni kukamatwa na kushtakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua na kuthamini juhudi za Serikali za kurejesha nidhamu ya uwajibikaji katika Utumishi wa Umma, hivyo katika hali na mazingira ya aina yoyote ile, kamwe haiwezi kutetea Watumishi wazembe na wasiotekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Hata hivyo, ingependa kuona Watumishi wa aina hiyo, wakichukuliwa hatua za kinidhamu na kiuwajibikaji kwa mujibu wa taratibu zilizopo **(Kanuni za Utumishi wa Umma, 2014**).

Aidha, nitumie fursa hii kuwakumbusha viongozi wote ikiwa ni pamoja na sisi Wabunge kwamba, dhamana ya uongozi tuliyonayo tunapaswa kuitekeleza kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo na Taratibu zilizopo. Kinyume na hapo tutakuwa tumeshindwa kutimiza wajibu wa kuwa mfano kwa wale tunaowaongoza.

### (h) Tathmini ya Utendaji wa Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA)

**Mheshimiwa Spika,** Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni muhimu sana katika Ulimwengu huu wa Sayansi na Teknolojia. Serikali za Mataifa yaliyoendelea na baadhi katika Mataifa yanayoendelea, zimetambua umuhimu wa TEHAMA katika kuimarisha misingi ya uwazi katika utendaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Ni kutokana na umuhimu wake Waziri Mkuu wa India, **Nalendra Modi**, anaamini kwamba; ***"Transparency is the key to good governency, and e – governance is the only effective way of transparent governance"***

Kwa tafsiri isiyo rasmi anachosema Modi ni kwamba; **"Uwazi ni ufunguo wa utawala bora, na utawala mtandao ndiyo njia mwafaka ya utawala wa wazi"**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu huo, Serikali ilianzisha rasmi Wakala wa Serikali Mtandao (e-Government Agency) Mwaka 2012 na kuipa majukumu ya kuratibu, kusimamia na kukuza utekelezaji wa Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma kwa lengo la kuhakikisha zinatumia TEHAMA ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi kwa haraka na ubora.

Katika kipindi cha miaka minne tangu kuanzishwa kwake, e-GA imeonesha mafanikio makubwa, ambayo ni pamoja na kupunguza gharama za uwekezaji na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA. Hatua hiyo, imeokoa fedha nyingi ambazo Serikali ingelipa kwa Wakandarasi ili kupata leseni za kuendesha na kutumia mifumo hiyo.

**Kwa mfano;** katika kipindi hicho e-GA imeweza kuokoa takribani **Tsh. Bilioni 4.7** kwa kusanifu na kutengeneza Mifumo Mitano kwa gharama ya **Tsh. Milioni 560.6,** wakati thamani halisi ya mifumo hiyo kwa bei ya soko ilikuwa **Tsh. Bilioni 5.2**

Aidha, Wakala umeweza kuziunganisha Taasisi nyingi za Umma katika Mifumo Sita (6) ambayo imesanifiwa na kutengenezwa na Wakala hiyo. Mfano ni Mfumo wa Mawasiliano kwa Njia ya Barua Pepe (Government Mailing System - GSM) ambapo **Taasisi 166** zimeunganishwa; na Mfumo wa Huduma kwa Wateja (Help Desk System) ambapo **Taasisi 142** zimeunganishwa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Wakala inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo ya uhaba wa Watumishi. Kwa sasa Wakala ina Watumishi 94 tu kati ya 326 wanaohitajika. Hali hii inasababisha mazingira magumu ya kazi, na kama si uzalendo wa Watumishi waliopo basi wangeweza kuchukuliwa na Taasisi na Makampuni binafsi yenye mazingira mazuri zaidi ya kazi.

Aidha, hakuna Sera, Sheria na mfumo mahususi wa kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao hapa nchini, jambo linalosababisha Wakala na Taasisi za Serikali, kukosa nguvu ya kisheria ya kusimamia shughuli za TEHAMA kwa ufanisi unaohitajika.

### (i) Mgogoro wa Kiuongozi katika la Shirika la Elimu Kibaha (SEK)

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 21 Oktoba, 2016 Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, ilitembelea Shirika la Elimu Kibaha, Mkoani Pwani. Katika ziara hiyo Kamati ilikutana na Watendaji na Wafanyakazi wa Shirika la Elimu Kibaha (SEK), na kutembelea uwekezaji wa Kampuni ya Organia Ltd. Kampuni hiyo imekodisha eneo la SEK kwa ajili ya uzalishaji wa Vifaranga wa Kuku wa Nyama na Mayai.

Wakati wa ziara Wajumbe walipata malalamiko ya Watumishi wa SEK kuhusiana na uongozi mbovu katika Taasisi hiyo. Watumishi hao walidai kwamba, Mkurugenzi amekuwa akiongoza kwa ubabe, kuna ufujaji wa mali za Shirika, na hakuna ushirikishwaji katika maamuzi ya msingi ya Shirika. Aidha, kumekuwa na ukiukwaji wa taratibu na Kanuni za Mikataba, jambo ambalo limesababisha SEK kuingia katika uwekezaji ambao hauna tija kwa Shirika na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanikiwa kupata nakala za baadhi ya Mikataba ya ukodishaji wa maeneo ambayo Shirika la Elimu Kibaha, limeingia na Kampuni ya Organia Ltd. Kupitia Mikataba hiyo Kamati imebaini kiwango kidogo cha gharama ya ukodishaji (*rent*) wa eneo la **Plot. No. 22** lenye ukubwa wa **Hekta 105.084**. Eneo hilo limekodishwa kwa kipindi cha miaka 33 kwa malipo ya pamoja ya **Dola za Marekani 21,016.8.** Hii ni sawa na Hekta moja kukodishwa kwa Dola za Marekani 200 katika kipindi chote cha miaka 33 (Dola za Marekani 6.06 kwa Mwaka kwa Hekta moja).

Mkataba mwingine ni ukodishaji wa eneo la **Hekta 87.23** lenye Mradi wa kuzalisha Kuku wa Nyama na Mayai, uliokuwa chini ya Shirika la Elimu Kibaha. Eneo na mali hizo vimekodishwa kwa kipindi cha **miaka 25** kwa thamani ya **Dola za Marekani 60,000** tu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaelewa Ofisi ya Rais – TAMISEMI inafahamu jambo hili, na imechukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kuiandikia Mamlaka ya Uteuzi na kupendekeza hatua za kuchukuliwa dhidi ya Mkurugenzi wa SEK. Hata hivyo, inapenda kutahadharisha kwamba, jambo hili ni la muda mrefu, na kadri linavyoachwa bila kuchukuliwa hatua, linatoa mwanya wa mgogoro wa Watumishi kuendelea, pamoja na mali za SEK kuendelea kufujwa.

Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Bunge liitake Serikali kuchukua hatua za haraka kuhusiana na mgogoro wa kiuongozi uliopo, ikiwa ni pamoja na Mkurugenzi kukaa pembeni ili kupisha uchunguzi wa kina. Aidha, Mikataba

ambayo SEK imeingia na Mwekezaji (Kampuni ya Organia) ipitiwe upya ili kujiridisha iwapo ina tija kwa Shirika hilo na Serikali kwa ujumla.

### (j) Mfuko wa Pensheni wa LAPF

**Mheshimiwa Spika,** LAPF ni miongoni mwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo inafanya vizuri nchini. Mfuko huu una historia ndefu sana tangu Mwaka 1944, wakati wa Serikali ya kikoloni ya Tanganyika ambapo ulihudumia Wafanyakazi wa ngazi ya chini kama vile Maakida na Makarani kwa kuwawekea akiba. Mfuko huo uliendelea na maboresho hadi sasa ambapo unahudumia Watumishi wa Umma na Sekta Binafsi

Mfuko huu umekuwa ukijiendesha kiushindani jambo ambalo limeufanya ukue na kuongeza Wanachama kila mwaka. Kwa mfano; katika kipindi cha miaka mitatu 2014, 2015 na 2016 idadi ya Wanachama iliongezeka kwa wastani wa Asilimia 15.41. Hadi kufikia Juni, 2016, Mfuko ulikuwa na jumla ya Wanachama **166,220.** Vilevile, katika kipindi hicho uwezo wa Mfuko kukusanya michango uliongezeka kwa wastani wa asilimia 32.8 kutoka **shilingi bilioni 159.22** Mwaka 2014/15 hadi kufikia **shilingi bilioni 279.1** katika Mwaka 2015/16.

Aidha, katika kipindi hicho LAPF ilitekeleza jukumu lake la msingi ambalo ni kulipa mafao kwa Wanachama wake, ambapo Mfuko ulilipa mafao kwa Wanachama 19,648 yenye thamani ya **shilingi bilioni 274.49.**

**Mheshimiwa Spika, k**wa upande wa uwekezaji hadi Juni, 2016 LAPF ilikuwa imewekeza jumla ya **shilingi trilioni 1.13**, katika Vitega Uchumi mbalimbali, huku asilimia 44 ya uwekezaji huo ikilelezwa katika Dhamana za Serikali. Kamati ilivutiwa na uwekezaji wa LAPF unaotekelezwa kwa ubia na Manispaa ya Morogoro, katika ujenzi wa Stendi ya Mabasi ya Kisasa katika eneo la Msamvu. Mradi huu ambao umegharimu **shilingi bilioni 24** ulikamilika Oktoba, 2016 na sasa kituo hicho kinatumika.

Kamati inashauri Mfuko kuangalia uwezekano wa kupanua uwekezaji wa aina hiyo katika Halmashauri nyingine nchini, ili kusaidia kuboresha mazingira ya huduma za Usafiri kwa Wananchi, kwani miradi ya aina hiyo inagusa moja kwa moja Wananchi wa maeneo husika.

Miradi mingine ambayo Mfuko umewekeza na ambayo inagusa jamii moja kwa moja, ni pamoja na jengo la Bunge Dodoma, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, na Chuo Kikuu cha Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua juu ya mchakato wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kuangalia uwezekano wa kuwekeza katika sekta ya Viwanda, ikiwa ni mwitikio wa ushauri wa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. Wazo hilo ni zuri, hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inasimamia kikamilifu uwekezaji unaotekelezwa na Mifuko ya Hifadhi nchini, kwa kutumia fedha za wanachama kwa lengo la kuhakikisha zinakuwa salama.

**(k) Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART)**

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 25 Januari, 2017 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, alizindua rasmi Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART), na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya Tatu kutekeleza mradi wa aina hii Barani Afrika, baada ya Afrika Kusini na Morocco.

Mradi huu umelenga kupunguza au kutatua kabisa kero za usafiri Jijini Dar es Salaam, ambazo zinasababishwa na; ongezeko kubwa la idadi ya Wakazi, kupanuka haraka kwa Jiji, uchakavu na upungufu wa Miundombinu iliyopo, pamoja na kukosa ubora kwa huduma ya usafiri ambayo inatolewa na Sekta binafsi kwa muda mrefu.

Mradi huu utatekelezwa kwa Awamu Sita (6) ambapo barabara zenye jumla ya kilomita 130.3 zitajengwa kwenye njia kuu zote za Jiji la Dar es Salaam, ambazo ni Morogoro, Kilwa, Nyerere, Alli Hassan Mwinyi na Bagamoyo. Awamu ya Kwanza ya mradi imekamilika ikiwa na barabara zenye urefu wa Kilomita 20.9.

**Mheshimiwa Spika,** huduma ya Mabasi yaendayo Haraka ilianza kutolewa tarehe 10 Mei, 2016 ambapo inakadiriwa Wananchi kati ya 120,000 hadi 150,000 wanatumia huduma hii kwa siku. Kuanza kwa mradi huu ni sehemu ya mafanikio ambayo Kamati inajivunia kwani Wajumbe walikuwa bega kwa bega na Serikali katika kuhakikisha mradi huu unaanza.

Kuanza kwa huduma hii kumekuwa na mafanikio kadhaa kwa Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na; kupunguza msongamano wa Magari barabarani, kupunguza gharama za usafiri hasa kwa matumizi ya gari binafsi, kutoa ajira kwa zaidi ya watu 900; fursa za kibiashara kama vile maegesho ya magari na mazingira rafiki kwa Walemavu, Wazee na Wanafunzi.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mafanikio hayo, Mradi umekuwa ukikabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo Wafanyabiashara Ndogondogo (Wamachinga) kuendesha biashara zao katika barabara na vituo vya Mabasi; na Watumiaji wengine wa barabara kutoheshimu miundombinu ya DART. Mfano; ni waendesha Pikipiki, Baiskeli, Magari na hasa Daladala ambao wamekuwa wakivamia barabara za DART, jambo ambalo mara nyingine limekuwa likisababisha ajali.

Vilevile, kwa kutambua umuhimu wa mradi huu na changamoto za usafiri katika maeneo ya jiji yaliyobaki, Kamati inashauri Serikali kuongeza jitihada katika kutekelezaji Awamu Tano zilizosalia ili kuwezesha Wakazi wa maeneo mengine ya Dar es Salaam kunufaika na huduma hii ya usafiri. Aidha, utekelezaji wa mradi huu una manufaa makubwa kwa ustawi wa jiji la Dar es Salaam na Taifa kwa ujumla kwani shughuli za kiuchumi katika jijini hili, zina mchango wa moja kwa moja katika uchumi wa Taifa letu.

**SEHEMU YA TATU**

## 4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 4.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusiana na shughuli ilizotekeleza katika kipindi chote cha mwaka mmoja, ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake. Maoni hayo ni haya yafuatayo:-

**(a) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;**

**i. Mheshimiwa Spika,** hatua za Serikali kuimarisha utendaji wa TAKUKURU, zimeanza kuonesha mafanikio, kwani Taasisi hiyo imeanza kuchukua hatua dhidi ya Watuhumiwa wa rushwa, na imeanzisha Kitengo cha Ufuatiliaji na Urejeshaji wa Fedha/Mali za Umma kutoka kwa Watuhumiwa (***Asset Tracing and Recovery).*** Aidha, **i**ko katika mchakato wa kuanzisha Maabara ya Utambuzi ***(Forensic Laboratory)*** ili kusaidia kuongeza ufanisi wa kiutendaji.

ii. Kushindwa kwa baadhi ya Halmashauri nchini kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Mpango wa TASAF wa Kunusuru Kaya Maskini, umesababisha baadhi ya Kaya zisizo na sifa kunufaika na mpango huo.

iii. Hatua ya TASAF kuhakiki na kubaini Kaya 55,692 zisizo na sifa ambazo zilikuwa zinanufaika na Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini na

kuziondoa katika utaratibu huo, imeokoa fedha nyingi ambazo zilikuwa hazifiki kwa walengwa. Aidha, hatua hiyo itatoa fursa kwa Kaya maskini zilizokuwa nje ya Mpango kuanza kunufaika.

iv. Ufinyu wa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, pamoja na mapungufu ya kisheria, vinaathiri utendaji wa Taasisi hiyo na hivyo kuzorotesha ufuatiliaji wa zoezi la ujazaji wa Fomu za maadili kwa Viongozi wa Umma;

v. Kukamilika kwa Ofisi ya Ushauri wa Mafuta na Gesi, kutaiwezesha kutoa ushauri wa kitaalam kwa Serikali juu ya kuzingatia Utawala Bora katika usimamizi wa raslimali za Gesi na Mafuta nchini;

vi. Kukosekana kwa Mfumo Shirikishi na endelevu wa Uhakiki wa Taarifa za Watumishi wa Umma, kumesababisha kuwepo kwa kundi la Watumishi hewa, pamoja kuchangia ongezeko la vitendo vya ubadhilifu na rushwa;

vii. Hatua ya baadhi ya Watendaji wa Serikali kutozingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zilizopo katika utendaji wao, kunatia doa uzingatiwaji wa dhana ya utawala bora nchini;

viii. Ukosefu wa Sheria mahususi inayosimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao (e-GA) unazinyima Taasisi za Serikali nguvu ya kusimamia shughuli za TEHAMA katika utendaji wa kiufanisi unaohitajika.

**(b) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;**

i. Kuchelewa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo katika robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha, kumeathiri utekelezaji wa Miradi mingi ya maendeleo;

ii. Kukosekana kwa sheria inayosimamia Agizo la kuzitaka Halmashauri nchini kutenga Asilimia Kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa ajili ya kusaidia Vijana na Wanawake, kumesababisha utekelezaji wa agizo hilo kusuasua;

iii. Uchache na ubovu wa miundombinu muhimu ya kielimu, kama vile Vyumba vya Madarasa, Ofisi za Walimu, Matundu ya Vyoo na Nyumba za Walimu, unaathiri jitihada za Serikali za kutoa elimu bora na bila malipo;

iv. Mfuko wa Pensheni wa LAPF, uongeze uwekezaji katika miradi yenye uhitaji mkubwa katika jamii na ambayo inagusa Wananchi moja kwa moja. Mfano; ni ujenzi wa Vituo vya Mabasi ambao LAPF imeanza kutekeleza kwa ushirikiano na Halmashauri za Manispaa nchini;

v. Mgogoro wa kiuongozi katika Shirika la Elimu Kibaha (SEK), umekuwa na athari za kiutendaji, ufujaji wa mali za Shirika na uwekezaji usio na tija kwa Shirika;

vi. Hatua ya Serikali kuondoa ukusanyaji wa Kodi ya Majengo (*propert tax)* katika Halmashauri nchini, kumepunguza kwa kiasi kikubwa mapato ya Halmashauri na hivyo kuathiri utendaji wake;

vii. Matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato yamesaidia Halmashauri nyingi nchini kuongeza mapato na kuziba mianya ya upotevu kwa njia ya rushwa na ubadhilifu;

viii. Kusuasua kwa fedha za bajeti zilizotengwa kwa ajili ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), kumeathiri utendaji wa chombo hicho ikiwa ni pamoja na kushindwa kufungua ofisi katika Wilaya nchini kwa lengo la kufikisha huduma kwa Walimu;

ix. Kuanza kwa huduma ya usafiri ya Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART), kumesaidia kupunguza adha ya usafiri kwa Wakazi wa Dar es Salaam;

## 4.2 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kuanisha maoni ya Kamati, naomba sasa nijielekeze katika mapendekezo ya Kamati ambayo yamezingatia kwa sehemu kubwa matokeo ya uchambuzi wa shughuli zilizotekelezwa katika kipindi chote cha mwaka mmoja, kama ifuatavyo:-

### *4.2.1 Utendaji wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) na hali ya rushwa nchini;*

**KWA KUWA,** hatua zinazochukuliwa na Serikali ili kuimarisha utendaji wa TAKUKURU zimeanza kuonesha matunda kwa kupunguza vitendo vya rushwa nchini;

**NA KWA KUWA,** Taasisi hiyo imeongeza uchunguzi, kuchukua hatua dhidi ya Watuhumiwa wa rushwa na kuokoa fedha za Umma kwa kutumia Kitengo

cha Ufuatiliaji na Urejeshaji wa Fedha/Mali za Umma kutoka kwa Watuhumiwa (***Asset Tracing and Recovery);***

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza Serikali iendelee kuiwezesha TAKUKURU kuimarisha utendaji wake ikiwa ni pamoja na kukamilisha mchakato wa kuanzisha Maabara ya Utambuzi ***(Forensic Laboratory)*** ili kusaidia kuongeza ufanisi wa kiuchunguzi.

### *4.2.2 Maboresho ya Mpango wa TASAF wa kunusuru Kaya Maskini nchini;*

**KWA KUWA,** Mpango wa TASAF wa Kunusuru Kaya maskini nchini umeonesha mafanikio makubwa, licha ya kasoro kadhaa zinatokana na baadhi ya Watendaji wa Halmashauri wanaohusika kukosa uwazi na uadilifu katika uwajibikaji wao;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo imesababisha uhakiki uliofanywa na TASAF Mwaka 2016 kubaini jumla ya Kaya **55,692** ambazo zilikuwa zinanufaika na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini bila kuwa na sifa stahiki; **KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kuimarisha uwezo wa Halmashauri katika kusimamia miradi ya TASAF ili itekelezwe kikamilifu na ufanisi. Aidha, iimarishe mifumo ya kuwatambua Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ili kuzuia Kaya zisizo na sifa kunufaika.

### *4.2.3 Tathmini ya ujazaji wa Fomu za Maadili ya Viongozi wa Umma;*

**KWA KUWA,** Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi nchini inashindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu kutokana na ufinyu wa bajeti;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo imeathiri zoezi la kutembelea Viongozi wa Umma waliojaza Fomu za Maadili kwa lengo la kukagua ili kujiridhisha iwapo walitoa taarifa sahihi;

**KWA HIVYO BASI;** Kamati inashauri Bunge liitake Serikali kuiwezesha Sekretarieti hii kifedha ili iweze kusimamia kikamilifu masharti ya Sheria ya Maadili kwa Viongozi wa Umma.

#### *4.2.4 Ofisi ya Rais ya Ushauri wa Mafuta na Gesi*

**KWA KUWA,** Sekta ya Mafuta na Gesi ni mpya nchini na uvunaji wa raslimali hizo ndiyo utachangia kwa sehemu kubwa kuiwezesha nchi yetu kuingia katika Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025;

**NA KWA KUWA,** Wananchi hawana elimu ya kutosha kuhusiana na uvunaji na usimamizi wa raslimali hizo, jambo ambalo limefanya wawe na mashaka kwamba, huenda raslimali hizo zisinufaishe kikamilifu Taifa kama ilivyo kwa Sekta ya madini;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali ikamilishe Muundo wa Ofisi ya Rais ya Ushauri wa Mafuta na Gesi, ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu ambayo ni pamoja na kutoa elimu na taarifa kwa Wananchi kwa kila hatua inayoendelea katika utafiti wa Mafuta na uzalishaji wa Gesi Asilia. Aidha, Ofisi hii inatarajiwa kutoa ushauri wa kitaalam wa namna utawala bora unavyoweza kuifanya Serikali isimamie raslimali hizi kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Taifa letu na kunufaisha vizazi vya sasa na vijavyo.

#### *4.2.5 Ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Serikali;*

**KWA KUWA,** Kamati ilibaini kwamba, Taasisi na Idara nyingi za Ofisi ya Rais, hazina majengo ya ofisi na hivyo kulazimika kupanga kwa Watu binafsi au Taasisi nyingine za Umma kwa gharama kubwa, au kuwa katika majengo yasiyoendana na hadhi ya Ofisi hizo;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo imesababisha Taasisi na Idara hizo kutumia gharama kubwa kwa ajili ya kodi ya pango, fedha ambazo zingeweza kuchangia katika ujenzi wa majengo ya Serikali, yatakayokuwa na hadhi;

**KWA HIYO, BASI,** Kamati inaishauri Serikali kuzisaidia Taasisi na Idara hizo kupata majengo yake, ili kuepusha gharama kubwa zinazotumika kulipa kodi ya pango, na pia kuziwezesha kuwa na ofisi zenye hadhi. Aidha, ni vyema Serikali ikatumia fursa ya Mpango wa kuhamia Dodoma, kutafuta maeneo na kuzijengea Taasisi hizo majengo yake.

#### *4.2.6 Halmashauri kutenga Asilimia Kumi (10%) ya mapato ya Ndani kwa ajili ya kuwezesha Vijana na Wanawake*

**KWA KUWA,** Halmashauri nyingi zimebainika kutotenga kikamilifu Asilimia Kumi (10) ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi Vijana na Wanawake;

**NA KWA KUWA,** hatua hiyo inachangia Vijana na Wanawake waendelee kukosa mitaji na uwezo wa kutekeleza shughuli zao za kiuchumi ili waweze kujikwamua na umaskini;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza Bunge lako Tukufu kuitaka Serikali kuandaa na kuwasilisha Bungeni, Muswada wa Sheria ambao utaweka masharti ya usimamizi wa agizo hilo, ili Vijana na Wanawake waweze kunufaika na utaratibu huo na hivyo kujikwamua kiuchumi.

#### *4.2.7 Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC);*

**KWA KUWA,** Tume ya Utumishi wa Walimu imeanza kazi kwa kusuasua kutokana na uhaba wa fedha za bajeti iliyotengwa katika mwaka huu wa fedha, na mapungufu katika sheria iliyoianzisha;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inasababisha Tume hiyo kushindwa kushughulikia kikamilifu changamoto zinazowakabili Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini na kusababisha kuendelea kuporomoka kwa elimu nchini,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali kuipatia Tume fedha za kutosha na kuifanyia marekebisho Sheria iliyoianzisha ili kuondoa kasoro zilizopo na hivyo kuiwezesha kushughulikia kero za Walimu, ili waweze kutimiza majukumu yao katika mazingira mazuri.

#### *4.2.8 Utoaji wa Elimu bila Malipo;*

**KWA KUWA,** Mpango wa Serikali wa kutoa elimu ya Msingi hadi Kidato cha Nne bila malipo, umewezesha kuwepo na ongezeko kubwa la Wanafunzi;

**NA KWA KUWA,** ongezeko hilo limezalisha changamoto za utoaji wa elimu bora kutokana na upungufu wa Miundombinu ya Kielimu kama vile Madarasa, Nyumba za Walimu, Matundu ya Vyoo, pamoja na upungufu wa Walimu;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kutafutia ufumbuzi changamoto hizo, ikiwa ni pamoja na kuajiri Walimu zaidi, kulipa madeni na kuboresha maslahi kwa waliopo, ili kunusuru kiwango cha elimu kisiendelee kuporomoka.

#### *4.2.9 Mgogoro wa Kiungozi katika Shirika la Elimu Kibaha (SEK)*

**KWA KUWA,** imebainika uwepo kwa Mgogoro wa Kiuongozi katika Shirika la Elimu Kibaha, unaodaiwa kusababishwa na Mkurugenzi Mkuu,

**NA KWA KUWA,** mgogoro huo umesababisha hali ya kutoelewana baina ya Watumishi na uongozi wa shirika, na hivyo kuzorotesha utendaji wa Shirika kiasi cha kuathiri utekelezaji wa malengo ya kuanzishwa kwa Shirika hilo;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri Serikali kupitia mamlaka ya uteuzi kushughulikia mgogoro huo kwa kumsimamisha Mkurugenzi ili apishe uchunguzi, kuchunguza na kuchukua hatua stahiki kwa kasoro zitakazobainika. Aidha, Serikali ipitie upya Mikataba ya uwekezaji ambayo Shirika limeingia na Kampuni ya Organia, ili kuona iwapo ina tija kwa Shirika na Taifa kwa ujumla.

#### *4.2.10 Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART)*

**KWA KUWA,** Awamu ya kwanza ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART), ilianza kutoa huduma ya usafiri mwezi Mei, 2016 kwa Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, na kuzinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 25 Januari, 2017;

**NA KWA KUWA,** huduma hiyo ya usafiri wa DART imeonesha mafanikio makubwa kwa kupunguza adha ya usafiri iliyokuwa ikiwakabili Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza Serikali iharakishe utekelezaji wa Awamu za mradi zilizosalia ili kuendelea kuboresha huduma ya usafiri kwa Wakazi wa jiji la Dar es Salaa. Aidha, ni dhahiri shahiri kwamba, mradi huo utakapokamilika utasaidia kuondoa au kupunguza kwa kiwango kikubwa kero ya foleni katika jiji la Dar es Salaam.

#### *4.2.11 Ufinyu wa Bajeti ya Matumizi Mengineyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;*

**KWA KUWA,** kwa kuwa imebainika kuwepo wa ufinyu wa bajeti ya Matumizi Mengineyo katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 na fedha kidogo iliyopo imekuwa haipatikani kikamilifu;

**NA KWA KUWA,** ufinyu huo umeathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa majukumu ya kiofisi pamoja na kupunguza motisha kwa Watumishi,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza Serikali iongeze fedha za matumizi ya kawaida, ili kuwezesha Ofisi zake kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, kiasi cha fedha kinachoidhinishwa kwenye bajeti kitolewe kikamilifu na kwa wakati ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

**SEHEMU YA NNE**

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kulithibitishia Bunge lako Tukufu, kwamba Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, itaendelea kutekeleza kikamilifu jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali, kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Lengo ni kuhakikisha, Serikali inatimiza kikamilifu na kwa tija, mipango ya kuwaletea maendeleo Wananchi na Taifa letu kwa ujumla, huku ikizingatia sheria na dhana ya utawala bora.

**Mheshimiwa Spika**, nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Mhe. Angellah Kairuki, (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene, (MB) - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Mhe. Suleiman Jafo, (MB) – Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kushirikiana vyema na Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake. Nikiri kwamba, ushirikiano wao huo uliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu.

Aidha, niwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, wakiongozwa na Ndg. Peter Ilomo - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu, Dkt. Laurean Ndumbaro - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, na Mhandisi Mussa Iyombe - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa namna walivyokuwa tayari wakati wote kuratibu shughuli za Kamati pale ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. Ni matumaini yangu kwamba, wataendelea kuonesha uwajibikaji wa aina hii wakati wote wa utumishi wao, kwa lengo la kuhakikisha Kamati inatoa mchango wake katika ujenzi wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa mchango wao adhimu katika shughuli za Kamati, kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja. Ni dhahiri shahiri kwamba, bila ushirikiano wao Kamati isingeweza kufikia hatua hii ya mafanikio. Kwa heshima kubwa naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, (Mb),
2. Mhe. Dkt. Pudenciana Kikwembe, (Mb),
3. Mhe. George Malima Lubeleje(Mb),
4. Mhe. Mwanne Ismail Mchemba(Mb),
5. Mhe. Ruth Hiyob Mollel(Mb),
6. Mhe. Hamad Salim Maalim(Mb),
7. Mhe. Halima Ali Mohammed(Mb),
8. Mhe. Khamis Ali Vuai(Mb),
9. Mhe. Mwatum Dau Haji(Mb),
10. Mhe. Angelina Adam Malembeka(Mb),
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali(Mb),
12. Mhe. Khalifa Mohammed Issa(Mb)
13. Mhe. Waitara Mwita Mwikwabe (Mb),
14. Mhe. Saada Mkuya Salum (Mb),
15. Mhe. Margaret Simwanza Sitta(Mb),
16. Mhe. Esther Alexander Mahawe(Mb),
17. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate(Mb),
18. Mhe. Zachariah Paulo Issaay (Mb),
19. Mhe. Salum Khamis Salum(Mb),
20. Mhe. Josephine Tabitha Chagula(Mb),
21. Mhe. Venance Methusela Mwamoto(Mb),
22. Mhe. Maida Hamad Abdallah (Mb),
23. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri(Mb),
24. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu(Mb),
25. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa(Mb),
26. Mhe. Saed Kubenea (Mb).

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Watumishi wa Bunge, wakiongozwa na Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa ushirikiano wao kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake. Vilevile, namshukuru Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, na Ndg. Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati, Sehemu ya Mambo ya Jumla, kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Kamati, na hivyo kuiwezesha Kamati kutimiza kazi zake ipasavyo.

Mwisho lakini si kwa umuhimu wake, napenda kuwatambua na kuwashukuru Makatibu wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, Ndg. Chacha Timasi Nyakega, Ndg. Victor Leonard Mhagama na Ndg. Eunike Donati Shirima wakisaidiwa na Ndg. Mariam Ally, ambao wamekuwa msaada mkubwa sana kwa Kamati katika kutekeleza shughuli zake hadi wakati huu inapowasilisha Taarifa yake.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza kwa kina Shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb
**Mwenyekiti**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala**
**na Serikali za Mitaa**
03 Februari, 2017

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza michango yetu; tunaanza na Mheshimiwa Maulid Said Abdallah Mtulia, ajiandae Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Raphael Jafary Michael.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kunijalia uzima. Lakini pili nikushukuru sana Mwenyekiti kwa kuamua kuwa mimi niwe mchangiaji wa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi zangu za dhati kwa Kamati hasa hii Kamati ya Serikali za Mitaa kwa kueleza na kwa kutimiza wajibu wao wa kuishauri Serikali; kueleza mambo kwa kina sana, nawashukuru sana muwasilishaji na wanakamati kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Kamati ya Katiba na Sheria. Katika Wizara yetu ya dada yangu pale anayeshughulikia ajira na walemavu; dada Jenista. Ukiangalia Kamati imejikita sana kwenye mambo ya kisheria, lakini mahali pengine kwenye taarifa hawajagusa chochote kwenye suala la vijana na walemavu. Ukiambatanisha vijana, walemavu na ajira maana yake hili ni kundi muhimu sana; vijana ni kundi muhimu ambalo linahitaji ajira na walemavu ni kundi muhimu ambalo linahitaji uwezeshaji. Lakini sijui kutokana na Kamati kuwa na mambo mengi bahati mbaya sana sikuona kwamba suala la ajira limepewa uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme, tuna tatizo kubwa sana la ajira na hasa kwa vijana. Mimi kama mwakilishi wa Jimbo la Mjini, Jimbo la Kinondoni linapambana sana na tatizo la vijana na hasa vijana kukosa ajira. Nilitegemea ama wakati mwingine Kamati itueleze Wizara yetu imefanya jambo gani katika ajira; katika kupitia utekelezaji wa Mpango wa Utekelezaji ndani ya mwaka mzima wa Kamati, ningefurahi sana kama Kamati ingetuonesha. Tuna tatizo kubwa sana la ajira, vijana wetu hawana ajira, Serikali lazima ijitahidi ihakikishe inatoa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikiliunganisha hilo la ajira na mikopo ya vijana, kwamba watendaji wetu wa Halmashauri na Serikali za Mitaa hawatoi umuhimu unaostahiki katika ile asilimia kumi ya mapato ya ndani ambayo inatakiwa iende kwa wanawake na vijana. Wakati mwingine wawakilishi tunagombana na watendaji kuonesha kwamba lazima tutenge hizi pesa, lakini wakati mwingine watendaji wanaona kwamba pesa ikibaki ndipo ipelekwe kwenye kundi lile la asilimia 10 ya wanawake na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe na niishauri Serikali na nikubaliane na Kamati utengenezwe utaratibu au waraka maalum wa kuwasisitiza watendaji wote wa Halmashauri kwamba suala la asilimia kumi si hisani ni suala la sheria; kwamba Halmashauri zote zitenge asilimia kumi; kiwe ni kipaumbele na isiwe mpaka matatizo au bajeti inapoonekana inaruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la TAMISEMI napenda kutoa ushauri kwa Serikali. Suala la TAMISEMI kuwa chini ya Ofisi ya Rais sisi wananchi bado halijatunufaisha na nadhani ni busara sasa kama Mheshimiwa Rais ataiona ni vizuri hii TAMISEMI ikarudishwa tena kwa Waziri Mkuu, ili Waziri Mkuu aweze kulisimamia. Kwa sababu kwa mtazamo wangu naamini Mheshimiwa Rais ana majukumu mengi sana na hili jambo linahusu Halmashauri na Manispaa zetu, hivyo Mheshimiwa Rais abaki katika kujikita kwenye kusimamia

Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zisimamiwe na Waziri Mkuu. Huu ni ushauri ambao naamini mtani wangu ataupokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, leo Makao Makuu yamehamia Dodoma, Dar es Salaam tunabaki kama jiji. Serikali ifike mahali sasa itambue kwamba ina wajibu wa kuyajenga majiji. Tuna Jiji la Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, na Mbeya. Haya ni majiji, ukiachilia mbali Tanga na mengineyo, ni majiji ambayo Serikali lazima ije na mpango wa kuhakikisha majiji haya yanakuwa ni majiji kweli yanafanana na majiji mengine na hasa ukizingatia kwa sisi watu wa Dar es Salaam baada ya Serikali kuhama yote tutabaki sisi kama sisi watu wa Jiji la Dar es Salaam na tunatakiwa tujengewe uwezo wa kutosha ili kuhakikisha Jiji letu la Dar es Salaam ambalo ndilo jiji kubwa kuliko majiji yote liwe ni jiji la mfano katika *East Africa.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la utawala bora. Tuna tatizo la utawala bora. Kamati imesema vizuri sana na mimi naipongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tukianza kwenye uzinduzi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi, Mheshimiwa Rais alisema magari yote ambayo sio ya mwendo kasi yanayopita katika njia ya mwendokasi yakikamatwa yang'olewe matairi. Mheshimiwa Rais mtani wangu, mimi najua Kiswahili yeye hajui na mara nyingi anapenda kutumia Kiswahili kwa lugha ya picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kwamba kwa kusema magari yang'olewe matairi nilivyomfahamu mimi, kwa kuwa hajui Kiswahili, nilitegemea kwamba anaonesha ni tatizo gari zisipite na gari itakayopita ikamatwe ipelekwe kwenye vyombo vya sheria, ipewe hukumu kali kwa mujibu wa sheria. Si kwamba wang'oe matairi kama walivyong'oa. Kwa sababu hata akisema mtu anatumbua naamini huwa anatumia lugha ya picha, hatumbui kwa maana ya kutumbua, anamwajibisha mtu aliyefanya makosa kwa kutokufuata taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inakuaje leo vyombo vya dola, polisi wanashindwa kumfahamu Mheshimiwa Rais kwamba ana matatizo ya kutofahamu vizuri Kiswahili badala yake wanawakamata mapikipiki wanayang'oa matairi kisha wanawapeleka mahakamani, sasa huyu mtu umeshang'oa matairi umemuadhibu, unampeleka mahakamani kwenda kufanya nini? Jeshi la Polisi lazima lielewe lugha ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipoambiwa kule njaa, aliwaambia mimi niwapikie, alikuwa na maana kwamba hii njaa ya Tanzania kila mtu atimize wajibu wake kuhakikisha anaepukana na njaa. Niwaombe watu wa Jeshi la

Polisi wamwelewe sana mtani wangu huyu kwamba hakukusudia wang'oe matairi ya watu na wale vijana waliong'olewa matairi yao warudishiwe. Mahakama ndiyo yenye uwezo wa kumtia mtu hatiani, si Jeshi la Polisi wala si tamko la Mheshimiwa Rais ambalo watu hawakulielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Kinondoni tuna tatizo na wakati mwingine ndiyo maana hatupendi sana Mheshimiwa Rais kuwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara, ajiandae Mheshimiwa Raphael Jafary Michael.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niseme tu kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa hiyo naunga mkono maoni yote ambayo yamewasilishwa na Kamati yangu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa ya kushiriki Kamati kwenye ziara na kuangalia miradi na kwenye mawasilisho mbalimbali ambayo yalifanyika kwenye Kamati yetu, yapo maeneo muhimu ambayo nataka kuchangia hapa. Jambo la kwanza; tulizungumza hii Kamati inahusika na mambo ya utawala na tukaangalia eneo la kero kwa wananchi, rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa imekuwa ni kubwa ingawa upande wa Serikali ukizungumza nao watakwambia rushwa imepungua kwelikweli, si kweli. Jambo hili limechagizwa sana na kauli ya Mheshimiwa Rais kwamba maaskari wanaruhusiwa kuchukua rushwa ndogondogo, 5,000 hela ya sabuni na kubrashia viatu. Bahati mbaya sana kwa sababu ya hofu na woga uliopo hakuna mtu ambaye alienda *front* kumshauri ama kubadilisha ile kauli na imekuwa ni kero kwa wananchi na hasa vijana wa bodaboda ambao wanajitafutia maisha katika jua kali, wanaombwa sana hizi fedha mnaita ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni maoni yangu kwamba ni muhimu upande wa Serikali wakaliangalia jambo hili upya na ni muhimu kuangalia pia kauli za viongozi wetu na hasa Mheshimiwa Rais. Haiwezekani kiongozi ambaye ameapa kuitii Katiba ya nchi na sheria na kanuni anasimama hadharani bila hofu wala woga anasema askari wakipewa sh. 5,000 ya kiwi ya viatu ni sawasawa kabisa na anasema ni hela ya kiwi, lakini hili jambo limekuwa ni kero

kwa wananchi wetu ambao kimsingi maisha ni magumu na kipato ni kidogo na unapokosa sh. 5,000 inaweza kupelekea hata kung'oa matairi na mambo mengine chungu nzima ambayo yanafanyika, hilo ni eneo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo tuliliona ni eneo la *TASAF*. Mimi ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, kwa hiyo nafahamu vizuri namna ambavyo watu wetu wamepata msaada mkubwa kupitia fedha hizi na ni mpango mzuri pamoja na kwamba zipo changamoto mbalimbali ambazo inabidi zifanyiwe kazi kwa maana ya kuboresha ili hii fedha iendelee kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wapo wananchi wengi sana ambao hawana uwezo na michakato haikuwapitia, wakazikosa. Kwa hiyo, niishauri Serikali, ni muhimu yale maeneo ambayo watu walikuwa wanakidhi vigezo, wana uwezo mdogo na hawakupata zile fedha, basi maeneo hayo yaangaliwe upya ili watu hao waweze kupata msaada wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni kwamba ni muhimu hizi fedha pamoja na kuwapa watu wetu ili kuwasaidia wapo wachache, kama tulipokwenda Zanzibar, Pemba na Unguja ikaonekana baadhi ya maeneo ya Tanzania Bara yamefanya hivyo, wale wazazi wanapewa zile fedha wanatumia wanabakisha kidogo wanaweka miradi midogomidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tuwekeze kwenye miradi midogo midogo kwa sababu mpango huu sio mpango wa miaka yote, maisha yao yote, kama wakijifunza ku-*save* kidogo wanatumia na wakaanzisha miradi midogomidogo hata akili zao zinachangamka katika kujipangia mapato na matumizi yao. Kwa hiyo tungependekeza jambo hili muhimu likachukuliwa kwa uzito. Wawezeshwe fedha lakini pia waelekezwe namna ya kuwekeza kwenye miradi midogo midogo ili iwasaidie huko baadaye. Hata kama fungu hili likiondolewa watakuwa wamejipanga vizuri juu ya namna ya kupata huduma kwa sababu lengo ni kuwasaidia hapa walipo na waweze kujiinua kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wamepata msaada, wengine wamesomesha watoto, wengine wamejenga hata vibanda hata kama ni vibovu lakini imesaidia kwa kweli. Kwa hiyo, ile kauli ambayo inaonekana kwamba kuna taarifa huu mpango haujasaidia; leo wale wazazi ambao hawana uwezo, watu wetu wale, badala ya kwenda kupanga foleni kwa Diwani au kwa Mbunge kuomba hela ndogondogo wanakwenda kupanga foleni kwa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo cha muhimu hapa fedha ni muhimu, ni kuboresha mazingira ambayo yana changamoto mbalimbali na uwazi uwepo, wale wahusika wapewe, hilo ndilo jambo la msingi sana. Mtu ambaye anashauri kwamba hii fedha iondolewe, kwa kweli huyu mtu ni wa kulaani sana, hawatakii mema watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la watumishi hewa. Ni kweli kwamba Serikali imechukua hatua ya kuangalia watumishi hewa, lakini jambo hili linachukua muda mrefu sana. Wapo watu ambao maslahi yao yamezuiliwa kwa sababu ya hoja ya watumishi hewa na hasa ajira mpya kwa vijana wetu. Sasa ni muhimu jambo hili kuwe na *deadline,* kwamba mnafanya kwa muda wa mwezi mmoja, miwili, mitatu au minne, jambo limalizike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watumishi hewa; kwanza watu wanataka kujua nani ni mtumishi hewa ajulikane na hawa ndio wanaotakiwa wawajibishwe; wale waliopokea fedha na wale viongozi ambao ni wa Utumishi waliotengeneza miundombinu ya kupata watumishi hewa, wasiwawajibishe watumishi wasiokuwemo. Kwa sababu kama kuna fedha inalipwa kutoka kwenye akaunti, wale wakubwa wawajibishwe. Hata hivyo, jambo hili liishe ili watu wetu wapate ajira na waweze kutumikia Watanzania kwa ubora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utawala bora. Leo asubuhi nilisikitika sana Mheshimiwa Simbachawene. Kwanza anajua hapa karibuni umetengenezwa mgogoro mkubwa sana Serikali za Mitaa. Lilizuka jambo la mihuri hapa mpaka wenyeviti wenzangu wa mitaa wakafikia hatua ya kuandamana, kuunda Kamati mbalimbali na kuanza kufanya zile kazi. Sasa hapa ni muhimu tukajua, zipo kazi za Wenyeviti wa Mitaa, zielekezwe vizuri. Mtendaji anapoajiriwa anajua kazi zake na Wenyeviti wa Mitaa waelekezwe. Sasa kutujumlisha kwamba wote tunapiga maeneo ya umma si kweli, mimi ni Mwenyekiti wa Mtaa, sina kesi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu maelekezo yaende kwamba kama kuna Mwenyekiti ambaye kwa kweli ametumia nafasi yake vibaya huyo awajibishwe. Wale ambao wamepewa, kwa mfano Mheshimiwa Waziri ukiulizwa tangu uchaguzi umefanyika mwaka 2014 ni mpango gani mmefanya kutoa semina kwa Wenyeviti wa Mitaa, Madiwani na hata watendaji? Mtu amekuja hapa Hombolo kapata mafunzo yake, kapata ajira akifanya makosa sio *fault* yake ni *fault* ya Wizara, kwa hiyo naomba Wizara itimize wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nimesikitika sana leo asubuhi, sisi tunasema Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wanajiita Marais; wewe umeunga mkono hiyo hoja kama ni kweli eti kwa sababu madaraka yanashuka kutoka kwa Mheshimiwa Rais, kwa hiyo nchi hii kila mtu ni Mheshimiwa Rais! Sisi tulichouliza ni kwamba, Wakuu wa Wilaya wanahujumu mpaka Waheshimiwa Wabunge, hatuheshimiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam amefanya ziara Dar es Salaam pale Ukonga, kwa heshima nimetoka nyumbani kwangu nimekwenda kwenye eneo lile, nikakuta, Mkuu wa Mkoa anatukana watumishi kwamba ninyi ni mizigo, ninyi ni misumari. Mwanamke, yule mama wa Kinondoni, ninyi wanawake mnasema hapa wanawake wapewe fursa wafanye kazi! Afisa Utumishi wa Kinondoni Makonda anamwambia wewe ni mzigo, hivi nani amekuweka hapa! Toka hapa potea pale mbele!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa, kwenye *public,* kwenye mkutano wa hadhara, yule mama ameshindwa hata kutembea miguu imekuwa mizito, hayo ndiyo mambo tunayokataa hapa. Mkuu wa Mkoa yupo kwenye mkutano eneo la mgogoro, limeunda Kamati pale, Diwani amefanya kazi yake, Afisa Utumishi amekwenda, Afisa Mipango ya Maendeleo wa eneo lile, Mkuu wa Mkoa anakuja pale kwa sababu ana polisi anamwambia Diwani apate fursa ya kutoa taarifa, mimi hata kusalimia alinizuia, akasema hiki kikao ni cha Mkuu wa Mkoa, halafu tuheshimiane namna gani? Hayo ndiyo mambo ya msingi ya kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani shule zinafelisha; mwaka jana Mkuu wa Mkoa wa Simiyu ameagiza mkoa mzima, eti wakuu wa shule amewatumbua, halafu mnataka matokeo yawe mazuri yataanzia wapi, hatuheshimiani kwenye kazi. Kwa nini Mkuu wa Mkoa asione kuna shida? Tumesoma ile sheria vizuri, kama kuna shida, kama kuna mkuu ninayempongeza sana ni Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, nilimwona kwenye *TV,* naomba mumpigie makofi basi hata huyu amefanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu amekwenda anajadili matokeo ya *form four,* ameita watumishi kwenye idara husika, anasema tulifanya kikao tukasema atakayezembea eneo lake atawajibishwa, anasema naomba idara husika ya elimu iwajibishe wahusika, *simple*. Kwa hiyo, ukishasema hivyo watafanya utafiti, watafanya *enquiry* fulani, itakuja taarifa anayehusika na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mambo ndiyo tunataka yafanyike. Hatutaki watu wazembe ila hatutaki watu waonewe tunataka mtu akiwajibishwa; na Waziri ni Mwanasheria wa eneo hili, wote wawili, Waziri wa Utumishi na Waziri wa TAMISEMI na nawaheshimu sana ndugu zangu, lakini tunataka utaratibu tu. Hivi Mkuu wa Mkoa kweli ni rais kwenye mkoa wake! Ni rais kwenye wilaya yake! Kwa hiyo kuna vitu ambavyo mnadanganya watu hapa, naomba tuheshimu hiki chombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema sisi ni kwamba hatupingi kila kitu, yapo mambo yanafanyika mazuri tunaunga mkono. Tunapiga kelele sana kwa mambo mabaya, kukatisha watu tamaa na matumizi mabaya ya madaraka. Hivi inawezekana Mheshimiwa *DC* amekwenda kwenye mkutano, anamwambia Diwani kamata weka ndani halafu tupige makofi? Ni kiongozi mwenzake halafu anataka ampe ushirikiano, hizo taarifa anazipataje na hao ni watu ambao kwa kweli wameletwa kwenye maeneo yale na kuna mtu amepigiwa kura na watu wake, kwa hiyo mnajenga chuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nkamia amesema hapa leo asubuhi, kwamba inawezekanaje *DC* anatukana wananchi halafu huyu anasema eti ndiyo Rais wa eneo lile… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsant. Mheshimiwa Raphael Michael ajiandae Mheshimiwa Mwalongo.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza na mimi nizipongeze Kamati zote kwa uwasilishaji mzuri, lakini ntajikita kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kidogo suala la asilimia 10 ya vijana na akinamama. Suala hili limekuwa mara nyingi likiongelewa na Waheshimiwa Wabunge wakilalamika kwamba fedha zile hazipatikani katika halmashauri. Kwa hili kidogo nitofautiane na mawazo ya Kamati, kwamba iletwe sheria Bungeni ya kuzilazimisha halmashauri zitenge fedha hii. Halmashauri zetu hazina fedha za kuendesha shughuli zake za kila siku, leo tukipanga kuzitengenezea sheria ya kuzilazimisha zitenge fedha hii maana yake tunataka kuzimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Kamati ingeshauri Serikali ihakikishe Fedha za Matumizi ya Kawaida *(OC)* zinapatikana katika halmashauri zetu ili fedha za *OC* zikipatikana zisaidie zile fedha za ndani zinazokusanywa kupangwa katika asilimia tano ya vijana na asilimia tano ya akinamama, lakini kulazimisha halmashauri kupata maziwa ya kulisha halmashauri zao mpaka ipatikane damu ni vigumu sana. Kwa hiyo, naomba hili kKmati kidogo iliangalie katika sura nyingine pamoja na maoni mazuri ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi halmashauri zina wajibu mwingine mkubwa wa kutenga fedha katika Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017. Yote hiyo ni wajibu wa halmashauri na hizo fedha ni lazima zitengwe, lakini halmashauri hazina uwezo wa kujiendesha. Vyanzo vya halmashauri vingi vimechukuliwa na Serikali Kuu, halmashauri zinajiendesha vipi? Utaratibu wa makusanyo ya halmashauri wenyewe umebadilika mno kutokana na maelekezo ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Bunge la Bajeti tulishauri hapa, katika maeneo ya manispaa na majiji yale makusanyo yaliyokuwa yanafanywa na mawakala yaliyofanyiwa tathmini na Benki ya Dunia kwa miaka zaidi ya 10 yasibadilishwe utaratibu wake kwa sababu Halmashauri nyingi zitadhoofika katika makusanyo ya mapato, lakini kwa bahati mbaya, wakati mwingine kwa kiburi cha wakubwa, mlikataa kusikiliza. Leo halmashauri nyingi zimeshindwa kutumia mawakala katika kukusanya fedha katika mpango wenu wa kutumia *commission,* halmashauri zinajiendesha vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusije tukakaa hapa tukizilaumu halmashauri tukiwalaumu Wakurugenzi bure wakati sisi wenyewe ndio tumewabana tukashindwa kuwafanya waweze kutimiza wajibu wao, Wabunge ni sehemu ya Madiwani, ni vizuri mjue shida ambazo Wakurugenzi na Madiwani wanazo katika Halmashauri zenu ili mkizungumza muwe mnaelekeza, maana wakati mwingine Serikali inavua majukumu yake na lawama zake inataka kuzihamishia kwenye halmashauri peke yake. Kwa hiyo, nadhani kwamba kwa hili Kamati ingeangalia vizuri na Serikali ni vizuri ikaangalia vizuri namna ya kuziboresha na kuimarisha Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mimi naendelea kusisitiza kwamba dhamira ya Serikali Kuu katika kuimarisha Serikali za Mitaa bado haijawa nzuri sana, ni vizuri Serikali Kuu iangalie mtazamo wake na dhamira yake ya kuimarisha Serikali za mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mdororo wa elimu pamoja na dhamira ya Serikali ya kutoa elimu, sijui bure ama bila malipo – maana mpaka sasa sielewi *terminology* halisi ni ipi, ni elimu bure ama ni elimu bila malipo. Nashauri kwamba miundombinu sio mizuri, lakini hata kama tukiimarisha miundombinu ya elimu ni vizuri tuangalie namna ya kuzisaidia shule za Serikali. Shule za Serikali hazifanyi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kilimanjaro kwa mfano, tulikuwa tuna utaratibu wa kuwalisha watoto chakula wakati wa mchana shuleni, chakula cha kawaida kabisa, lakini wazazi walikuwa wanalazimishwa kutoa michango kwa ajili ya kuhakikisha watoto wao wanakula shuleni. Baada ya tamko la Serikali la elimu bure *mindset* za wazazi na wananchi zikaamini kwamba sasa hawapaswi tena kuchangia chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri mkaainisha, mkitamka elimu bure mmedhamiria nini? Inawezekana mmedhamiria ada, kwamba wazazi hawatalipa ada ile ya sh. 20,000 katika shule za kutwa na shilingi 70,000 katika shule za mabweni, maana shule za msingi hazikuwa na ada. Ni vizuri mka-*specify* mnazungumzia nini katika suala la elimu bure ama elimu bila malipo ili wananchi waelewe Serikali hasa ni nini ambacho haichangii na wananchi wanapaswa kuchangia nini ili watimize wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya nchi hii ilikuwa ya ujamaa na kujitegemea, bado mmeandika kwenye Katiba kwamba iko hivyo kwa sasa. Wananchi *mindsets* zao ni hivyo hivyo kwamba nchi hii ni ya ujamaa na kujitegemea, kwa hiyo huduma zote zinatolewa na Serikali. Wananchi ndio tulikuwa tunawabadilisha kidogo wafahamu kwamba na wao wana wajibu wa kuchangia baadhi ya huduma. Leo mnakuja na propaganda za kisiasa za elimu bure, matokeo yake mnawabadilisha wananchi wanatoka walipokuwa wanakwenda mbele mnawarudisha nyuma bila kuwa na *fallback position* kwamba mnawasaidiaje katika hatua hizo. Kwa hiyo, ndugu zangu nafikiri Waheshimiwa Wabunge waliangalie hili kwa mapana ili waone namna ya kulisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utawala bora. Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, tukiwalaumu tunawaonea bure kwa sababu nimeona hata *spirit* ya Waziri wa Ofisi ya Rais ,TAMISEMI, ndiyo hiyo hiyo ya udikteta fulani na ndiyo maana anaweza akasema ni halali Wakuu wa Mikoa kufanya wanachoweza kufanya kusumbua viongozi wenzao katika maeneo mbalimbali, sasa inaonekana maelekezo ya nini wafanye Wakuu wa Mikoa yametoka juu, si maamuzi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri sana kwamba ni vizuri ninyi viongozi wa juu mbadilike, badilisheni mwelekeo wenu. Serikali ya Awamu ya Nne ilikuwepo, ya Awamu ya Tatu ilikuwepo, Wakuu wa Mikoa kweli hawakuwa hivyo, walikuwepo wala Katiba haijabadilika, wajibu wao baina yao na Halmashauri unaeleweka na wanaujua, ni kwa nini Serikali ya Awamu ya Tano Wakuu wa Mikoa ndiyo wabadilike, wamezaliwa upya, wameanguka kutoka mbinguni? Kwa nini waende kukamata watu, wakamate Walimu, wakamate Madaktari, wawaweke ndani kama wanaweka ng'ombe na mbuzi na ninyi mnaangalia mnaona jambo la kawaida? Kwa nini mnaondoa ule moyo wa wafanyakazi na watumishi kufanya kazi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Ofisi ya Rais, TAMISEMI ikaliangalia hili jambo kwa uzito wake ili wafanyakazi wale wafanye kazi kwa moyo. Wafanyakazi na watumishi katika maeneo mbalimbali hawana moyo kwa sababu ya maelekezo mnayowapa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, wamepoteza mwelekeo wa wajibu wao kabisa, sasa hivi wamekwenda kuvuruga kabisa mikoa na wilaya zao na halmashauri, kwa hiyo ni jambo la msingi sana kuliangalia katika uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa. Rushwa imekuwa ni utamaduni katika nchi hii kwa muda mrefu, lakini inavyoonekana kuna jitihada ambazo inaonekana zinafanyika ambazo huwezi kukwepa kuziona kwamba ni za muhimu, lakini jitihada hizi zinafanywa na mtu mmoja; inakuwa ni *one man show* kwamba anayeweza kupambana na rushwa ni mtu mmoja, ni Mheshimiwa Rais. Hajaweza kuimarisha mifumo yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalongo, jiandae Mheshimiwa Balozi Adadi

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Awali ya yote niwapongeze sana Wenyeviti wa Kamati zote mbili jinsi walivyowasilisha taarifa zao kwa umahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita sana na Taarifa ya Tawala za Mikoa (TAMISEMI). Kwanza kabisa liko tatizo kubwa sana ambalo nafikiri ni vizuri

tukaishauri Serikali ikaona jinsi ya kufanya. Tunalo tatizo kubwa sana la watendaji katika vijiji na watendaji katika kata. Maeneo mengi watendaji hawa ndiyo wanasimamia maendeleo, watendaji hawa ndio wanaosimamia usalama wa wananchi kule vijijini, lakini hakuna watendaji kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine utakuta mwanakijiji mmoja wamemteua pale ndiye angalau awe anasaidia kazi za utendaji halafu wanakijiji wale ndiyo wanachanga angalau kumsaidia hela ya sabuni yule mtendaji wanayemsaidia. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Njombe Mjini, Kijiji cha Idunda, ni kijana wa pale kijijini ndiyo amekuwa kama Mtendaji na ni muda mrefu kijiji hakina Mtendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo linalojitokeza ni nini? Wananchi wachange kwa ajili ya maendeleo yao, lakini wachange tena kwa ajili ya kumwezesha Mtendaji waliyemweka kwa muda sasa, vitu hivi vinaleta shida sana. Pamoja na ufinyu wa bajeti ambao Serikali inakuwa ikilalamika mara kwa mara, huu ni wajibu wake kuhakikisha kwamba Watendaji wanapatikana na Watendaji hawa ndio watakaosaidia kusimamia maendeleo kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watendaji wa Kata hakuna, kila Kijiji, kila Kata utaona Mtendaji anakaimu, anakaimu, anakaimu. Wanakaimu kwa miaka na Mtendaji akishakuwa Kaimu anakuwa ni Mtendaji anayekaimu Kata na wakati huo huo ni Mtendaji wa Kijiji fulani. Kwa hiyo, unaona kabisa pale kwenye Kata panakuwa hakuna Mtendaji ambaye anasimamia maendeleo katika ile kata. Hivyo naiomba Serikali iangalie kwa namna gani; pamoja na ugumu wote wa tatizo kubwa la ajira na tatizo la ufinyu wa bajeti; wapatikane watendaji; watendaji ni muhimu sana katika vijiji vyetu; ili kusudi waweze kusimamia maendeleo kwenye vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba ku-*declare,* mimi ni mmiliki wa shule na katika suala la elimu kwanza kabisa nipongeze sana Mkoa wa Njombe na Halmashauri yangu ya Mji wa Njombe Mjini kwa kufanya vizuri katika mitihani ya kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ziko changamoto nyingi kwenye sekta ya elimu ambayo sasa ni vizuri sana TAMISEMI wakajipanga vizuri na wakaangalia namna gani watasaidia. Wananchi wanajitahidi, wanajenga madarasa, wanaandaa thamani za madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini liko tatizo la Walimu, na kinachofanyika kule mashuleni ni kwamba, kwa kuwa Walimu ni wachache, yako madarasa ya awali katika kila shule ya msingi. Utaona utawala wa shule unaiambia Kamati ya Shule kwamba darasa hili la awali halina Mwalimu, kwa hiyo Kamati ya Shule inafanya utaratibu wa kuratibu ni kwa namna gani itapata Mwalimu; hivyo Kamati ya Shule inaajiri Mwalimu kwa ajili ya darasa la awali; wakati mwongozo unasema hakuna Mwalimu wa darasa la awali na kwamba Walimu wote wataajiriwa na Serikali na watalipwa na Serikali. Matokeo yake sasa hali hiyo inatia dosari nia nzuri ya Serikali ya kutoa elimu bila malipo pale ambapo sasa wazazi wanaanza kuchangia kwa ajili ya Mwalimu wa darasa la awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, Serikali iangalie hilo na kama kunahitaji maelekezo, basi itoe maelekezo kwamba Mwalimu wa darasa la awali awe ni Mwalimu mwenye cheti na aliyeajiriwa na Serikali. Kama Kamati ya Shule itaona kuna umuhimu wa kuajiri Mwalimu basi iajiri Mwalimu kwa ajili ya madarasa mengine lakini si kwa darasa la awali; kwa sababu darasa lile sasa linaonekana kwamba ni darasa hafifu au darasa la hali ya chini sana ndiyo maana wanaajiri yeyote tu kule kijijini aendelee kufundisha darasa la awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika madarasa haya ya awali, liko tatizo lingine ambalo sasa linaanza kujitokeza. Mwongozo unasema kwenye sera kwamba watoto wakifika miaka minne na kuendelea wakasome madarasa ya awali katika maeneo ambako shule za msingi zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta kwamba Shule nyingine ziko zaidi ya kilometa sita kutoka Makazi ya wananchi na wananchi wa vitongoji hivyo wamejenga madarasa mazuri sana yanasimamiwa na Serikali zao za Vijiji lakini watawala wa Idara ya Elimu wanazuia sasa watoto wasisome katika yale madarasa ya awali wapelekwe katika madarasa yaliyoko karibu na shule ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia umri wa yule mtoto ana miaka minne, atembee kilomita sita kwenda mahali ambako iko shule ya msingi, atembee kilomita sita kurudi. Huyu mtoto lazima atachukia shule lakini vilevile ni hatari kwake. Hayuko mtoto mdogo mwenye umri huu ambaye anaweza akatembea kwenda shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ni kwamba; katika yale madarasa ambayo Serikali za Mitaa zimejenga au Serikali za Vijiji zimejenga na yako vizuri, Serikali iyasimamie yale madarasa ifuatilie kwa utaratibu mzuri ili kusudi watoto

wale wasome kule kule wanakoishi na waweze kupata elimu kule kule wanakoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala haya ya utawala huko vijijini, liko tatizo la posho na mkono wa ahsante kwa Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Mitaa. Bila kuwa na Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Mitaa hatuwezi kabisa kufanya chochote kama Serikali. Ni vizuri Serikali sasa ikaagiza rasmi kwamba kila Mwenyekiti wa Mtaa posho yake ni kiasi gani; maana ile posho sasa inakuwa ni ya kufikirika tu; inafikirika tu kwamba leo Halmashauri ina kiasi gani cha fedha basi apewe; haina basi anaambiwa leo Halmashauri haina kitu lakini ukifikiria kazi anayoifanya Mwenyekiti wa Kijiji ama Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa Serikali ikatoa mwongozo rasmi kwamba, watendaji hawa, viongozi hawa waliochaguliwa na wananchi katika maeneo yale wanastahiki nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ulimwengu wa sasa hayuko mtu ana uwezo wa kufanya kazi bila malipo. Hebu tuingiwe hata na huruma tu Serikali tuone kwamba watendaji hawa, Wenyeviti wa Mitaa na Wenyeviti wa Serikali za Vijiji wana kazi kubwa wanayoifanya, wanaamshwa usiku, wanasuluhisha mambo mbalimbali kule vijijini, wanasimamia maendeleo, tunakwenda kule tunafurahia majengo yamejengwa vizuri lakini wao wenyewe hawana kipato chochote na wala hawapewi mkono wa ahsante wanapomaliza ile kazi yao ya kutumikia wananchi baada ya miaka mitano ikipita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la uwezeshaji wa vijana na akinamama. Tumeweka hii asilimia 10 lakini ukijaribu kuangalia asilimia 10 hii imekuwa bado haitoshelezi kuwawezesha hawa wananchi. Tuiombe Serikali sasa, ile fedha milioni 50 ambayo ilisema itaitoa, mchakato huu umekwenda muda mrefu mno na mchakato unapokwenda muda mrefu unakosa maana iliyokusudiwa matokeo yake unazalisha hadithi nyingine na kuona kwamba wananchi hawatatekelezewa ile ahadi. Hebu tuombe huu mchakato uende haraka iwezekanavyo ili kusudi fedha hiyo ipatikane na wananchi hawa wafanye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Halmashauri zinafanya jitihada nyingi sana katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata ile asilimia 10, lakini asilimia hii 10 ni ndogo mno. Wenyewe tunajua kabisa hali ya Halmashauri zetu zilivyo hivyo tuone kabisa kwamba kama hii milioni 50 itapatikana itasaidia sasa

kupunguza ile kiu ya wananchi kufanya maendeleo na kuwapa hamasa zaidi ili waweze kujikimu katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimalizie na suala la *TASAF;* Naipongeza sana *TASAF* kwa jitihada zote walizofanya, sana sana. Wanatusaidia sana, wamepunguza kiwango cha uhaba wa fedha kwa wananchi, lakini nafikiri waende mbele zaidi. Wafikirie sasa kwa fedha ile kidogo wanayowapa wawape malengo, kwamba ile ile fedha kidogo wananchi wale wajaribu kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine wawape *time frame,* kwamba fedha hii watapewa mpaka lini; kwa sababu kuna watu sasa wameshajisahau kabisa wanajua fedha ile sasa wao mpaka siku watakapokufa ndipo itakapokoma. Ni vizuri sasa wananchi wale wakaandaliwa, wakaambiwa fedha hii wanapewa mpaka lini na ikabuniwa miradi midogo midogo ya mazingira wanayotoka hawa wananchi ili waweze kuwasaidia, kwa sababu wote tunaamini kwamba hayuko mtu mwenye uwezo wa kumpa mtu fedha siku zote za maisha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naipongeza sana *TASAF* na uongozi wake wote pamoja na Wizara inayosimamia kwa usimamizi mzuri. Tuombe sana wajitahidi sasa wabuni miradi midogo midogo, washirikiane na Mabaraza ya Madiwani kuona kwamba namna gani sasa fedha ile hata kama ni kidogo inaweza ikasaidia kuwawezesha wananchi wale ili kuwa na vitu endelevu kusudi kesho kama *TASAF* inakoma kutoa hiyo fedha wananchi wasijikute kama wameachwa jangwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Balozi Adadi, wajiandae Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Taska Mbogo na Mheshimiwa Mohamed Bashe.

**MHE. BALOZI ADADI. M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia taarifa za Kamati hii. Kwanza nawapongeza Wenyeviti wote wa Kamati kwa mchanganuo mzuri na mambo mazuri, mapendekezo na maoni ambayo wameyatoa kwenye Kamati zao. Nitajikita kwenye Kamati zote mbili kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati ya Katiba nilitegemea sana wangeweka msisitizo pia pamoja na mambo mengine suala la msongamano

na ucheleweshaji wa kesi Mahakamani. Kamati hii ya Katiba ina mwingiliano sana na Kamati yangu ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imetembelea sana Magereza na imeona namna ambavyo mahabusu pamoja na wafungwa walivyosongamana ndani ya Magereza, ni tatizo kubwa sana. Tatizo hili linatokana hasa na makosa mawili tu au matatu. Utaona makosa ya mauaji na makosa ya madawa ya kulevya ndiyo ambayo yanachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahabusu wako wengi sana wa makosa ya mauaji, madawa ya kulevya na Wahamiaji haramu. Sasa hawa watu wamekaa gerezani muda mrefu, mtu anakaa miaka miwili, mitatu, minne anasubiri apangiwe kesi Mahakama Kuu. Kwa hiyo unaona kwamba Kamati hii ilikuwa na uwezo wa ku-*force* Serikali hasa Mahakama Kuu kuangalia uwezekano wa kubadilisha taratibu zao, kanuni zao kuendana na wakati kwa sababu mahabusu wanakaa sana wakisubiri kesi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa hiyo *High Court Session. High Court Session* inapangwa, inaweza kukaa miaka mitatu mahabusu wanasubiri *High Court Session* iweze kuitwa. Ni muhimu sasa hivi Kamati ipendekeze kwa Jaji Mkuu waangalie uwezekano wa kubadilisha kitu kinaitwa *High Court session.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wafungwa kule ambao wamehukumiwa kunyongwa. Wamejaza Magereza na kama unavyojua ukihukumiwa kunyongwa hufanyi kazi yoyote, wanakula tu, wanasubiri kunyongwa. Kunyongwa kwenyewe hakujulikani watanyongwa lini. Sasa sijui mamlaka zinazohusika zinafikiria namna gani kwa sababu wanaendelea. Sasa hivi karibu miaka ishirini, thelathini kuna watu wamehukumiwa kunyongwa wako kule hawanyongwi, vifaa vya kunyongea vimekaa mpaka vimeota kutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kama sheria hiyo mamlaka inaona kwamba haitekelezeki basi iletwe Bungeni tuifute, maana hata kwenye kupunguziwa adhabu wafungwa ambao wanataka kupunguziwa adhabu wale waliohukumiwa kunyongwa hawapunguziwi adhabu hata siku moja sasa sijui ni kwa nini. Ni vizuri suala hilo Kamati pia ingeshauri ili tuibane Serikali ili mamlaka zinazohusika zifikie maamuzi ya hawa watu ambao wamehukumiwa kunyongwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mamlaka zinazohusika zinashindwa basi zirekebishe ziteremshe kwa Mwakyembe huenda atasaini watu wanyongwe, lakini vinginevyo kwa kweli wanajaa na wahamiaji haramu ambao wako mle wanajaa. Maafisa uhamiaji, mhamiaji haramu anakosa anamtupa jela hata bila kupelekwa Mahakamani. Ni vizuri Sheria hiyo pia iangaliwe na kuletwa hapa Bungeni tuweze kuiangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la ajali. Suala la ajali ni kubwa sana na zinaleta athari kubwa sana. Watu wanakufa sana kwa ajali, watu wanapata vilema kwa ajali. Nilitegemea pia tuungane na Kamati hii ya Katiba na Sheria tuweze kulazimisha Serikali ilete mapendekezo ya kubadilisha suala hilo, kwa sababu mambo mengi ambayo yanatokana na ajali ni mambo *personal* (mtu binafsi). Ajali ambazo zinatokea karibu asilimia 70 na ushee zinatokana na matatizo ya mtu binafsi. Ni vizuri Sheria hiyo tukaiangalia upya na iletwe Bungeni tuweze kuifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Kamati ya Utawala Bora na Serikali za Mitaa, hii kitu inaitwa TAMISEMI. TAMISEMI ni jalala, limechukua kila kitu. Kwenye Majimbo yetu huwezi ukazungumza chochote bila kuangalia TAMISEMI. Ukiangalia afya TAMISEMI, sijui shule TAMISEMI, barabara TAMISEMI, matatizo ya maji TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ina mambo mengi sana na kwenye Halmashauri inakuwa ni tatizo, kwa sababu tuna mipango mizuri ya kutekeleza bajeti hii ya TAMISEMI lakini hela hakuna, hela zimeanza kuja juzi. Nashauri tu kwamba, tuilazimishe Serikali hizi fedha zilizopangwa kwenye Halmashauri zetu ziletwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Muheza tuna mipango mingi sana ambayo tumepanga kwenye bajeti, lakini mpaka sasa hivi sijui hata kama robo zimefika ambazo tumepokea kwenye mpango wa maendeleo. Kwa hiyo, naomba hela hizi ziletwe ili tuweze kukamilisha mambo ambayo yamepitishwa hapa Bungeni na mambo mengi ya maendeleo ambayo tumeamua kuyafanya katika kipindi hiki cha fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Madaraka ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa; suala hili sasa hivi linakwenda kubaya na nashauri Serikali iliangalie kwa kina. Hawa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wanaonekana hawajapata semina yoyote ya kuelewa madaraka ya ukamataji. Wao wanaelewa tu mtu mpeleke ndani. Mtu amekubishia kwenye mkutano unaamua akamatwe apelekwe ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari Polisi anachukua miezi sita kusomea namna ya kumkamata mtu, namna ya kuondoa haki ya mtu, sasa huwezi ukajibishana na mtu tu kwenye mkutano wewe Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa unaamua huyu mtu umweke ndani. Ni suala ambalo ni *sensitive* na ningeshauri Kamati suala hili tuwabane Serikali hawa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wapate semina, waelewe maana ya ukamataji, waelewe maana ya kuweka watu ndani vinginevyo itakuwa *chaos* hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana kupongeza suala la mradi wa mabasi wa DART, ni mradi ambao unatakiwa upongezwe. Kwa kweli huu mradi sijui kwa nini umechelewa, lakini haya mabasi yangeweza kuwa kwenye Jiji la Dar es Salaam sasa hivi naamini Dar es Salaam upungufu huu wa usafiri ungeweza kupungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala ambalo ndugu yangu aliyesema la kutoa matairi alilosema Mheshimiwa Rais, zile ni mbinu za Askari, Rais amewashauri tu Askari namna ya kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hiyo, si kutoa matairi ni vielelezo mojawapo ambavyo vitatolewa Mahakamani kuthibitisha huyu mtu alikuwa anaingia kwenye barabara ya mwendokasi. Ile ni barabara ya mabasi ya mwendokasi na yanapokukuta wewe ni maiti. Sasa ni lazima askari wawe wakali na wahakikishe kwamba kweli wanatekeleza hizo sheria inavyopaswa. Kwa hiyo, Rais alifanya kuwashauri tu askari, hiyo ni mbinu mojawapo ya kuwakamata hao watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ni suala ambalo tunatakiwa tulipongeze kwamba hawa wapanda bodaboda wanapoingilia haya mabasi kwa kweli waelewe kwamba ni kifo. Kwa hiyo, ni lazima kwamba Sheria iwe kali kwenye suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napongeza sana suala la *TASAF,* suala ambalo linatujengea imani sana kwa wananchi. Kuna matatizo madogo madogo ambayo wanatakiwa wayarekebishe lakini huu mpango wa *TASAF* uongezwe na tunaunga mkono sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono mapendekezo yote na ningeshukuru mapendekezo haya ambayo tumeyashauri, basi yachukuliwe ili tuwabane Serikali vizuri, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Richard Mbogo, jiandae Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa hii nafasi. Nami kwanza nianze kuunga mkono hoja ya Kamati hii ambayo *report* yake ni nzuri kweli kweli na imesheheni mambo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nianze kwa kuchangia upande wa Mfuko wa kusaidia Kaya masikini *(TASAF)*. Mfuko huu tunamaoni kwamba uendelee kuwepo. Uendelee kuwepo kwa misingi kwamba sisi ni Wabunge, tumezunguka, tumefanya ziara maeneo mbalimbali, wazee bado wanalilia uwepo wa *pension*. Sasa kama wazee tu wanalilia walipwe *pension* kwa ajili ya kuwasidia sasa je, hizi kaya masikini kwanini tuziondoe? Kwa hiyo tunaomba sana Serikali huu mfuko uendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi ni kuboresha, katika kupitia majina kila baada ya miaka mitatu ikibidi iwe miaka miwili, kwa sababu kumekuwa na changamoto za maeneo mbalimbali, Watendaji wetu kule chini wanakuwa wanachakachua majina wanaweka watu ambao hawana sifa za kufaidika na huu mfuko. Katika kuboresha, badala tu ya kuangalia kutoa fedha, tuone jinsi gani tutoe fedha kiasi na tutoe hata shughuli ndogondogo kama za ufugaji wa aina mbalimbali wa ndege au wanyama ili ziweze kuwaongezea kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili lililozungumzwa kwenye ripoti ya Kamati ni kuhusu fomu za maadili, Watumishi wengi wa Serikali kwa mujibu wa sheria tunatakiwa tujaze fomu za maadili, lakini kwenye ripoti ya Kamati humu wamehimiza kuhusu TEHAMA. Serikali iangalie jinsi gani TEHAMA iweze kutumika ili tuweze kupunguza gharama na kuwa na ufanisi pia kwenda na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, uwasilishaji wa fomu za maadili Wabunge wengi waliweza kusafiri tena kurudi kuzileta fomu kwenye Kanda, Watumishi wa Serikali wamesafiri kwenda kwenye Kanda kuwasilisha fomu, ilikuwa ni gharama magari ya Serikali yametumika na fedha za Serikali. Kwa hiyo, tuombe sasa tupate mfumo wa kuwasilisha hizi ripoti kimtandao – *web based reporting. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nichangie kuhusu utawala bora. Kweli Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wameteuliwa na Mheshimiwa Rais katika kutekeleza na kumsaidia, lakini tuombe wajaribu kuangalia ile sheria inayowaruhusu kutoa amri mbalimbali kama vile amri za kukamata. Ni makosa

gani ambayo yanapaswa kuingia kwenye hiyo amri ya masaa 48 ya kuweza kukamatwa. Kwa hiyo, yaangaliwe ni makosa ya aina gani, kwa sababu sheria ilitungwa na wana mamlaka hiyo ya kuitumia basi waende kwenye Kanuni na kuangalia ni makosa ya aina gani, hatubezi utendaji wao bali tunaunga mkono wanavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litakuwa sambamba pia na masuala ya kiutawala kwa upande wa utumishi. Tumesikia kauli mbalimbali, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa anamshusha mtu cheo au anamfukuza kazi badala ya kufuata taratibu za kiutumishi katika kuchukua hatua hizo. Kwa hiyo, tuombe sana Serikali wayaangalie makosa ambayo yamekwishafanyika kwa kipindi hiki na Waziri husika afanye utaratibu wa kutoa barua au mwongozo ambao utaweza kusaidia utendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tunapenda sana katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni mfuko ule wa kuwakopesha vijana na akinamama kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri zetu. Ufuatiliaji umekuwa ni hafifu sana, *OC* ziende kwa wakati ili mapato yetu ya ndani yaweze kutengwa. Inatakiwa asilimia 60 iende kwenye miradi ya mendeleo. Ndani ya asilimia 60, asilimia 10 ni kwa ajili ya vijana na akinamama. Sasa Halmashauri nyingi mpaka sasa hivi ukiwauliza miezi hii sita wametenga kiasi gani utakuta hakuna Halmashauri ambayo imeshatenga zaidi ya hata asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *OC* ziende ili mapato ya ndani yote yasitumike kwenye shughuli za kila siku na vijana wetu na akinamama waweze kukopeshwa fedha na ndiyo utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Tume ya Utumishi ya Walimu. Tume hii imeanzishwa na kwa mujibu wa Kamati kuna changamoto sana kwenye upande wa bajeti na baadhi ya sheria na kanuni zinazoongoza. Tujaribu kuangalia kwanza mfumo. Tume hii sasa hivi inavyofanya kazi kwenye Wilaya kuna zile Kamati za kinidhamu, kwa hiyo kama Wilaya ina Halmashauri mbili au tatu sasa ushughulikiaji wa ile Kamati unakuwa ni mgumu kidogo kwa sababu ya *composition* ya Wajumbe wa ile Kamati wanatoka sehemu mbalimbali na ruzuku fedha zinakuwa hazipatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri mfumo huu uende kihalmashauri na Mkurugenzi azifadhili hizi Kamati za nidhamu za Walimu kwa ajili ya ufanyaji kazi. Kama zitakutana mara tatu kwa mwaka au mara mbili ili kuwa na mapitio kabla ya bajeti na baada ya bajeti na Walimu wanapata *promotion* mbalimbali. Pia

*coordination* ndiyo itaenda vizuri kati ya TAMISEMI na Utumishi kuhusu upandaji wa madaraja ya Walimu, mambo ya kinidhamu ndiyo yataenda vizuri. Kwa hiyo, tunaomba Tume hii Sheria ibadilishwe ambayo itakuwa inaweza kuongoza katika kuhakikisha kwamba Walimu wetu, maslahi yao na kesi zao ambazo zimekuwa ni nyingi na ndiyo ajira kubwa ya Halmashauri au upande wa TAMISEMI idadi kubwa ni Walimu. Kwa hiyo, ni muhimu sana tuweze kubadilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho tungeomba sasa upande wa Serikali kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu zinalenga kwenye kufuatilia *promotion* au madaraja ya Walimu na mishahara yao ibadilishwe na iendane na bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Kamati hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Taska Mbogo ana udhuru, nafasi yake anachukua Mohamed Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Nami nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuleta sote pamoja katika Bunge la mwaka huu tukiwa salama na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia katika maeneo makubwa mawili. Eneo la kwanza ni eneo la utumishi. Tumeona *commitment* ya Serikali juu ya kufanya jitihada kubwa ya kurudisha nidhamu ya Watumishi wa Umma, lakini nataka niiombe Serikali kuna *two approach*, kuna *carrot* na *stick.* Nimeona matumizi ya *stick* yamekuwa makubwa zaidi kuliko *carrot* mahali ambapo imefikia watumishi wetu wamekuwa waoga sana katika maeneo mbalimbali. Watu wamekuwa hawafanyi maamuzi, watu wameingiwa na hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba Wizara ya Utumishi, *commitment* ya Serikali kurudisha nidhamu iende na *incentive package* kwa watu wanaofanya vizuri na wanaofanya maamuzi katika sekta mbalimbali katika utumishi wa umma ili jambo hili liweze kuwatia moyo wale waadilifu. Hatusemi wanaofanya vibaya wasiadhibiwe. Hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika Utumishi ni suala la ku-*develop Institutional capacity.* Dhamira ya Serikali ya Rais, mimi nakubaliana sana na *approach* ya Rais Magufuli. *When you are in crisis* tumia hiyo *mechanism* ya *crisis* ku-*sort out problem,* wakati una *develop Institution* zako.

Kwa hiyo, ningeomba mwaka huu mmoja tumetumia *fire approach* sasa Serikali ifanye kazi kubwa ya ku-*develop institutional capacity* ili Mheshimiwa Rais atakapomaliza kipindi chake cha miaka kumi taasisi ziendelee. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ni lazima tujenge *capacity* za Taasisi? Tunapotegemea sana uwepo wa mtu, anapokuwa hayupo tunarudi kule tulikotoka, tutakuwa hatuisaidii nchi kule tunakotaka kwenda. Kwa hiyo hili ni jambo muhimu sana la kufanya ili tuweze kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Wizara ya TAMISEMI, nampongeza Waziri wa TAMISEMI na Naibu wake wanajitahidi, lakini wameondoa vyanzo vya mapato hasa katika Miji na Manispaa. Wajitahidi basi hata fedha za *OC* ziende. Kinachotokea sasa hivi fedha za *OC* haziendi ambazo ziko *budgeted* kabisa na zimepitishwa na Bunge, haziendi kwa wakati, hazifiki matokeo yake fedha za mapato ya ndani sasa zinatumika kuendesha ofisi za Hamashauri, matokeo yake zinaathiri *development activity* katika maeneo yetu. Kwa hiyo, hili ni jambo muhimu sana Serikali ikaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mtazame uwezekano wa kurudisha hivi vyanzo vya mapato ambavyo vimeondolewa kwenye Halmashauri. Kwa sababu tunapopunguzia *capacity* ya Halmashauri ya kifedha maana yake na tumeamua kwenda na *approach* ya *D by D* shughuli za maendeleo na hali ya uchumi kwa wananchi wetu ni ngumu. Ni muhimu sana tuone namna gani tunazipa uwezo Halmashauri zetu kutatua changamoto zinazokabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI kama wenzangu wamesema, TAMISEMI ni kama jalala, lakini sitaki kutumia neno jalala imeamuliwa kwamba kwa *approach* ya utawala tuliyochagua ni kwamba ndiyo *coordination center.* Leo tumeunda Tume ya Utumishi ya Walimu *(Teachers Commission)* imeenda TAMISEMI, ingawa mimi kwa mtazamo wangu naiona haina meno, lakini la pili kuna madai ya Walimu ambayo ni makubwa mno. Lazima tuje na *mechanism* ambayo itajenga *hope* kwa Walimu wetu kwamba madai yao haya *within this span of period* yatakuwa yamelipwa. *I don't believe* mpaka leo bado tunafanya uhakiki, tunahakiki mpaka lini? Hili ni jambo ambalo ni lazima tujiulize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira imekuwa changamoto, wewe ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu unaona Wizara ya Afya ikija, Wizara ya Elimu ikija, suala la ajira linavyokuwa ni mjadala mkubwa na upungufu wa

watumishi hasa wa kada ya afya katika Halmashauri zetu. Mheshimiwa Simbachawene na Dada yetu Mheshimiwa Angellah Kairuki, uhakiki wameshafanya *for almost one year,* hebu wafungulie hizi ajira ili tuondoe watoto wetu wanao *graduate* mitaani tuweze kuwa-*absorb* katika ajira, pia tuweze kuondoa kero! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo *by June* katika Mji wa Nzega tutakuwa na zahanati 15 mpya, tutakuwa na vituo vya afya vitatu vipya, hakuna *manpower!* Leo Nzega tuliamua kuachana na *approach* ya kushusha vyeo Walimu ambao hawa-*perform* vizuri na kuwaadhibu, *no!* Tuliamua kuangalia changamoto zao. Mwaka jana matokeo ya darasa la saba Halmashauri ya Nzega ilikuwa ya mwisho Kimkoa, mwaka huu imekuwa ya pili kwa sababu tulienda ku-*tackle* matatizo ya Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Mji wa Nzega haukuwa na *division one* na *division two almost* lakini *performance* ya mwaka huu kidogo ime-*grow,* Halmashauri ya Mji wa Nzega imekuwa ya 73. *It's very important* tukaangalia hizi *crisis* katika *Local Government* na *Brother* Simbachawene *you have a lot of* mzigo. Kwa hiyo, ni vizuri kupitia Bunge hili na nimshauri kwenye Bajeti inayokuja matatizo ya Walimu tuje na *clear plan* kwamba madai ya Walimu ni kiwango hiki, tutayalipa ndani ya kipindi hiki ili Walimu wetu wawe na matumaini kule walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF*. *TASAF* imesaidia sana watu wetu lakini umefika wakati wa *approach* ya *TASAF* kubadilika iwe ni *developmental approach,* kwamba fedha zinazopelekwa kwenye kaya maskini ziwe ni fedha ambazo zina wa-*commit* wale watu maskini kuja na miradi ya maendeleo ambayo hawa wataalam wa *TASAF* mwaka kesho kabla hawajakupa fedha wanaangalia *performance* ya mwaka jana, fedha tuliyokupa na mradi ulioanzisha. Ni muhimu Idara ya Maendeleo ya Jamii katika *Local Government* ikafanya kazi *very close* na wataalam wa *TASAF* na Watendaji wetu wa Vijiji ili kusaidia kaya hizi maskini badala ya kupewa fedha kwenda kula ziwe fedha za *investment* ili tuweze kuondokana na umaskini katika *Local Government*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia hoja ya asilimia 10 nataka Serikali itafakari. Tuna asilimia 10 katika Halmashauri, tuliahidi kwenye Ilani shilingi 50 *million* ya kila kijiji. Tuna fedha za Mfuko wa Uwezeshaji, hizi fedha ziko *scattered* katika maeneo mengi. Umewadia wakati kama Serikali itazame hizi fedha ambazo zina *target* kwenda kukopesha vijana na akinamama tuziwekee *proper framework* kisheria ili ziweze kufikia watu kwa wakati. Ukichukua milioni 50 ya kila

kijiji, ukachukua asilimia 10 ya Halmashauri katika kila Halmashauri zikawa *under one basket* halafu tukachukua fedha za uwezeshaji zinazowekwa Wizara ya Mheshimiwa Jenista, fedha hizi tukazitengenezea sheria zitatusaidia sana kuondokana na changamoto za *financing* kwa watu wetu maskini.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bashe ni kengele ya pili.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa mchana umekwisha. Jioni mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Ruth Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Desderius J. Mipata na Mheshimiwa Taska Mbogo.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni. Leo tunaanza saa kumi jioni.

*(Saa 6.55 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Waheshimiwa Wabunge, karibuni kwenye awamu yetu ya jioni na sasa namwita Mheshimiwa Ruth Mollel, kwa taarifa niliyopewa anazungumza dakika tano na Suzan Kiwanga dakika tano, Mheshimiwa Desderius Mipata ajiandae.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja ambayo ipo hapo mezani na na-*declare* kwamba mimi pia ni Mjumbe mmojawapo wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Naona Mheshimiwa Suzan Kiwanga hajaja mimi nitaendelea tu na dakika zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu kubwa ambalo nalikazia ni eneo la Utawala Bora ambalo Kamati imezungumza na kuainisha maeneo mbalimbali ambayo hayazingatii utawala bora katika Awamu hii ya Tano. Tukiangalia katika ile taarifa ya Kamati tumeona jinsi watu wanavyoswekwa jela kwa kutokuhudhuria tu vikao, ambayo ni kinyume za kanuni na taratibu za uendeshaji Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hata kule Singida, Daktari ameswekwa rumande, kwa sababu kuna mgonjwa alikufa. Mimi sitetei uzembe lakini kuna *factors* nyingi ambazo zinaweza kufanya mgonjwa kufariki dunia. Kwa vile huyu Daktari amewekwa rumande, nasikia ame-*resign* na sioni ni jinsi gani huyu Daktari angerudi tena akaweza kufanya kazi vizuri katika ile hospitali. Hata wale watumishi wengine ambao wanafanya kazi na yule Daktari watapoteza morali kabisa ya kufanya kazi. Sidhani kama wale wagonjwa watapata tiba stahiki na huduma stahiki kwa jinsi ambavyo mwenzao ametupwa rumande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao ndio wanyonge tunaowazungumzia, maana yake hakuna Mbunge atakwenda kutibiwa huko Singida tunakozungumza. Kwa hiyo ni muhimu Serikali ikazingatia kanuni na taratibu za kuchukulia watumishi hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona jinsi gani Mtwara kule, Walimu Wakuu wameteremshwa vyeo kwa sababu tu ya matokeo ya *form four*. Hiyo siyo sahihi, kwa sababu tunamtafuta mchawi. Mchawi ni Serikali yenyewe, haijawekeza kwenye elimu. Kama Mwalimu ana wanafunzi 100 darasani, hana vitendea kazi, marupurupu yake hayajalipwa, utamtegemeaje huyu Mwalimu afanye kazi kwa ufanisi? Kwa hiyo Serikali, ijikite katika kuangalia *factors* ambazo zinateremsha elimu yetu na inafanya wanafunzi wetu wasiweze kufaulu vizuri madarasani. Hivyo kwa kweli hiyo haipendezi hata kidogo, Serikali isitafute mchawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikaangalia pia hii Mihimili miwili ya Bunge na Mahakama. Nakumbuka juzi Spika alisema kwamba Bunge tuko huru kabisa, sikubaliani kama sisi Bunge tuko huru! Juzi hapa tumenyimwa Bunge *live* na sisi ni Bunge, hakuna mtu amesimama kulisemea mbali ya Wapinzani, halafu tunasema Bunge tuko huru, tuna uhuru gani? Tukitaka kusafiri nje, mpaka tupate kibali Ikulu, tuna uhuru gani? Wakati iko namna ya kudhibiti matumizi ya Serikali, unaifanya katika bajeti *tool*. Inasema Bunge ninyi kwa mwaka huu mtapata milioni kadhaa kwa ajili ya safari zenu, lakini siyo tuombe ruhusa kwa *Executive*. Ina maana Bunge limekuwa *compromised* na hakuna mtu anayelisemea. Kwa hiyo, sisi hapa ni Bunge butu, hatuna meno na huu ndiyo ukweli na lazima tuukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia upande wa Mahakama, Mahakama tumenyimwa kufanya mikutano ya kisiasa na hiyo ni kinyume cha Katiba. Mahakama iko kimya, wala haijasema kitu. Jana Mheshimiwa Rais amesema kwamba wale Mawakili wanaowatetea watu ambao wamekosa wawekwe ndani, itakuwaje wawekwe ndani na juzi tumepitisha sheria ya *Paralegals* ya kutetea wanyonge. Sasa huyo Wakili unamweka ndani atamtetea nani?

watatetewa wale wenye pesa, kwa hiyo wale wanyonge watashindwa kutetewa. Hiyo haiendi sawa na lazima turudi katika misingi ya mihimili mitatu kila mmoja iwe inamwangalia mwenzake lakini kwa sasa hivi ilivyo Mahakama na Bunge tumekuwa *compromised* na huo ni ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja suala la *decentralization* kwa upande wa kimitaa. Ilipitishwa sera miaka kadhaa ya *decentralization by devolution* lakini kwa jinsi ambavyo Serikali inafanya sasa hivi, inapoka mamlaka ya Serikali za Mitaa. Tanzania ina kilomita za mraba karibu 945,000. Lazima Serikali za Mitaa iwe *very strong* na kwa mtindo huu, wamenyanganywa *property tax* na je, huu utawala bora tunaousema ni upi, wakati mkono wa Serikali wa *Local Government* unanyimwa pesa ambazo zingewasaidia kupeleka huduma kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili haliko sawa na ili neno la *good governance* tunalizungumza tu lakini kwa kweli hatulizingatii. Nashukuru sana Suzan Kiwanga amerudi sijui kama bado ana dakika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ungemalizia tu dakika tatu tu!

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ilikuwa ni hili la *TASAF*. *TASAF* tumekwenda kutembelea maeneo mbalimbali na wanafanya vizuri. Mimi naungana na wengine wote waliozungumza, napendekeza kwamba *TASAF* iendelee na *TASAF* sasa iwekewe mfumo mzuri kuweza kuwatambua. Kwa sababu inaelekea siyo kila mara Serikali ikishindwa kitu inafikiri kwamba itafanya kitu tofauti badala ya kuangalia imeshindwa wapi na kurekebisha. Kwa hiyo Serikali iangalie kwa nini huu mfumo haufanyi kazi vizuri na ni jinsi gani watu hewa wanaingizwa kuchukua hizo pesa za *TASAF* ifanyie kazi na siyo kumtafuta mchawi mwingine tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mipata, jiandae Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nishukuru pia Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Viongozi wa Kamati zote mbili kwa namna walivyotoa taarifa zao nzuri na inaonekana kwa kweli ni taarifa

nzuri za kufanyia kazi. Katika kuunga mkono nina maeneo mawili ya kuchangia na nikipata nafasi naweza nikachangia eneo la tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni suala la Utawala Bora. Suala la utawala bora kwa kadri wenzangu walivyokwisha kulisema kwa kweli ni kitu ambacho siyo cha ku-*acquire* mtu hivi, ni kitu ambacho lazima mtu aandaliwe. Ni vizuri Viongozi wakapata mafunzo, bila kuwapa mafunzo mambo yataenda mchakamchaka lakini athari zake mtaziona kubwa mno. Hii haitatusaidia katika nchi. Watu wapate mafunzo katika ngazi zote kuanzia Vijiji, Wilaya Mikoa na Taifa, ni muhimu sana. Natoa mfano mmoja wa jambo ambalo limeniathiri, katika eneo langu ambalo nadhani ni maagizo ya kupokea halafu watu hatuwezi kukaa tukaona athari ili tuone tunaweza tukashauri ngazi za juu namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, nina shule yangu moja inaitwa Mirundikwa, shule ya Sekondari. Shule hii imejengwa kwenye majengo ambayo yaliachwa na Jeshi miaka ya 1998. Kwa kutoa barua kukabidhi vijiji kwamba eneo hilo linaachwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ligawiwe vijiji na mimi nilikuwa kwenye Kamati mojawapo ya kugawa vijiji vinavyozunguka eneo lile lililobaki. Eneo hilo lilikuwa ni shamba la Mirundikwa *State Farm* zamani, Wanajeshi walipoingia mwaka 1998. Walipoingia na kukomesha shughuli zao mwaka 1998 wakaliacha eneo na Halmashauri mwaka 2000 wakaanza kulitumia, tukagawana na kuanza kujenga miundombinu, tukajenga shule nzuri sana ya sekondari katika suala la kuondoa kero hizi za elimu kulingana na jinsi mnavyotuagiza. Tumejenga shule nzuri sana, imefikia kiwango cha *form six.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumeambiwa kwamba tarehe 1 Januari shule hiyo inafutwa, itafutwe sehemu nyingine Wanajeshi wanaenda pale. Shule hii ilikuwa inafanya vizuri sana katika Wilaya ya Nkasi, ni moja kati ya *High School* iliyokuwa inafanya vizuri sana. Takwimu zinaonesha tu hapa mwaka jana kulikuwa na mchepuo wa *HGK, HGL* na *HKL*, wasichana peke yake walikuwa 32, *division one* tulipata wanne shule ya kwanza hiyo, *division two* tukapata 14 na wote waliobaki ni *division three.* Kwa hiyo ilikuwa ina-*perform* vizuri sana na wananchi wakaiunga mkono wakaendelea kujenga miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wametuparaganyisha kwa maagizo ya haraka kwamba sasa shule itoke ili lianzishwe jeshi hapo. Sisi tunaomba mtuachie hii shule tumeijenga wenyewe, katika kutafuta wananchi wetu waweze kupata elimu, waweze kuishi maisha bora. Hata hao wanaotoa maamuzi kama wasingepitia shule, wasingekuwa na ubavu wa kutoa maamuzi haya. Jambo hili mimi limeniumiza sana katika eneo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kusema kwamba, athari zimepatikana kubwa zaidi ya watoto mia tatu hamsini na kitu hawana pa kwenda, wamepata athari ya kisaikolojia, wanaanza kwenda shule moja, moja wamegawanywa kwenye shule mbalimbali za Wilaya yetu jambo ambalo litapunguza sana *performance* yao. Sasa jambo hili lazima kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi inalazimika leo kutenga bajeti yake imetumia zaidi ya milioni 50 kutoka kwenye vyanzo vyao kwa hiyo haiwezi kuendesha shughuli zake zingine. Kwa mujibu wa Mthamini ni zaidi ya milioni 871 zinatakiwa, hii milioni 871 zinatakiwa ili kurejesha miundombinu kwenye shule ambayo tunaijenga upya ambayo tunajenga katika eneo la Kasu. Sasa wananchi waliokuwa wamemaliza shughuli zao, wamemaliza wakaanzisha mpaka shule ya *high school* leo wanaanza upya, Serikali haina mchango hata kidogo, kwa kuanza upya hii ni athari kubwa sana na watu wameathirika na kwa namna hiyo hawawezi kuipenda Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi ni mazuri lakini utaratibu huu unaweza kuwa na lengo zuri la kiusalama lakini athari zinazopatikana kwa wananchi mziangalie nazo. Halafu shule hii ni ya wananchi, tumejenga wenyewe na hawajatushirikisha kutoa mawazo ili shule hii iendelee. Naomba Waziri anayehusika hili jambo aliangalie kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuna athari kubwa, Halmashauri na wananchi wana kipato kidogo, walijikusanyia wakajenga miundombinu mingi mpaka ikawa shule nzuri yenye Kidato cha Sita sasa hakuna shule tena. Maeneo ya Jeshi yapo, ungesema acheni sekondari tafuteni maeneo mengine sisi tungewapa eneo lingine, kwa nini msifanye hivyo mchukue shule yetu? Haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Luwa Sumbawanga kuna eneo ambalo lililkuwa la Jeshi zamani na halijaathirika chochote na lipo mpaka sasa, waliliacha kama la kwao na wala hawakulikabidhi kwa wananchi. Kwa nini wasichukue hata eneo hilo lingeweza kufanya hiyo kazi? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Rais aisikie habari hii na Viongozi wote ambao mnahusika mtuchangie, kama mnataka lazima iwepo shule Wizara ya Elimu leteni hela. Wizara ya Ulinzi ambayo mnataka tujenge sekondari pale leteni hela! Waziri Mkuu uliyeamua katika utekelezaji wa shughuli za Serikali shule yetu ifutwe tuliyojenga wenyewe tuletee pesa tujenge kwenye Sekondari yetu ya Kasu. Wananchi wanafanya kazi za kilimo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala hili la Utawala Bora. Kuna kijiji changu kinaitwa kijiji cha Kasapa, ni kijiji cha asili kilianzishwa miaka ya 1960. Mwaka 2010 kwa Tangazo la Serikali Na. 301 kimekuwa kijiji kamili na sisi tunategemea kilimo. Juzi tarehe Mosi mwezi Januari watu wa *TFS* wameenda kusema kijiji hiki kiko kwenye msitu wao, maeneo yote ya watu wanayolima ambayo ni mashamba wamesema ni maeneo yao, kwa hiyo, mazao yamefyekwa katika maeneo yale! Katika kipindi hiki ambacho hali ya chakula ni tete!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuongea nao na wakati huo nikaenda hata kwa Mkuu wa Mkoa kuona uwezekano wa maeneo hayo ambayo zaidi ya hekta 2000 zimelimwa mahindi wayaachie angalau miezi minne ili waweze kuvuna na kuondoka kama ni lazima wakati taratibu nyingine zinafanyika. Wamenikatalia, sikusikilizwa hata na Mkuu wa Mkoa kwa kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limenifadhaisha na limefadhaisha wananchi. Kijiji kile kilitupa kura sisi, mimi na Mheshimiwa Magufuli kiwango cha juu, tuseme watu wote walitupatia kura. Leo hii wanashangaa kuona Mbunge wao hana uwezo wa kutetea jambo hilo angalau kwa miezi michache! Hatujasema tumekataa, tumesema angalau miezi ambayo watu wamelima mazao tayari! Kwa nini wafyeke mazao yote! Nimeenda kushuhudia wamefyeka ekari 15 zaidi ya hekta 2000 kwa mujibu wa Mhifadhi mwenyewe na yenyewe wamesema hakuna mtu wa kuingia na hakuna mtu anayeingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Kaya 395 zimeathirika na wala hawaendi shamba wamekaa tu. Watu zaidi ya 2000 ambao wanategemea kilimo katika kijiji kile hawatakuwa na chakula, mjiandae kutuletea chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejitahidi kwa kadri nilivyofanya, nimeshirikiana na *DC,* nimeshirikiana na Mkuu wa Mkoa, lakini haikuzaa matunda! Nikaenda kumwona Mtendaji Mkuu wa *TFS* nikamwelezea hoja anaielewa, lakini anakuwa mwoga nadhani bila shaka, baadaye alisema hapana, imeshindikana! Hii ni kuogopa! Mazingira yanayofanywa na Watendaji mimi nafikiri ni ya uwoga bila sababu kwa sababu, Mheshimiwa Rais ni Kiongozi ambaye anataka utawala wa uwajibikaji…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Taska Mbogo na ajiandae Mheshimiwa Abdallah Chikota. Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nami naomba niongelee suala la ripoti yetu ya Kamati ya Katiba na Sheria, na-*declare interest* mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie ufinyu wa bajeti. Kamati yetu ya Katiba na Sheria tulishindwa kukagua miradi ambayo iko nje ya Dar-es-Salaam kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Kamati imepewa milioni 20, milioni 10 kwa safari za ndani, milioni 10 kwa safari za nje. Kamati ina Wajumbe 25 sasa kama ni safari ya nje watakata tiketi ni shilingi ngapi hiyo? Milioni 10 si itakuwa imekwisha? Kwa hiyo, matokeo yake Kamati hii ilishindwa kabisa kwenda kujifunza jinsi Kamati nyingine za Katiba na Sheria zinavyofanya kazi zake nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye Kamati yetu tuliletewa Muswada wa *Legal Aid* ambao tumetoka kuupitisha ndani ya wiki hii. Ilipaswa sisi kama Kamati tusafiri twende nchi jirani, Kenya walishapitisha huo Muswada, *South Africa* walishapitisha huo Muswada au Uganda, tukajifundishe, je, tunahitaji kuboresha kitu gani kwenye ule Muswada?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii ya Katiba na Sheria haikupata hiyo nafasi ya kwenda kujifunza kwa nchi za wenzetu wa jirani ile Miswada inasemaje. Matokeo yake tukaletewa huo Muswada, tukajadili kwenye Kamati yetu, tukawa tuna-*struggle* sisi wenyewe mpaka tukaweza kufanikisha kuleta huo Muswada humu Bungeni. Hilo naona ni tatizo na naomba kwenye bajeti ijayo Serikali ijaribu kufikiria na ijaribu kutuongezea bajeti na kuziongezea bajeti Kamati nyingine ili zisiwe zinapitisha vitu bila kuangalia nchi nyingine wanafanyaje, kwa sababu siku zote mtu unaangalia je, nyumba ya jirani wanafanyaje ili uweze kufananisha na kile kitu ambacho ninyi mmeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona kuna hitilafu siyo vibaya mtu uka-*copy* kutoka kwa jirani yako au ukajifundisha kutoka kwa jirani yako. Kwa hiyo, naomba suala la Bajeti za Kamati Serikali itakapokuja na bajeti ya mwezi wa Julai ijaribu kufikiria kuongeza bajeti ya hizi Kamati zetu, hasa Kamati yetu ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine Kamati yetu ilishindwa kwenda kukagua maafa kule Kigoma wakati kile Kitengo cha Maafa kiko chini ya Kamati yetu ya Katiba na Sheria. Samahani siyo Kigoma ni Kagera! Kagera walivyopata maafa sisi Kamati ya Katiba na Sheria tulipaswa twende kule tukakague yale maafa yameathiri kiasi gani, lakini hatukuweza kwenda kwa sababu ya ufinyu wa bajeti wakati lile fungu la Kitengo cha Maafa, fungu lake

liko kwenye Kamati yetu, lakini hatukuweza kwenda kule Kagera kukagua huo mradi kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, naomba suala hili kwa kweli Serikali mwezi wa Julai itufikirie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naomba Kamati ya Katiba na Sheria tunapoagiza maagizo, kwa mfano, tuliwaagiza *NSSF* watuletee mkataba wao walioingia na wale waliojenga zile nyumba za Kigamboni, zinaitwa *Dege Eco Village,* tuliagiza kwenye Kamati kwamba, watuletee ule mkataba kwa sababu *NSSF* huwa sera zao zinapitia kwenye Kamati yetu, tuliwahi kwenda kukagua zile nyumba pamoja na lile daraja la Kigamboni ilitushirikisha, lakini tulipoagiza kwenye Kamati tuletewe ule mkataba walioingia kati ya *NSSF* na lile shirika lililojenga hizo nyumba za *Dege Eco Village,* huo mkataba hatujaletewa mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashangaa Kamati na mimi nikiwa mmoja wa Wajumbe kwenye ile Kamati, kama Kamati inaagiza Mkataba kwa nini hao *NSSF* wasilete huo mkataba wakati sisi tulihitaji na nafikiri ni jukumu letu kwa sababu tunasimamia sera zao tuuone ule mkataba, lakini ule mkataba haukuweza kuletwa kwenye Kamati yetu. Kwa hiyo, naomba nalo hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitoa maagizo, tulienda kukagua Ofisi ya Makamu wa Rais tukakuta lile jumba limejengwa kwa nusu ya kiwango. Tumeingia pale Ofisi ya Makamu wa Rais ina muda sijui wa mwezi mmoja, lakini tulikuta mipasuko, *finishing* ilikuwa chini ya *grade,* siyo *standard!* Tukaagiza kwamba tuletewe ripoti ya fedha zilizotumika kwenye hilo jengo na tukaagiza marekebisho yafanywe, lakini ripoti ile hatujaletewa mpaka leo! Ni mwaka mzima tangu tulivyopita kwenye Jengo la Makamu wa Rais. Tulishindwa kwenda kutembelea Jengo la Makamu wa Rais lililoko Zanzibar kwa ufinyu wa bajeti, lakini Jengo la Makamu wa Rais la hapa Dar-es-Salaam tulilitembelea na kuna makosa tuliyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo tulikuta jengo halina mlango wa kutokea unapotokea moto. Jengo limejengwa chini ya kiwango! Tulikuwa tumetoa hizo tuhuma na tukawaambia kwamba, watuletee wamefikia wapi, lakini hawakuwahi kuleta mpaka leo ni mwaka mzima. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba tunapotoa maagizo kama Kamati yatekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nataka kuongea kuhusu mambo ya mamlaka ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Nafikiri kila *professional* watu waheshimiane, mtu mwingine aheshimu *professional* ya mwenzie, kama ni

Daktari aheshimike kama ni Mwalimu aheshimike. Kama ni Mkuu wa Wilaya afanye kazi zake za Ukuu wa Wilaya, lakini asimuingilie kwa mfano Daktari! Daktari ni *professional,* yuko *professional,* Mwalimu yuko *professional,* Injinia wa Mkoa yuko *professional* au wa Wilaya yuko *professional,* kwa nini aingiliwe katika utendaji wake wa kazi? Kila mtu aheshimu *profession* ya mwenzie. Tukiheshimiana hivyo kila mtu atatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitawezekana kwamba, mtu anakuwa ni Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa anaenda kutoa maagizo ya mambo ya *Engineering* wakati yeye siyo *Engineer,* anajuaje *standards* za *engineering?* Mtu ni Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya anaenda kutoa maagizo ya Daktari, yeye hajasomea udaktari, hana *profession* ya udaktari! Anatoaje maagizo kama hayo? Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa anaenda kutoa maagizo ya Afisa Kilimo, yeye hajasomea kilimo! Anajuaje mambo ya kilimo? Mkuu wa Mkoa siyo Mwalimu. Kila *profession* iheshimiwe! Mkuu wa Wilaya afanye kazi zake, Mkuu wa Mkoa afanye kazi zake tuheshimiane katika *profession* zetu ili tuweze kujenga hii nchi kwa sababu, usitoe maagizo ambayo hujasomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hilo liweze kufikiriwa na watu waweze kuwajibika kwenye nafasi zao ili wasiogope kwa sababu, hili litazua utendaji mbaya wa kazi maana mtu atashindwa kutimiza wajibu wake kwa sababu atasema kwamba, nikifanya hivi Mkuu wa Wilaya atanifokea! Nikifanya hivi Mkuu wa Mkoa atanifokea! Matokeo yake ni yule mwananchi wa chini ambaye anahitaji zile huduma za *Engineer* au huduma za Daktari ndiye anayeathirika, Mkuu wa Wilaya hawezi kuathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niongelee suala la Halmashauri. Kwa mfano mdogo tu kule kwetu, ile Halmashauri ya Mpanda haina gari la kuzolea taka na hizi Ofisi za Wizara hii ya TAMISEMI imeziachia majukumu hayo Manispaa. Manispaa nyingine ni maskini siyo tajiri na hazina uwezo wa kununua hayo magari ya kuzolea taka, matokeo yake taka zinarundikana barabarani na kusababisha kipindupindu unasikia hakiishi*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo tu kule Kalema kuna kipindupindu na pale Mpanda taka zinaweza zikakaa wiki moja hazijazolewa kwa sababu hawana gari la taka na hawana uwezo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Taska. Mheshimiwa Chikota na wajiandae Mheshimiwa Maida, Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Omary Mgumba.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia taarifa hizi za Kamati mbili, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa na ile ya Katiba na Sheria. Mchango wangu utajikita katika maeneo manne, eneo la kwanza linahusu utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyooneshwa kwenye taarifa zote mbili kwamba, utekelezaji wa miradi bado sio wa kuridhisha kwa sababu fedha kutoka Hazina hazipelekwi kwa wakati. Hii ina madhara sana kwa sababu, mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye ngazi ya Wizara inapopanga mpango mpya wa bajeti wakati fedha zile za mwaka uliopita hazijapelekwa kwa wakati huwa wanakuwa katika kigugumizi kwamba, nini kifanyike katika mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipobadilisha *budget circle* tulikuwa na matarajio sasa kwamba, kwenye *quarter* ya kwanza au ya pili, fedha za maendeleo zingetolewa, *budget circle* imebadilishwa, mambo ni yaleyale, fedha hazitolewi kwa wakati. Sasa hivi Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaandaa bajeti, lakini hawajapata fedha nyingi za maendeleo! Kwa hiyo, wanaishia katika kugombana tu kwamba, watekeleze ipi? Ile bajeti ya mwaka jana iwe kama bakaa kwamba ni miradi ambayo haikutekelezwa ili watenge fedha nyingine mwaka huu au wa-*assume* kwamba fedha zitaletwa ili watekeleze hiyo miradi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinapochelewa hata hili tatizo ambalo limebainishwa kwenye Kamati ya Sheria kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais inatengenezwa chini ya kiwango ni kwa sababu ya fedha kutolewa kidogo kidogo, kwa hiyo, hata Mkandarasi hawezi kutekeleza mradi kama ilivyopangwa kwenye mpango wa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili utahusu huu mradi wa *TASAF*, hakuna anayepinga mradi huu. Mradi huu kwa kweli umenusuru kaya maskini na umeleta mchango mkubwa sana katika kuboresha maisha ya kaya maskini katika nchi yetu, vilevile umewezesha sasa kaya maskini kupata huduma za kiafya, kielimu, ambapo bila mradi huu hawa wananchi wasingepata huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto mbili ambazo nimeziona katika utekelezaji wa mradi huu. Kwanza lile zoezi la kuwatoa wanufaika ambao hawana sifa. Wale wanufaika walichaguliwa kwa kupitia mchakato ambao ulihusisha watu wengi sana na baadaye wakaanza kupata ule msaada, lakini lilipokuja zoezi sasa la kuwatoa hawa watu wameondolewa na wanaambiwa sasa hivi kwamba, warejeshe fedha zote ambazo wamelipwa chini ya mpango huu, wengine hawana uwezo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika Jimbo langu, Kijiji cha Namisangi kuna wananchi ambao wakisikia mlio wa gari tu wanakimbia kwa sababu wamepewa barua na Mkurugenzi warejeshe zaidi ya sh. 400,000 na hawana uwezo wa kurejesha. Kwa hiyo, naomba Wizara husika sasa imchukulie hatua yule Mratibu ambaye kwa uzembe wake alipeleka fedha kwa watu ambao sio wahusika, lakini isiwe hawa wananchi ambao sasa wanapata taabu ya kulala porini wanaogopa kukamatwa kwa sababu ya fedha ambazo walikuwa wananufaika wakati ule mchakato ulipoendeshwa kwa taratibu ambazo zilifuatwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna changamoto katika uratibu wa mradi huu kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa mipya. Kwenye Halmashauri mpya unaambiwa kwamba, wanufaika wataendelea kupata huduma kutoka kwenye Wilaya Mama, kwa hiyo, inakuwa ngumu sana Mkurugenzi wa Wilaya Mpya kufuatilia zoezi hili kwa sababu, bado Mratibu anatumika wa ile Wilaya Mama. Nafikiri wakati umefika sasa kwa Wizara husika ione kwamba, eneo la utawala likianzishwa basi na taratibu za Wilaya ile kunufaika na mradi huu ziendelee kama ilivyo Wizara nyingine, hili suala la kwamba, waendelee kuratibiwa kutoka kwenye Halmashauri Mama inaleta urasimu na inakuwa ni vigumu katika kusimamia mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu yangu ya tatu ni kuhusu Tume ya Utumishi wa Walimu *(TSC)*. Imeoneshwa hapa na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa kwamba kuna kusuasua kuanzishwa kwa Tume hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kwa sababu, baada ya kupitisha Sheria hii tuliona kwamba, ni mkombozi kwa Mwalimu, lakini bado kuna kusuasua. Sasa wakati sheria hii ilipoanzishwa watu walitoa maoni yao kwamba, tusibadilishe jina, hii Tume ipewe nyenzo. Tunakokwenda sasa hivi inalekea hii Tume haitapewa nyenzo, kwa hiyo, inakuwa tumebadilisha jina tu, lakini utaratibu ni ule ule. Ni kama tulivyofanya kwenye sekta ya elimu, Ofisi ya Mkaguzi wa Shule tukabadilisha kwamba, Mdhibiti wa Ubora wa Elimu, lakini

tumebadilisha jina tu rasilimali bado ni chache na Wakaguzi bado wanapata shida na hawawezi kuzifikia shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipotenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu tutakuwa tunawadai Walimu wawajibike wakati haki zao hatujawapa. Tunakimbilia kuwavua vyeo, sijui kuwateremsha madaraja, wakati vitu vyao vya msingi hatuwatekelezei! Hebu niiombe Serikali yangu itenge fedha za kutosha ili tuanzishe hii Tume ya Utumishi wa Walimu, Walimu wapate stahiki zao, Walimu wapate motisha, Walimu wawe na chombo kimoja cha kuwatetea halafu baadaye tuwabane katika uwajibikaji. Haiwezekani tuwabebeshe mzigo mkubwa, lakini inapokuja kuzungumzia maslahi ya Walimu sisi tunarudi nyuma. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kwamba, Walimu hiki chombo kinaanzishwa haraka na kinatengewa fedha za kutosha ili kiweze kutatua kero za Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie suala la utawala bora. Yamesemwa mengi sana kuhusu madaraka ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Hili suala ni *two way traffic,* kuna watendaji ambao ni wabovu, naomba Waheshimiwa Wabunge tunapochangia tusiwalee wale watendaji wabovu. Kuna watendaji ambao wapo kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa ni nusu miungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *DMO* mmoja katika Halmashauri fulani akipata fedha za *Busket Fund* anaangalia zile semina tu za kuhamasisha sijui kutoa mabusha, kufanya nini, lakini dokezo la kununua dawa, amepata fedha migao miwili ya *Busket Fund,* hajanunua dawa, lakini zile za posho za kwao wameshatumia tayari! Kwa hiyo, wananchi wanapata shida kwa sababu ya uzembe wa mtu mmoja, anapochukuliwa hatua tusione kwamba ni matumizi mabaya ya sheria, hapana ni *two way traffic!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine wale Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wasitumie vibaya ile sheria iliyoanzisha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sura Na. 97 ya mwaka 2002 inatoa maelekezo, iko wazi kabisa. Inatoa maelekezo nini kifanyike mtu anapokamatwa kwa masaa 48 lakini Wakuu wengi wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, hawaitumii. Hata Wakurugenzi kwa sababu kuna ishara sasa hata Wakurugenzi wanataka kuingia huko kwamba kuna maeneo mengine hakuna maelewano kati ya Mameya na Wakurugenzi. Kwa hiyo, tutengeneze mafunzo sasa kwa Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maida kama hayupo Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Omary Mgumba ajiandae.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kukushukuru wewe na kukupongeza kwa kufika huu mwaka salama kwa sababu kuna wakati kidogo afya iliyumba, Mungu akubariki kwa sababu tunakuhitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kuwapongeza Mawaziri wote, Mheshimiwa dada yangu Kairuki pamoja na Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Waziri wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia katika Utawala Bora. Kabla sijaanza kuchangia nitoe pole sana kwa wananchi wa Jimbo la Kilolo kwa *accident* ya *bus* ya Vitu Laini ambayo ilitokea hivi karibuni na kuua watu wengi na jana pia ndege moja ndogo ilianguka katika Jimbo la Kilolo, nawapa pole sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia; jana Mheshimiwa Rais alipokuwa kwenye shughuli ile ya haki kuna kitendo ambacho kilitokea pale, kitendo cha yule mama ambaye alipiga kelele alihakikisha kwamba anapata nafasi ya kuongea na Mheshimiwa Rais, lakini ukifuatilia malalamiko ambayo yule mama alikuwa anayalalamikia ni utawala bora. Kwamba ameingia kila mlango lakini alikosa kusikilizwa na kupewa haki zake. Ameingia Mahakama zote yule mama ameshindwa kusikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa najiuliza hivi ni akinamama wangapi hasa wajane ambao wanakosa haki zao? Je, watakuwa na ujasiri kama ule? Hii ni changamoto kwetu viongozi kwamba kama hatuwasikilizi watasubiri mpaka Mheshimiwa Rais atakapokuja kwenye mikoa yetu na wilaya zetu ndipo wasimame haki zao zipatikane. Naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia tunafanyaje jambo hili. Kuna watu wale wa Haki za Binadamu nafikiri wapo, kile kitengo nafikiri kikiimarishwa kikapewa nguvu kingeweza kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukienda Mahakamani kesi zinachukua muda mrefu, ukienda mahabusu na magereza zetu zimejaa, lakini ukienda pale kesi ambazo mimi nikiri nilishawahi kuwa Mkuu wa Wilaya, nilikuwa naingia mara kwa mara kwenye magereza, unaweza ukashangaa kesi nyingine siyo za mtu kukaa mahabusu, ukikaa pale utashangaa. Nafikiria sasa ni wakati muafaka Jeshi la Polisi na Mahakama wakashirikiana, sio lazima mtuhumiwa akituhumiwa leo lazima akamatwe leo, upelelezi unaweza ukafanyika akiwa hata bado

hajakamatwa, wakati anakamatwa basi moja kwa moja upelelezi unakuwa umekamilika na haki inatendeka, aidha, kuachiwa au kufungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamelalamika kuhusu utendaji wa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Kwanza nianze kwa kuwapongeza kwa sababu wenyewe wamekiri kwamba hawajapata semina. Mimi niwape tu semina kidogo ndugu zangu hasa Wakuu wa Wilaya kwa sababu na mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya, kwamba maamuzi yao yazingatie taratibu na haswa washirikishe Kamati zao za ulinzi na usalama, siyo kuanza tu kutoa maamuzi bila kushirikisha ile Kamati ya ulinzi na usalama. Naamini wakishirikisha Kamati ile basi busara zitatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia washirikishe vyombo na taasisi za dini, kuna wazee maarufu, linapotokea jambo haina haja ya kukurupuka, lazima usikilize pande zote mbili ndipo utoe maamuzi. Kwa sababu kuna baadhi ya watu ambao ni watendaji wazuri tunaweza tukawapoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia awamu hii imesaidia sana kutia nidhamu kwenye kazi. Leo hii ukienda Ofisi yoyote ukikaa pale kwenye benchi huwezi kukosa mtu wa kuja kukuuliza kwamba bwana una shida gani, umesikilizwa? Kwa hiyo, nikupongeze Mheshimiwa Kairuki kwamba sasa watumishi wanaanza kurudi kwenye *line* isipokuwa tu Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na Watendaji wengine wapunguze, wawasiliane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linasikika sana kwa sababu nao kwa kiherehere wanataka kila jambo litoke kwenye vyombo vya habari, mambo mengine yanakuwa kimya kimya, ukitaka kila kitu kitoke madhara yake ndiyo hayo. Hiyo nidhamu ni nidhamu ya uwoga, waache uwoga wafanye kazi wataonekana tu. Mheshimiwa ameshajua nani atabaki na nani ataondoka, wasiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la *TASAF*. Niseme wazi kwamba suala la *TASAF* ni kitu kizuri, niwapongeze sana *TASAF* kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Mimi ni Mjumbe wa TAMISEMI tumezunguka mikoa mingi, tumeangalia kazi ambazo zinafanyika na nyingine ukienda kama Pemba kule unaweza kushangaa mambo ambayo wanayafanya, wameenda mbali zaidi na sasa hivi wanafanya na mambo ya uchumi kwa kutumia fedha zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwa kuwa baadhi ya sehemu kumeonekana kuna matatizo turekebishe yale matatizo, tatizo kubwa lipo kwa Watendaji wa Halmashauri zetu, kwa sababu hawa Watendaji ndiyo

wanapelekewa pesa, kwa hiyo, wao kwa sababu ya mazoea ya miaka ya nyuma walishindwa kubadilika. Sasa hivi nafikiri tukae tuone tunafanyaje ili *TASAF* iweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiri wazi hata Waheshimiwa Wabunge mmeona msongamano wa wale watu ambao walikuwa wanahitaji msaada kwetu umepungua, umepungua kwa sababu ya *TASAF;* wengi wanakuwa wamemaliziwa matatizo yao huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho kabisa ni ajira. Tunashukuru sana kwa kazi ambayo mmeifanya, mmefanya uhakiki vizuri sana tena tunakuombea na Mungu akubariki. Sasa kazi iliyobaki ni ajira maana vijana ambao tumewasomesha sasa wasije wakaingia kwenye mambo mengine mabaya, juzi Dangote alitangaza kazi za udereva walioomba wengi ni kutoka Vyuo Vikuu kwa sababu hakuna kazi. Kwa hiyo, nafikiri wewe tangaza ajira na hivi umeshaanza basi wengi watapata na mimi niombe kwa kupitia nafasi hii vijana watulize munkari kwamba ajira sasa zitamwagwa na Serikali yetu hii itatujali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kwa sababu muda ninao nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu. Kwa kweli kazi aliyoifanya ni kubwa, mabadiliko tunayaona na mwenye macho haambiwi tazama anaona mwenyewe, kazi iliyobakia ni sisi kuwasaidia. Tuwasaidie tufanye kazi tuwe kitu kimoja ili tusonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kanyaga twende, ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Omary Mgumba, ajiandae Mheshimiwa Vedasto Ngombale.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango huu katika mada iliyopo mbele yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze moja kwa moja kwenye asilimia kumi ya vijana na akinamama. Niungane na wajumbe wenzangu waliotangulia, wengi wameshachangia mada hii hasa kutilia msisitizo kwenye hii asilimia tano ya vijana na asilimia tano kwa akinamama. Pamoja na kuchelewa kwa fedha za *OC* kwenda Halmashauri kwa sababu jambo hili ni la kisheria na jambo hili ambalo kwa sisi ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tuliahidi kwa wananchi.

Naishauri Serikali ni vizuri ikafunguliwa akaunti maalum katika Halmashauri zetu kutenga fedha ili kila mwezi kwenye mapato bila kujali *OC* imekuja au haikuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi kwenye bajeti zetu kule kwenye Halmashauri kama tulivyoona asilimia kumi inakwenda kwa vijana na akina mama, asilimia hamsini kwenye miradi ya maendeleo na asilimia arobaini kwenye matumizi ya ndani. Sasa mara nyingi wakati mwingine bajeti zinawekwa kubwa kwa ajili ya kupata hiyo asilimia 40 ya *OC* na matokeo yake kila hela inayokusanywa kwa kisingizio kwamba *OC* haijaja hela yote inatumika katika matumizi ya kawaida na matokeo yake hakuna mradi wowote wa maendeleo unakuwa umetekelezwa kwa kutumia fedha za ndani wala kwenda kwenye hii asilimia kumi kwa vijana na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri kwamba kila mwezi kila fungu ambalo tulilolipangia kwenye mipango yetu katika Halmashauri likawekwa kwenye akaunti yake ili kama *OC* haijaja basi athari iwe kwenye *OC,* katika ile miradi ya maendeleo iendelee ili tukifika mwisho tunajua *OC* tumekwama wapi ili wajibane wapi na ile miradi yetu ya maendeleo asilimia ile hamsini iliyotengwa hata kama tusipoimaliza yote lakini angalau kwamba kwingine tutakuwa tunaipunguza, la sivyo itakuwa kila kitu inaishia kwenye *OC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye suala la semina kwa viongozi. Ndugu zangu kama tulivyoona asilimia arobaini ya bajeti ya Serikali inakwenda kwenye miradi ya maendeleo. Hiyo miradi ya maendeleo inakwenda kule chini na watekelezaji na wasimamizi wakubwa ni Madiwani, lakini mpaka tunavyosema hivi hao wasimamizi wa miradi mikubwa na kutazama *value of money* kule chini hawana semina yoyote. Maana yake ni nini? Hawajui wanachoweza kukisimamia, kipi ni kipi. Ni vizuri pamoja na kujibana tukawapa mafunzo hawa Madiwani ili wawe na uelewa mpana wa kusimamia kile wanachopaswa kusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; pia hata wale Viongozi wetu kule wa Serikali za Vijiji, kwa sababu kule hela zote hizi zinakwenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji na Afisa Mtendaji. Afisa Mtendaji ni mwajiriwa wa Serikali ana mshahara, lakini huyu *signatory* ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji hana posho wala mshahara na ukizingatia ile asilimia ishirini haiendi huko. Kwa hiyo, anasimamia kitu ambacho yeye hafaidiki na chochote, sasa matokeo yake hata kudanganywa na Watendaji ili miradi hii isitekelezwe kwa kiwango kilichokubaliwa inakuwa ni rahisi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali yangu tukaangalia ni namna gani tunaweza kuwalipa chochote hawa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Mitaa au posho ili waweze kusimamia miradi yetu kwa weledi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye utawala bora; suala hili la utawala bora hasa katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa uteuzi mzuri alioufanya kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, lakini pamoja na uteuzi huo bado hawa watu wanahitaji semina elekezi. Nasema hivyo kwa sababu kuna mambo mengi yanatokea hasa kwenye mgongano wa kimadaraka kule katika Halmashauri zetu.

Nitoe mfano tu kwenye Halmashauri yetu, unakuta Baraza la Madiwani wakati mwingine limeamua kwa mujibu wa kanuni na sheria lakini anaweza kuja Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa akasitisha yale maamuzi ya Baraza la Madiwani yasifanyike na matokeo yake Mkurugenzi anakuwa katika wakati mgumu amsikilize nani, alisikilize Baraza la Madiwani au amsilikize Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tuna ushahidi dhahiri upo umetokea kwenye Halmashauri zangu na matokeo yake Mkurugenzi huko analaumiwa na huku analaumiwa. Wakati mwingine tunawalaumu Wakurugenzi siyo maamuzi yao lakini kwenye kutumikia mabwana wawili na wakati mwingine majukumu yao hawayajui na mipaka ya kazi zao hawaijui, wanakuwa wanayumba yumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja tu ambao ulifanyika ndani ya Baraza la Madiwani; tumefanya maamuzi sahihi ya kuhamisha Halmashauri yetu kutoka Morogoro Mjini kwenye vijijini kwamba kikwazo kilikuwa pesa, tumepata pesa baada ya kushauriana na Wizara ya TAMISEMI yenyewe kwa msaada mkubwa ambao ametupa Mheshimiwa Waziri Simbachawene na timu yake, yule mdaiwa sugu matokeo yake akatulipa…

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo, kuhusu utaratibu!

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jali muda wangu maana muda wenyewe mchache, siku yenyewe moja tunaijadili hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary hebu kaa kwanza.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa hiyo, kwanza nampongeza Mheshimiwa Simbachawene kwa ushirikiano mkubwa sana alioipa Halmashauri ya Morogoro mpaka huyu mdaiwa sugu

akatulipa hela zetu, tukapanga muda ndani ya mwezi mmoja tuhamie Makao Makuu kwenda Mvuha, kutoka Mjini kwenda Vijijini, lakini kabla ya maamuzi yale hayajafanyika, anajiandaa Mkurugenzi na timu yake anakuja Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa kupitia *RAS* anawabeba Wakuu wa Idara kawapeleka Mvuha kawabwaga pale anasema anayetaka kazi ndiyo hapa nimemfikisha, asiyetaka hamna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lile halina choo, halina ofisi wala kitu chochote, lakini kwa kukubali kwamba ni mkubwa amesema hawa watu wakakaa kule, matokeo yake nini? Huo ni mfano mmoja mdogo sana. Sasa ni vizuri hawa watu wakapewa semina elekezi ili kila mmoja ajue madaraka yake na kila mtu ajue mipaka yake. Kwa sababu hawa wananchi Baraza la Madiwani ndiyo tunatakiwa tutetee maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu watumishi kutokujiamini katika kutoa maamuzi, huu ni mfano hai upo ndani ya Halmashauri ya Morogoro, tuna tatizo kubwa sana kule la wakulima na wafugaji, lakini ni kosa kwa kiongozi wa kuchaguliwa, uwe Mbunge au Diwani kusema kuna tatizo la wakulima na wafugaji. Umetokea mfano Diwani mmoja wa Kolelo amewekwa ndani mara mbili na vyombo vyenye mamlaka kwa kusema kwenye Kata yake kuna tatizo la wakulima na wafugaji, anaonekana ni mchochezi, sisi Wabunge ndiyo tulienda kumtoa zaidi ya mara mbili. Tunasema haya ni nini? Lakini Mungu siyo Athuman baadae yakaja kutokea mapigano makubwa sehemu ile ile viongozi waliyokuwa wanakataa kwamba hakuna mapigano ya wakulima na wafugaji; hakuna tatizo la wafugaji kuvamia kwenye mashamba ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi ni kwa nini? Kwa sababu hawa viongozi wetu walishapewa miongozo kwamba sehemu yoyote kwenye tatizo la wakulima na wafugaji likitokea basi Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa hana kazi. Sasa wakati mwingine wanatumia kuficha maovu kwa kuogopa wao kuja kuchukuliwa hatua. Niombe sana tuwape moyo hawa viongozi, ni bora waseme ukweli ili tutatue tatizo kuliko kuficha baadaye mambo yanakuja kuharibika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TASAF*; kwanza niipongeze sana Serikali kwa mradi huu wa *TASAF* umesaidia sana kaya maskini, lakini naomba sana elimu iongezwe hasa kule vijijini hakuna elimu, wananchi hawajapata elimu sawasawa, kwa sababu wanaamini hasa wazee kwamba huu ni mradi wa kusaidia wazee, hawajui kwamba ni mradi wa kusaidia kaya maskini. Sasa ni lazima iongezwe ijulikane kuna tofauti ya kusaidia wazee na kusaidia kaya maskini. Mara nyingine unaona kuna mgogoro wanakwambia kijana ana

nguvu zake lakini yupo kwenye mradi wa *TASAF*, kumbe ni kijana lakini hana uwezo kiuchumi. Kwa hiyo, ni vizuri elimu ikaongezeka kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niongelee sasa kwenye Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu suala la *NSSF*. Niungane na maoni ya Kamati kwa sababu ya utawala bora na kwa sababu tuna mihimili mitatu, Bunge, Mahakama na Serikali na Serikali imeshaanza kuchukua hatua katika wale watuhumiwa ipo kwenye vyombo vya uchunguzi, ni vizuri sana tukaipa nafasi Serikali ikamaliza uchunguzi wake, lakini naomba kuishauri baada ya uchunguzi huo walete taarifa hapa Bungeni ili ukweli ubainike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vedasto Ngombale ajiandae Mheshimiwa Hamad Salim Maalim.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Mchango wangu nitaanza kujielekeza kwa ndugu zangu wa TAMISEMI. Serikali ya Awamu ya Tano toka iingie madarakani haijaongeza nyongeza ya mishahara, lakini pia watumishi wamepandishwa madaraja lakini hakuna mabadiliko ya mishahara kutokana na madaraja waliyopandishwa. Sasa naomba Serikali iwaangalie watumishi ambao watastaafu katika kipindi hiki, kwamba wao walistahili wapate nyongeza hizo kwa mujibu wa sheria, lakini kwa kuwa sasa Serikali imeamua kutofanya hivyo maana yake kuna uwezekano wa watumishi hawa kukosa haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali watumishi wataostaafu katika kipindi hiki basi lazima wazingatie kwamba watastaafu kwa kukokotoa kwa hesabu zipi? Kwamba watakokotolewa kwa hesabu zile ambazo kabla mshahara haujabadilishwa au mpaka hapo sasa ambapo Serikali itaamua kuongeza nyongeza hizo za mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la waraka uliotolewa na Serikali kuhusiana na vigezo vipya vya namna gani sasa shule zinaweza zikapata usajili. Kuna waraka mpya umetolewa kwamba ili shule iweze kusajiliwa lazima shule hiyo iwe na madarasa 10, nyumba tatu za Walimu, matundu 10 ya vyoo. Suala hili nafikiri Serikali haijafanya utafiti wa kutosha kwa sababu mazingira ya maeneo ya vijijini ni ngumu sana kwa shule kuwa na uwezekano wa kujenga vyumba 10 vya madarasa, nyumba tatu za Walimu ili waweze kufikia vigezo vya kuweza kupata usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali lazima ikumbuke pia wana jukumu kubwa la kuhakikisha linafuta ujinga, linaondoa vijana ambao watakuwa na matatizo ya kushindwa kuhesabu, kusoma na kuandika, sasa kama hili halitazingatiwa maana yake upo uwezekano wa Serikali kuzalisha vijana wengi wenye shida ya kupata ujuzi huo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali bado haijawaangalia Wenyeviti wa vijiji na vitongoji, wanafanya kazi kubwa lakini bado Serikali haijawaona. Naishauri Serikali ione uwezekano wa Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji waweze kupata posho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mahusiano mazuri kati ya watendaji wa Serikali na wawakilishi wa wananchi kwa maana ya Madiwani pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Katika Halmashauri Wakurugenzi wengi wapya walioteuliwa hawana mahusiano mazuri na Waheshimiwa Madiwani na hoja kubwa katika utendaji wao wa kazi, wanasema sisi ni wateule wa Rais, kwa hiyo mara zote, hata katika mambo ambayo yanahitaji kutumia hekima na busara msingi mkubwa unakuwa kwamba sisi ni wateule wa Rais kwa hiyo tunafanya vile tunavyoona. Niishauri Serikali itoe semina kwa Wakurugenzi hawa, lakini pia inatakiwa wawashauri watumie hekima na busara ili kuona kwamba haya mambo yanakwenda katika utaratibu unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *TASAF* ambalo limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, mimi pia kwa msisitizo niseme, Serikali imefanya makosa na lazima ikubali kwamba imefanya makosa. Kwa sababu, wananchi hawa hawakwenda kwa Serikali kuomba msaada kwamba wasaidiwe katika kaya maskini hapana, ilikuwa ni utaratibu wa Serikali. Kama hivyo ndivyo Serikali ilijipanga na ikaweka taratibu zake kwa kutumia Maafisa wake. Kwa hiyo, Maafisa wa *TASAF* wanapokwenda katika kijiji fulani na kuhitaji kupata vigezo vya nani anastahili apate usaidizi huu, hilo lilikuwa ni jukumu la hao Maafisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilichotokea sasa hivi wakasema kwamba Serikali imeleta agizo la kwamba vigezo havikufuatwa ili wananchi husika waweze kupata hizo stahili, matokeo yake, kwa mfano katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini katika Kijiji cha Miteja, Mkurugenzi ameagiza kwamba fedha zile ambazo zilipelekwa kwa wananchi ambao hawakustahili zilipwe na Serikali ya Kijiji na Serikali ya Kijiji sasa inatakiwa itoe zaidi ya milioni tano, hii imefanyika katika Kata ya Mandawa na Kata nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niitake Serikali izingatie tena haya maagizo yake, haikuwa ni ombi la wananchi kupata hizo pesa, ulikuwa ni utaratibu wa Serikali, kwa hiyo Serikali lazima hili iliangalie kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitambulisho vya Taifa; hili suala imefikia mahali kwamba wananchi wanashindwa kuelewa, walikuja hawa watu wa *NIDA*, wamefanya zile *process* zote za kupata taarifa kutoka kwa wananchi lakini mpaka sasa hivi, kwa mfano kwenye Jimbo langu la Kilwa Kaskazini wananchi hawafahamu vitambulisho hivyo watavipata lini, Serikali nalo hilo iliangalie ili wananchi wapate vitambulisho hivyo vya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni suala la Mabaraza ya Ardhi; chombo hiki cha baraza la ardhi ni chombo kizuri sana na kimesaidia wanyonge kupata haki zao. Niishauri Serikali ihakikishe chombo hiki kinakuwepo katika ngazi zote. Kwa sasa, chombo hiki kinapatikana katika ngazi ya kijiji na ngazi ya Kata, baadaye ngazi ya Wilaya huwezi kupata chombo hiki, uende mpaka kwenye ngazi ya Mkoa na kule kwenye ngazi ya Mkoa kuna Mwanasheria mmoja tu. Kwa hiyo, naishauri Serikali ihakikishe panakuwa na Baraza la Ardhi la Wilaya ili basi kupeleka huduma hizi kwa wananchi. Pia sisi watu wa Kusini katika Mahakama Kuu Kanda ya Kusini kuna Jaji mmoja tu, kwa hiyo, utoaji wa haki unacheleweshwa kwa sababu Jaji mmoja hawezi kukidhi haja ya usaidizi wa sheria kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hamad Salim Maalim ameomba udhuru, anafuata Mheshimiwa Mussa Mbarouk, Mheshimiwa Conchesta ajiandae.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami kwanza nichukue fursa hii kushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia na nitaanza na TAMISEMI. Kwa mujibu wa taratibu zilizopo Serikali zipo za aina mbili, kuna *Central Government* na *Local Government*, lakini sasa kuna kitu au utaratibu ambao umeanzishwa wa kuondoa makusanyo ya *property tax* ambacho kilikuwa ni chanzo cha mapato katika Halmashauri zetu tumekipeleka katika Serikali Kuu kwa kukusanywa na *TRA*. Naona hili ni kama kuzizika Serikali za Mitaa, kwa hiyo nakumbusha kwamba Serikali za Mitaa ndizo zinazoziba aibu ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na miradi mingi ambayo inatekelezwa na Serikali za Mitaa, kwa mfano uchongaji wa barabara za vijijini,

miradi ya maji vijijini, pamoja na kwamba inapelekewa fedha na Serikali Kuu lakini bado wenye mamlaka ya kusimamia ni Serikali za Mitaa. Sasa kuzinyang'anya Serikali za Mitaa chanzo hiki cha *property tax* ni kuziua Serikali hizo. Kwa hiyo, nashauri kwamba ikibidi *property tax* irudishwe katika Serikali za Mitaa kama kweli tunataka miradi ya wananchi inayofika moja kwa moja katika Halmashauri zetu iweze kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala zima la mapato, leo ukienda kwenye Halmashauri zote zipo hoi kimapato, baada ya kunyang'anywa chanzo kile zimekuwa kama zimechanganyikiwa, zimekuwa zikitegemea tu kupata ruzuku kutoka Serikali Kuu ambayo nayo inacheleweshwa, inaletwa katika robo ya mwisho ya Mwaka wa Fedha wa Serikali, matokeo yake sasa inafanywa miradi kwa kukurupuka, miradi mingi inakuwa chini ya viwango na hapohapo pia ndipo watu wanapopiga 'dili'. Nashauri bado tuzitazame sana Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tukumbuke pia Serikali za Mitaa kama alivyotangulia kusema mmoja imekuwa ni kama jalala, mizigo yote imesukumwa kwenye Serikali za Mitaa; elimu ya msingi na sekondari zinasimamiwa na Serikali za Mitaa, miradi ya maji vijijini inasimamiwa na Serikali za Mitaa na miradi mingine ya afya bado inasimamiwa na Serikali za Mitaa. Hata hivyo, tukija kwenye elimu kwa mfano, elimu kwa mujibu wa utaratibu siyo biashara ni huduma, lakini kuna utaratibu ambao umeanzishwa tena wa kukusanya mapato kutoka kwenye hizi *English Medium Schools,* matokeo yake sasa wamiliki wa shule nao kwa kuwa wanatozwa fedha nyingi, wanaongeza ada matokeo yake wananchi au wazazi wanashindwa kuwapeleka watoto katika hizi shule za *English Medium. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali, ikibidi tuondoe hii tozo ya kodi katika hizi shule za *English Medium*, vilevile pia hata kwenye sekondari. Tunasema hapa elimu bure lakini ukiangalia, kwa mfano katika sekondari kumesamehewa sh. 20,000 tu ya ada, vikorombwezo vyote bado mzazi anatakiwa kulipia, tena baya zaidi kunatakiwa *counter books, counter book* moja sh. 5,000 mtoto anatakiwa atumie zaidi ya *counter books* 12, hapohapo tena kuna nguo za michezo, kuna *uniform,* viatu *pair* mbili, majembe, tumewasaidia tu kuondoa hilo suala la madawati baada ya fedha iliyobaki katika Bunge kuingiza fedha hiyo kwenye madawati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Halmashauri napo labda nimpongeze tu Mheshimiwa Rais kwa hili suala la kumaliza tatizo la madawati lakini bado elimu bure siyo bure. Katika baadhi ya shule wanashindwa hata kulipa walinzi,

wanashindwa hata kulipa maji, wanashindwa hata kulipa umeme! Hebu fikiria watoto wanashinda kutwa nzima lakini maji yamekatwa, yote hii inatokana na kutamka kwamba elimu itakuwa bure lakini siyo bure kwa asilimia mia moja. Nashauri Serikali kama tumeamua elimu iwe bure basi iwe bure kwelikweli kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kingine pia naishauri Serikali, TAMISEMI haina uwezo wa kulipia maji na umeme katika shule zetu za sekondari, sasa ikibidi shule za sekondari, shule za msingi, taasisi za kidini kama makanisa na misikiti, hili naona pia tungeondoa kabisa hilo suala la kuzichaji masuala ya bili ya umeme na maji tusiwe tumependelea, ili taasisi na shule hizi ziwe zinatumia maji pasipo malipo, tutasaidia kupunguza mzigo kwa wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni kawaida kwamba hata inapotokea kukiwa na majanga tunatumia viongozi wetu wa kidini kumwomba Mwenyezi Mungu aisalimishe nchi yetu na majanga na matatizo mengine sasa je, tunasaidiaje taasisi za kidini. Nashauri kupitia shule za msingi na sekondari pamoja na taasisi za kidini hizi tuondoe haya masuala ya malipo ya maji na umeme ili kama tunasema elimu bure iwe elimu bure kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika elimu natoa ushauri hata shule za *private* za sekondari tumekuwa tunawatoza kodi kubwa sana, matokeo yake na wao wanaongeza *school fees* ambayo imekuwa sasa ni kilio kwa wananchi. Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakuwa ni mashahidi, kila Mbunge hapa ana orodha ya watoto siyo chini ya 20, wote wamefaulu wazazi hawana uwezo unatakiwa Mbunge uchangie, utachangia watu wangapi? Naishauri Serikali elimu iwe bure kama katika baadhi ya nchi za wenzetu, wenzetu wanawezaje sisi tushindwe, upo usemi unaosema wao waweze wana nini, sisi tushindwe tuna nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala zima la Katiba na Sheria; mimi niliipitia taarifa hii lakini kuna baadhi ya maeneo naomba yafanyiwe marekebisho kidogo, kwa mfano, Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakuwa mashahidi, sote katika Wilaya zetu kuna Magereza, ukiwa ni mwenyeji wa kutembelea Magereza utakuta kuna akinamama ambao wana watoto wachanga wananyonyesha. Mama ndiye amefanya kosa labda ameiba, labda amefanya kosa lingine huko ametiwa hatiani, lakini mtoto mchanga anayenyonyeshwa ambaye hawezi kuishi bila mama yake inabidi naye ageuke mfungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naishauri Serikali, kwa wale akinamama ambao wengine ni wajawazito wanajifungulia kule gerezani, lakini na kwa wale akinamama wote ambao watakuwa wana watoto wachanga, hawa watoto dini zote zinaamini kwamba mtoto mdogo kuanzia miaka 14 kuja chini ni malaika, kwa nini tumtese malaika huyu akae gerezani hali ya kuwa yeye hakufanya kosa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, kama mama ana mtoto mchanga basi ama asamehewe apewe kifungo kile cha kufanya kazi za kijamii kama kusafisha hospitali, ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Mahakama, lakini kitendo cha kuwafanya watoto wachanga wawe wafungwa, hawapati haki za watoto za kucheza na watoto wenzao, hawapati muda wa kujinafasi, lakini pia mama zao wanakuwa wanyonge wanaona kwamba mimi nimekosa, mtoto wangu naye anafungwa amekosa nini. Naishauri Serikali tuangalie mtindo mwingine wa kuwafikiria hawa watoto ambao mama zao wamekuwa wafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Sheria na Katiba kuna kipengele hiki tumekipitisha hapa cha kwamba wasaidiwe wale wasiokuwa na uwezo. Mimi naomba hili jambo kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria tuliangalie vizuri, kwa sababu ni watu wengi ambao wana kesi hawana uwezo wa kuweka Mawakili, vilevile pia kuna suala zima la ajali. Nchi nyingi zilizotuzunguka inapotokea ajali wahanga wa ajali wanaokufa ama wanaopata vilema vya maisha, utaratibu katika baadhi ya nchi Mawakili wa Kujitegemea wanakwenda hospitalini au wanakutana na familia za wale wahanga wanaweka makubaliano, kwamba kwa sababu mtu wenu amefariki, ameacha wajane na watoto yatima, sisi tutaisimamia kesi ya *compensation,* kwamba huyu mtu alipwe fidia ili aweze kusomesha watoto wake ambao wamebaki yatima au kama ana mjane au wagane waweze nao kupata haki yao ya malipo yanayotokana na *insurance*, lakini nchini kwetu…………*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Kubenea na Mheshimiwa Frank George Mwakajoka wajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache juu ya hoja hizi za taarifa za Kamati, Kamati ya Katiba pamoja na TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na taarifa ya Kamati ya Katiba. Napenda tu kuongelea kuhusu utawala bora na nitajielekeza katika chaguzi zinazoendelea katika nchi yetu. Kuchagua viongozi na uchaguzi ukiwa huru na haki ni sehemu mojawapo ya kupanga viongozi na njia mojawapo ya kulea demokrasia katika nchi yoyote iliyopo duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magomvi mengi ambayo yanatokea katika nchi tunazozisikia duniani zilizo nyingi inatokana na uchaguzi usio huru na haki na dhuluma zinazotokea katika uchaguzi, manyanyaso yanayotokana na uchaguzi, wakati mwingine kulazimika kutangaza matokeo ambayo siyo halali na hufanya wananchi wachukie na baadaye wanaamua kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu nimeshiriki chaguzi hizi za juzi ambazo zimemalizika za Madiwani. Tulikuwa na Kata moja tu katika mkoa wetu, Kata ya Kimwani na nilishiriki kikamilifu mpaka mwisho. Mambo niliyoyaona napenda niyaseme hapa, kwamba sasa hivi uchaguzi katika nchi yetu umegeuka, Jeshi la Polisi limekuwa Chama cha Siasa na wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matendo niliyoyaona, bunduki, mabomu na vitisho ni dhahiri kwamba Watanzania hawawezi kuingia katika uchaguzi wakijiamini na matokeo ninayoyaona watu watakuja kuchoka na haya mambo ambayo yanafanywa na Jeshi la Polisi. Ukiisoma vizuri, mimi hakuna mahali ambapo nimeona katika Sheria ya Uchaguzi ambapo Askari wanahusika kwenda na mabomu, ninachojua wanakwenda kulinda vituo, wako Mgambo, wako Polisi, wanakwenda kulinda vituo. Kipindi hiki nimeshuhudia Polisi wanakuja na mabomu wanazuia wananchi kutoka vijijini kwenda kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako hapa vijana wa bodaboda ambao unakuta wakati mwingine wale wapigakura wanatoka mbali mno na vituo, kutokana na jiografia mbalimbali jinsi nchi yetu ilivyo. Mtu analipa bodaboda kwenda kupiga kura Polisi wanamzuia njiani yule bodaboda kumpeleka huyo mtu kwenda kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo machafu ambayo nimeyaona na kwa kweli sisi Waheshimiwa Wabunge tunapaswa kukemea mambo haya. Uchaguzi ni jambo huru, uchaguzi ni watu wanakwenda kuchagua viongozi wao, tunajua katika nchi yetu kwamba tunakwenda kwa mfumo wa Vyama Vingi, ni lazima vyama vifanye ushindani na hata kiongozi atakayepatikana ajue kwamba hicho cheo amekifanyia kazi. Hakuna sababu ya kufikishana tunakofikishana, nina wasiwasi kwamba sasa kadri tunavyokwenda tunalea vijana wetu katika

kuleta chuki na baadaye huko mbele yanaweza kutokea mambo ambayo tunayaona katika nchi hizi za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeshuhudia Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, ma-*OCD,* yaani kwenye Kata moja tu yenye wapigakura 8,000, lakini Serikali nzima ipo pale na watu wakishasikia kwamba Mkuu wa Mkoa yuko pale, Mkuu wa Wilaya yuko pale, kuna watu wengine hawakuzoea hayo na Watanzania walio wengi wako tofauti huwezi ukalinganisha na Wakenya, hawapendi mambo ya ugomvi. Kwa hiyo, unapokwenda kuwanyanyasa watu mwishowe wanaona hawana haja ya kwenda kupiga kura, matokeo yake watu wanashindwa kupata haki yao. Naomba Serikali iyatazame na hata Tume ya Uchaguzi iyatazame ili tuweze kupata viongozi wetu wazuri na tuendelee kulea demokrasia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni kauli ambazo zinatolewa na viongozi wa juu ambazo mimi naziita kama kauli za mzaha, zinaweza kutolewa na Wakuu wa Mikoa na Wilaya, lakini zinapotolewa na viongozi wetu wa juu kwa kweli zinashangaza, siwezi kusema zinatisha au zinashangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano; Mkuu wa Nchi alipotembelea Mkoa wa Kagera na mnajua Mkoa wa Kagera ulikumbwa na tetemeko, katika mkutano huo alikuwepo Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ambaye ni Mbunge wa Bukoba Mjini, alipewa nafasi ya kuongea na nafasi hiyo aliitumia kutoa mawazo kwa niaba ya wananchi, mawazo aliyoyatoa ndiyo mawazo tunayopaswa kutoa sisi Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotoa mawazo lazima Serikali ione kwamba huyu mtu ni mwakilishi wa wananchi, aliiomba Serikali na alishasema hata ndani ya Bunge hili kwamba tungependa katika Mkoa wa Kagera, tunajua hamuwezi kujengea watu wote, lakini Serikali inaweza ikatoa ruzuku katika viwanda vya mabati, viwanda vya nondo na viwanda vya saruji ili wananchi wa kule waweze kupata vifaa kwa bei ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo siyo la ajabu, wakati Mamlaka ya Kuuendeleza Mji wa Dodoma *(CDA)* enzi zile za Awamu ya Kwanza, jambo hili limewahi kutokea, vifaa vilijengwa na ikapigwa chata kuonesha kwamba ni ofa ya kuja kutengeneza Mji wa hapa Dodoma. Kitu hicho kinaweza kufanyika hata Mkoa wa Kagera na hata mahali pengine ambapo watu wanaathirika namna hiyo. Majibu yaliyotolewa na viongozi wa juu – maana yake hatuwezi kutamka majina, ukitamka hapa utakutwa hapo mlangoni, niseme Serikali, nikitamka

hapa Askari wanaweza kunisubiria hapo maana yake na wenyewe mmeshawafanya wamekuwa wanasiasa, alisema anamwambia Mheshimiwa Lwakatare akajenge kiwanda!

Waheshimiwa Wabunge ninyi mtajenga viwanda? Mimi nimekua, sasa hivi nina umri mkubwa wa kutosha tumejifunza kuhusu madini ya *tin* yaliyopo Kyerwa Karagwe tangu nikiwa mtoto wa miaka nane tu niko darasa la tatu, sijawahi kuona Mbunge ambaye anajenga kiwanda pale na wamekuwepo Wabunge mbalimbali pale. Kwa hiyo, kiongozi wa nchi anapotamka maneno ya namna hii, mimi nayaita ni maneno ya mzaha lakini pia inatonesha vidonda vya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kusema Mheshimiwa Mbunge akileta mawazo, hata kama anatoka *opposition* alichaguliwa! huwezi kumwambia basi nenda kajenge kiwanda hata mimi nitakusaidia, Mheshimiwa Lwakatare hela ya kujenga kiwanda ataitoa wapi, wengine wananiambaia eti yeye alijenga wapi, Chato hakuna kiwanda cha mabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya, hatuwezi kuacha kusema tutakuwa waoga mpaka lini? Maana yake Rais wa Nchi au Kiongozi Mkuu wa Nchi au hata kama ni Waziri ni dhamana anawakilisha watu wake na Mkoa wa Kagera hatupendi sana kuomba omba na mara nyingi hamleti msaada kule, miaka nenda rudi hamjatuletea misaada. Tuna uwezo wa kujitegemea, lakini hii imetokea na tetemeko tunajua siyo la Chama, ni maafa ya nchi lakini wananchi hawakupewa kauli za kuwastahi waweze kukaa vizuri, wakitulizwa wanajua kwamba Rais wao amewaambia maneno mazuri. Kwa hiyo, ningependa Viongozi kauli hizi sizifurahii na watu wengine katika Mkoa wa Kagera kusema ukweli hawakufurahishwa na kauli hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kuongelea kuhusu suala la TAMISEMI kidogo, labda niongelee kuhusu elimu tu. Kwamba elimu ni bure sawa, inatolewa au labda ni ya malipo lakini niongelee Bukoba Vijijini tu ambako nafanyia kazi na Mheshimiwa Rweikiza nafikiri na yeye ataniunga mkono pale. Mnakumbuka huku nyuma kuna Mkuu wa Wilaya moja anaitwa Mnari, amewahi kuwapiga Walimu wa Bukoba Vijijini viboko. Pamoja na kuwapiga au asiwapige, mazingira ya kule siyo mazuri na pia hakuna Walimu. Katika kipindi cha bajeti hapa niliomba kwamba mtusaidie Walimu Bukoba Vijijini. Mwaka huu tumepewa zawadi ya Kinyago. Pale Mkoani wanatoa vikaragosi vile, tumepewa hicho, tunaomba Mheshimiwa Simbachawene atusaidie, atupe Walimu Bukoba Vijijini. Hilo ndilo ombi langu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Frank Mwakajoka dakika tano na Cecilia Paresso dakika tano.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa napenda kuwapa pole sana wananchi wangu wa Mji wa Tunduma kwa ajali ya moto ambayo imetokea katika soko kuu la Mji wa Tunduma na kuteketeza maduka mengi ambayo wamepoteza mali zao nyingi sana, nawapeni pole sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze na suala la utawala bora katika nchi hii. Nchi hii utawala bora kwa kipindi cha Awamu ya Tano inaonesha kabisa utawala bora katika nchi hii sasa umetoweka kabisa. Nasema kwamba utawala bora umetoweka, sasa hivi hali ya watumishi katika nchi hii imekuwa ni tete, kila mtumishi amekaa akisubiri matamko, ana wasiwasi na shughuli ambazo anakwenda kuzifanya, haamini kama kesho ataamka akiendelea kuwa mtumishi wa umma katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hali ilivyo katika nchi hii sasa hivi. Jeshi la Polisi sasa wanakamata watu hovyo hovyo, Jeshi la Polisi wanaagizwa, Jeshi la Polisi wanasema wameshindwa kufanya kazi zao bila maagizo kutoka juu, hili jambo tumeliona hata kwenye uchaguzi uliopita. Katika uchaguzi uliopita wa Serikali za Mitaa, Madiwani na Wabunge tumeona hali ilivyokuwa tete katika uchaguzi huu. Imeonesha kabisa kwamba katika kituo cha uchaguzi hasa siku ya kupiga kura walikuja Polisi wengi ambao walikuwa wana mbwa na silaha nyingi kabisa, kiasi kwamba waliwatisha wapiga kura lakini pia walizuia hata Mawakala ambao walikuwa wanatakiwa kuhakiki uhesabuji wa kura wasiingie katika vituo vya kupigia kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tu kwamba kutokana na jambo hili, hata leo Chama cha Mapinduzi wanajinafasi kwamba wamepata kura nyingi na wameshinda lakini tunataka kusema kwamba asilimia kubwa ya matokeo yaliyojitokeza yanaonesha kabisa yalihujumiwa. Tunasema yalihujumiwa na hili tunalizungumza hapa watu wengi watazomea na wataona ni jambo ambalo kama vile tunatania, lakini tunazungumza ukweli na hili lina mwisho. Itafika mahali Watanzania watachukia na watakataa dhuluma pamoja na uonevu unaojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana jambo la uchaguzi na jambo la haki za watu wanapokwenda kupiga kura ni lazima lilindwe. Sheria za nchi sasa

hivi hazifuatwi na viongozi wengi wanakaa madarakani kwa sababu eti amesimamia vibaya uchaguzi na kuiba kura kuhakikisha kwamba CCM wanashinda uchaguzi. Jambo hili linasumbua sana na watu sasa hivi wameanza kukata tamaa ya kwenda kupiga kura.

Mheshimiwa Mweyekiti, nikupe mfano mmoja; Kata ya Kijichi wapiga kura walikuwa karibuni 16,800 mwaka 2015 kwenye Uchaguzi Mkuu lakini safari hii wapiga kura waliojitokeza ni 5,000 tu. Hii inaashiria kwamba Watanzania wameanza kukata tamaa na wanaona hawana haja ya kwenda kupiga kura kwa sababu hata wakipiga kura, kura zao na matokeo yao yanahujumiwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka kusema kwamba ni vizuri pia Serikali hii ikajua kwamba hizi ni haki za watu na watu wanavyokwenda kufanya uchaguzi, waacheni wafanye uchaguzi wamchague kiongozi wanayemtaka atakayeweza kuwaongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine imetokea sasa hivi, kila jambo linalozungumzwa na mtu hata kiongozi akisema kwake kuna njaa wanasema umekuwa mchochezi. Ni vizuri Serikali ikajaribu kutoa ufafanuzi, uchochezi maana yake nini? Jambo la kweli ambalo linazungumzwa nalo limeshakuwa uchochezi. Nchi hii watu watashindwa kuzungumza, watakaa kimya na wakikaa kimya tunakoelekea siyo kuzuri hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa kwenye kampeni maeneo mbalimbali. Ukizungumzia hali halisi ya chakula katika nchi hii nashangaa baadhi ya viongozi ndani ya Serikali hii wamekwenda kutoa matangazo katika mikoa mbalimbali kwamba mtu yoyote atakayesema kwamba kuna njaa anatakiwa kukamatwa. Haya ni mambo ya ajabu kabisa. Njaa haifichiki hata siku moja, njaa iko wazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na namshukuru Mheshimiwa Mwakajoka kwa kunipa dakika tano. Nami nianze kuchangia kwenye suala zima la mamlaka makubwa ambayo nafikiri *RC* na *DC* na *DAS* wanazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi sana kuona leo kwa sababu mwaka jana hapa wakati sisi Wabunge wa Kambi ya Upinzani tunajaribu kuonesha matatizo na changamoto na udhaifu ambao baadhi ya *RC* na *DC* wanayo katika maeneo yetu, tulibezwa hapa, hatukusikilizwa lakini leo humu baadhi ya Wabunge wa CCM nao wameona hiyo shida na wameanza kusema. Nafikiri huu utakuwa ni mwanzo mzuri ili tuendelee kuelewana sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba hawa *RC* na *DC* wamekuwa Miungu watu, wameona kwamba wana mamlaka makubwa kuliko mtu yeyote, hawatambui nafasi za Wabunge, wanaweza ku-*revoke* maamuzi ya Baraza na kuyaingilia, hata pale ambapo hayastahili. Ifike mahali hizo semina elekezi ambazo mlizisema zimefutwa nadhani iko haja ya kurudisha na kukaa na hao watu na kuwaambia. Siyo semina tu, hata akili nyingine tu ya kawaida ya busara ya *RC* au *DC* kujua mipaka yake, kujua namna ya kushirikisha hawa watu hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima muangalie mfumo mwingine, sijui wateuliwe wengine au wafanye nini hawa wameshindwa kazi, wamekuwa Miungu watu. *RC* anakaa kwenye kikao anaongea anasema, nadhani mnaelewa hapa kuna Waziri naweza kuwa na maamuzi makubwa kuliko Waziri hata Waziri mwenyewe anaelewa, anasema kwenye kikao na Waziri yupo, huyu ni *RC*. Sasa kama wanasema vitu kama hivi mbele ya Mawaziri unategemea nini kwa Wabunge?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RC* anakuja kwenye eneo lako, Wabunge mnaomba kuonana nae hana muda na Wabunge. Haya ni masikitiko, lakini sasa angalau tunaanza kuelewana humu ndani na angalau haya machungu na ninyi Wabunge wa CCM mmeanza kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utawala wa sheria; sioni sasa kama kuna utawala wa sheria. Kuna Mbunge mmoja ameongelea kuhusu mlundikano wa kesi au mlundikano wa wafungwa Magerezani, lakini leo kama kuna kesi ya uchochezi ya mwana CHADEMA haichukui miezi mitatu hukumu tayari na inasikilizwa haraka sana, lakini kuna watu wamekaa gerezani kwa kesi ama za kusingiziwa au ambazo siyo za kisingiziwa miaka tisa, miaka 10, miaka mitano, miaka miwili wanasema upelelezi bado, lakini mwana-CHADEMA akisema jambo tena anaambiwa mchochezi na hii tafsiri ya uchochezi itabidi mtuambie uchochezi ni nini maana yake neno uchochezi linatumika vibaya, anaambiwa ni mchochezi, anapelekwa Mahakamani haraka hukumu miezi sita, miezi nane, miezi mitatu jela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama kuna utawala wa sheria, ni lazima mjitafakari upya, muangalie kama tuna Katiba, kama tuna sheria, kama kweli kuna kutenda haki kwa nini haki inatendeka kwa watu wachache na watu wengine wananyanyaswa kwa sababu ni washabiki wa upande fulani au wa Chama fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie suala la mwisho kuhusu Madiwani; Madiwani wamekuwa ni Wasaidizi wetu hata sisi Wabunge kwa maana kama tukiwa hapa Bungeni kwenye vipindi virefu vya Vikao vya Bunge, wao ndiyo wamekuwa wakikaa na wananchi na wakiwasikiliza kero zao, lakini Madiwani wamesahaulika. Madiwani leo wanapewa posho ya sh. 350,000 basi na hizo posho za vikao, tena wako Wakuu wa Wilaya wengine wanafuta posho za Madiwani ambazo zingine ziko kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wakuu wa Wilaya wengine wanasema posho hii haitakiwi, hii haitakiwi, kweli kuna zile ambazo haziko kwa mujibu wa taratibu, lakini zile zilizoko kwa mujibu wa taratibu *DC* wanaingilia, wanazifuta. Tumewasahau Madiwani, hatufikirii kuwaongezea posho zao, tumewaacha Madiwani hawapewi mafunzo, *capacity building* haipo tena, angalau kwenye awamu zilizopita walikuwa wanapewa. Sasa unampeleka Diwani asimamie mradi wa mabilioni, yuko kwenye Kamati ya Fedha lakini hajajengewa uwezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rashid Shangazi, jiandae Mheshimiwa Joram Hongoli na Mheshimiwa Hasna Mwilima ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia jambo ambalo liko mbele ya Bunge letu Tukufu. Nitaanza na suala zima la kuchangia katika Kamati ya Katiba na Sheria ambayo na mimi ni Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu haikufanya kazi vizuri kwa sababu bajeti ilikuwa ni finyu. Kuna maeneo ambayo tulipaswa kwenda kufanya ili tuweze kuona uzoefu na pesa ambazo zimekwenda kwenye miradi lakini tumeshindwa kufanya hivyo. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba, kama utakumbuka Bunge letu Tukufu liliridhia kwamba na sisi tutoe mchango kwa wenzetu wale waliopatwa na tetemeko kule Kagera lakini pia Kamati yetu ambayo inaitazama Ofisi ya Waziri Mkuu tulishindwa kwenda hata kuwaona wenzetu wale waliokumbwa na ile kadhia. Kwa hiyo, nitarajie kwamba jambo hili tuliangalie kwa kina katika bajeti zijazo, Kamati hizi ziweze kupewa uwezeshaji wa kutosha ili zifanye kazi yake kamili ya kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika katika Wizara ya Sheria na Katiba, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Tume hii haikutengewa fedha kabisa ya kufanya kazi, zaidi ya mishahara na *OC* hakuna kingine ambacho kimewekwa katika Tume hii. Sasa tutakubaliana kwamba sasa hivi kwa kadri utandawazi unavyoongezeka na kadri ambavyo hata shughuli za kiuchumi zinazidi kupanuka, uwekezaji unaongezeka katika nchi yetu, basi pia matukio ya uvunjaji wa haki za binadamu nao unaongezeka. Kwa hiyo, tulitarajia kwamba, Tume hii iongezewe nguvu ya kifedha ili iweze kufanya kazi. Matukio yale yalilyokuwa yanatokea mwanzo siyo yanayotokea sasa. Sasa hivi teknolojia jinsi inavyokua na matukio nayo ya unyanyasaji na uvunjifu wa haki za binadamu nayo ndivyo yanavyozidi kuongezeka. Kwa hiyo, natarajia kwamba ofisi hii itaongezewe uwezo ili iweze ikafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulipotembelea Ofisi ya Waziri wa Sheria, tulikutana na changamoto kwamba hata jengo la ofisi liko katika mazingira ambayo siyo mazuri sana. Mheshimiwa Mshua ambaye niko naye hapa karibu aliweza hata kupoteza fahamu tukiwa ndani ya ofisi ya Waziri wa Sheria na Katiba, kwa maana kwamba ofisi haikuwa hata na mazingira mazuri kiasi kwamba hata watumishi pale sijui hata afya zao zitakuwa katika hali gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niendelee katika Ofisi ya Rais, Utumishi pamoja na Serikali za Mitaa, kwamba tuna tatizo katika Halmashauri ya Lushoto. Pesa ambazo tunazipata kutokana na *own source* tunazipeleka kulipa Watumishi wa Serikali ambao bado hawajapata vibali vya ajira kutoka Serikali Kuu. Takribani shilingi milioni 28 zinatumika kulipa Watumishi wa Halmashauri. Kwa hiyo hii inachangia kwamba pesa hizi ambazo zilipaswa kwenda kwenye asilimia tano ya akinamama na asilimia tano ya vijana na pia asilimia 20 kwa ajili ya kuwawezesha Wenyeviti wa Serikali za Vijiji kupata posho zao zinashindwa kwenda katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo limekuwa ni tatizo, Wenyeviti wa Vijiji katika Halmashauri yangu wana miaka zaidi ya 10 hawajawahi kupata fedha, hili ni tatizo kubwa linawafanya sasa wanashindwa hata kutekeleza wajibu wao. Kwa hiyo, niiombe Wizara hii ya Utumishi ihakikishe kwamba inatupokea mzigo wa watumishi hawa ili angalau pesa hii iende kwenye maeneo ambayo yanahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la watumishi pia linaenda katika Idara ya Afya. Tumejenga zahanati 10 ambazo ziko tayari lakini hazina watumishi. Tumeiunga kauli mbiu ya Serikali ya Awamu hii ya Tano ya kujenga zahanati kwa kila kijiji, lakini sasa zahanati zile zinaanza kuchakaa bila kutumika. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba hawa watumishi wa afya wanaajiriwa kwa haraka ili waende kuwatumikia wananchi hawa wa Halmashauri ya Lushoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la ufungaji wa mazao kwa mtindo wa Lumbesa. Namwomba ndugu yangu Mheshimiwa Simbachawene kwamba hili tangazo bado halijaenea vizuri huku katika Halmashauri. Huku kwenye Halmashauri bado wanasubiri hawa wanaofunga Lumbesa kwenye yale mageti ya kukusanya ushuru, nadhani kwamba ingependeza zaidi kwa sababu hawa wanaofunga haya mazao wanafunga kutoka kwenye magulio na kwenye vijiji basi hii kazi wapewe Watendaji wa Vijiji wakishirikiana na Wenyeviti, kule kule wanakofungasha haya mazao ndiko ambako waanze kuwabana ili angalau hili tatizo liweze kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza tatizo hili tunamaanisha kwamba akinamama ndiyo wanaoathirika sana kwa sababu ndiyo wazalishaji wakubwa katika halmashauri zetu. Utakuta wameshavuna viazi, wameshavuna nyanya na karoti halafu anakuja mwanaume anafunga kwa kadri anavyoweza, gunia moja linafungwa mpaka debe 10. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba, ule waraka ambao ameutoa basi aendelee kuukazia ashuke mpaka katika ngazi za vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *TASAF; TASAF* nayo ina changamoto kwa sababu vile vigezo ambavyo vimeainishwa vya kaya maskini inawezekana katika zile hatua za awali, wananchi hawakujitokeza vizuri kwenye mikutano, kwa hiyo wakajiangalia walioko kwenye mikutano maskini ni nani wakaandika wale walioko kwenye mikutano, lakini baada ya uhakiki, inaonekana kabisa kwamba maskini halisi waliachwa majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naiomba Serikali pamoja na nia njema hii ya kuhakiki, naomba niendelee kwa sababu hata mimi katika pitapita zangu kuna mmoja ambaye alikuwa ni mnufaika wa *TASAF* yeye alikuwa siku za *TASAF* ndiyo ambazo ananunua bia na tulivyombaini tukatoa taarifa na akaondolewa kwenye ule mpango. Kwa hiyo, tuendelee kufanya utafiti ili watu hawa ambao hawastahiki wasiwepo katika hilo eneo la kupata hizi fedha za uwezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niongelee kuhusu asilimia tano kwa vijana na akinamama kwamba Halmashauri nyingi zinashindwa kutenga hii pesa katika Halmashauri zao na sababu ziko wazi. Huko nyuma, Serikali ya Awamu ya Nne ilikuwa imetoa matamko mengi ya kujenga haya majengo ya sekondari ambayo hakukuwa na mafungu, kwa hiyo Wakurugenzi nao kwa kuwa wanabanwa wakawa wanatafuta mahali gani wataweza kupata hizi pesa. Kwa hiyo, niombe kwamba sasa hivi hizi pesa hebu tuzitengenezee utaratibu mzuri Halmashauri wakati zinakaguliwa hasa na Kamati ile ya Serikali za Mitaa, tuangalie ni asilimia ngapi wametoa kwa ajili ya hawa vijana, ni asilimia ngapi zimetoka kwa ajili ya akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itapendeza kutokana na hili lindi la watu wenye ulemavu kuongezeka kwenda mijini, nashauri Bunge hili kwamba tufike mahali kwa nini tusipunguze japo asilimia moja katika hizi, tukatoa asilimia moja kwa vijana na asilimia moja kwa akinamama ili tukatengeneze asilimia mbili zikaenda kwa wenzetu walemavu kwa sababu huko kwenye Halmashauri ikiwa tunaweza kuwatambua itakuwa ni eneo zuri pia la kupunguza wao wasiende mijini. Kwa hiyo, kama tutaona linafaa tunaweza tukaliingiza, hizo asilimia angalau na wenzetu hawa wenye ulemavu waweze kupata asilimia hii kutoka katika mapato ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nikazie kwenye asilimia 20 ambayo inapaswa kwenda kwa Wenyeviti wa Vijiji na Serikali za Mitaa. Hizi pesa Mheshimiwa Waziri Simbachawene haziendi. Halmashauri hazitengi hizi pesa, Wenyeviti hawapati posho na wakati mwingine inakwamisha hata tunapohamasisha shughuli za maendeleo, wanakosa nguvu ya ushawishi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri akazie hili kwamba Halmashauri ziwatengee pesa hizi za posho Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Wenyeviti wa Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joram Hongoli na Mheshimiwa Hasna Mwilima ajiandae.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa maana ya Rais mwenyewe, Baraza la Mawaziri na watendaji wote wa Serikali kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kuiweka nchi yetu vizuri ili watu wakae sawa na mwisho wa siku wananchi wapate usawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu, nianze kuipongeza Kamati yangu kwani nami nipo kwenye Kamati ya Katiba na Sheria, kwa kazi kubwa ambazo tumezifanya kwa ushirikiano wa pamoja. Pamoja na pongezi hizo, kama walivyosema wenzangu, changamoto za Kamati zipo na zimetusababishia pengine tusiweze kutekeleza majukumu yetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa ambayo tumekumbana nayo ni Kamati kutokuwa na fedha za kutosha hasa fedha kwa ajili ya ziara. Kama walivyosema wenzangu, kiasi kilichotengwa ni kidogo mno hivyo kimetusababishia kukwamishwa katika kutekeleza majukumu yetu. Kamati inapopewa fedha ya ziara inaiwezesha kwenda kujifunza juu ya majukumu yake. Kwa hiyo, Kamati inapokuwa haipati fedha za kutosha inashindwa kutekeleza majukumu yake vizuri ya kuisaidia na kuisimamia Serikali.

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika bajeti zinazokuja tuombe Serikali iweze kutoa fedha za kutosha tukizingatia kwamba Kamati ya Katiba na Sheria ni Kamati ambayo inasaidia wananchi wake kupata haki. Kwa hiyo, tusipojifunza kwa nchi nyingine au kwa wengine wanafanyaje shughuli zao inakuwa ni vigumu kutunga sheria ambayo itakuwa inatenda haki. Kwa hiyo, tuombe awamu inayokuja angalau Kamati zipate fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake hasa ya kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ziara zinatuwezesha sisi Wabunge kuweza kujua fedha zilizopelekwa kwenye taasisi mbalimbali kama zimefanya kazi ile ambayo imekusudiwa. Kwa hiyo, inatusaidia kujua *value for money*. Sasa Kamati inaposhindwa kwenda kwenye eneo husika kwa maana ya *site* na inapewa taarifa kwenye makaratasi tu lakini haiwezi kuona kitu kilichotendeka kwa uhalisia basi ile *value for money* hatuwezi kuiona vizuri. Kwa hiyo, niiombe Serikali yetu katika bajeti inayokuja ijitahidi kuhakikisha kwamba inatoa fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya ziara ili Wabunge waweze kwenda ziara na kukagua miradi mbalimbali ambayo tumeitengea fedha ili kuona ilivyotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linahusu *OC* kwenye Halmashauri zetu. Halmashauri zimekuwa hazipelekewi fedha za kutosha kwa maana ya *OC* na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake. Kwa mfano, Kitengo cha Ukaguzi, siku hizi tunasema Udhibiti Ubora wa Elimu. Kitengo hiki kimeshindwa kufanya kazi yake kabisa, shule nyingi zimeshindwa kufikiwa na wameshindwa kwenda kukagua kutokana na kukosa fedha hasa kwa ajili ya mafuta ya kuendea kwenye maeneo hayo. Hii ni hatari kama tunakuwa na shule ambazo

hazikaguliwi. Kuna shule nyingine utakuta miaka mitatu au mitano imepita hazijakaguliwa. Labda ukaguzi unaofanyika ni ukaguzi ule wa muda mfupi wa kuangalia mambo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji shule zetu ziweze kukaguliwa, Walimu waweze kupitiwa ili wakaguzi waweze kuwashauri juu ya mbinu za kujifunzia na kufundishia. Tusipofanya hivyo, itakuwa ni vigumu kuwaweka Walimu katika wakati wa kisasa na kuweza kuenenda kadri inavyopaswa kufundisha kulingana na *syllabus* na mambo ya taaluma yanavyobadilika. Kwa hiyo, ni muhimu hizi Halmashauri zipewe *OC* za kutosha ili taasisi zote zinazosimamiwa na Halmashauri kwa maana ya Ukaguzi na sekta nyingine ziweze kutekeleza majukumu yake vizuri na hatimaye tutaweza kupata elimu bora na tutaweza kuwa na watendaji wazuri kwa kuwa wana *OC* ambazo zitawawezesha kwenda kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nipongeze (kama walivyopongeza wenzangu) juu ya Mfuko wa *TASAF, TASAF* amekuwa mkombozi wa wanyonge. Huko vijijini sisi Wabunge tunaopita huko tumeona jinsi maisha ya watu yanavyobadilika na kuna maeneo mengine tumeshahamasisha hao wananchi ambao walikuwa wana kipato cha chini waweze kuanzisha miradi midogo midogo ili waweze kujikimu katika maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali pindi itakapopata hela za kutosha iendelee kuongeza fedha za *TASAF* ili wananchi wengi maskini waweze kunufaika na fedha hizi kwa ajili ya kujikwamua katika maisha yao na hatimaye kuendelea kuanzisha miradi midogo midogo ambayo hiyo itawaondoa kutoka kwenye umaskini na hatimaye kuwa na hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye *TASAF* pia kuna tatizo limejitokeza kama wenzangu walivyosema, kuna baadhi ya wananchi walifanyiwa tathmini na wakaonekana kwamba wao ni kaya zile za hohe hahe (kaya maskini) na wakaingizwa kwenye mpango wa kupewa fedha lakini baadaye maafisa wetu wamepita na kusema kwamba hizo kaya hazina sifa za kuendelea kunufaika na mfuko wa *TASAF*. Baadhi ya kaya zilizo nyingi, kuna hizo kaya za wazee ambao hawana uwezo na kuna kaya nyingine wameondolewa kwenye mpango, uwezo wao ni mdogo, wanashindwa kusomesha watoto wao shule na hatimaye kuleta usumbufu na matatizo makubwa. Wengine wametoroka nyumba zao wakihofia kwamba watakamatwa na Serikali kwa kuwa maafisa waliokuwa wanaenda huko wanawatishia kwamba wasiporudisha hizo fedha basi watafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua Watanzania wanaogopa kufungwa, kwa hiyo wamekuwa wakiacha nyumba wakikimbia kuogopa kushikwa na mkono wa sheria kwa maana ya kurudisha fedha hizi. Tuombe basi Serikali ijaribu kuliangalia jambo hili, kama kweli ni kaya maskini, naomba tujaribu kuwaachia waendelee kunufaika na fedha hizi ili hatimaye waweze kusaidia familia zao kuweza kupata mahitaji muhimu hasa mahitaji ya kujikimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni juu ya uhamisho wa watumishi wa Serikali. Tulikuwa na zoezi la uhakiki, natumaini kwamba Serikali sasa imeshahakiki watumishi, imeshajua nani ni mtumishi hewa, nani ni mtumishi ambaye hana sifa za kuendelea kufanya kazi katika Serikali. Sasa kwa kuwa uhakiki umekwisha basi turuhusu hao watumishi wetu waweze kupata uhamisho. Sasa hivi kuna Walimu wengi wanaomba uhamisho wanakataliwa, kuna watumishi wa sekta ya afya wanakataliwa uhamisho kwa kisingizio kwamba bado tunafanya uhakiki wa watumishi hewa. Tuombe Serikali iweze kufungua milango hasa ya uhamisho ili watumishi wetu waweze kuhama. Kwa sababu ilivyo sasa hivi tukiwaacha hawa watumishi waendelee kuishi huko walipopangiwa kazi wasipate uhamisho ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana wameoa, kuna mabinti wameolewa wanataka kwenda kwa wenzao, lakini wanazuiwa kwa sababu ya kisingizio cha uhakiki wa watumishi. Kwa hiyo, tuombe kwa kuwa Serikali yetu ina mpango na inadhibiti maambukizi ya UKIMWI, tukiwaacha hawa vijana huko ambao wameoa na kuolewa baadaye tutakuta tumewapoteza kwa kujiingiza kwenye vitendo ambavyo vitawapelekea kupata UKIMWI kwa sababu ya kukaa na wenza wao mbali. Kwa hiyo, niombe Serikali yangu iweze kufungua milango ya uhamisho ili vijana wetu waweze kuhama na waweze kwenda waliko wenzi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie na wenzangu wamelizungumzia ni juu ya semina za viongozi. Semina hizi ni muhimu hasa kwa hawa wanaoteuliwa, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Kwa hiyo, tuombe wapewe semina za kutosha ili waweze kuongoza vizuri. Naamini kwamba wametoka kwenye kazi mbalimbali na kama walivyosema wenzangu kuna wengine hawaifahamu vizuri kazi ya Ukuu wa Wilaya na wengine Wakuu wa Idara, tuwape mafunzo ili waweze kusimamia vizuri majukumu yao na wasiwabughudhi watu. Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna baadhi ya maeneo wamekuwa wakiwatishia wananchi na watumishi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasna Mwilima na Mheshimiwa Flatei ajiandae.

**MHE. HASNA S.K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba na mimi nichangie kwenye Kamati hizi mbili ambazo zimewasilishwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu, nitazungumzia sana suala la watumishi. Kwenye Halmashauri yetu ya Uvinza tuna tatizo kubwa sana la watumishi. Hivi karibuni tulipokea barua kutoka Wizara ya TAMISEMI ikimtaka Mkurugenzi kuwasimamisha kazi watumishi wote ambao walikuwa wanafanya kazi kama vibarua ili wakae pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mbunge mwenzangu hapa kutoka Lushoto alikuwa anatolea mfano kwamba wao Halmashauri yao wanatumia shilingi milioni 28 kwenye *own source* kwa ajili ya kuwalipa watumishi ambao hawana vibali. Sasa nikawa najiuliza maswali, kwa nini Halmashauri zingine ziruhusiwe kuendelea kufanya kazi na wale watumishi ambao hawana vibali na Halmashauri zingine tuletewe barua ya kuwasimamisha watumishi ambao wameshafanya kazi zaidi ya miaka minne. Zaidi ya miaka minne mtu anafanya kazi, anaitumikia Serikali halafu ghafla tunawaweka pembeni tunasema kwamba ninyi ni vibarua hamna ajira rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona hili nilizungumzie kwa sababu Halmashauri hizi mpya zilizoanzishwa 2012 zina uhaba mkubwa sana wa watumishi. Kwa hiyo, tutaomba Mheshimiwa Waziri husika, wa Utumishi na Waziri wa TAMISEMI waone namna ya kuliangalia hili. Tunaweza tukaendelea kutumia *own source* yetu kama ambavyo wenzetu wa Lushoto wanavyotumia ili tuwalipe hawa watumishi waendelee kutekeleza majukumu ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo pia kubwa la watendaji wa vijiji na leo kupitia wenzangu waliochangia nimejifunza kitu. Kwenye Halmashauri ya Uvinza Watendaji wa Vijiji 75% ni Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari na Walimu Wakuu wa Shule za Msingi. Leo tunasema watoto wanafeli kwenye shule za msingi, leo tunasema watoto wamefeli, matokeo sio mazuri kidato cha nne. Itakosaje kuwa matokeo mabaya wakati Walimu Wakuu hao hao kwenye baadhi ya Halmashauri ndiyo tunawatumia kama Makaimu Watendaji wa Kata na Makaimu Watendaji wa Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe tu Wizara husika, Wizara ya TAMISEMI iliangalie hili ili ikitoa waraka, natambua kwamba kuna waraka mbalimbali huwa zinatolewa Serikalini, ili wakae chini wachunguze ni Halmashauri zipi zinazotumia Walimu Wakuu wa shule kama Watendaji wa Vijiji na Halmashauri zipi zinazotumia Watendaji wa Vijiji kupitia jamii zetu. Kwa nini tusitumie tu jamii? Kwa sababu kama kwenye kijiji mimi ninavyofahamu unaitishwa Mkutano Mkuu wa Kijiji wanaulizana nani miongoni mwetu anastahili kukaimu nafasi ya Mtendaji wa Kijiji? *Then* wanapiga kura yule aliyechaguliwa anakaimu kuliko kama sisi wengine Walimu hao hao ni wachache, hatuna watumishi lakini na hao hao wanafanya na majukumu ya kijiji. Kwa hiyo, niliona hili nilizungumzie kwa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni uhaba wa watumishi kwenye sekta ya elimu na afya. Halmashauri yetu tumejitahidi sana kuhamasisha, tuna vijiji 61, tunazo zahanati 33, lakini tumehamasisha hadi sasa tuna takriban zahanati 15 zimejengwa lakini hakuna watumishi. Kwa hiyo, unakuta tuna zahanati ambazo tayari tungeweza kuzianzisha lakini kwa uhaba wa watumishi wa afya tunashindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu waliochangia kusema kwamba zoezi la uhakiki wa watumishi limeshachukua takriban mwaka mzima, limekwenda vizuri na sisi tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Utumishi, lakini sasa waone ni namna gani wanaweza wakatoa ajira mpya ili sasa vijana wetu waliomaliza vyuo mbalimbali waajiriwe, huu uhaba wa watumishi kwenye sekta za afya, elimu na kilimo uweze kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo nataka kulizungumzia ni ugumu wa miundombinu na mazingira katika Halmashauri mpya. Na-*declare interest* kwamba nimekuwa *DC* siku za nyuma, tulikuwa tunaona kutoka Wizara ya TAMISEMI, wale wanaoshughulika na masuala ya *Local Government* wanatembelea zile Halmashauri mpya kuangalia changamoto ambazo wanazo na kuona ni jinsi gani wazisaidie ili ziweze kusonga mbele. Sasa Halmashauri ya Uvinza, tunatumia majengo yaliyoachwa na kambi zile za wakimbizi. Takriban *four years* tuko pale! Tunaishukuru Serikali juzi kupitia hii bajeti tunayomaliza 2016/2017 tumepata shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kujenga jengo la Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tangu Halmashauri ile ianzishwe hatuna magari ya kuwasababisha Wakuu wa Idara na Mkurugenzi waweze ku-*move* kwenye vijiji wasimamie miradi ya maendeleo. Sasa naomba Serikali iweze

kuangalia Halmashauri hizi maana unasikia Halmashauri kongwe zina miaka 20 bado zinapelekewa magari mapya lakini zile Halmashauri ambazo ni changa wala hazifikiriwi kupelekewa magari ili waweze kufanya kazi zao za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Waziri wa TAMISEMI aangalie Halmashauri hii ya Uvinza kwa jicho la huruma. Nashukuru sana tumepata Mkurugenzi, ni mpya lakini anajua majukumu yake ya utendaji wa Halmashauri. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri tuangalie namna ya kuwezesha Halmashauri ya Uvinza ili tuweze kusonga mbele katika kutekeleza majukumu yetu ya maendeleo....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Muda wako umekwisha.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza nitauelekeza kwenye sehemu hii ya *TASAF*. Kwanza, nikubaliane na wachangiaji wenzangu kwamba *TASAF* inasaidia sana kwenye maeneo yetu hasa kwa kuziinua familia hizi ambazo zina hali duni. Changamoto ambayo tunapata kwenye maeneo yetu ni kwamba wanapoleta hizi fedha za *TASAF* mara nyingi watu hawa au familia hizi zinapata changamoto pale ambapo kunakuwa na michango ya vijiji. Fedha zinakuja kwa ajili ya kuwawezesha hawa wafaidika wa *TASAF* wenyewe wakati huo huo Wenyeviti na Watendaji wa Serikali wanawatoza michango kwa pesa hizi za *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe kidogo Wizara itoe maelekezo kwa sababu pia hawa ndugu zetu wengine wamesamehewa michango kwa hiyo wanapopata ule mwanya wa kupata hizi pesa za *TASAF* wakati huo huo wanakamatwa michango na wanatakiwa kuchanga tena kwa kutumia pesa ambazo Serikali imewapatia kwa ajili ya kujisaidia kwa maisha yao. Kwa hiyo,

niombe Serikali itoe elimu katika Serikali zetu za Mitaa hasa vijiji ili Watendaji waweze kuwasamehe watu hawa ambao pia Serikali imeona wana haki ya kupata hii pesa ambayo inasaidia kuwainua hasa hizi familia ambazo zina tatizo la kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tena kujielekeza kwenye sehemu nyingine hasa hii ya ajira. Namshukuru kwanza Mheshimiwa Kairuki ameeleza jinsi ambavyo ajira zinategemea kuachiwa kwenye kada mbili za afya na elimu. Kwenye Halmashauri yangu ya Mbulu Vijijini tuna shida kubwa sana ya watumishi hawa hasa kwenye kada ya *VEO* na *WEO*. Sasa hivi watumishi hasa Walimu ndio wanakaimu nafasi za Maafisa Watendaji. Hebu niambie leo hii tuna tatizo la Walimu, tena Walimu wa sayansi wanakaimishwa nafasi hizi ili kusaidia mpango mzima wa *governance* huku chini. Pamoja na nafasi hizi ambazo Waziri amezitangaza leo wanazotegemea kutoa ajira za afya na elimu, wajitahidi kufungua ajira kwenye nafasi za Watendaji wa Vijiji na Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka nitoe mchango mwingine katika suala la *property tax,* hii kodi ya majengo ambayo kimsingi ukiangalia sheria sasa inakwenda kukusanywa na *TRA*. Kwa sababu sheria hii bado haijatungwa na Bunge na tunategemea iletwe baadaye tuone jinsi tutakavyosaidia kwa sababu TAMISEMI wametoa maelekezo ambayo siyo mazuri sana kwenye Halmashauri zetu. Kwa mfano, Halmashauri yangu imepewa waraka ambapo inatakiwa ikusanye kodi ukiangalia wameweka viwango vya kukusanya kodi kwenye maeneo ambayo hayafai. Wamepanga pia kukusanya kodi kwenye nyumba za tembe na kwenye nyumba za majani. Mimi sikatai kodi inakusanywa na ni sheria na inatakiwa kukusanywa lakini siyo sahihi sana kukusanya kodi kwenye nyumba za tembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya kule nina wapiga kura wangu wananchi wanaoitwa Wahadzabe wao wamezoea kukaa porini, lakini sasa tunawaomba tuwajengee nyumba ili wakae kwenye nyumba. Wakisikia sasa Halmashauri inakusanya kodi inayoitwa kodi ya majengo hasa kwa nyumba za nyasi na tembe wanapata maswali makubwa na kutaka kuendelea kukaa porini. Mheshimiwa Waziri naomba uangalie suala hili na lipo kwenye Jimbo langu la Mbulu Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia pia suala zime la upandishaji wa madaraja. Wako watumishi mwaka jana walipandishwa madaraja na wengine baada ya waraka kutoka wamesimamishwa kupandishwa madaraja. Niiombe TAMISEMI iangalie namna gani nzuri ya kuwapa pia motisha watumishi

hawa ambao kimsingi wenzao wameshapandishwa madaraja baada ya waraka kutoka wamesimamishwa na hawezi kupandishwa madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukija kwenye Halmashauri yangu ya Mbulu Vijijini *specific* asilimia 90 ya Wakuu wa Idara wanakaimu. Sasa basi niombe kwa sababu Halmashauri tumeshaleta mapendekezo ya kuwapandisha hao Wakuu wa Idara, Serikali iweze kutoa mwanya wakuu hawa wapandishwe. Mtu ameshakaimu miaka mitano unategemea nini? Naomba Serikali iangalie namna gani ya kuwapandisha na kuwarasimisha hawa Wakuu wa Idara ambao wamekaimu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la asilimia tano za wanawake na vijana kwa habari hii tunayosema mikopo ya vijana. Ni vigumu kwa Halmashauri zetu za vijijini kuweza kutoa hizi hela kwa sababu gani? Hela za *OC* hazikwenda na Wakurugenzi wengi wanatumia pesa hizi hizi ili kuendeshea shughuli zao. Kwa hiyo, ni vizuri basi hizi fedha za *OC* ambazo kimsingi ziko kwenye kila bajeti ya Halmashauri za Wilaya ni vyema zikapelekwa kwa wakati ili Watendaji au Wakurugenzi waweze kuzitumia na hatimaye basi wasiende kwenye hela za vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye utawala bora. Mimi kwanza nishukuru sana, nina Mkurugenzi mzuri naamini hakupata semina au amepata semina lakini anafanya kazi yake vizuri, nampongeza sana. Pia nimeona wenzangu wengi wamelalamika sana habari ya Watendaji yaani Ma-*DC*. Mimi nampongeza *DC* wa kwangu anafanya kazi nzuri na nashukuru Mungu kama hajapata semina mimi naona kwa kweli anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vibaya sana kila mtu kusema hapa Ma-*DC* wanafanya kazi mbaya, hapana, mimi nafikiri sio wote. Wapo wa kupongezwa na mimi nampongeza wa kwangu kwa sababu naona anafanya kazi nzuri. Pia nampongeza Mkuu wa Mkoa wangu naona kabisa anafanya kazi nzuri ambayo kimsingi ana-*operate* ile *human right* ambayo naiona mwenyewe. Pia namshukuru sana Mungu labda mimi inawezekana nimepangiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niunge mkono wenzangu waliosema wanahitaji semina elekezi. Ni vizuri basi Serikali ikaona, kama wenzangu na wengine wamepata tatizo hili la utawala bora ni vizuri hizi semina elekezi zikawekwa na zikapangiliwa kuliko kuwafanya wananchi, watendaji na Wabunge wenzetu wakawa na hali ya sintofahamu katika maendeleo, haiko vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Mawaziri wanaofanya kazi na nashukuru sana wamefika kwenye eneo langu. Nawapongeza sana kwa sababu wanafanya kazi kubwa. Nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kuwateua pia hawa Wakuu wa Wilaya, ndugu zangu Wabunge kama wasingeteuliwa Wakuu wa Wilaya wapya ingekuwa biashara kama ilivyo. Sasa hivi ukiangalia Serikali imeanza kukaa katika *line* yake. Leo hii watumishi wamekuwa na nidhamu. Ukienda kwenye Halmashauri zetu na maeneo mengi ya kazi hakika utaona wananchi wanatekelezewa na wanasikilizwa katika maeneo mengi. Kwa hiyo, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kweli kwanza kwa kuangalia na kuiweka Serikali vizuri kwani sasa hivi Serikalini kuna nidhamu na wananchi wanasikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nichangie haya tu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa nawashukuru sana, huyo ndiyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa nafasi za Wabunge sasa namwita Mheshimiwa Kairuki dakika 10 na Mheshimiwa Simbachawene dakika 10.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kuchangia hoja hii ya Taarifa ya Shughuli ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa mwaka huu wa fedha. Kwanza kabisa, niseme naunga mkono hoja hii ya Kamati na niipongeze sana Kamati chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rweikiza na Makamu Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa namna ambavyo wamekuwa wakitushauri na kutusimamia kama Serikali katika majukumu mbalimbali tunayoyatekeleza. Kipekee zaidi niwashukuru kwa ziara mbalimbali walizozifanya katika maeneo yetu tunayoyasimamia na zaidi katika kutembelea miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema kwamba, yote yaliyowasilishwa na Kamati tutayafanyia kazi na tutaleta utekelezaji katika Kamati kuona ni kwa namna gani tumeweza kuyatekeleza. Vilevile nipende kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia taarifa hii kwa ushauri wao na kwa changamoto ambazo wamezibainisha na niwahakikishie kwamba tutazifanyia kazi na kuzitekeleza na naamini wataweza kuona mrejesho wake namna ambavyo tutazitekeleza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kuna hoja kubwa katika suala zima la utaratibu wa hatua za kinidhamu katika utumishi wa umma. Ni jambo

ambalo nimeliona limesemewa sana na Kamati lakini Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kiasi kikubwa wamelisema suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa nidhamu na ajira katika utumishi wa umma unatekelezwa kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu lakini zaidi ya yote sheria yetu mama ambayo ni Katiba ya nchi yetu. Vilevile kama Wizara ya Utumishi wa Umma tumekuwa tukitoa miongozo mbalimbali ambayo inasimamia utumishi wa umma na kuongoza viongozi wote ambao wanatekeleza masuala ya nidhamu pamoja na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo mamlaka mbalimbali za ajira na nidhamu. Ukiangalia katika kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni ya 35 ya Kanuni za Utumishi wa Umma zimeeleza bayana ni namna gani mamlaka za nidhamu zitaweza kutekeleza majukumu yake katika kuchukua hatua za kinidhamu. Hata itakapotokea Wakuu wa Mikoa au Wakuu wa Wilaya au kiongozi mwingine yeyote wa Serikali anapochukua hatua stahiki za kinidhamu ni lazima mamlaka ile ya ajira na nidhamu ndiyo itekeleze jukumu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ieleweke bayana na napenda kuwatangazia wote tuzingatie misingi ya kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Umma pamoja na Kanuni ya 35 ya Kanuni zetu za Utumishi wa Umma. Hata katika makundi mengine ya utumishi, tunao watumishi wa Bunge, tunao watumishi wa Mahakama, tunao wanataaluma wengine, tunao watumishi wengine katika vyombo vya ulinzi na usalama, nao pia ni makundi ya utumishi wa umma lakini ipo miongozo ya mamlaka zao pia za ajira na kinidhamu. Kwa hiyo, niombe sana viongozi wetu wengine wa kisiasa pamoja na viongozi mbalimbali na mamlaka za ajira na nidhamu waweze kuhakikisha kwamba wanatekeleza misingi hii kama ilivyoanishwa katika sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nisisitize mahusiano. Jambo kubwa ukiangalia sehemu zingine unakuta mahusiano ni tatizo. Kila mmoja aone ana wajibu wa kuhakikisha kwamba kunakuwa na mahusiano mazuri na viongozi wa Serikali vilevile pamoja na viongozi wa kisiasa. Naamini tukiwa na mahusiano na mawasiliano mazuri kwa kiasi kikubwa migongano ambayo ipo itaweza kuondoka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa pia hoja kuhusiana na semina elekezi. Nipende tu kusema kama Serikali na asubuhi nilikuwa na swali nimejibu, tumekuwa tukitoa mafunzo ya aina hii na hatutasita kuendelea kutoa mafunzo kama haya tena. Hata Utumishi mwezi huu tumepanga tena mafunzo ya siku

saba kwa viongozi hawa kuhusiana na masuala mbalimbali ya kiutumishi, masuala ya maadili ya utumishi wa umma nao kama viongozi vilevile masuala mengine ya rushwa, nidhamu pamoja na masuala ya fedha. Niwaombe sana viongozi hawa wote wanaohusika waweze kuhakikisha kwamba wanazingatia sheria, kanuni na utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia kwa Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia kuhusiana na hoja za *TASAF* na nashukuru kwamba mmeweza kuona ina manufaa. Niwahakikishie kwamba tutaendelea kufuatilia ili kuhakikisha kwamba changamoto zote zinazojitokeza na upungufu wote uliopo basi unaweza kuchukuliwa hatua. Tumeanza kuchukua hatua ya kuboresha usimamizi zaidi pia tunaangalia suala zima la mfumo wa utambuzi, ni namna gani kaya hizi maskini zinazostahili kuingizwa kwenye mfumo zinaweza kutambuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote wameeleza hapa, wapo ambao walikuwa hawahudhurii katika mikutano ya hadhara ya wananchi ya kuibua kaya hizo, wako ambao wengine walikuwa wanasema hela hizi ni za *freemason* matokeo yake zimekuja kuingizwa zingine ambazo hazistahili na zile zinazostahili zimekuwa zikiachwa nyuma. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tutayafanyia kazi, tumeanza kuondoa kaya 55,692 lakini zaidi tutaangalia *control mechanisms.* Pia nilimsikia Mheshimiwa Bashe tutaenda kuangalia kwa kina ili kuona tuje na mfumo gani mzuri zaidi ambao utaweza kutusaidia katika kutekeleza mfumo huu wa maendeleo ya jamii bila kuleta matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikia kuna mtu anasema kuna kaya zimechukua hizi fedha ambazo hazistahili kwamba iweje leo hii waambiwe warudishe. Nipende tu kusisitiza kwamba kila fedha iliyochukuliwa kwa kaya ambayo haistahili ni lazima itarudi *whether* ni kaya maskini au ni tajiri lazima itarudi kwa sababu kama angekuwa ni maskini angekuwa kwenye mpango kihalali. Yule ambaye ameondolewa hastahili kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa na ofisi yetu ya Takwimu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya suala zima la ajira, niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tayari tumeshaanza kufungulia ajira. Tulishaajiri nafasi 5,074 na tayari wamesharipoti na kwa sasa tuko katika hatua ya kuajiri watumishi wengine wa sekta ya elimu pamoja na maabara watumishi 4,348. Baada ya hapo tutaingia katika sekta ya afya pamoja na sekta zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikia Waheshimiwa Wabunge walioeleza upungufu katika sekta ya afya, ni kweli tuna upungufu wa takribani asilimia 51.3 ambao ni sawa na watumishi 54,459. Tunachokifanya sasa tunaangalia pia uwezo wetu wa kibajeti, tungependa kuajiri watumishi wengi sana. Kwa ujumla kwenye Serikali tuna upungufu wa watumishi 160,172,000 lakini kwa sasa tunajitahidi kwenye maeneo yenye vipaumbele na kwenye Halmashauri zenye upungufu mkubwa kuona ni kwa namna gani tunawapatia watumishi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja pia kuhusiana na uhakiki wa matamko ya fomu za maadili. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameshawasilisha matamko yao. Kweli kwa kipindi hiki tumeweza kuvuka lengo ukiangalia waliowasilisha tarehe 31 walikuwa ni zaidi ya asilimia 87, ni namba ambayo kwa kweli ilikuwa haijawahi kufikiwa huko nyuma. Kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Zaidi niwahakikishie pia tutaendelea na uhakiki, tumeshafanya uhakiki kwa viongozi wa umma 116 na lengo letu kabla ya kufika mwezi Juni tutakuwa tumefanya uhakiki wa viongozi 500. Kwa hiyo, tunaomba tu Waheshimiwa viongozi wa umma waweze kutoa ushirikiano watakapofuatwa kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki wa mali zao na madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja pia ya maabara ya uchunguzi au *forensic laboratory*, tunazo maabara za aina mbili. Kuna moja yenye uwezo wa kufanya uchunguzi wa kieletroniki na nyingine ina uwezo wa kufanya uchunguzi wa kimaandishi. Ile ya uchunguzi wa kieletroniki imeshaanza kazi. Tunawashukuru Kamati kwa kuifuatilia na tayari wameshachunguza majalada takribani 109. Kwa upande wa *document forensic* au uchunguzi wa maandishi, kwa sasa kwa mujibu wa kifungu cha 59 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ni Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ndiyo ambaye anaruhusiwa kuwaruhusu TAKUKURU kuweza kuwa na maabara hii ya kuweza kufanya uchunguzi wa kimaandishi. Tayari tumeshawasilisha na tunaendelea vizuri na tunaamini ataweza kukubali maombi haya ili TAKUKURU maabara yake iweze kufanya kazi kwa ajili ya kuharakisha uchunguzi na kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa kesi zetu mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukisikia watu wanasema uhakiki hauishi. Tumekuwa tukifanya uhakiki kwa umakini mkubwa sana na niseme uhakiki kwa watumishi hewa tumeshamaliza, lakini mwisho wa siku bado utakuwa endelevu pindi tutakapokuwa tunaona kuna watu ambao wameingia hawastahili watakuwa wakihakikiwa na watakuwa wakiendelea kuondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tunachokifanya ni uhakiki wa vyeti vya kitaaluma na nipende kusema kupitia Bunge hili tumeshatangaza kwa mtumishi wa umma ambaye aliombwa awasilishe cheti chake cha taaluma cha *form four, six* na cheti cha ualimu au taaluma nyingine akashindwa kuwasilisha lakini bado tukatoa fursa aweze kuwasilisha *index* namba na bado akashindwa, basi itakapofika tarehe 1 Machi tunaanza mchakato wa kuanza kufukuza kazi mtumishi wa aina hiyo. Kwa hiyo, niombe kupitia Bunge hili iweze kusikika vizuri kabisa na waweze kuzingatia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema uhakiki hauishi hapana, huu ni uhakiki mwingine kabisa. Ni lazima tuwe na watumishi wa umma ambao kweli wamebobea na kweli wameenda shule. Wako watu wengine wana vyeti vya ualimu hata kwenye chuo cha ualimu chenyewe hakuwahi kufika kabisa, unategemea nini? Tunalaumu hapa kwamba ni masuala ya elimu bure fedha inaenda kidogo, kuna mambo mengine ni kama haya ndiyo ambayo yanachangia. Kwa hiyo, tunaomba mtupe fursa tujitahidi kuweka mambo sawa kuhakikisha kwamba tuna watumishi wa umma wale tu ambao kweli walisomea, kweli vyeti vyao ni vya halali na hawajaingia katika ajira kwa sifa ambazo hawastahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia kuna hoja nyingine kuhusiana na hatua za kinidhamu ambazo zimechukuliwa dhidi ya watumishi wa umma au viongozi waliobainika kusababisha watumishi hewa. Nipende tu kusema kwamba hadi sasa Serikali imeshawachukulia hatua watumishi wa umma 1,595 kwa mujibu wa Sheria zetu za Utumishi wa Umma na taratibu zao za nidhamu ziko katika hatua mbalimbali. Kati ya watumishi hao 1,595 watumishi 16 wanatoka katika Wizara sita, watumishi tisa wanatoka katika Sekretarieti za Mikoa na 1,564 wanatoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tutaendelea kusimamia na kuhimiza utekelezaji wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali iliyopo katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia kuna hoja kuhusiana na Wakala wa Serikali Mtandao kwamba inawezekanaje mpaka sasa bado wana ukosefu wa sheria inayoanzisha Wakala huu. Nipende tu kusema kwamba tunashukuru na tunapokea ushauri wa Kamati na tayari tumeanza kuufanyia kazi, tuko katika hatua nzuri ya kuandaa Waraka kwa ajili ya kuanzisha Wakala huu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Simbachawene dakika 10.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inayoongozwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza na Makamu Mwenyekiti wake Dkt. Pudenciana Kikwembe pamoja na wajumbe wote kwa ujumla akiwepo Mzee wangu Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba. Tunawashukuru sana kwa namna mnavyotupa ushirikiano na mara zote mmekuwa ni walezi wetu na kusema kweli Kamati hii tunafanya nayo kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwa michango mizuri kupitia kazi hii ya Kamati iliyofanyika kwa muda wa miezi 12. Kazi hii ni kubwa na mambo mengi wameyasema. Nitangulize tu kusema kwamba yote tumeyapokea na tumeyachukua na tutayafanyia kazi yote kwa ufanisi na kwa ufasaha mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyosemwa ni mengi lakini siyo rahisi kwa muda niliopewa kuweza kuyajibu yote na kwa kuwa wajibu wangu na mimi ni kuchangia, basi nitumie nafasi hiyo kusema baadhi ya yale tu ambayo naona yamesemwa sana na watu wengi na mengine haya tutaendelea na mfumo ule wa Kanuni za Kudumu za Bunge kuendelea kufanya kazi kwa pamoja ili tuweze kuyamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa na la kwanza ambalo limesemwa sana na wote ni namna ambavyo Wakuu wetu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanavyohusiana katika kufanya kazi ya umma na kuleta maslahi tunayoyatarajia wote. Imesemwa hapa kunakuwa na misuguano katika baadhi ya maeneo ya Wilaya na Mikoa kati ya viongozi hawa wa kiserikali na viongozi wawakilishi wa wananchi kwa maana ya viongozi wa kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa tofauti zao ukiondoa udhaifu wa baadhi ya wengine ambao ni hulka zao na hapa ndiyo maana inasemwa hata habari ya semina elekezi. Siku za nyuma mambo ya semina hizi yalilaumiwa sana na kupingwa kweli kweli kwamba semina elekezi, semina elekezi. Tukasema tutoke kwenye semina elekezi *as long as* mtu ana *CV* nzuri amesoma, akipewa vitabu vya kufanyia kazi lakini wakati anapoteuliwa akaelekezwa naamini atafanya kazi vizuri kama ana hekima na busara kwa sababu naamini suala la uongozi siyo tu kuwa na *PhD*, *Masters* au *First Degree* pia hekima ni kitu cha msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu hizi zinatusaidia tu kujua vitu lakini hekima inatusaidia kujua useme na ufanye nini kwa wakati gani. Kwa hiyo, nitoe rai na niwasihi sana baadhi ya wenzetu hawa Wakuu wa Mikoa na Wilaya wajitahidi pamoja na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu lakini pia wawe na hekima na busara kwa sababu sasa wao ni viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika hili wakati mwingine na wao kama binadamu wanakuwa *tempted*, anatokea kiongozi anasema mimi ni mwakilishi wa wananchi bwana, huwezi kuniambia kitu na unamwambia kiongozi mwenzio vile na yeye atakwambia anavyoweza kusema. Ndiyo maana yanatoka majibu kama yale na mimi ni mteule wa Rais, ni kwa sababu kulikuwa kuna *reaction* fulani iliyopelekea na yeye akawa *excited* akafikia hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitoe rai kwa sote, sisi kama viongozi wa kisiasa na viongozi wengine wote, tunapokwenda mbele ya jamii basi tusichukue nafasi hiyo ya kutambiana kwamba mimi ni nani, mimi ni nani, bali wote tujitahidi kuwa waadilifu na kujua kwamba nafasi zetu ni kubwa kwa jamii. Wakati mwingine ni mambo ya mahusiano tu, unamkuta Mbunge au Diwani, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya iko pale au ya Mkuu wa Mkoa iko pale hajawahi kwenda hata siku moja ku-*pay courtesy call,* wanakutana kwenye matukio. Hili si jambo jema kwa sababu pia viongozi hawa sheria imewapa madaraka na mamlaka makubwa tu na kwa sababu ya muda sina haja ya kuisema. Niwasihi na niwaombe viongozi wenzangu kwamba wale ni viongozi wenzetu tushirikiane nao, tufanye kazi nao pamoja kwa faida yetu sote lakini kwa maslahi mapana ya wananchi wetu na kwa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la pili lililoguswa sana ni kwamba *flow* ya fedha kwenda kwenye shughuli za Mamlaka ya Serikali za Mitaa si nzuri sana. Takwimu za Kamati zinaonesha kwa utafiti walioufanya na ambao na sisi tunao ni kwamba 85% zimekwenda kwa ajili ya maendeleo, kwa hiyo utaona ni 15% ndiyo haijaenda na bado tuna miezi kadhaa hapa, nadhani tunaweza tukafikia hatua nzuri ya 100% kwenye fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *OC* zimekwenda 46% kwa fedha iliyotoka Serikali Kuu lakini sehemu ya *OC* pia ni pamoja na *own source*. Makusanyo ya ndani ya Halmashauri na yenyewe ni sehemu ya *OC*. Kwa hiyo, niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge tuyasimamie sana makusanyo ya ndani ili yaweze kutusaidia kutekeleza majukumu mengine ambayo yangeweza kutekelezwa na *OC* ile ambayo imepungua iliyotakiwa kuletwa na Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufahamu kwamba mahusiano ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu huwezi kuyaachanisha kwa sababu kwa *nature* yake Serikali Kuu ndiyo imezaa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kazi yake ni kuzilea Mamlaka za Serikali Mitaa. Tunahitaji mishahara, tunahitaji fedha za maendeleo ambazo Serikali Kuu inatafuta na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni lazima zitimize wajibu wake kuhakikisha kwamba zinatunza fedha za makusanyo na kuhakikisha kwamba zinaenda kwenye maendeleo pia kwa maana ya sehemu ile ya usimamizi wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko Mamlaka za Serikali za Mitaa nyingine ambazo hata pamoja na kukusanya *own source* kubwa tu inayofikia kwa mwezi hata zaidi ya milioni 100 ambayo ni kiwango kidogo, ziko zinazokusanya mpaka bilioni moja kwa mwezi, zinashindwa kuwalipa hata posho za vikao halali Madiwani. Huku ni kugombanisha Serikali Kuu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa maana ya Madiwani. Kwa sababu haiwezekani wewe umekusanya fedha, kikao kile kwa mwezi kinatakiwa kifanyike kwa chini ya shilingi milioni 20, wewe unazipeleka kwenye matumizi mengine mnapeana likizo, mnapeana safari watumishi, Wakuu wa Idara wanapeana safari zinatumika zinakwisha halafu wanasema Serikali haileti *OC* ndiyo maana hatuwalipi posho za vikao. Kuanzia sasa Halmashauri ambayo itawakopa Madiwani huyo Mkurugenzi hana sifa ya kuendelea kuwa Mkurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine lililosemwa sana ni suala la mihuri ya Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji. Nilikwishalisema, Wenyeviti hawa wa Mitaa na Vijiji mbali ya masuala ya ulinzi na usalama lakini mihuri yao ile ndiyo inayowatambulisha kwa wananchi wao wanaowaongoza. Mihuri yao ile ndiyo inayowafanya watu wamalizane katika mahusiano ya mikataba midogo midogo katika maeneo yao. Ni lazima mamlaka za juu ziheshimu madaraka na majukumu waliyopewa hawa viongozi wa chini, Wenyeviti wa Mitaa na Wenyeviti wa Vijiji na hata Wenyeviti wa Mashina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kitendea kazi hicho ni muhimu kwao na vizuri wakaachiwa na ndiyo maana nilisema warejeshewe na hii niliisema siyo kwa Dar-es-Salaam ni kwa nchi nzima. Viongozi hawa nchi nzima warejeshewe kitendea kazi hiki ili wafanye kazi yao vizuri. Ndiyo wanaotambulisha mgeni anapoingia au kutoka kwenda sehemu nyingine lakini ndiyo wanaoandika vibali hata vya mifugo, mfugo ukauzwe hapa na ndiyo wanaosababisha kule chini kunakuwa na amani na utulivu, lazima tuwape nafasi yao hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ma-*WEO* na ma-*VEO* ambao hawajaajiriwa na Serikali Kuu haitatokea hata siku moja kwa idadi ya vijiji tulivyonavyo tukatimiza idadi yao kutokana na watumishi wa umma tulionao na changamoto tulizonazo za upungufu katika idara mbalimbali. Niendelee kusisitiza kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni mamlaka kamili zinazoweza kuamua kutafuta watu wa kuwaajiri hata kwa mikataba na wakawalipa fedha hiyo kutoka kwenye *own source*. Hawa ndiyo watakaosababisha ufanisi na makusanyo hata kwenye Halmashauri zenyewe. Kwa hiyo, hili halijazuiwa lakini kadiri tutakapopata vibali vya ajira tutaendelea kuwaajiri kupitia Serikali Kuu. Mheshimiwa Kairuki akitoa vibali sisi tutaendelea kuajiri lakini kwa upungufu tulionao Halmashauri ziendelee kuwaajiri hawa watendaji watakaotusaidia wenye sifa zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni miradi ya Halmashauri ambayo haijakamilika. Iko miradi ambayo haikuwa ya Serikali Kuu lakini ilipangwa na Halmashauri zenyewe na ikawa vipaumbele vyao na wakasema wataitekeleza miradi hiyo kwa kutumia *own source* zao. Nitoe rai na niagize Mamlaka ya Serikali za Mitaa pale ambapo wana mikataba na wakandarasi au na *suppliers,* wanawatesa wenzao wanahangaika, wao walishaanza kutekeleza upande wao wa mikataba, wametekeleza miradi hiyo, lakini hawawalipi kwa kisingizio cha kwamba Serikali Kuu haijatoa fedha. Mlikubaliana kwamba mtawalipa kutoka kwenye *own source,* muwalipe *suppliers and contractors* kwa sababu ni kuwaonea na wengi wamefilisika na wengi hata wamekufa kwa sababu ya madeni hayo, hii haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nichukue nafasi hii kuzungumzia juu ya *property rates…*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Hiyo ni kengele ya pili, nakupa sekunde 10. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshamaliza maandalizi yote ya kukusanya kodi ya majengo katika Halmashauri 30 ambazo tulikubaliana hapa na tukapitisha sheria na kwa sasa wako tayari kuanzia mwisho wa mwezi huu kukusanya fedha hizo. Hata zikikusanywa na Waziri wa Fedha kwa sababu ndiye anayeshika Sera na Sheria ya Fedha, mwisho wa siku zitarudi huku kuja kutusaidia katika miradi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa *Attorney General*, dakika 10!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata fursa hii ya kuchangia kwenye hoja hizi mbili muhimu. Nikushukuru wewe kwa kunipa fursa na pia niwashukuru Wenyeviti wa Kamati hizi mbili kwa taarifa zao muhimu sana wakati Bunge linapotekeleza jukumu lake la kikatiba la kuishauri na kuisimamia Serikali. Mimi kwa moyo mmoja niseme kwamba naunga mkono hoja za Kamati hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichosemwa katika taarifa hizi zote mbili ni cha kweli. Nilikuwepo wakati Mheshimiwa Shangazi anachangia kilichojiri juu ya hadhi na mazingira ya kazi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipokuwa anazungumza kuhusu Mbunge mmoja aliyezimia alisema ni Wizara ya Katiba lakini ukweli ilikuwa ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, hii inaonesha ni kwa kiasi gani hizi taarifa zimezungumza ukweli. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata fursa ya kuchangia hapa kuisaidia Serikali iweze kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kushauri, imetolewa hoja kwa mfano juu ya wafungwa wa kunyongwa, wanaitwa *condemned* kwamba labda wanakaa sana pale na hawanyongwi labda tubadilishe sheria, hapana. Mamlaka haya yapo kwenye Katiba, Ibara ya 45 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo imempa Rais mamlaka ya kusamehe kosa lolote lile hata hilo la kunyongwa au kuwashushia adhabu. Inategemea kwamba hawa waliotumia fursa yao kutokuwanyonga wametumia mamlaka yao ya Kikatiba halali kabisa. Pia hatuwezi tukafuta hili kwa sababu anaweza akaja Rais mwingine akasema aah aah, hawa wawe wananyongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Waheshimiwa Wabunge *Law Reform Commission,* ile Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ilishafanya utafiti hii miaka ya karibuni tu kwamba hii adhabu tuiondoe au tusiiondoe? Wananchi walisema hii adhabu ibaki pale. Mahakama ya Rufaa ya Tanzania iliwahi kusema kwamba hii ni adhabu halali kwa hiyo, iko pale. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wale watu kuwepo pale isitufanye tukawa na nia ya kutaka kurekebisha ile sheria. Hilo la kwanza niliomba nichangie kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, imezungumzwa juu ya ukiukwaji wa taratibu na Sheria za Uchaguzi wakati wa uchaguzi wa Madiwani. Wote tunajua utaratibu, kama sheria au utaratibu umekiukwa, ushauri wangu tu ni kwamba yule ambaye anaona taratibu zimekiukwa basi anaweza akaenda Mahakamani akafungua shauri la kupinga matokeo ya uchaguzi. Ndivyo tulivyofanya hata katika uchaguzi mkuu, huo ndiyo utaratibu. Ndiyo ushauri wangu kwenye suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limezungumzwa pia na Mheshimiwa Mussa na amelizungumza kwa hisia, hata mimi linanihusu, linaumiza. Wakati fulani unaenda gerezani unamwona mama ana mtoto mdogo na mimi nimeenda sana magerezani. Nimemsikia Mheshimiwa Mwamoto akizungumzia lile Gereza la Kahama pale, mimi nilienda pale kwa mara ya kwanza Desemba, 2003 nikiwa na Waziri Mwapachu, wakati huo mimi ni msaidizi wake, Mzee Mwapachu alilia machozi kutokana na hali iliyopo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali imechukua hatua imeboresha hali hii. Kifungu cha 144 cha Sheria ya Mtoto sasa kinaweka utaratibu wa namna gani mama aliye na mtoto gerezani anapaswa atendewe. Siwezi kutafsiri kwa Kiswahili hapa, lakini nisome, kinasema hivi:-

*"(1) Where a mother is in prison with her child under any circumstances, all measures shall be taken by the prison authorities to ensure that the child receives the required child care in the form of adequate diet, nutrition and child health care including immunization".*

*(2) The prison authorities shall inform the District Social Welfare Officer about the child who is in prison with his mother and who is no longer breastfeeding.*

*(3) Where the social welfare officer has received information from the prisons authority, he shall determine the most suitable place for the child, which may be –*

*(a) the parent who is not in prison;*

*(b) a relative;*

*(c) a guardian; or*

*(d) a fit person;*

*(4) In the absence of persons referred to under subsection (3), the Social Welfare Officer shall cause the child to be admitted in an approved residential home until such times when the mother is discharged from prison.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sheria ya Serikali tayari imeshaweka utaratibu wa aina hiyo. Hata hivyo, tunakubali ushauri ambao umetoka kwa Mheshimiwa Mussa kwenye suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imezungumzwa hapa ni hii hoja ya msongamano wa mahabusu magerezani na ni kweli Wabunge wamesema kwa hisia. Sisi jana tulikuwa pale Dar-es-Salaam kwenye *Law Day* na ndicho ambacho pia Rais amesisitiza sana. Taasisi za umma ambazo zimepewa majukumu ya kusimamia *administration* ya *justice* tutekeleze majukumu yetu kwa ufanisi. Kama ni Mahakama hivyohivyo, kama ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni hivyohivyo, kama ni Jeshi la Polisi hivyohivyo, kama ni Jeshi la Magereza hivyohivyo, kila mmoja awajibike. Kwa hiyo, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge ambao wamesema kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo pengine ningeomba kulichangia, limezungumzwa hapa suala kuhusu kauli za Rais. Kwanza niseme hivi, kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 18(a) inatamka kwamba kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake; inawezekana kwamba baadhi ya wananchi mara nyingi labda wanatafsiri hizo kauli za Rais kwa sababu ya kutumia haki hii. Nilivyokuwa nasoma *Lake Secondary*, Mwalimu mmoja alitufanyia zoezi akasema hivi, kadri habari inavyotoka kwa mtu mwingine kwenda kwa mtu mwingine ndivyo inavyobadilika. Akatufanyia zoezi, akamnong'oneza kitu mwanafunzi wa kwanza kwenye dawati pale, yule wa mwisho kabisa alikuja na taarifa tofauti kabisa na alichoambiwa na Mwalimu na mengine haya huwa tunayasikia wakati hata sisi hatukupata kusikiliza kitu kama hicho.

**MBUNGE FULANI:** Rais hajamnong'oneza mtu anaongea hadharani.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwanza Mheshimiwa Rais anatambua na anazingatia mgawanyo wa madaraka kati ya mihimili mitatu ya dola. Pili, anatambua na kuzingatia utawala wa sheria… *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aah, aah, huo uwongo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Anachokifanya Mheshimiwa Rais ni kuhimiza utawala wa sheria na uwajibikaji wa taasisi na vyombo vya umma na Serikali katika utekelezaji wa majukumu yao na hili ni sharti la msingi. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge*

*walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwa sababu hata Ibara ya 26 ya Katiba ndiyo inayoweka utawala wa sheria na ndicho Rais anachosisitiza na hata jana amesisitiza sana na hili lilikuwa liko wazi.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuko ndani ya Bunge hatuko sokoni. Kama mtu una hoja utafuata taratibu za kikanuni. Mheshimiwa Halima *please*!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwambie aache uwongo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima si jambo la kistaarabu wala si jambo la kiungwana na hasa kwa Kanuni zetu, huwezi ukatoa tu sauti yako ukazungumza unavyotaka. Tuna Kanuni kama anasema jambo ambalo wewe unaliona sio sahihi ziko taratibu zake. Ziko taratibu za kukihukumu mpaka Kiti kwa Bunge hili. Sasa natoa *warning* ya mwisho.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwambie.

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa Halima, *no, no, no!*

**WABUNGE FULANI:** Mtoe nje.

**MWENYEKITI:** Umesikia, tuko ndani ya Bunge, mmesema, mkijua kupiga mjue kukinga. Mheshimiwa *AG* endelea. *(Makofi/Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa hiyo, anachokisisitiza Mheshimiwa Rais ni utawala wa sheria na hata jana amesisitiza sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tekelezeni majukumu yenu kwa ufanisi, Mahakama hivyohivyo, Magereza hivyohivyo, Polisi hivyohivyo, TAKUKURU hivyohivyo. Sasa huyu ndiyo ana *mandate,* ndiyo Mkuu wa Nchi ana wajibu wa kutusisitizia. Anaposisitiza kauli zake wakati fulani kwa sababu ya uhuru huu wa Kikatiba ya kuwa mtu na fikra na mawazo yake anaweza kuwa ameelewa vibaya akamtafsiri vibaya lakini ukweli ni kwamba Rais bado yuko kwenye Katiba anatekeleza tu wajibu wake kwa ufanisi. Ibara ya tisa inatukumbusha kwamba mamlaka ya nchi na vyombo vyake vyote

vinawajibika kuelekeza sera ya shughuli zake zote katika lengo la kuhakikisha kwamba sheria za nchi zinalindwa na kutekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa mara nyingine tena nikushukuru na naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa *Chief Whip*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie muda huu ambao umenipa kupata nafasi ya kuchangia hoja ambazo zimeletwa mbele yetu na Kamati mbili za Kudumu za Bunge. Nami nianze kwa kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Yeye pamoja na Makamu Mwenyekiti lakini na Wajumbe wa Kamati hiyo ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi cha mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwe mkweli, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kamati hii imefanya kazi kubwa sana ya kutushauri Serikalini katika mambo ambayo yanahusu utendaji kazi wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba niseme kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naishukuru sana Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitumie pia nafasi hii nimpongeze sana Rais wetu, Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli; Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan; Waziri Mkuu, ndugu yetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa na Serikali nzima kwa maana ya watendaji wote ndani ya Serikali ya Awamu ya Tano. Nasema hivi kwa sababu, kwa kweli mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Mheshimiwa Rais wetu na Serikali nzima wamejipambanua kwa nia njema ya kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. Watanzania wanalifahamu hili na sifanyi vibaya kusema kwamba ndiyo maana hata uchaguzi huu mdogo uliopita Watanzania wameonesha imani kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa mchango mzuri walioutoa katika taarifa hizi mbili za Kamati. Nasi kama Serikali, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwa yale ambayo ni mambo yanayohusu Wizara moja na nyingine, Ofisi ya Waziri Mkuu itachukua nafasi ya kuyaratibu ili kuona mawazo mazuri haya yaliyosemwa na Wabunge na Kamati hizi mbili yanafanyiwa kazi kwa maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja zilizotolewa, jambo ambalo lilichukua nafasi kubwa hapa ilikuwa ni suala zima la ajira kwa vijana. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kazi hii ya kutambua ni namna gani Serikali ya Awamu ya Tano itajikita katika kupunguza tatizo la ajira nchini imeshaanza kwa kiasi cha kutosha. Naomba niwahikikishie Waheshimiwa Wabunge tunaposhughulikia tatizo hili la ajira tutaangalia Watanzania wote bila kujali itikadi zao za vyama, bila kujali dini, bila kujali kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliamua kwa kuanza kufanya utafiti wa kutambua nguvu kazi iliyoko katika nchi yetu ya Tanzania. Hilo ndilo lilikuwa jambo la msingi ili tuweze kushughulikia ajira. Baada ya utafiti wa mwaka 2014 tulitambua viwango mbalimbali vya nguvu kazi iliyopo katika nchi yetu ambavyo vinaweza kusaidia na kutupeleka kwenye maendeleo tunayoyataka. Tuliona ni muhimu pia tuzitambue sekta kiongozi ambazo zina uwezo wa kutoa ajira za kutosha kwa vijana wa Tanzania. Tulibainisha sekta tano ambazo zinaweza kuwa ndizo sekta hasa za kutoa ajira nchini kilimo ikiwa ni sekta mojawapo, mawasiliano na teknolojia, utalii, ujenzi na sekta nyingine ambazo ndizo tuliona tuanze kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya utafiti wa mwaka 2014 tulichokigundua ni kwamba tunayo kazi kubwa ya kufanya kama Serikali. Tuligundua kwamba kiwango cha nguvu kazi ya juu kilichopo katika nchi yetu ya Tanzania ni asilimia 3.6 na tunatakiwa kukipandisha kiwango hicho cha nguvu kazi mpaka asilimia 12 ndipo tuweze kutengeneza ajira. Pia tuligundua kiwango cha nguvu kazi tulichonacho katika nchi yetu ya Tanzania ili kuweza kutatua tatizo la ajira ni asilimia 16.6 na tunatakiwa kukipandisha mpaka asilimia 14. Tuligundua kiwango cha nguvu kazi tuliyo nayo nchini ya ujuzi wa hali ya chini ni asilimia 79 hadi 80. Ukiwa na ujuzi mkubwa wa kiasi kidogo, ukiwa na ujuzi wa hali ya juu wa kiasi cha kawaida huwezi kutoa ajira wala kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilishukuru sana Bunge lako Tukufu katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ili kuinua viwango vya ujuzi na nguvu kazi katika nchi yetu, mlitutengea fedha na sisi sasa tumeweza kutengeneza progamu nne muhimu sana za kuweza kutengeneza ajira kwa wananchi wa Tanzania. Ili kuinua ujuzi na kuwafanya vijana wa Tanzania waajirike tumeamua kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Tumetengeneza ajira ya kukuza ujuzi kupitia mfumo wa uanangezi;

(ii) Tumetengeneza programu ya kukuza ujuzi kwa kurasimisha ujuzi katika mfumo usio rasmi wa mafunzo;

(iii) Tumetengeneza programu ya mafunzo kwa vitendo *(internship)* kwa wanafunzi wetu ili waweze kuajirika na kujiajiri; na

(iv) Tumetengeneza programu ya kukuza ujuzi kwa Watanzania waliopo makazini waweze kuendana na soko la ajira na teknolojia tuliyonayo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini hayo yakifanyika kwa mwaka mmoja tumejiwekea lengo la kukuza ujuzi na kuwafanya vijana wa Kitanzania wajiajiri ama waajirike wasiopungua 27,000. Kwa hiyo, kazi hiyo inaendelea vizuri. Nataka kusema hapa kazi hiyo imekuwa nzuri kwa sababu Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imetushauri vizuri sana na tumefanya nao kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea yote yaliyozungumzwa kuhusu *NSSF* na ni kweli tunaendelea kufanya kazi nzuri. Nichukue nafasi hii kuipongeza sekta ya hifadhi ya jamii katika nchi yetu ya Tanzania kwa kazi nzuri wanazozifanya. Sekta ya hifadhi ya jamii imeendelea kukua na mpaka sasa rasilimali zilizopo kwenye sekta hii ya hifadhi ya jamii zimefikia thamani ya shilingi trilioni 10.2 katika nchi yetu ya Tanzania, ni mtaji mkubwa sana. Uwekezaji katika sekta hii tu ya hifadhi ya jamii umefikia thamani ya shilingi trilioni 9.2 katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, unaona kwamba sekta hii ina mchango pia mkubwa sana wa uchumi wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kama Serikali tutaendelea kusimamia sekta ya hifadhi ya jamii vizuri kwa kuzingatia miongozo na sheria tulizonazo pamoja na kuboresha mafao ya wastaafu katika sekta ya hifadhi ya jamii lakini tutaitumia pia sekta hii kukuza uchumi wa Tanzania na kutengeneza ajira kwa Watanzania wote katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya pekee sana kuwashukuru sana Wabunge lakini kulishukuru sana Bunge lako Tukufu kwa jinsi ambavyo mmekuwa mstari wa mbele kuishauri Serikali katika mambo yale ambayo mnaona kwamba yanaweza kuendeleza maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania. Naomba niwahakikishie Serikali ya Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli ni Serikali sikivu, ina nia njema ya kuleta maendeleo ya nchi yetu na tutaendelea kufanya hivyo bila kusita. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote kwa pamoja

tufanye kazi na wote lengo letu liwe ni kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, michango imekwisha sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kuja kuhitimisha hoja yake. Una dakika 30 ukimaliza mapema ni vizuri zaidi.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA YA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitambue michango ya Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge lako hili Tukufu waliochangia kuhusu taarifa ya Kamati yetu ya Katiba na Sheria. Waheshimiwa Wabunge 21 walichangia kwa kuzungumza lakini pia Wabunge watatu walichangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitambue michango ya Waheshimiwa Mawaziri waliosimama mbele ya Bunge lako hili hususani Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja. Nami nitajikita kwenye baadhi ya hoja ambazo ziliibuka na kuzitolea maelezo na pia kuliomba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema natoa shukrani za kipekee kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia taarifa yetu hii ya mwaka ambao ni 21. Naanza na hoja ya Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Kamati inakubaliana dhahiri kabisa na mapendekezo yake kwamba Bunge liazimie kuitaka Serikali kufanya jitihada za kutosha kupunguza misongamano magerezani, tatizo la ucheleweshwaji wa kesi Mahakamani zinazohusiana na makosa ya mauaji na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kwamba Kamati ina uwezo wa kulazimisha mahakama na kubadilisha taratibu ili kesi zichukue muda mfupi, sina hakika sana na hoja hii. Niseme tu kwamba kwa kuwa nilipata fursa ya kutumikia mhimili wa Mahakama kwa muda mrefu kidogo nafahamu zipo taratibu za kimahakama ambazo zinafuatwa na Mahakama zetu ikiwa ni pamoja na Katiba na Sheria ya Utumishi wa Mahakama pamoja na *Judicial Administration Act* ambayo ilipitishwa na Bunge lako hili Tukufu mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mchakato wa kunyongwa wafungwa waliohukumiwa kunyongwa na kama Serikali inashindwa basi kifungu husika kibadilishwe kama ambavyo imezungumzwa na Mheshimiwa Adadi nitalitolea ufafanuzi hapo mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Mheshimiwa Abdallah Mtolea kuhusu watu wenye ulemavu na kwamba Kamati iliombe Bunge liazimie kwamba bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu iongezwe hasa kwa Fungu la 65 linalohusika na kazi na ajira ili kuwe na mazingira bora ya kutengeneza ajira kwa vijana. Kamati pia inapenda kuikumbusha Serikali kwamba kile kiasi cha asilimia 10 kilichotengwa kwa ajili ya vijana na wanawake basi kiasi hiki kisipunguzwe na ile asilimia 50 iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo pamoja na *OC* asilimia 40. Kwa hiyo, Kamati inaitaka Serikali kwamba kile kiwango cha asilimia 10 kilichotengwa kwa ajili ya akinamama na vijana kiwe ni kiwango asilia isipungue hata shilingi moja ili sasa vijana wetu pamoja na akinamama waweze kufaidika na kiasi hiki cha asilimia 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunatambua kwamba, nchi yetu inaongozwa na Chama cha Mapinduzi. Kwa mujibu wa ukurasa wa 110 wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ilitengwa kiasi cha Sh. 50,000,000 kwa ajili ya kila kijiji. Tunaiomba Serikali kuhakikisha kwamba kiasi hiki cha fedha sasa kimetolewa ili kwenda kusaidia vijiji vyetu katika maeneo yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inakubaliana na mawazo ya Mheshimiwa Mtolea kwamba Serikali iweke msisitizo mkubwa katika kusimamia haki na maslahi ya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu adhabu ya kifo, katika taarifa yetu ya Kamati kuhusu Muswada Na.4 wa mwaka 2016 iliishauri Serikali kupunguza misongamano magerezani na kufuata sheria ili adhabu ya kifo ambayo inatambulika kwa mujibu wa Kanuni za Adhabu (*Penal Code),* Sura ya 16 iweze kutekelezwa. Adhabu hii ya kifo ipo katika kifungu cha 197 na kifungu cha 196 ambacho kina-*establish* kosa la kuua. Kamati iliishauri Serikali kwa kuwa kuna mrundikano mkubwa wa wafungwa waliohukumiwa kunyongwa adhabu hii iweze kutekelezwa mara moja kwa sababu jukumu hili ni la kikatiba na la kisheria. Pia kama Serikali inaona adhabu hii haitekelezeki basi ni vyema ikawasilisha maoni ili iweze kuondolewa kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaendelea kuishauri Serikali utekelezaji wa adhabu hii uendelee kama ambavyo umeainishwa katika kifungu cha 197 cha Kanuni za Adhabu, Sura 16. Tunafahamu ni mateso makubwa sana

wanayapata wale waliohukumiwa kunyongwa wakisubiri adhabu ya kifo. Wao wenyewe wako tayari kupatiwa adhabu yao ya kifo iwapo itatekelezwa hata kama ni kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengine ni Mheshimiwa Taska Mbogo ambaye yeye amezungumzia suala la *NSSF* ambalo sitalizungumzia zaidi hapa kwa sababu tayari Mheshimiwa Waziri ameshalidokezea kuhusiana na mchango mkubwa wa hifadhi za jamii katika Taifa letu. Pia kama ilivyoagizwa katika taarifa za Kamati, Kamati inaendelea kusisitiza kwamba maagizo ya Bunge yatekelezwe na taasisi zote kama yalivyoelekezwa kuhusiana na uwasilishwaji wa mikataba ya uwekezaji unaofanywa na taasisi hii ya *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taasisi za usimamizi wa haki, katika taarifa yake Kamati imesisitiza Mahakama na Tume ya Haki za Binadamu ziongezewe bajeti katika mwaka wa fedha ujao wa 2017/2018 ili kuboresha utendaji kazi wa taasisi hizo. Bajeti hiyo itasaidia utolewaji wa semina ili wadau wawe na uelewa wa kutosha wa sheria zinazopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lucia Michael alizungumzia kwamba jukumu la Polisi sasa limebadilika kutoka ulinzi wa amani na kuelekea kwenye ukusanyaji wa kodi. Kamati pia inaendelea kushauri Serikali kwamba siyo jukumu la Polisi kukusanya kodi kama ambavyo inafanyika leo hii Polisi wanakusanya kodi kwa makosa mbalimbali ya barabarani ambapo wanawakamata washtakiwa na wanakusanya kodi kama wao ni *TRA*. Kamati inaitaka Serikali jukumu la ukusanyaji kodi liendelee kubaki *TRA* na kulitaka Jeshi la Polisi kuacha mara moja kufanya kazi hizi ambazo hawawajibiki kwa mujibu wa taratibu na sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chikota alizungumzia kuhusiana na fedha kutolewa chini ya kiwango kilichopitishwa. Msimamo wa Kamati ni kwamba fedha ziongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ucheleweshwaji wa kesi mahakamani ombi la Mheshimiwa Adadi, kama nilivyosema hapo awali jibu katika taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Katiba na Sheria, tarehe 3 Mei, 2016, Kamati iliagiza Wizara na taasisi zake kuhakikisha kwamba Mahakama inapunguza wingi wa kesi yaani *backload of cases* mahakamani na kwamba haki itolewe kwa haraka na kwa mujibu wa sheria kwani *justice delayed is justice denied.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nimpongeze Mheshimiwa Jaji Mkuu Msatafu Mohamed Chande Othman kwa jitihada zake kubwa alizofanya katika kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani ambapo naamini Kaimu Jaji Mkuu wa sasa hivi anaweza kuendeleza ile njia nzuri ambayo alianzisha Mheshimiwa Jaji Mkuu Mstaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa ya Kamati kwa ujumla, Mheshimiwa Mtolea alisema kwamba taarifa imebeba maudhui mengi ya kikatiba na kisheria. Labda niseme tu kwamba Kamati ya Katiba na Sheria mpaka sasa imeshawasilisha Bungeni taarifa tisa, tatu za kibajeti na sita za Miswada ya Sheria. Kamati pia ilitoa maoni na mapendekezo ya jumla kuhusu Wizara na taasisi inazozisimamia, masuala ya kazi, ajira na watu wenye ulemavu yapo katika taarifa rasmi ya Kamati yaliyosomwa hapa Bungeni tarehe 19 Aprili, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ngombale alizungumzia kuhusu Mabaraza ya Ardhi pamoja na uboreshwaji wa Kamati. Kamati pia inaishauri Serikali hususani Wizara ya Katiba na Sheria na tutaona uwezekano wa kukaa na Wizara hii ili kuweza kuzungumza na Mheshimiwa Waziri kuona uwezekano wa kesi za ardhi kurudishwa katika Mahakama ya Tanzania; kwa sababu tunafahamu kwamba kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 107 inaitaja Mahakama kama ndiyo mhimili wa utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba upo mkinzano unaotokana na Mabaraza kuwa chini ya mihimili tofauti. Mfano, Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Vijiji yapo chini ya TAMISEMI, Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya yapo chini ya Wizara ya Ardhi lakini pia ipo Mahakama Kuu ambayo inawajibika chini ya Mahakama. Hivyo, Kamati inaona kuna mwingiliano mkubwa wa haki katika Mahakama na Serikali na ipo sababu kubwa hapo baadaye kuwepo na kesi nyingi za kikatiba kupinga hukumu zilizotolewa katika Mabaraza ya Ardhi kwa kuwa jukumu la mwisho la utoaji haki lipo chini ya Mahakama ya Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Omary Mgumba amechangia kuhusiana na mgogoro wa wakulima na wafugaji. Jambo hili sina hakika kabisa kama limeelekezwa kwenye Kamati yangu au ile Kamati ya Utawala lakini nataka niseme tu kwamba ni kweli kabisa mgogoro wa ardhi ni mkubwa sana katika nchi yetu na tunaona kabisa kwamba ile misingi imara aliyotuachia Mwalimu Nyerere ya Watanzania kupendana inakwenda kuvunjika iwapo migogoro hii ya wakulima na wafugaji haitatatuliwa mara moja. Hivyo, tunaona

kabisa kwamba Wizara ya Kilimo na Mifugo imeshindwa kutatua mgogoro huu na tunaiomba Ofisi ya Waziri Mkuu sasa kuingilia kati ili kuweza kuondoa matatizo haya yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima itambulike kwamba hakuna mgogoro wa ardhi, mgogoro uliopo ni mwingiliano wa kijinai yaani *criminal trespass* kati ya wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, hatuna migogoro ya ardhi na naamini kabisa kwamba nchi yetu ina ardhi kubwa, mgogoro huu iwapo utatatuliwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa utaweza kwisha mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Frank Mwakajoka alizungumzia kuhusiana na watu kukata tamaa kupiga kura. Kamati yetu kwa kuwa inasimamia Tume ya Uchaguzi tunaiagiza Serikali kuongeza fungu kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi ili kuendelea kutoa elimu ya mpiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wananchi kukamatwa kwa kutoa taarifa za njaa, tunaishauri pia Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kazi na Ajira kuendelea kutoa taarifa kuhusiana na majanga na maafa ili iweze kuondoa kero kubwa ambayo inajitokeza hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cecilia Paresso alizungumzia kuhusiana na ucheleweshwaji wa kesi kwamba viongozi wa CHADEMA wamekuwa wakikamatwa na kesi zao hazichukui muda mrefu. Ni jukumu la utendaji haki kama ilivyo katika Katiba kwamba ni lazima haki iendelee kuonekana imetendeka. Naamini kabisa kwamba siyo jambo la busara kwa kiongozi kuendelea kubaki mahakamani kwa muda mrefu. Kwa hiyo, tunaishauri Mahakama kuendelea kusikiliza kesi haraka hususani zinazowahusu viongozi wa vyama vya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia itambulike kwamba zipo taratibu za rufaa ambazo zimeainishwa katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawaomba wale wote ambao wana malalamiko kuhusiana na kesi basi wafuate taratibu za rufaa ambazo zimeainishwa katika Katiba, lakini pia katika sheria mbalimbali za nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la akinamama magerezani, Mheshimiwa Mbaruk alizungumzia suala hili. Kamati inakubalina na mawazo ya Mheshimiwa Mbunge kwamba maslahi ya watoto yazingatiwe yaani *best interest of the child* pale ambapo wafungwa wanajifungulia magerezani. Kamati inasisitiza kwamba watoto wanaozaliwa katika mazingira haya watazamwe kwa umakini kwa ajili ya haki zao kama watoto kwa mujibu wa

Sheria ya Watoto ya mwaka 2009 lakini pia na Mkataba wa Haki za Watoto wa mwaka 1989. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Paresso pia aliendelea kusisitiza kuhusiana na mrundikano wa wafungwa gerezani na utawala wa sheria. Suala hili Kamati inalitambua na inaungana na maoni ya Mbunge kwamba Serikali na Mahakama zifanye jitihada za kutosha kupunguza mrundikano wa kesi na wafungwa magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango iliyotolewa kwa ujumla ni kuhusu mrundikano wa wafungwa magerezani, wingi wa kesi mahakamani na kasi ndogo ya kumaliza kesi, haki za watu wenye ulemavu, suala la ajira na vijana, uongezaji wa bajeti katika Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ukaguzi wa miradi ya maendeleo, muda wa kikanuni uongezwe na jengo la Mwanasheria Mkuu wa Serikali lipewe kipaumbele. Kamati inakubalina na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge na inaomba yawe sehemu ya mapendekezo ya Kamati na Bunge hili iyakubali kama maazimio ya Bunge yalivyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba Bunge lako sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo pamoja na yale mengine ambayo nimeyasoma katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Nakupongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati yako na Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri mliochangia, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Taarifa hii sasa inakuwa ni taarifa rasmi ya Bunge ambayo inakwenda Serikalini kufanyiwa kazi na inakwenda kwa mujibu wa Kanuni ya

117(15). Kinachofanywa hapa kinafanywa kwa mujibu wa Kanuni, ni lazima Bunge lijadili taarifa za Kamati kwa kila mwaka. Nakupongeza sana Mwenyekiti na Serikali mmejibu vizuri sana. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii uliyonipa ya kuweza kujumuisha hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kusema katika hoja hii ni Waheshimiwa Wabunge 22 na wale waliochangia kwa maandishi ni 14. Nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri, Mheshimiwa Angellah Kairuki na Waziri, Mheshimiwa George Simbachawene kwa maelezo yao ambayo wameyatoa hapa ambayo kwa kiasi kikubwa yamejibu hoja mbalimbali ambazo zimeboresha uelewa wa hoja ambazo ningezisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa imepata wachangiaji 22 waliochangia kwa kuzungumza na 14 waliochangia kwa njia ya maandishi. Eneo la kwanza wamezungumzia Tume ya Utumishi ya Walimu *(TSC)* na wamegusia kero zinazowakabili walimu ambazo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutolipwa madai yao ya likizo;

(ii) Uhamisho;

(iii) Mishahara na kadhalika;

(iv) Walimu kunyimwa uhamisho;

(v) Mazingira magumu ya kazi;

(vi) Mrundikano wa wanafunzi darasani, ukosefu wa nyumba za kuishi na kadhalika.

(vii) Kushushwa vyeo kwa walimu na matamko ya watawala – Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya;

(viii) Bajeti ya Tume iongezwe ili iweze kujitanua katika wilaya nchi nzima;

(ix) Kasoro zilizobainika katika Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu zirekebishwe ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto zinazowakabili walimu; na

(x) TAMISEMI ihakikishe inatenga fedha za kutosha katika bajeti ijayo ili kuondoa kero za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni la utawala bora na rushwa. Katika eneo hili wachangiaji wamebainisha mambo yafuatayo:-

(i) Wasimamizi wa Serikali hawafuati sheria, kanuni na taratibu za utawala;

(ii) Watendaji wasijielekeze katika kuwajibisha watumishi tu bali wawajengee uwezo na mazingira bora ya kazi kabla ya kuwawajibisha;

(iii) Vita ya rushwa asiachiwe Mheshimiwa Rais peke yake, viongozi wote na jamii nzima wahusike katika mapambano haya;

(iv) Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wazingatie dhana ya utawala bora pamoja na sheria zinazoongoza utendaji wao;

(v) Watendaji wa Serikali waheshimu dhana ya mgawanyo wa madaraka *(separation of powers)* kwa mihimili mitatu yaani Serikali, Mahakama na Bunge ili kuepusha mgongano wa kiutendaji;

(vi) Haki za binadamu zizingatiwe wakati wa kuwawajibisha watumishi wanaopatikana na makosa ya kiutumishi;

(vii) Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wapewe semina elekezi kuhusiana na utekelezaji wa majukumu yao;

(viii) Watendaji wa Vijiji na Mitaa na Madiwani wapatiwe mafunzo ya kiutendaji na mishahara; na

(ix) Viongozi wawe makini kabla ya kutoa matamko na waache woga katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, ni Halmashauri kutenga asilimia 10 ili kusaidia wanawake na vijana. Katika eneo hili wachangiaji wamegusia mambo yafuatayo:-

(i) Halmashauri nyingi nchini zimeshindwa kutekeleza agizo hili la Serikali kwa kukosa uwezo wa kifedha;

(ii) Hatua ya Serikali kuondoa ukusanyaji wa kodi ya majengo *(property tax)* katika Halmashauri imeathiri kwa kiasi kikubwa uwezo wa mapato ya Halmashauri;

(iii) Serikali haipeleki kikamilifu ruzuku katika Halmashauri; na

(iv) Serikali iangalie mpango wa kuelekeza shilingi milioni 50 za kila kijiji kusaidia vikundi vya vijana, akinamama na *SACCOS*. Katika eneo hili ni Halmashauri 13 tu ambazo zimepelekewa fedha katika kundi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la nne ni *TASAF*. *TASAF* Awamu ya III imejielekeza katika kunusuru kaya maskini. Katika eneo hili wachangiaji wamegusia mambo yafuatayo:-

(i) Mpango huu umekuwa na mafanikio makubwa kwa kusaidia kaya maskini kuweza kumudu mahitaji ya msingi kama vile chakula, elimu na afya;

(ii) Umepunguza utegemezi wa kaya maskini kwa Waheshimiwa Wabunge;

(iii) Miradi ya maendeleo inayotekelezwa na *TASAF* ishirikishe wananchi wanaonufaika; na

(iv) Wananchi waelimishwe kuhusiana na mpango wa *TASAF* wa kusaidia kaya maskini.

Hapa ni kweli kwamba Serikali haichangii mchango wake katika *TASAF*. Tunayo takwimu hapa, katika miaka mitano iliyopita Serikali imetoa mchango kidogo sana katika fungu hili. Mwaka 2012/2013 bajeti ya Serikali iliyopitishwa ilikuwa shilingi bilioni nne, kiasi kilichotolewa ni shilingi bilioni 2.5, kiasi kilichobaki ni shilingi bilioni 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka uliofuata kiasi kilichoidhinishwa ni shilingi bilioni 18.5, kiasi kilichotolewa ni shilingi bilioni tatu, kilichobaki ni shilingi bilioni 15.5. Mwaka uliofuata kiasi kilichoidhinishwa ni shilingi bilioni 14, kilichotolewa ni sifuri, kilichobaki ni shilingi bilioni 14. Mwaka uliofuata iliidhinishwa shilingi bilioni 14, ilitolewa shilingi milioni 600 ikabaki shilingi bilioni 13.4. Mwaka uliofuata (mwaka jana) iliidhinishwa shilingi bilioni 14, ilitolewa sifuri, ikabaki shilingi bilioni 14.

Kwa hiyo, katika miaka mitano hii Bunge liliidhinisha shilingi bilioni 64.5 na iliyotolewa ni shilingi bilioni 6.1, ikabaki shilingi bilioni 58.4. Kwa hiyo, kwa kweli Serikali haijatoa mchango wake mkubwa katika eneo la *TASAF*. Kamati inasisitiza kwamba Serikali iongeze mchango wake ili wananchi waweze kunufaika na mpango huu wa *TASAF III*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tano ni utumishi wa umma. Katika eneo hili wachangiaji wamegusia mambo yafuatayo:-

(i) Hatua ya Serikali kusitisha ajira na upandishaji vyeo kwa watumishi imeathiri watumishi ambao wanakaribia kustaafu. Serikali iruhusu ajira kwani kuna wahitimu wengi ambao wako mitaani wakisubiri ajira za Serikali;

(ii) Watumishi wanaofanya kazi wapewe motisha;

(iii) Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri na Watendaji wengine ambao hawakuwa katika utumishi wa umma kabla ya uteuzi wao wapewe semina elekezi kuhusiana na namna ya kutekeleza majukumu yao; na

(iv) Maamuzi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya dhidi ya watumishi yanavunja moyo watumishi hao na kusababisha baadhi yao waone kwamba haina thamani kuwa mtumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la sita ni utoaji wa elimu ya msingi bila malipo. Katika eneo hili, wachangiaji wamepongeza hatua ya Serikali kwani imekuwa na mafanikio ambayo hata hivyo yana changamoto mbalimbali, nazo ni kama ifuatavyo:-

(i) Uhaba wa vyumba vya madarasa;

(ii) Uhaba wa nyumba za Walimu;

(iii) Matundu ya vyoo na kadhalika;

(iv) Uhaba wa Walimu;

(v) TAMISEMI inashindwa kugharamia uendeshaji wa shule za Serikali kutokana na kuwa na mambo mengi; na

(vi) Bado wazazi wanawajibika kuchangia mahitaji ya wanafunzi kwani Serikali ilichoondoa ni ada na michango ya uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yalikuwa mambo ya jumla lakini Waheshimiwa Wabunge katika michango yao vilevile wamegusia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waitara katika mchango wake amesema mambo kadhaa na akalaumu kwamba kuna viongozi ambao wanatoa matamshi ambayo yanakatisha tamaa, akamsema Rais kwamba ametoa matamshi ambayo sio mazuri. Mimi nasema hii siyo sahihi. Mheshimiwa Rais amejipambanua kwamba yeye hapendi rushwa, amesema wazi kwamba rushwa kwake ni mwiko. Hata ndani ya Chama cha Mapinduzi ambacho ndiyo chama chake, amesema uchaguzi mwaka huu atakayetoa rushwa hatateuliwa kugombea nafasi yoyote. Pia amefanya kazi kubwa sana ameanzisha Mahakama ya Mafisadi ambayo inapinga rushwa na mambo mengine ambayo tumeyaona. Amezungumzia mambo mengi lakini sitayasema yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kiteto amesema kwamba Mabaraza ya Madiwani, *RCC* na kadhalika visifanyike wakati wa vikao vya Bunge. Kamati inaunga mkono hoja hii nzuri kwani Waheshimiwa Wabunge

wana mchango mkubwa kwenye Mabaraza ya Madiwani, vikao vya *RCC* na vikao vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Japhary Michael amezungumzia mambo mengi, mojawapo ni kuhusu elimu bure. Hakuna elimu bure, elimu inalipiwa na anayelipia ni Serikali na Serikali inalipia kutokana na kodi za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwalongo amesema kwamba Watendaji wa Vijiji, wa Mitaa na wengine waajiriwe wasikaimu muda mrefu. Kamati inaunga mkono, ni hoja nzuri, wakikaimu muda mrefu wanakuwa hawana maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia pia suala la kuwa na shule za awali katika shule za msingi na maeneo mengine na akasema kwamba ni vizuri shule za awali ziwe pale ambapo wanafunzi hao wapo kwa sababu ni wadogo kutembea umbali mrefu ni vigumu sana. Kamati inaunga mkono hoja hii ili kufanikisha ili azma ya kuwa na 'K' tatu zile, Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Mtoto akianzia shule ya awali anapata msingi mzuri anapokwenda shule ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini amezungumzia Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa kupewa posho. Ni jambo jema, tunashauri Serikali ijitahidi kuongeza mapato ili iweze kuwalipa posho Wenyeviti wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini amezungumzia *TASAF II* kwamba ni jambo zuri limewasaidia sana wananchi hasa kaya maskini. Takwimu zilizopo zinaonesha kwamba katika miaka mitatu iliyopita *TASAF III* imetumia zaidi ya shilingi bilioni 400 na zaidi ya kaya milioni moja zimenufaika na mpango huu. Watu wengine wanatumia vizuri mpango huu na wanajinufaisha wanakuwa na miradi ya kujikwamua na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ameshauri kwamba mpango huu uboreshwe ili fedha hizi zitumike vizuri zaidi. Kamati inaunga mkono hoja hii kwa sababu kuna baadhi ya watu ambao wakipata hela hizi za *TASAF* wanalewea pombe na kuna wengine ambao sio watu maskini kama ilivyosemwa na wachangiaji wengi lakini wamo kwenye mpango huu. Kwa hiyo, Kamati inashauri kwamba ni vizuri mpango huu ukaboreshwa. Mpango mzuri zaidi ni kama alivyosema Mheshimiwa Rais kwamba hizi pesa badala ya kutolewa bure watu waajiriwe kwa kazi ndogondogo hizi za usafi kwenye mitaa, kuzibua

mitaro, kupanda miti, kujenga madarasa, kujenga kliniki na kadhalika ili waendelee kupata pesa lakini vilevile tupate maendeleo kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab amezungumzia Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi Dar es Salaam. Amepongeza na kwa kweli Kamati inashukuru kwa mchango huo, mradi huu ni mzuri sana. Tangu uanze mwezi Mei, 2016, barabara ile ya Morogoro sasa haina msongamano wa magari, imekuwa ni barabara nzuri. Tunashauri kwamba mradi huu usimamiwe vizuri zaidi ili barabara nyingine *Phase II, Phase III* mpaka *Phase VI* zikamilike. Barabara ya Kilwa, Barabara ya Bagamoyo, Barabara ya Pugu na nyingine zijengwe kwa utaratibu huo wa mabasi yaendayo kasi ili Jiji la Dar es Salaam liondokane na kero za msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia pale kwenye mradi ambao umekamilika wa Kimara *Ferry* (Kivukoni), pale Ubungo *interchange* pajengwe *flyover* haraka sana basi linakaa pale dakika 10, 15 likisubiri kuruhusiwa kwenda. Sasa inakuwa tena siyo kasi ni kama mabasi mengine ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Richard Mbogo katika utawala bora amezungumzia kwamba baadhi ya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na viongozi wengine wanatumia vibaya madaraka yao. Wanakamata watu hovyo, kuwaweka ndani hovyo, kuwapunguza madaraka na kadhalika. Kamati inaunga mkono hoja hii kwamba kwa kweli ni vizuri Serikali ikaangalia sheria inazingatiwa kwa sheria zipo. Kamati za nidhamu, za ajira zitumike na siyo mtu mmoja kutoa maamuzi ambayo wakati mwingine yanakinzana na sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe amezungumzia mambo mengi lakini moja amesema kwamba hela ya *TASAF* hii inayotolewa kwa wananchi iwe *accounted for*. Kabla ya kupewa fedha nyingine aeleze ile ya kwanza ameitumiaje. Ni wazo zuri katika kuboresha utoaji wa fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Tunza katika mchango wake wa maandishi amesema ni vizuri Serikali ikaangalia matumizi ya gesi na mafuta tuliyogundua. Watu wapate elimu kuhusu matumizi au fursa zilizopo katika utajiri huu. Inawezekana baadhi ya wananchi wakafikiri kwamba baada ya kugundua mafuta na gesi basi hakuna kufanya kazi, ni kula tu, hapana wafahamu kwamba kuna fursa na wazitumie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ruth Mollel amechangia akasema kwamba Bunge siyo huru na akatoa mfano kwamba hakuna Bunge *live*. Sisi

tunasema hii siyo kweli, Bunge kutokuwa *live* haina uhusiano wowote na kutokuwa huru. Tuliamua wenyewe hapa ndani kwamba Bunge lisiwe *live* kwa sababu ambazo zilielezwa humu ndani pamoja na gharama, *TBC* ilishindwa kuendesha mradi huo wa Bunge kuwa *live*. Kwa hiyo, hii haina uhusiano na Bunge kutokuwa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akatoa mfano mwingine kwamba Mahakama zimenyamaza kuhusu mikutano ya hadhara ya vyama. Mahakama haiwezi kutoa maamuzi bila mtu kwenda mahakamani. Ni lazima mtu afungue kesi na ndipo asikilizwe Mahakama itoe uamuzi. Kwa hiyo, Mahakama zipo huru mwenye malalamiko yoyote aende Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Omary Tebweta amezungumia mambo mengi lakini mojawapo ni kuhusu asilimia 10 kwenda kwa vijana na wanawake, asilimia 50 maendeleo na asilimia 40 kwenye *Other Charges* (Matumizi Mengineyo). Ameeleza vizuri na sisi tunakubaliana naye kwamba baadhi ya Halmashauri zinatumia mwanya huu kujipatia hela ya matumizi mengineyo. Inatenga fungu la asilimia 40 kwa Matumizi Mengineyo, inatenga labda shilingi bilioni mbili ikifahamu fika kwamba haiwezi kupata shilingi bilioni mbili kwa mapato mengine ya ndani lakini inapanga makusudi shilingi bilioni mbili ili hela yote iingie kwenye Matumizi Mengineyo. Tunashauri utaratibu huu udhibitiwe na asilimia 40 iwe ni kweli asilimia 40 ya yale mapato ambayo wamepata sio Mapato Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza amezungumzia uchaguzi kutokuwa huru. Kamati haikubaliani naye. Uchaguzi ni huru na ni wa haki. Hata juzi kwenye kata zile zilizorudia uchaguzi CCM imeshinda kwa haki. Mtu yeyote ambaye haridhiki na matokeo Mahakama zipo, aende mahakamani alalamike, apeleke ushahidi ahukumiwe. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Unatafuta Uwaziri Mzee?

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia niombe sasa Bunge lako Tukufu likubali Taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, mmefanya kazi nzuri. Toa hoja.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mmefanya kazi nzuri, sasa nitalihoji Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hatua hiyo, hii sasa ni taarifa rasmi ya Bunge kwenda Serikalini. Nawapongeza wote, Mawaziri mmefanya kazi nzuri, *AG, Chief Whip,* hongereni sana. *(Makofi)*

Nina tangazo, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Katibu wa Wabunge wa CCM na Mjumbe wa Kamati Kuu, anaomba kuwatangazia Wabunge wa CCM wahudhurie sherehe za miaka 40 ya CCM Kitaifa zitakazofanyika *Dodoma Convention Center* Jumapili, tarehe 5 Februari, 2017, saa saba mchana na Wabunge wengine wenye hamu ya kuja wanakaribishwa vilevile. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.14 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 4 Februari, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*